2023

KITABU CHA NYENZO

Huduma za Familia ya Kiadventista

NITAKWENDA NA FAMILIA YANGU:

FAMILIA NA AFYA YA AKILI

Huduma za Familia
ya Kiadventista

NITAKWENDA NA FAMILIA YANGU:

FAMILIA NA AFYA YA AKILI

WILLIE NA ELAINE OLIVER

ALINA BALTAZAR, JEFF BROWN, KATELYN CAMPBELL WEAKLEY, CLAUDIO NA PAMELA CONSUEGRA, JASMINE FRASER, DAWN JACOBSON-VENN, JOSEPH KIDDER, RICK MCEDWARD, JOHN NIXON, SR. WILLIE & ELAINE OLIVER, SVEN DSTRING, MINDY SALYERS, DAVID & BEVERLY SEDLACEK, JOHN B. YOUNGBERG

REVIEW AND HERALD PUBLISHING ASSOCIATION
Tangu 1861 www.reviewandherald.com

Huduma za Familia
ya Kiadventista

Hakimiliki © 2021 na Review and Herald® Publishing Association

Haki zote zimehifadhiwa
Mhariri: Willie na Elaine Oliver
Mhariri Mkuu: Dawn Jacobson-Venn
Msanifu na mpangaji: Daniel Taipe
Mbunifu wa ukurasa wa kwanza: JMrocek/via Getty Image
Mtafsiri: Moseti Chacha: Simu +255 712 282224

Mtunzi anawajibika kwa usahihi wa kweli na nukuu zote zilizomo humu

Wachangiaji:
ALINA BALTAZAR, JEFF BROWN, KATELYN CAMPBELL WEAKLEY, CLAUDIO NA PAMELA CONSUEGRA, JASMINE FRASER, DAWN JACOBSON-VENN, JOSEPH KIDDER, RICK MCEDWARD, JOHN NIXON, SR. WILLIE & ELAINE OLIVER, SVEN DSTRING, MINDY SALYERS, DAVID & BEVERLY SEDLACEK, JOHN B. YOUNGBERG

Vitabu vingine vya Huduma za Familia katika mtiririko huu:

Nitakwenda na Familia Yangu, Umoja katika Jumuia
Kufikia Familia na Yesu: Kufanya Wanafunzi
Kufikia Familia na Yesu: Kuimarisha Wanafunzi
Kufikia Familia na Yesu: Uanafunzi na Huduma
Kufikia Familia na Yesu: Kukua katika Uanafunzi
Kuufikia Ulimwengu: Familia zenye Ustawi na Umilele
Uamsho na Matengenezo: Kujenga Kumbukumbu za Familia
Uamsho na Matengenezo: Familia Kufikia Juu
Uamsho na Matengenezo: Familia Kufikia Walio Nje
Uamsho na Matengenezo: Familia Kufikia Ng'ambo

Vyote hivi vinapatikana katika tovuti hii:
www.family.adventist.org/resourcebook

Nukuu za Biblia zimechukuliwa kutoka katika toleo la "Swahili Union Bible"

Idara ya Huduma za Familia: family@gc.adventist.org
Halmashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato

YALIYOMO

Utangulizi 6

Jinsi ya kutumia kitabu hiki 8

MAWAZO YA MAHUBIRI

Lisha Moyo Wako: Kupata Afya ya Kiroho na ya Kimhemuko katika Ulimwengu Uliovunjika 11
Willie na Elaine Oliver.

Kisa cha Familia Mbili 21
John Nixon, Sr.

Ibada ya Familia: Uzio Unaolinda 32
John B. Youngberg

Kwa Moyo Wako Wote Maisha Yote! 44
Jasmine Fraser

Safari ya Kukata Tamaa 53
Rick McEdward

VISA VYA WATOTO

Kukuza Zukini Nzuri 65
Elaine Oliver

Kushughulika na Hisia za Hasira 67
Dawn Jacobson-Venn

Mpango wa Kutoroka 70
Mindy Salyers

SEMINA

Kulea Ustawi wa Mihemuko katika Familia 75
Willie na Elaine Oliver

Kuishi na Mwenzi mwenye Ugonjwa wa Akili 84
Willie na Elaine Oliver`

Athari ya Unyanyasaji wa Kingono kwa Watoto 90
Alina Baltazar

Kuunda Mtazamo wa Kilimwengu wa Mtoto wako kupitia katika Mfano, Kufundisha na Kuhudumia ……..……...……. 104
Joseph Kidder na Katelyn Campbell Weakley

NYENZO ZA UONGOZI

Kwani kuna nini katika Ushoga? ……..…...…..……..…..…… 117
Willie na Elaine Oliver

Kunidhamisha Watoto Wetu kwa Upendo ……...… 119
David na Beverly Sedlacek

Athari za Kiakili za Huzuni ……..……...……..…… 125
Claudio na Pamela Consuegra.

Namna ya Kiume ya Kuongoza ...……..……..…..……..…… 133
Jeff Brown

Pembetatu ya Familia ……..……...…..…… 147
Sven Ostring

MAKALA ZILIZOCHAPISHWA UPYA

Kufariji Wenye Huzuni ..……...……..……..…… 152
Willie na Elainer Oliver

Upotevu Wenye Utata ……..……..……...…. 155
Willie na Elaine Oliver

Tumaini Mbele ya Talaka – Sehemu ya 1 ……..……....……,..……. 157
Willie na Elaine Oliver

Tumaini Mbele ya Talaka – Sehemu ya 2 ……..…….. 159
Willie na Elaine Oliver

Ni Wapi Tulipokosea? ……..……..……..…..…… 161
Willie na Elaine Oliver

NYENZO

Kujenga Upya Madhabahu ya Familia ……..…..……...……. 164

Mazungumzo halisi ya Familia: Majibu kwa Maswali
Kuhusu Upendo, Ndoa na Tendo la Ndoa ……...…….. 165

Mazungumzo Halisi ya Familia na Willie & Elaine Oliver ……..……...… 166

Kuunganika: Ibada kwa Wenzi wanaopendana ……..……. 167

Biblia ya Wenzi 168

Tumaini kwa Familia za Leo 169

Mungu Ananipenda Pamoja na Hisia Zangu Zote 170

Ndoa: Biblia na Vipengele vya Kiteolojia 171

Ngono: Masuala ya Kawaida kwa Mtazamo wa Kibiblia 172

Faraja ya Siku: Kuishi katika Kipindi cha Huzuni 173

KIAMBATISHI 'A' – UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA FAMILIA

Sera ya Huduma za Familia na Tamko la Kusudio 175

Kiongozi wa Huduma za Familia 177

Familia ni Nini? 179

Miongozo ya Kamati na Kupanga 181

Wasilisho Zuri Litafanya Mambo Manne 183

Amri Kumi za Uwasilishaji 184

Uchunguzi wa Mwonekano wa Maisha ya Familia 185

Maelezo Mafupi ya Maisha ya Familia 188

Uchunguzi wa Shauku ya Huduma za Familia 190

Uchunguzi wa Elimu ya Maisha ya Familia ya Jumuia 192

Kielelezo cha Tathmini 194

KIAMBATISHI 'B' – MATAMKO YALIYOPITISHWA

Uthibitisho wa Ndoa 197

Tamko kuhusu Nyumbani na Familia 199

Tamko kuhusu Unyanyasaji wa Watoto Kingono 200

Tamko kuhusu Migogoro ya Kifamilia 202

Tamko kuhusu Mtazamo wa Kibiblia wa Watoto ambao Hawajazaliwa, na Matokeo yake katika Kutoa Mimba 206

Miongozo ya Kanisa kwa Mabadiliko ya Kitamaduni Kuhusu Ushoga, Na Vitendo vingine vya Ngono 211

UTANGULIZI

Mtunga Zaburi anatamka kuwa, "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu." (Zaburi 42:1).

Huu ni uwakilishi mzuri wa ayala mwenye kiu akitafuta kijito cha maji jangwani. Mtunga Zaburi kwa uzito huo huo wa mnyama anayetafuta maji ya uzima, anamtafuta Mungu aliye hai, aliye chimbuko la uhai, nguvu, ujasiri, na tumaini. Aya hiyo haioneshi sababu hasa au asili ya uchungu wa Mtunga Zaburi, hata hivyo anashughulika na kile kilichompeleka hadi katika mfadhaiko mkubwa, wakati huo huo ile hali ya kutambua kwamba tumaini halisi kwa hali yake hiyo linapatikana katika Mungu aliye hai pekee.

Wataalam wa afya ya mhemuko wanapendekeza kwamba hali inayosonga kama vile kifo cha mpendwa, matatizo ya ndoa na familia, au talaka vinaweza kusababisha madhara kwa afya ya akili ya mtu. Pamoja na hayo, magonjwa sugu, athari katika ubongo inayoweza kutokana na ajali, kupoteza ajira, mashambulizi ya kivita, vyote hivi pia vinaweza kuchangia katika uwezekano wa ugonjwa wa akili.

Jumuia zote duniani sasa hivi zimejawa na wingi wa watu wanaopitia katika huzuni, kukata tamaa, na mashaka kila siku. Ugonjwa wa UVIKO-19 ambao haujapata ufumbuzi kikamilifu – ukiongeza na msongo katika familia nyingi kutokana na kupoteza kazi, na migogoro inayoongezeka katika familia – pamoja na mapambano ya kivita yanayoendelea katika sehemu nyingi za ulimwengu, vyote hivyo vinahatarisha ustawi wa akili ya familia na ya mtu mmoja mmoja kila mahali.

Hapa ndipo huduma za familia zinapoweza kusaidia na kutegemeza familia kwa nyenzo za kuwasaidia kuwasiliana kwa ufanisi zaidi, kuimarisha ile hali ya kujitoa kwa dhati katika ndoa, kuwa wazazi bora, na kudumisha tumaini kuu kwa Mungu – ambaye ni chimbuko bora la msingi wa afya ya akili. Hata hivyo si ni Mungu ndiye aliyetuasa katika Wafilipi 4:6, 7 kuwa, "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."

Ni ombi letu kwamba kitabu cha Nyenzo za Huduma za Familia cha mwaka 2023 – kinachoweka msisitizo katika Familia na Afya ya Akili – kitumike kama nyenzo ya thamani kwa wachungaji, viongozi wa Huduma za Familia, na washiriki wote waliojitoa kikamilifu kutegemeza familia, siyo tu katika masuala ya afya ya mhemuko, bali pia kwa ustawi wao wa kiroho ili kuweza kuishi maono haya ya "Nitakwenda na Familia Yangu."

Maranatha!

Willie na Elaine Oliver, Wakurugenzi
Idara ya Huduma za Familia

Halmashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato

Makao Mkuu ya Ulimwengu

Silver Spring, Maryland

family.adventist.org

JINSI YA KUTUMIA
NYENZO HII

Kitabu ambacho ni nyenzo ya Huduma za Familia ni kitendea kazi kinachotolewa kila mwaka kilichopangiliwa na Idara ya Huduma za Familia ya Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato kikiwa na nyongeza kutoka katika maeneo mbali mbali ulimwenguni, ili kuyapatia makanisa mahalia kote ulimwenguni nyenzo au vitendea kazi kwa ajili ya Sabato maalum za majuma ya msisitizo.

Ndani ya kitendea kazi hiki utapata dhana za mahubiri, semina, visa vya watoto, nyenzo za uongozi, Makala zinazochapishwa upya na mapitio ya vitabu; vyote hivyo ili kukuwezesha katika siku hizi maalum pamoja na program nyingine utakazotaka kutekeleza kwa mwaka mzima. Utapata pia taarifa za kutumia katika kiambatishi 'A' zitakazokusaidia kutekeleza huduma za familia katika kanisa lako mahalia.

Hiki kitendea kazi pia kimejumuisha mafundisho kwa njia ya PowerPoint kwa ajili ya semina na vitini. Wawezeshaji wa semina wanahimizwa kutengeneza hayo mafundisho kwa namna wanayoona kuwa bora kwa kuongezea visa vyao wenyewe na picha ambazo zitaakisi namna mbalimbali za jumuia walizo nazo. Ili kupakua mafundisho haya unaweza kutembelea tovuti hii: www.**family.adventist.org/2021RB**

Ili kupata mada nyingine zaidi katika masuala ya Maisha ya familia, unaweza kupakua vitendea kazi vya mwaka uliopita kuhusu familia katika tovuti ifuatayo:

www.family.adventist.org/resources/resource-book/

JUMA LA NYUMBA NA NDOA YA KIKRISTO
TAREHE 11- 18 FEBRUARI

Juma la Nyumba na ndoa ya Kikristo linafanyika mwezi wa pili likijumuisha Sabato mbili, yaani 'Siku ya Ndoa ya Kikristo' yenye msisitizo katika ndoa za Kikristo, na siku ya 'Nyumba ya Kikristo' yenye msisitizo katika malezi. Juma la nyumba na ndoa ya Kikristo linaanza Sabato ya pili na kuishia Sabato ya tatu ya mwezi wa pili.

SIKU YA MSISITIZO WA NDOA YA KIKRISTO
SABATO YA TAREHE 11 FEBRUARY

Tumia dhana ya hubiri la ndoa katika huduma ya ibada na semina ya ndoa katika kipengele chochote cha program wakati wa shangwe hii.

SIKU YA NYUMBA YA KIKRISTO (IKISISITIZA MALEZI)
SABATO YA TAREHE 18 FEBRUARY

Tumia dhana ya hubiri la malezi katika huduma ya ibada na semina ya malezi katika kipengele chochote cha program hii wakati mkishangilia.

JUMA LA MAOMBI LA FAMILIA KUWA PAMOJA
TAREHE 3-9 SEPTEMBER

Juma la ukaribu wa familia au kuwa pamoja limepangwa kuwa ni juma la kwanza la mwezi wa tisa, ukianzia Jumapili ya kwanza na kuishia Sabato inayofuata ambayo ni Siku ya maombi ya kuwa pamoja kwa familia. Juma hilo la ukaribu wa familia pamoja na siku yake ya maombi vinakazia sherehe za kanisa kama familia

Kitendea kazi cha ziada chenye sehemu ya kusoma kila siku na shughuli za familia kitatolewa kwa ajili ya Juma la Maombi la Kuwa Pamoja kwa Famila. Kupakua kitendea kazi hiki tafadhali tembelea tovoti hii: www.family.adventist.org

SIKU YA MAOMBI YA FAMILIA KUWA PAMOJA
(KWA AJILI YA NDOA, FAMILIA, NA MAHUSIANO)
SABATO YA TAREHE 9 SEPTEMBER

Tumia dhana ya hubiri la familia katika huduma ya ibada inayopatikana katika kitabu hiki.

MAWAZO
YA MAHUBIRI

Mawazo ya mahubiri yamekusudiwa kuwa hamasa, na mwanzo wa hubiri lako mwenyewe. Omba kwa ajili ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Hebu maneno yako yawe ni mwendelezo wa upendo wa Mungu kwa kila moyo na kwa kila familia.

LISHA MOYO WAKO:
KUPATA AFYA YA KIROHO NA YA KIMHEMUKO KATIKA ULIMWENGU ULIOVUNJIKA

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

AYA ZA MAANDIKO

Yohana 14:1-3; 12, 13, 15, 18

I. UTANGULIZI

Ikitokea kwamba umekaribishwa kula donati, bajia, kachori, mandazi, chapati, mchanganyiko wa mbogamboga na mayai uliokaangwa, uji wa ulezi, emengo, banitsa, changua, michembe, gallo pinto, nyuka gi rabuon, kosai, ikirunguri, shakshuka na kadhalika, utafahamu kwamba umekaribishwa nini? Itategemea unaishi wapi katika dunia hii au unatoka wapi, ndipo utambue ni nini utakachochagua katika dimbwi hilo la vitafunwa, na kufahamu kuwa ni mlo wa kifungua kinywa.

Kulingana na kliniki ya "Mayo" – taasisi maarufu ya tiba iliyokuwa katika nchi ya Marekani – ili kupunguza uwezekano wa matatizo ya moyo, kuna aina moja ya mlo ambao lazima uepuke. Utakubaliana nami kwamba watu wengi sehemu mbali mbali za dunia katika kukua kwao walisikia wazazi wao wakiwaambia kuwa mlo wa kifungua kinywa ndio mlo wa siku ambao ni muhimu sana. Na kwa baadhi yenu wanaopenda historia, dhana hii ya "Kifungua kinywa ndio mlo muhimu wa siku hiyo" ilibuniwa na Waadventista wawili – James Caleb na John Harvey Kellog – karne ya 19, ili kuuza lishe ya nafaka waliyokuwa wamevumbua kwa kusudi la kutumiwa katika kifungua kinywa. Ikiwa una mashaka, unaweza kutafuta katika mtandao.

Daktari Naima Covassin aliyekuwa mtafiti katika maabara ya maumbile ya moyo kwenye kliniki ya Mayo aligundua katika utafiti wake hivi karibuni kwamba watu wanaokula kifungua kinywa mara kwa mara waliongezeka kilo 1.3 kwa mwaka

ukilinganisha na wale ambao hawatumii kifungua kinywa kila siku, wakiongezeka kila 3.6 kwa mwaka. Kulingana na Daktari Covassin, ongezeko la uzito ni mafuta yaliyo hatari, na yana uhusiano wa karibu na shinikizo la damu, kisukari, na magonjwa ya moyo.[1]

Watafiti wanapendekeza kuwahi kuamka na kupata kifungua kinywa chenye lishe kamili ili uanze siku vyema. Chakula cha asubuhi kinachojumuisha nafaka, protini, matunda na mboga mboga, na juisi ya matunda isiyoongezwa sukari ndani yake, ni muhimu katika kuzuia matatizo makubwa ya moyo baadaye katika maisha.[2]

Kwa hiyo – bila maswali – mama alikuwa sahihi.

> Ujumbe wetu leo ni huu: ***Lisha Moyo Wako***: *Kupata Afya ya Akili na ya Kimhemuko katika Ulimwengu Uliovunjika*
>
> Tuombe.

II. AYA ZA MAANDIKO

Yohana 14:1-33, 12, 13, 15, 18

"1 Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. 2 Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. 3 Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo. 12 Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba. 13 Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. 15 Mkinipenda, mtazishika amri zangu. 18 Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu."

III. UFAFANUZI NA MATUMIZI

HIVI KWELI, NI MOYO UNAOSUMBUKA?

Wanaohusika na matatizo ya moyo siyo kina-mama pamoja na wachunguzi wa kitabibu pekee. Yesu pia anahusika. Katika fundisho la leo, Yesu alifahamu kwamba kikundi kidogo cha wafuasi wake kingeshtushwa kwa tangazo lake la kuondoka, pia

---

[1] Roth, I. (April 25, 2018). Mayo clinic minute: Why breakfast may be key to trimming your belly. Newsnetwork.mayoclinic.org/ discussion/mayo-clinic-minute-why-breakfast-may-be-key-to-trimming-your-belly/? Retrieved May 18, 2022.

[2] Keillor, J. (July 2, 2020). *Start your day right.* Connect.mayoclinic.org/blog/take-charge-healthy-aging/newsfeed-post/start-your-day-right/ Retrieved May 18, 2022.

dhana yake ya kuwa kondoo wa kafara hivi karibuni.[3] Kwa hiyo Yesu anawapatia wanafunzi wake – pamoja nasi leo – agizo dhahiri akisema, "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi." (Yohana 14:1). Hata hivyo, anawasilisha ujumbe huu wa matumaini – kwamba yuko pamoja nasi sasa, na kwamba atakuja tena hivi karibuni, kwa hiyo hakuna haja ya kufadhaika na kuwa na wasiwasi.

Ellen G. White anatoa nuru katika kitabu cha *The Desire of Ages*, uk. 663 kuhusu kipindi hiki kilichokuwa kati ya Yesu na wanafunzi wake kwa kusema "Dhana ya kuondoka kwa Yesu ilikuwa kiyume kabisa na kile wanafunzi walichokuwa wakiogopa. Haikumaanisha kutengana mara ya mwisho, bali alikuwa akienda kuandaa makao kwa ajili yao, na kwamba angerudi tena… wakati akiandaa makao kwa ajili yao, walitakiwa kujenga tabia ya namna ya watakaoingia makao hayo ya mbinguni.[4]

Ili kuwa na uhakika kwamba Yesu hakuwa anaeleza kuhusu kiwango cha lehemu, au upsuaji wa kuvusha mishipa, alizungumzia aina tofauti ya matatizo ya moyo – aina inayoweza kuwekwa katika kundi la wasi wasi, hofu, mashaka, msongo au hisia za kutojali. Aina ya matatizo ya moyo inayoweza kuonekana kama kupoteza matumaini, ukosefu wa Imani, mshituko, au kutokuwa na uhakika. Aina ya matatizo ya moyo inayokufanya usipate usingizi ukifikiri kuhusu fedha, ukiuma kucha zako unapokuwa una mashaka kuhusu watoto wako, unapoongea na rafiki yako kwenye simu ukihisi hitaji kubwa la ushauri kwa sababu ya ndoa iliyo mashakani, au ukihangaika kuhusu changamoto ngumu katika mahusiano ya ndoa yako ambazo hazionekani kuisha.

Pengine leo moyo wako umedunda kwa wasi wasi au hofu kuhusu baadhi ya masuala yako ya fedha, au tataizo ya mwenzi wako au Watoto wako. Hii ndiyo aina ya matatizo ya moyo ambayo Yesu anazungumzia. Sisi sote tumeshapitia katika uzoefu wa matatizo kama haya. Ni aina ya mfadhaiko wa moyo, matatizo ya Imani, matatizo ya ukosefu wa amani yanayojirudia rudia katika maisha yetu. Matatizo yanayoonekana kujitokeza kila siku katika maisha yetu; aina ya matatizo ambayo hatuwezi kuyazoea na wakati mwingine hatujali.

Ni dhahiri kwamba matatizo ya moyo – yawe ya kimwili, kimhemuko, au ya kiroho – ni tishio kubwa kwa ustawi wetu kama wafuasi wa Kristo. Tunashukuru kwa ajili ya utafiti wa kisayansi maana sasa tunafahamu kwamba mlo wa asubuhi wenye afya utasaidia mishipa yetu inayopitisha damu. Lakini tunaweza kujiuliza kwamba, inakuwaje kwa undani wa Imani yetu, mashaka yetu, na wasiwasi wetu? Je, kuhusu hofu isiyokoma? Hebu tuwe wakweli – inawezekana – sisi kama wafuasi wa Yesu katika ulimwengu uliovurugikiwa, tukasikiliza maagizo yake na kuwa na moyo usiofadhaika? Inawezekana kweli? Ndiyo, inawezekana. Kwanza Yesu ambaye ni

[3] Borchert, G. L.., Ed. (1996). *The new american commentary*, Vol. 25A John 1-11. Nashville, TN: Broadman and Holman Publishers).

[4] White, E.G. (1940). *The desire of ages*, p. 663. Mountain View, CA: Pacific Press Publishing Association.

Mwana wa Mungu, Yesu masihi; Yesu Bwana wako na Bwana wangu; Yesu aliye mwokozi wako na wa kwangu, ndiye anayesema kuwa, "Msifadhaike mioyoni mwenu…" (fungu la kwanza).

JE, NI NINI UNACHOLISHA MOYO WAKO?

Kulingana na Neno la Mungu – yaani kulingana na Yesu mwenyewe – kuwa na moyo usiofadhaika wenye Imani kunatokana na kile unacholisha moyo wako. Kama vile tu ugali unavyoleta tofauti katika mwili, kile unachoulisha au unachounyima moyo wako kinaleta tofauti kubwa kiroho na kimhemuko.

Waulize wataalam, nao watakuambia kwamba kuna funguo tatu za ustawi wa kimwili: mlo wenye afya, mazoezi ya kila mara, na pumziko la kutosha. Ukipuuza mojawapo ya haya mambo matatu, utakuwa unatafuta matatizo. Ndivyo ilivyo hata kwa moyo wa Imani na ustawi wa kimhemuko. Ni lazima vilishwe vizuri na kutunzwa vizuri ili kuwa imara na kuwa na afya kiroho na kimhemuko. Tukiangalia Neno la Yesu kwa upande mwingine, tunamsikia akisema kuwa, "Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi." (Fungu la kwanza). Yesu anatuambia kwamba ufunguo wa afya ya moyo – ambyo ni pamoja na afya ya kimhemuko – ni kumwamini na kujilisha kwa yeye. Kile ambacho mioyo yetu inahitaji ili kubakia na afya na kuwa imara ni kulishwa mara kwa mara kutoka kwa Kristo na maisha hai ya kumfuata yeye. Kama vile tu misuli ya miili yetu, kadiri tunavyoendelea kufanyia mazoezi Imani yetu, ndivyo inavyozidi kuwa imara. Kadiri unavyopata uzoefu wa kuwa na Mungu, ndivyo unavyojiamini kwamba utakuwa kile anachosema utakuwa; na kwamba atatimiza ahadi alizotoa!

Isaya anatukumbusha katika sura ya 41:10 kuwa, "Usiogope, kwa maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu."

Yoshua analeta tumaini katika moyo wenye hofu kwa kusema, "… usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe kila uendako." (Yoshua 1:9)

Ellen G. White anatushirikisha maneno katika kitabu chake cha *Mind, Character and Personality,* vol. 1 uk. 68 kuwa, "Mtazame msaidizi wako, Yesu Kristo. Mualike na kukaribisha uwepo wa neema yake. Mawazo yako yanaweza kuhuishwa siku kwa siku, na ni fursa yako kukubali neema na pumziko, inuka uache wasiwai, msifu Mungu kwa mibaraka yako.[5]

[5] White, E.G. (1977). *Mind, character, and personality,* vol. 1, p. 68. Nashville, TN: Southern Publishing Association.

Mtunga Zaburi anaelekeza katika sababu ya tumaini letu katika Zaburi 27:1 kuwa, "Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, Nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, Nimhofu nani?"

Ukiangalia kwa haraka, utaona kama majibu haya yanafanana, yananukia kwa namna iliyo sawa, unaweza kuyahisi kwa namna iliyo sawa, yanaonekana kwa urahisi kama vile tuko katika Shule ya Sabato. Naam, ni kweli! Wafuasi wengi wa Yesu wana moyo uliofadhaika ukichomoza kutoka katika dhana kwamba maisha yao hayana uhusiano na kumtumia Yesu – yaani kujilisha kwa Neno lake – hakuna zoezi lolote la Imani ndani yake na hakuna pumziko la kweli ndani yake. Matokeo yake ni kwamba hawawezai kustahimili wasiwasi wa maisha unaojitokeza kila uchao. Wakiwa na njaa ya maelekezo kutoka kwa Kristo katika Neno lake, wakiwa na kiu ya amani ya kudumu inayoweza kupatikana tu katika kusimama kwenye ahadi zake, tunaishia katika kutafuta virutubisho maeneo yasiyo sahihi.

Mara nyingi tunakwepa mlo wa kiroho na kugeukia kwenye ufumbuzi wa kidunia. Hatimaye tunajilisha mambo ya kidunia tukidhani kwamba yatatuletea mambo ya kiroho. Kwa mfano unaweza kujilisha habari zilizo katika mitandao, ukidhani kwamba ukizungumzia vizuri mrengo wa siasa unaoupenda utapata hekima idumuyo katika dunia hii inayobomoka. Unaweza kujiunga na sehemu ya mazoezi katika ujirani na kuanza kujisifia kuhusu maumbile yako yatokanayo na mazoezi, ukiamini namna potovu kwamba kumudu mwili wako kutakupatia uwezo wa kutawala nafsi yako iliyokumbwa na hofu na vitisho.

Wakati huo huo, mioyo yetu ya Imani ambayo haijalishwa ikiwa inapitia katika kipindi kirefu cha uzembe na kutojali. Mioyo yetu ya Imani yenye matatizo, ambayo hapo awali ilikuwa imepimwa kwa mazungumzo magumu na marafiki wasioamini huko chuo kikuu tukiwa kazini. Mioyo iliyofanyishwa mazoezi kwa maombi nyakati za msongo na magumu, sasa inakaa juu ya kochi na kulishwa takataka kwa mitandao ya kijamii. Ndiyo maana tunajihisi wadhaifu, tusiokuwa na ulinzi, na tusio salama kadiri tunavyokabiliana na mashaka, wasiwasi na ukosefu wa uhakika wa maisha.

Ellen G. White anatoa ushauri katika kitabu cha *An Appeal to the Youth*, uk. 79 kwamba, "Kadiri unavyofanya Maandiko kuwa mafunzo yako, na kupata uzoefu wake, utajengeka na kuwa imara dhidi ya majaribu ya Shetani."[6]

Hata hivyo, ikiwa tutatembea katika Neno la Mungu, tutakutana na Zaburi 46:1, 2 panaposema kuwa, "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, Ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari."

[6] White, E. G. (1864). *An appeal to the youth*, p. 79. Battle Creek, MI: Seventh-day Adventist Publishing Association.

Na Yakobo anasema kuwa, "Lakini hekima itokayo juu, kwanza ni safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki." (Yakobo 3:17)

Ni wazi kuwa, hatusemi ugonjwa wa akili siyo halisi, au kwamba hali yako haiwezi kuhitaji msaada wa kitaalam. Mungu alitupatia zawadi kama vile ushauri (au msaada) kwa mwili wa Kristo – kama mtume Paulo anavyowaandikia Wakorintho katika sura ya 12 – kwa kulijenga kanisa. kwa hiyo ikiwa itatokea uchunguzi ukaonesha kwamba una wasiwasi, usiogope kutafuta ushauri wa mtaalam bingwa kama ushauri huo unaweza kupatikana katika maeneo yako. Hata hivyo, tunatambua kwamba sehemu kubwa ya wasiwasi wetu wa kila siku, hofu yetu,mashaka yetu, na msongo wetu unajidhihirisha kwa kumezembea kujilisha lishe kamili kutoka katika Neno la Mungu. Hatujabinafsisha upendo wake, furaha yake, amani yake, ustahimilivu wake, wema wake, uaminifu wake, upole wake wala kujitawala kwake. (Wagalatia 5:22, 23). Na pia tumesahau kwamba Mungu anatupenda kwa upendo wa milele. (Yeremia 31:3).

Ikiwa tayari unafahamu kwamba una matatizo ya moyo, wataalam watakushauri hatua lukuki zinazoonekana rahisi, zinazoweza kuanzisha mtindo wa maisha wenye ustawi. Achana na uovu mwingine wa aina yoyote ile, tawala kiasi cha lehemu mwilini mwako, simamia lishe yako, fanya mazoezi angalau dakika 30 kila siku, epuka msongo kadiri iwezekanavyo, jali hali ya usafi, linda uzito wako ubakie na afya, hakikisha unapata vitamini muhimu, pata chanjo zako kwa wakati na kila kitu kinachohitajika ili kudumisha afya bora siku hizi.

Lakini inapohusu mioyo yetu ya Imani, kwa sehemu fulani mambo matatu yanaguswa. Mioyo yetu inayofadhaika ikihitaji kulishwa na Yesu, ikiwezeshwa katika maisha kumfuata yeye, na kupokea mibaraka ya pumziko la Sabato kwa uzito wote. Hii itatusaidia kupokea pumziko la kiroho, kimwili, na kimhemuko ambalo Mungu amekusudia tupate kila juma. Kumbuka maneno ya Yesu mwenyewe baada ya kuagiza kuwa tusifadhaike mioyoni mwetu. Alitumia maneno *"Mimi"* mara tano katika aya mbili tu. Ni namna ya kutusihi kuweka nanga ya mioyo yetu katika tumaini analotupatia na ahadi kwamba atarudi hivi karibuni kutuchukua tukaishi naye milele, kwenye makao yafuraha yasiyokuwa na msongo wala mafadhaiko.

KWA HIYO BASI, LISHE YA YESU IKOJE?

Je, tunalishaje mioyo yetu kwa uwezo wa Yesu? Uwezo huo unakuja kuunganika na ahadi za Neno lake katika Biblia, na uwezo wa uwepo wake, unaopatikana ndani ya watu wake. Kama vile tu mtu anayejenga afya ya moyo wake wa kimwili kwa kufanya mazoezi ya kukimbia, anavyojiandikisha katika matangazo kwenye utambuzi na kujiunga katika klabu ya riadha ili kuwajibika – kama wengi wa rafiki zetu na ndugu wa karibu wanavyofanya – Neno la Mungu na watu wake ni muihimu kwa ajili ya

uimara wa moyo wa Imani utakaotubariki kiroho na kutuimarisha kimhemuko, hasa kwenye mahusiano yetu ya karibu sana na wenzi wetu, Watoto wetu, na wana familia wengine.

Yesu anatoa ahadi katika fungu la 18 anaposema kuwa, "Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu." Mara nyingi mioyo yetu inapofadhaika hata tukahisi kuwa mbali na Yesu, huwa ni kwa sababu tuko mbali kutoka katika maeneo matatu – Neno lake, Watu wake, na Siku yake ya kupumzika – mahali alipoahidi kupatikana kila siku. Zaidi ya hapo, tunaishi katika dunia ambayo upatikanaji wa Neno la Mungu haujawa rahisi. Mfano mmoja ni huu: ukijisajili katika tovuti hii: www.RevivalAndReformation.org ya idara ya Chama cha Huduma za Kichungaji ya Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato kwa ajili ya kupata "Amini Manabii Wake, au Muunganiko katika Maombi, au hata Kesha la Asubuhi Kila Siku na Mwongozo wa Kujifunza Biblia, utaendelea kujiunganisha na Mungu pamoja na kanisa lake na Mapenzi yake katika maisha yako.

Pale moyo wako wa Imani unapokuwa umelishwa na Yesu, kigezo muhimu ni kuhakikisha kwamba umefanyishwa mazoezi na kupimwa katika mtindo wa maisha au mwenendo unapomfuata Yesu. Mara tu baada ya kuwaambia wanafunzi wake kujilisha kwake, Yesu kwa ujasiri alitangaza kwamba wangeishi maisha ya Imani waliyoipata na kwamba wangefanya mambo ya ajabu kuliko aliyofanya yeye! "Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya; naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba" (Yohana 14:12). Wanafunzi wake walihitaji mioyo iliyolishwa kwa Yesu, kwa sababu wangeingizwa katika maisha ya kufanya kazi zisizo za kawaida, kazi za kutisha, wakati mwingine zinazovunja moyo, kwa jina la Yesu. Huu ndiyo mtindo wa maisha unaopaswa kuukumbatia ili uweze kulisha moyo wako na kupata afya ya kiroho na ya kimhemuko katika ulimwengu huu uliovunjika.

Je, inawezekana Imani yako ni dhaifu kwa sababu hautaki kuondoka hapo ulipo? Je, inawezekana sababu inayofanya ushindwe kuwa tayari kukabiliana na mashaka ya maisha – pamoja na changamoto za ndoa yako au familia yako – ni kwa kuwa umeweka jitihada katika kuyakwepa? Je, inawezekana kwamba namna pekee ya kuimarisha moyo wako wa Imani ili uweze kupata uzoefu wa afya ya kiroho na ya kimhemuko ni kugeukia kwenye fursa zitakazoupima? Hata hivyo, Yesu aliwaambia wanafunzi wake – ujumbe unaotuhusu sisi leo pia – "Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana." (Yohana 14:13). Ikiwa itatubidi kupata afya ya kiroho na ya kimhemuko katika ulimwengu uliovunjika, tutahitaji kuisikia sauti ya Yesu na kumwomba jambo lolote tunalohitaji ili kupata hiyo afya iliyo muhimu sana kwetu.

Jambo la mwisho, Yesu anatupatia maagizo kwa ajili ya afya ya moyo akisema kuwa: "Mkinipenda, mtazishika amri zangu." (Yohana 14:15). Moyo wako wa kimwili

hautakuwa na afya, na kudumu kuwa hai au kuneemeka, ikiwa utakula kila kitu unachotaka, wakati wowote unaotaka, kwa kiasi chochote unachotaka; ndivyo ilivyo hata katika moyo wako wa kiroho na kimhemuko unavyodumu kuwa hai kwa kumtii Yeye ambaye ni mwenye upendo, anayefanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema. Ni dhahiri kwamba tayari tunafahamu kwamba anatupenda. Lakini ikiwa tunampenda, tutaonesha upendo huo kwa kutii. Na utii kwa mapenzi ya Mungu maana yake ni afya ya moyo. Aina ya afya ya moyo itakayoweza kuondoa wasiwasi na hofu. Mwenye hekima anasema katika Mithali 19:23 kuwa, "Kumcha Bwana huelekea uhai; Atakaa ameshiba; hatajiliwa na ubaya."

IV. HITIMISHO

UHALISIA KATIKA NDOA LEO HII.

Ukweli ni kwamba, mara nyingi, waume na wake siku hizi wamechoka; na hali hiyo ya kuchoka inaletwa mpaka kwenye mahusiano kila siku. Bila shaka, maisha katika karne ya 21 yameghubikwa na mambo yanayochukua muda, na maudhi yanayoleta msongo. Katikati ya kazi, shule, kanisa. na majukumu ya kijamii, msongo unaongezeka, na unatishia hata kuwa kitovu cha magonjwa ya wakati wetu. Msongo huo unapokuwa umezidi, unaathiri afya yetu ya kimwili, kiroho, na kimhemuko. Aina hii ya mazingira majumbani mwetu inasababisha uhalisia wa ndoa na familia zenye msongo. Mkao huo unajazwa na mabishano, kutokukubaliana, mapambano, mvutano na magomvi.

Ni katikati ya hali ya hewa kama hii, ndipo Yesu anaposema kuwa, "Msifadhaike mioyoni mwenu," (Fungu la kwanza).

Mpango wa Shetani ni kudhoofisha uwezo wetu wa kiroho, kimwili na kimhemuko kwa kutufanya tushikike kwa shughuli za kila siku kuliko tunavyotakiwa – ili kila wakati tuwe tunakimbia bila sababu kutoka kwenye shughuli hii kwenda kwenye shughuli zingine – na hivyo kutubakiza tukizunguka hapa na pale bila kazi maalum. Ikiwa tutalisha mioyo yetu ya kiroho kwa makapi yasiyokuwa na virutubisho vya lishe kuweza kuipatia mioyo yetu afya na uimara, kila changamoto inayoonekana kama mwinuko katika ndoa itageuka kuwa mlima wa kukata tamaa na uharibifu ambao utazidi na hatimaye kushinda uwezo wa mahusiano yetu.

Hivyo kusikiliza ujumbe wa Yesu kunamaanisha kulisha mioyo yetu kwa virutubisho vinavyopatikana katika Neno lake vinavyotegemeza, vinavyotia uhai, na kuleta ustahimilivu. Mioyo yetu ikijazwa na ujumbe huu uletao nguvu, itakuwa imara na yenye nguvu kiroho, na kimhemuko kiasi kwamba tutajikuta kwa wakati muafka tunatamka maneno "Samahani, naomba unisamehe," au "Ninakupenda." Huo utakuwa ni ushuhuda stahiki kwamba sisi ni wanafunzi wa Yesu, na kwamba tunailisha mioyo

yetu kwa Neno lake la uzima. Ni kweli kwamba kuwa mwanafunzi wa Yesu ni zaidi ya kudai kuwa Mkristo, ni kudhihirisha tabia yake ya kubariki familia, jumuia zetu na makanisa yetu.

KIELELEZO

Jim Cymbala ambaye ni mchungaji mkongwe wa Broklyn Tabernacle Church kule Brooklyn, New York anashirikisha moja ya vitabu vyake vingi:

> "Katika kukua kwangu, nilidhani Mkristo haswa lazima awe ni mtu anayetembea mabega yakielekezwa nyuma kwa sababu ya nguvu isiyo ya kawaida iliyopo ndani yake, akinukuu Maandiko na kuwafanya wote waliopo watambue kwamba amefika. Lakini nimejifunza kwamba muumini aliyekomaa ni yule aliyekunjwa, akiegemea kwa Bwana kwa uzito wote, na kukiri kutokuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote bila Kristo. Mkristo haswa siye yule aliyefanikiwa sana, bali ni yule ambaye amepokea vingi. Neema ya Mungu, upendo na rehema vinabubujika kupitia kwake kwa wingi kwa sababu anatembea katika utegemezi mkamilifu.[7]

Kwa hiyo, kadiri unavyojaribu kupata nafasi na shughuli hapo nyumbani wewe na mwenzi wako au familia, chuma tunda la Roho – kwa ajili ya afya ya moyo – kila siku (Wagalatia 5:22, 23). Hivi virutubisho vya lishe vinavyoletwa kutoka mbinguni, yaani upendo, furaha amani, uvumilivu, utu wema, Fadhili, uaminifu, upole, na kiasi, vitakulinda kiroho, na kimhemuko. Hii itahakikisha kwamba, "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi." (Yohana 13:35)

Mpendwa, moyo wako hauhitaji kufadhaika kwa sababu ya wimbo huu kumhusu Yesu:

Na tumwabudu huyo Mfalme, Sifa za nguvu zake zivume
Ni ngao ni ngome yeye milele, Ndizo sifa zake kale na kale.

Tazameni ulimwengu huu, Ulivyoumbwa ajabu kuu
Sasa umeweka mahali pake, Hata utimize majira yake

Kwa ulinzi wako kwetu Bwana, Twakushukuru u mwema sana
Hupewa chakula kila kiumbe, Kila kitu kina mahali pake.

Wanadamu tu wanyonge sana, Twakushukuru wewe Bwana
Kamwe haupungui wako wema, Mkombozi wetu rafiki mwema.

---

[7] Cymbala, J. (1993). *Fresh faith*, p. 45. Grand Rapids, MI: Zondervan Publishing House.

Ni Yesu huyo anayesema kuwa, “Msifadhaike mioyoni mwenu…” Na ndiye Yesu huyo huyo aliyegeuza maji yakawa divai katika harusi ya Kana ya Galilaya (Yohana 2). Ni Yesu huyo huyo aliyemfufua Lazaro kutoka kwa wafu (Yohana 11). Ndiye huyo huyo aliyeponya upofu wa Batiamyo (Marko 10). Yesu huyo huyo ndiye aliyemponya mwanamke aliyekuwa akitokwa damu miaka kumi na mbili, na kumfufua binti wa Yairo kutoka katika wafu (Marko 5). Ni yeye huyo aliyemponya yule mtu aliyekuwa amepooza kule Kapernaum, aliyeshushwa katika dari na rafiki zake wanne (Marko 2). Ni Yesu ndiye aliyewaponya wakoma kumi kutoka katika ugonjwa uliokuwa ukitisha (Luka 17). Halafu ni yeye huyo ndiye aliyelisha watu 5,000, wanaume, wanawake na watoto kwa mikate mitano na visamaki viwili (Marko 14). Ndiye Yeu huyo huyo aliyetembea juu ya maji (Mathayo 14). Na ni yeye huyo ndiye anayetuagiza kuwa, “Msifadhaike mioyoni mwenu.” (Fungu la kwanza Yohana 14)

Kadiri tunavyoendelea kuchakata kile tunachotakiwa kufanya na ujumbe ambao tumeusikia, hebu Mungu na atusaidie kujilisha katika aina hii ya lishe mara kwa mara. Kufanya hivi kutatusaidia kufurahia afya ya kiroho na ya kimhemuko katika ulimwengu huu uliovunjika, kwani Yesu ndiye kifungua kinywa pekee kinachoshibisha.

VISA VYA
FAMILIA MBILI

NA JOHN NIXON, SR.

AYA ZA MAANDIKO

Mathayo 24:37-39; Luka 17:28

I. UTANGULIZI

Hiki ni kisa cha familia mbili - kufanana na kutofautiana kwao. Familia zote mbili zinakabiliana na zahama kutoka katika ulimwengu wa nje kiasi cha kuwekwa katika majaribu makubwa. Hali ya kisekula ya nyakati zao ilipima ukiroho wa nyumba zao. Familia zote ziliepuka uovu. Familia zote zilimfahamu Mungu wa kweli na kumwabudu yeye. Lakini mwishowe walitofautaina. Somo tunalojifunza kutoka katika kisa hiki liko kwenye tofauti kati ya hizi familia, kwa nini familia moja ilipona kwa ujumla wake na familia nyingine ilisambaratika. Luti ni mwanamume aliyepoteza familia yake: Nuhu ni mwanamume aliyeokoa familia yake.

MKAO WA ULINGANIFU

Dunia mbili hizi; ile ya kabla ya gharika, na ile ya miji ya Sodoma na Gomora zinatoa changamoto za juu kabisa kwa waumini wa wakati wao. Katika maeneo mbali mbali katika Agano Jipya, ulimwengu wa kabla ya gharika na miji ile ya Sodoma na Gomora kila mmoja unatoa ishara za eskatolojia ya uasi wa mwisho dhidi ya Mungu na matokeo yake. Unabii wa Yesu katika Mathayo 24 unaelekeza katika nyakati za Nuhu kama mfano wa hali ya dunia kabla tu ya kurudi kwake.

> "Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile aliyoingia Nuhu katika safina, wasitambue, hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." – Mathayo 24:37-39

Yuda naye anaonesha muunganiko wa nyakati za mwisho na miji ya Sodoma na Gomora akizema kuwa, "Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyokuwa kando-kando, waliofuata uasherati kwa jinsi moja na hawa, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele." – Yuda 1:7

Kile kinachoteka usikivu kuhusu matukio yote haya mawili katika Agano la Kale, ni visa vya nyakati hizo vikielezwa kupitia katika uzoefu wa familia. Tunaona visa hivyo kutoka ndani. Familia mbili hizi zilipokea neema ya Mungu katikati ya uangamivu wa hukumu ya kimbingu (Mwanzo 6:8 na 19:16). Lakini ni familia moja tu ndiyo iliyovuka zahama bila kujeruhika. Asili ya familia zinazostahimili kiroho inadhihirishwa katika visa vyao

I. SIKU ZA NUHU

> "Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua. Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini." – Mwanzo 6:1-3

Anguko la ubinadamu lilianza pale tofauti kati ya haki na ukosefu wa haki ilipopuuzwa. Wana wa Mungu walijichagulia wake kwa mtazamo wa nje badala ya ule wa ndani – uzuri wa umbile la nje badala ya tabia – "nao wakajitwalia wake wowote waliowachagua."

Wazao wa Sethi wakaoana na wazao wa Kaini na kusababisha kuondoka kwa ule utengano uliokuwapo kati yao. Huko kupotea kwa utengano kukasababisha kuondoka kwa tofauti kati yao. Ni kanuni ya maisha kwamba "Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema." (1 Wakorintho 15:33). Katika ule ulimwengu kabla ya gharika, haki na ukosefu wa haki vilikuwa vimechanganyika hadi haki ikamezwa na ukosefu wa haki, hivyo elimu ya Mungu ikaanza kupotea duniani.

Nuhu alikuwa mhenga wa kizazi cha kwanza akizaliwa takribani miaka 120 baada ya kifo cha Adam. Kwa miaka 900 hivi, huyu mtu wa kwanza duniani alilea wajukuu wake katika magoti akiwaeleza kisa cha Paradiso iliyopotea – uzuri wa bustani ambayo wakati huo ilikuwa ikilindwa na Malaika kwa upanga ung'aao – mti wa uzima ambao walikuwa wamezuiliwa, pia kutembea katika bustani na kuzungumza na Mungu uso kwa uso, joka na mti wa ujuzi wa mema na mabaya uliozuiliwa, na zile hatua mbali kutoka katika uadilifu zilizowaongoza katika laana ya dhambi.

Ilikuwa vigumu kukataa uwepo wa Mungu wakati Adam akiwa duniani. Aliweza kueleza kwa ushawishi wa kweli kile ambacho amekiona kwa macho yake. Aliweza

kuonesha makovu ya mwili wake kutoka katika upasuaji uliofanywa ili Hawa apatikane. Lakini kwa kifo chake, kile kipingamizi cha mwisho dhidi ya unyonge kilipotea, na dhambi ikajitokeza wazi wazi na kwa vurugu. Dunia ikajaa ufisadi mkubwa uliosababisha hali iliyoharibika kwa namna isiyoweza kuelezeka, na hivyo wanadamu wakawa wameanguka wakimsababishia Mungu huzuni ya moyo.

> "Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote. Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo." – Mwanzo 6:5, 6

Huu ulikuwa ndio wakati ambapo Wanefili, waliokuwa watu wenye umbo kubwa na wenye nguvu, wanadaiwa kuwa, "… watu hodari zamani ,watu wenye sifa." (Mwanzo 6:4). Wazao wao walikuwa majitu waliowatisha wapelelezi wa Musa waliotumwa kwenda kupeleleza nchi ya Kanaani (Hesabu 13:33). Lakini jina Wanefili kwa lugha ya Kiebrania lina maana ya "walioanguka" likionesha kwamba ingawaje walionekana maarufu mbele ya wanadamu, kwa kipimo cha Mungu walikuwa ni wenye dhambi. Ufafanuzi kutoka katika Patriarchs and Prophets unaelezea kuwa, "hatia yao katika kujiachia kwenye uovu ilikuwa inawiana na ustadi wao na uwezo wao wa kiakili." Uovu wao ulifanyika wazi na kwa kuthubutu." (Partriarchs and Prophets, uk. 90, 91)

> "Wanadamu walimwondoa Mungu kutoka katika elimu yao, na kuabudu viumbe walivyoona bora machoni pao; matokeo yake waliendelea kuwa duni kimaadili." (PP, uk 91)

Hii ilikuwa ni dunia ambayo Nuhu alikuzia familia yake. Hakuchagua hali ya jamii, na hakuweza kutawala ulimwengu uliokuwa nje ya milango yake. Lakini alikuwa na uwezo wa kutawala maisha yake mwenyewe na nyumba yake, na alifanya hivyo kwa uadilifu na uaminifu mkubwa kwa Mungu.

II. SIKU ZA LUTU

> "Na kadhalika, kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, walikuwa wakila na kunywa, walikuwa wakinunua na kuuza, wakipanda na kujenga." – Luka 17:28

Pamoja na kwamba Biblia inaelekeza katika vurugu kama ishara ya nje ya ufisadi wa nyakati za Nuhu, bado Sodoma na Gomora ilifahamika kwa ukware, na zaidi ya hapo, wakifuata mambo ya mwili yasiyo ya asili. (Yuda 1:7). Lakini wakati vitendo vichafu hivyo vikiendelea, maisha ndani ya miji ya Sodoma na Gomora yaliendelea siku kwa siku kana kwamba hakuna kitu kipya kinachotendeka. Kwa kweli ilikuwa imegeuka kawaida, na huu ndio ulikuwa uangamivu wa Sodoma na Gomora

Watu wa Sodoma na Gomora walipojaribu kuvunja mlango wa nyumba ya Lutu ili kuwajua wageni wawili waliokuwa nyumbani mwake, hawa walikuwa "…vijana kwa wazee, watu wote waliotoka pande zote." (Mwanzo 19:4). Pale dhambi inapokuwa imeenea bila kizuizi, huwa ishara kwamba Roho wa Mungu amekataliwa na kwa hiyo anakuwa ameondoka kabisa, kinachobakia ni hukumu ya kimbingu.

Kwa hiyo tunaona hapa mrandano. Hawa wawili, Nuhu na Lutu walikuza familia zao katika hali ambayo ilikuwa ni hatari kwa maisha ya familia ya kiungu, lakini walitoka katika hali hizo kwa namna tofauti.

HALI YA KUPENDA MALI AU HALI YA UKIROHO

> "Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya Bwana, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari. Basi Lutu akajichagulia Bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatengana wao kwa wao." – Mwanzo 13:10, 11

Lutu alipoamua kuchagua mahali pa kukuzia familia yake, alijenga uamuzi wake katika matazamio ya kuongeza mali yake, siyo kwa kutambua jinsi ambavyo kaya yake ingeathirika. Hakushauriana na Bwana. Lutu aliweka familia yake mahali palipokuwa na uwezekano mkubwa wa uovu. Alifanya maamuzi akiangalia uwezekano wa kupatikana kwa mali, na kwa kufanya hivyo alifanya familia yake kujifunza kuthamini mali kuliko vitu vingine. Thamani hizi ziligeuka kuwa kitovu cha majanga yaliyoipata familia pale mIji ya Sodoma na Gomora ilipoangamizwa.

Wakati Lutu anahamisha familia kwenda sodoma, tayari alikuwa Tajiri (Mwanzo 13:5). Hakuhitaji kitu. Na kwa sababu ya kupenda mali, alipoteza vyote, yaani familia na mali yake. Alienda Sodoma akiwa Tajiri; alitoka mikono mitupu." (*Counsels on Health*, 270). Upotevu wa kwanza ulikuwa ni mbaya zaidi. Lutu aliangukia katika maisha ya anasa na hiyo anasa ikasababisha uharibifu wa Imani yake.

> "Lutu alipoingia Sodoma, alikuwa amedhamiria kujitenga kabisa na uovu, na kusimamia nyuma yake vyema. Lakini alishindwa kabisa. Mivuto yenye uharibifu iliyomzunguka ilikuwa na athari kwa Imani yake mwenyewe, na muunganiko wa watoto wake na wakazi wa Sodoma ulifanya shauku yake ifanane na ya kwao." (*Adventist Home,* uk. 138)

Ili familia istawi kiroho, ni lazima maamuzi yajengwe kwenye tunu za kiroho. Kama ilivyokuwa siku za Lutu, ndivyo ilivyo hata leo. Mivuto ya mali imetuzunguka kote kote. Ahadi ya kupata mali, na furaha inayotokana na kupata hiyo mali ni kigezo

muhimu cha ubepari. Hata hivyo, mfumo unasukumwa na maslahi binafsi, umiliki binafsi unaochochewa na faida, na kumiliki mali kama hatima yake.

Mpaka kufikia mwaka 2021, kulikuwa na wamilionea zaidi ya milioni moja katika nchi ya Marekani, labda zaidi ya hapo. Kulingana na taarifa moja, wamilionea milioni moja walijitokeza mwaka huo wa 2021 pekee katika nchi hiyo ya Marekani. Sasa hivi kuna wamilionea milioni 14.6 katika Marekani peke yake, na mwaka uliojitokeza pekee kwa kutengeneza wamilionea.[8]

Kukiwa na mali nyingi kati yetu, na ule uwezo wa kuipata hiyo mali ukifunguka kwa watu wengi, inakuwa rahisi sana kwetu kuanguka katika mtazamo wa "kuishi kama dunia hii." Lakini pia, tunapoweka mali kuwa kitovu cha mfumo wa tunu zetu, tunahatarisha afya zetu za kiroho na afya za familia zetu. Kwa uzoefu wa Lutu na familia yake, "matokeo yako wazi mbele yetu." (*Adventist Home*, 138).

Kinyume chake, Nuhu alijenga maisha yake na shauku ya familia yake katika utume aliokuwa amepewa na Mungu. Maisha yake yote yalisukumwa na shauku hiyo. Ule mradi wa Safina ulidai matumizi ya vipaji vyote na talanta zake – werevu wa usanifu wa kuweza kuweka katika uhalisia maagizo ya Mungu ya ujenzi, kujengeka kwa mwili kulikomwezesha kuandaa na kukusanya vifaa vya kujengea, stadi za uongozi hata kupanga wafanyakazi ili kuhakikisha uwezo wao wote na talanta zao vinatumika vizuri kwa upeo mkubwa wa fikira na mwili kuwezesha utendaji wa siku kwa siku hadi utume ukamilike.

Hata aliwekeza mali yake binafsi. Nuhu alimimina fedha zake zote katika ujenzi wa Safina hadi zikaisha. Hakuwa na wasiwasi wa kutenganishwa na kitu chochote pale alipoongoza familia yake kuingia katika Safina kwa sababu hakuwa amebakiza kitu nyuma yake. Mradi huo ulimtaka Nuhu kuwa na Imani kubwa. Alijenga Safina katika ardhi kavu, katika dunia ambayo haikuwahi kuona mvua. Wanasayansi walipingana naye na kumdharau. Wenye akili walimdhalilisha. Wakorofi na wasio na adabu walimbeza. Lakini Nuhu aliendelea kujenga.

Maisha yote ya Nuhu yalisukumwa na tabia ya Imani yake. Mwisho wake ilibidi awape mgongo kabisa watu wa kizazi cha wakati wake kadiri walivyoendelea kumgeuzia Mungu migongo. Kulikuwa na uchaguzi wa wazi kabisa kati ya viwango vya dunia aliyokuwa akiishi, na viwango vya ufalme ambao alikuwa ameambatana nao. Na matokeo yake yako wazi mbele yetu.

[8] Robert Frank, "A million new millionaires were created in the U.S. last year, and the richest got richer, report says", CNBC, March 17, 2022 https://www.cnbc.com/2022/03/17/million-new-millionaires-were-created-in-us-last-year-report-says.html

UAMUZI AU KUTETEREKA

Moja ya ishara za kile kilichotokea katika Imani ya Lutu alipokuwa akiishi Sodoma ilikuwa ni namna alivyoitikia ujumbe kwamba ule mji ulikuwa unaenda kuangamizwa. Kama hakuwa na uhakika kwamba wageni wake walikuwa Malaika pale alipowakaribisha tu, basi kile kitendo kilichofanyika katika mlango wake kilimfanya aelewe dhahiri.

> "Kisha wakawapiga hao watu walioko mlangoni kwa upofu, wadogo kwa wakubwa, hata wakachoka kwa kuutafuta mlango." – Mwanzo 19:11

Onyo la Malaika lilikuwa na msisitizo, kwa namna vitendo vyao vilivyokuwa katika kutetea familia yake dhidi ya kundi la watu waliokuwa wamepinda. Siyo tu kwamba walikuwa wametoa wito wa wokovu kwa Lutu, bali pia walimpatia amri waliyokuwa wameagizwa kumpatia.

> "Basi wale watu wakamwambia Lutu, Je! Unaye mtu hapa zaidi? Mkwe, wanao, na binti zako, na wo wote ulio nao katika mji, uwatoe katika mahali hapa; maana tutapaharibu sisi mahali hapa, kwa kuwa kilio chake kimezidi mbele za Bwana; naye Bwana ametupeleka tupaharibu." – Mwanzo 19:12, 13

Ujumbe ulikuwa dhahiri, na onyo lilikuwa la haraka. Hapakuwa na nafasi ya kuwa na mashaka kuhusu umuhimu au uharaka wa agizo, hata hivyo Lutu alifanya jambo lisilo la kawaida. Alisita.

> "Hata alfajiri ndipo malaika wakamhimiza Lutu, wakisema, Ondoka, mtwae mkeo na binti zako wawili waliopo hapa, usipotee katika maovu ya mji huu. Akakawia-kawia; nao wale watu wakamshika mkono, na mkono wa mkewe, na mkono wa binti zake wawili, kwa jinsi Bwana alivyomhurumia, wakamtoa wakamweka nje ya mji." – Mwanzo 19:15, 16

NEEMA YA MUNGU KWA LUTU

Kwa namna fulani, "Nuhu akapata neema machoni pa Bwana." (Mwanzo 6:8). Lutu alipata rehema katika ustahimilivu wa Bwana. Hapa kile kinachovutia katika kisa cha Sodoma na Gomora, Lutu alikuwa ni muumini wa kawaida tu kama wewe na mimi. Hakuwa jitu la Imani kama Abraham, au mkuu kama Musa. Hakuitwa mkamilifu katika kizazi chake kama Ayubu alivyokuwa. Lutu alichagua kuishi Sodoma, na alichagua Sodoma kwa sababu potovu. Kwanza alikuwa viungani mwa mji, kisha akasogelea ndani ya mji. Alibakia pale pamoja na hali yake kwa sababu tu alikuwa anaisha vizuri.

Lutu hakushiriki dhambi za Sodoma. Watu wa Sodoma walimchukia kwa sababu alihubiri dhidi ya dhambi; wala hakuwa mmoja wao. Lakini hata hivyo, pamoja na kwamba hakuwa mtumishi mkamilifu, bado Mungu alikusudia kumwokoa pamoja na yote hayo.

Wale Malaika wa kuharibu walidumu katika utume wao wa kuipeleka familia ya Lutu penye usalama. Mungu alikuwa amekusudia kuwaokoa kama alivyokuwa amekusudia kuwaangamiza waovu, na zaidi ya hapo alielekeza uwezo wake katika kuharibu kwa kipimo hicho hicho alichojielekeza kuokoa.

Malaika walikuwa wameagizwa kwamba wasije wakafanya chochote hadi Lutu na familia yake watakapofika mahali pa usalama (fungu la 22). Lakini hata hivyo, wakati wakiongozwa kutoka nje ya mji na malaika wa Mungu, Lutu alionekana kukinzana na wokovu, Imani yake ilikuwa imedhoofu kiasi hicho. Hakuwa anaamini majaliwa ya Mungu kwa ajili ya usalama wake, na akasihi ajiokoe katika sehemu nyingine atakayochagua mwenyewe. Malaika walikubaliana na ombi lake, lakini hali haikuwa kama Lutu alivyotazamia.

Kadiri familia ndogo ilivyokimbia kuelekea katika mahali walipodhani ni salama, mke wa Lutu alianza kupunguza kasi yake. Hatua zake zilizanza kudorora mwisho akashindwa kuendelea, lakini siyo kwa ajili ya uchovu. Walihisi joto kutoka katika moto uliokuwa unawake nyuma yao, na kilio cha mauti kilisikika katika masikio yao. Katika haraka na wasiwasi, Lutu hakutambua kwamba mke wake alikuwa ameanguka nyuma yake. Alikuwa amechanganyikiwa kwa kutokuwa na uhakika wa kufanya kile alichoagizwa; kichwa chake kilikuwa katika kuvurugika.

Ghafla mke wa Lutu alisimama na kuangalia nyuma, macho yake yalipoona ule mji alioupenda kuliko kitu kingine chochote, aliona mwonekano wa mwisho wa dunia hii. Mara akaganda na kuwa nguzo ya chumvi, mfano wa mnara wa maangamivu ya moyo uliokuwa umegawnyika. Alikuwa karibu atoke mjini na kupona kama angepiga hatua zingine chache. Badala yake alipotelea ukingoni mwa wokovu.

Kisa hiki kilinitisha nilipokuwa mtoto. Sikuweza kukielewa vizuri. Mama Lutu alikuwa akifanya kila kitu alichoambiwa na Malaika. Ni kwamba, aligeuza tu kichwa chake. Je, kufanya hivi kulistahili kifo? Ni kweli kwamba, Malaika walikuwa wamemwambia asigeuke kuangalia nyuma, lakini pengine alisahau. Katika vurugu za yote hayo yaliyokuwa yakiendelea, labda alichanganyikiwa. Kugeuza kichwa mara moja tu, na akafa! Je, hili ndilo somo kutoka kwa mke wa Lutu?

Kwa kweli siyo. Kama Mungu angetaka kumwangamiza mke wa Lutu, angemwacha mjini. Mungu alikuwa anajaribu kumwokoa huyu mama. Tunachoona katika uwanda kwenye ile nguzo ya chumvi, ni mwanamke aliyekataa wokovu kwa sababu hakutaka gharama ya huo wokovu. Mke wa Lutu alidharau ukombozi wa Mungu kwa sababu

hukumu yake kwa Sodoma ilihusu pia mali yake. Nyumba yake alikuwa ikiwaka moto pale. Alichukia wokovu wa Mungu kwa sababu haukuhusu nguo zake za Fahari, fedha zake, marafiki wake, na hata watoto wake waovu ambao hawakuwa tayari kusikia maonyo. "Aliona kama ameonewa kwa sababu ilimchukua miaka mingi kukusanya mali yote ile ambayo sasa inaharibiwa na moto." (*Patriarch and Prophets,* uk. 161)

Siyo kile kitendo cha kugeuka nyuma klichomwangamiza mke wa Lutu. Kule kugeuka ilikuwa ni ishara tu ya kile kilichokuwa ndani ya moyo wake. Alikuwa ameshageuka moyoni kabla hajafika hapo alipogeuza kichwa kuangalia nyuma. Kule kusitasita kwa mume wake kukimbia kutoka Sodoma kulidhoofisha uamuzi wake. Gharama ya kusitasita kwa Lutu ilikuwa ni uhai wa mke wake.

Msiba wa mke wa Lutu unatukumbusha kanuni ya Biblia ya kujitenga. Biblia haitufundishi kwamba kuwa na mali ni dhambi, au kwamba mali yenyewe ni uovu. Abraham alikuwa tajiti kuliko Lutu, lakini mali hiyo haikugharimu hali yake ya kiroho. Hatari ya mali siyo kule kuwa nayo, bali ni mali kuwa na sisi. Kisa cha Lutu kinatukumbusha umuhimu wa jinsi ya kuhusiana na mali.

Kujitenga kunamaanisha kukabidhi mali yetu kwa Mungu kwa agano. Tuwe tayari kutumia hiyo mali kwa kusudi lake au kuiachia kwa amri yake. Ikiwa Imani yetu ni ile inayotakiwa, Mungu anaweza kuchukua mali yetu bila kueleza kwamba kwa nini anaichukua. Paulo anaunganisha kujitenga na kuridhika anaposema kuwa,

> "Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, nimefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa." – Wafilipi 4:12

UWEZO WA NUHU WA KUAMUA

Ukilinganisha na ile hali ya kusitasita ya Lutu, Imani ya Nuhu ilidhihirika kwa uwezo wake wa kuamua. "Kwa imani Nuhu akiisha kuonywa na Mungu katika habari za mambo yasiyoonekana bado, kwa jinsi alivyomcha Mungu, aliunda safina, apate kuokoa nyumba yake. Na hivyo akauhukumu makosa ulimwengu, akawa mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani." (Waebrania 11:7). Wakati Imani ya Lutu ikidhoofu katika kipindi alichoishi Sodoma, Imani ya Nuhu ilibakia imara ilipopimwa.

Kumwamini Mungu ni zaidi ya Imani katika uwepo wake. Kuamini kwamba Mungu yupo, ni hatua ya mwanzo, kwa uchache ndicho kiinachohitajika ili kufamhamu Mungu. (Waebrania 11:6). Imani inapokomaa inavuka kusadiki. Inagauka kuwa msingi wa mtazamo mpya wa ulimwengu. Biblia inaelezea Imani komavu inapotamka kuwa:

> "Tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele." (2 Wakorintho 4:18)

Mfano huu wa "kuelekeza macho yetu" katika kitu ambacho hakionekani unatuonesha uhalisia wa uwanja wa kiroho. Yesu aliposema kuwa, "ufalme wangu siyo wa ulimwengu huu," ndivyo alivyomaanisha. Kuna mtazamo wa kilimwengu na seti ya tunu ambazo hazitokani na dunia hii wala hazifanani na za dunia hii. Kuna eneo la uhalisia ambalo halionekani kwa macho ya kawaida ya kininadamu, bali linaonekana kwa macho ya Imani. Huu mtazamo wa kilimwengu ndio ulioongoza katika uamuzi wa Nuhu ukilinganisha na kusitasita kwa Lutu.

Mada inayojirudia rudia katika kisa cha maisha ya Nuhu ni ule utii wa mara moja kwa agizo la Mungu. Wakati Lutu akijaribu kujadili kuhusu wokovu wake kwa sababu ya hofu, Nuhu alitii kwa Imani – mtumbwi dhidi ya gharika katika ulimwengu ambao haujawahi kushuhudia mvua. Lakini Nuhu alikuwa na Imani imara, na ilionekana katika matendo yake.

- "Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya." (Mwanzo 6:22)
- "Nuhu akafanya kama vile Bwana alivyomwamuru." (Mwanzo 7:5)
- "Wakaingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, mume na mke, kama vile Mungu alivyomwamuru Nuhu." (Mwanzo 7:9)

Kwa miaka 120 Nuhu hakutikisika kutoka katika kusudi la Mungu kwa ajili ya maisha yake. Alipokea dharau na shutuma kwa huduma yake bila malalamiko, na hakuwahi kuomba abadilishiwe jukumu. Watoto walizaliwa, wakakua, wakawa watu wazima, wakaoa na kuolewa, wakapata watoto wao wenyewe, ambao pia walikua wakawa watu wazima, nao pia wakapata watoto, na Nuhu alikuwa anaendelea kuhubiri. Mivuto ya matendo yake ilielezea vyema familia yake kwa namna ile ile ambayo mivuto ya matendo ya Lutu alikuwa kwa familia yake." Familia yake ilifaidi kutoka katika mvuto wa Imani yake na utii wake kwa Mungu.

"Ni kanuni kwamba, watoto wanarithi tabia na mwelekeo wa wazazi wao, na wale watu wa karibu kama mifano yao." (Patriarchs and Prophets, uk.117). Na kwa kuwa "Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu."

Watoto wa Nuhu walipozaliwa, tayari Nuhu alikuwa ameanza kushughulika na mradi wa Safina. Walipofikia umri wa kushika nyundo, walishiriki katika huo mradi sambamba na mzazi wao. Walichangia katika kujenga chombo ambacho kingeokoa maisha yao, chini ya usimamizi wa baba yao.

Ham, Shem, na Yafeti walimwangalia baba yao wakati wakikua na wakafahamu kwamba huyo mzee alimaanisha alichokuwa akifanya. Nuhu alikuwa mfano kwa vijana wake na mvuto wa maisha yake ulikuwa na mguso wa kina kwao.

Katika shairi lake, "Mahubiri tunayoona," Edgar Guest ana msitari stahiki unaosomeka hivi: "Kwa kuwa ninaweza kushindwa kukuelewa na ushauri mkubwa unaoutoa, lakini hakuna shaka kwa namna unavyotenda, na jinsi unavyoishi."

Neema ya Mungu kwa Nuhu ilihamishiwa kwa vijana wake; waliokolewa kwa mfano wake. Nuhu alikuwa akipanda mbegu ya wokovu katika familia yake kwa namna alivyoishi kama mtu wa Mungu"

> "Kama zawadi kwa uaminifu wake na uadilifu wake, Mungu aliokoa wanafamila wake wote pamoja naye." Maisha yake yalikuwa ni ya kuwatia moyo wazazi ili wawe na uaminifu. (Patriarchs and Prophets, uk. 98)

Kila mzazi ni mchungaji, na kila familia ni kanisa la kwanza. Hapa kuna ukweli wa kawaida ambao nimejifunza kwa miaka yangu katika huduma, mwanamke aliyependa, atamfuata mume wake katika kutenda mema, na watoto watafuata. Mara nyingi unaweza kuona wanawake kadhaa kanisani bila mwanamume, lakini ni mara chache utaona mtu mcha Mungu kanisani bila mke wake pembeni yake na watoto wake.

Mke wa Nuhu alimfuata mume wake hadi ndani ya Safina kwa sababu Nuhu alikuwa imara katika usahawishi wake, wakati mke wa Lutu hakumfuata mume wake kwenda sehemu salama kwa sababu alikosa msimamo.

Hapa kuna ahadi ambayo wazazi wanaoamini huwa wanaidai.

> "Naam, Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari wataokoka; kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana wako wokovu." – Isaya 49:25

Ni ahadi nzuri na inatupatia tumaini pale watoto wetu wanapotanga mbali. Lakini tunapodai ahadi hii, tukumbuke kwamba ina masharti. Hiyo ni dhana wala siyo Imani, kwa sisi kumwomba Mungu aokoe watoto wetu bila ushiriki wetu. Ni lazima tufanye sehemu yetu kama Nuhu alivyofanya sehemu yake. Familia yake iliokolewa kwa Roho Mtakatifu kufanya kazi kupitia kwa Nuhu.

> "Uzoefu wa Nuhu ulikuwa mfano wa kuigwa kwa Wakristo ambao wanafahamu kuwa wanaishi katika nyakati za mwisho wakijiandaa katika kubadilishwa. Kazi yao kuu ya umisionari inatakiwa kufanyika nyumbani."[9]

[9] Francis D. Nichol, editor, The Seventh-day Adventist Bible Commentary in seven volumes (Washington, D.C., 1978), 1:254

Rasilimali kubwa aliyo nayo baba kama kichwa cha nyumba siyo ukali au msimamo mkali. Siyo namna ya kijeshi anayoonesha katika amri zake kwa familia ili watii. Baba aliye imara siye anayewatawala kwa fimbo ya chuma wale walio chini ya dari yake. Ni yule baba ambaye kwa mfano wake mwenyewe anaonesha maana ya kuwa mtu wa Mungu.

Ina maana kubwa kuwa na baba ambaye unaweza kumtegemea, baba ambaye maisha yake yamejengeka katika tabia ya Kristo. Baba wa namna hiyo anaweka viwango kwa watoto wake toka ndani ya mioyo yao, kiwango cha ndani ambacho hakiwezi kuondoka. Hata wakati wanapokuwa hawaishi kulingana na viwango hivyo wao wenyewe, dhamiri zao zitakuwa zinawaambia kwamba wanatakiwa kuwa bora kuliko walivyo; kwamba wanatakiwa kuwa kama baba yao. Hii ndiyo aina ya kiongozi ambaye kila familia inapaswa kuwa naye kama kicha cha familia.

MFANO

Mimi na mke wangu tulibahatiwa kuwa na wazazi wa kiume ambao hawakuwa na elimu ya juu sana lakini walikuwa na bidii katika kufanya kazi, na walikuwa waaminifu, wenye Imani ya dhati kabisa. Siyo kwamba ninawafananisha na Nuhu, ambaye Biblia inamtamka kama "mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake." Kwa kweli hawakuwa wakamilifu, hata katika utoto wetu tuliona mapungufu yao. Lakini nilichojifunza katika miaka yangu hii ni kwamba watoto watasamehe mapungufu ya wazazi wao ikiwa watakuwa na Imani kwao. Watapuuza makosa ya wazazi wao, lakini hawawezi kustahimili unafiki.

Baba zetu walipotupeleka kanisani siku ya Sabato, au walipochukua Biblia nyumbani katika ibada ya jioni, walimaanisha kila neno walilotufundisha na kututaka tutii. Waliamini kile walichofundisha na kukiishi kadiri walivyoweza. Ndivyo mtu wa Mungu unavyoweza kuokoa familia yako; inahusu kila kitu. Ni lazima tudhamirie na kuuza kila kitu kwa ajili ya Mungu

HITIMISHO

Na sasa tumekuja kwa ujumla wote. Tofauti kati ya familia ya Nuhu na ile ya Lutu, na hasa wale waliokuwa vichwa vya familia, ilikuwa ni uimara wa kiroho dhidi ya udhaifu wa kiroho. Hali ya jamii iliyokuwa ikiwazunguka ilifanana. Tofauti ilikuwa ni ndani, siyo nje. Tofauti ilikuwa ni sababu ya familia moja kubakia imara wakati familia nyingine ikivunjika. Ilikuwa ni tofauti kati na hali ya kiroho na mali, na ule uwezo wa

kuamua dhidi ya kusitasita. Tabia hizi zinajengeka katika uimara au udhaifu wa Imani yetu kwa Mungu. Kadiri tunavyokua katika Imani, tunathibitisha upendo wetu na matumaini yetu kwa Mungu na kuhakikisha furaha yetu.

KIELELEZO

Kuna kisa cha baba aliyeamshwa na sauti ya kijana wake usiku wa manane, "Baba kuna mtu ndani ya nyumba!" Yule baba aliruka kutoka kitandani na kujikuta mbele ya mtu akiwa ameshikilia kisu kwenye koo la binti yake. Huyu mvamizi aliyeyuka kuelekea mlangoni kadiri baba alivyomkabili. Hawa wanaume wawili wakapambana bila kutoleana neno lolote.

Baba alihisi damu ikimwenda mbio na kila hisia ilijikusanya kadiri alivyotafuta fursa. Yule mvamizi akageuza kichwa chake kwa sekunde kutazama pa kukimbilia, na baba akapata mwanya. Alimrukia mvamizi na pambano jipya likaanza. Kisu kikaanguka, na binti akakimbia, wakati huo huo yule mvamizi naye akakimbia. Baba akawakumbatia Watoto wake, yule mvulana na binti yake, alikuwa ameokoa familia yake.

Tukio hili lilipokoma baba akatoa taarifa polisi. Mmoja wa maaskari akauliza kuwa, "ulikuwa unawaza nini katika kichwa chako?" "Nilipokuwa nimesimama tukiangaliana na yule mtu uso kwa uso, mkono wake ukiwa kwenye koo la binti yangu, niliweka nadhiri kichwani pangu wakati ule ule. Yule mtu asingeondoka hapa na binti yangu bila kujali nini kitakachotokea kwangu, hata kama ingegharimu maisha yangu!"

KUWEKA KATIKA MATUMIZI

Kuna mvamizi ameingia katika nyumba zetu sisi sote, akiwa na dhamiri ya kuua. Mkono wake upo katika shingo ya watoto wetu akisubiri fursa ya kuwaondoa kwako milele. Hii ni kweli katika siku zetu hizi kuliko ilivyowahi kuwa wakati mwingine wowote. Lakini hakuna haja ya kuogopa, Bwana yuko upande wetu, na atatupatia namna ya kuponyoka na pia mahali palipo salama katika Mwana wake, Yesu. Kristo ni Safina ya salama kwa wote wanaomwamini. Lutu au Nuhu? Tunapaswa kuchagua.

IBADA YA FAMILIA
UZIO UNAOLINDA

NA JOHN B. YOUNGBERG

AYA ZA MAANDIKO

Malaki 4:5-6; Yoshua 24:15

I. ULINZI DHIDI YA MADHARA YA KIMWILI

Katika kitabu cha Ayubu sura ya kwanza, inaletwa mandhari ya mbinguni; Shetani akijiona kama mtawala wa sayari yenye dhambi ya dunia, akimlalamikia Mungu kuhusu Ayubu, mtu mwenye haki. Akisema kuwa, "Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia…"

Shetani anakiri kwamba Mungu anamlinda Ayubu kutoka katika mipango yake miovu ya kusababisha madhara. Je, hicho si ndicho familia nyingi zinahitaji? Uzio unaolinda kuzungukia familia? Ninapendekeza katika hubiri hili kwamba ibada ya familia ndio huo uzio unaolinda. Katika kitabu cha *Child Guidance,* uk. 520 Ellen G. White anasema kuwa, "Kina baba, kina mama, hata mkizidiwa kazi kiasi gani, msishindwe kukusanya familia katika madhabahu ya Mungu. Omba uongozi wa Malaika watakatifu nyumbani kwako."

Futi mia tano za ukingo wa mto wenye miamba zilisababisha mlio wa Sandi kana kwamba alikua akikimbia kwa kasi katika mbio za utelezi wa sileji. Mteremko uliong'arishwa na maporomoko ya barafu ya mto Tuolumne ulikuwa unateleza kama barafu yenyewe. Ndipo mungurumo unaotosha kumfanya mtu kiziwi wa maporomoko ya Le Conte ulisikika kwenye masikio yake kwa sauti ya juu. Je, angewezaje kuacha mtindo wake wa kuteleza kwa namna hatarishi kabla hajadumbukia katika gema la kina cha futi mia mbili mbele yake? Kitu pekee ambacho huo mto uliweza kutoa katika kujiokoa ni utando wa mwani wa rangi ya kijani uliong'ang'ania kwenye miamba myembamba. Je, ni kweli kwamba siku yake iliyoanza kwa furaha na vicheko ingehitimika kwa kifo kinachotokana na kuendesha sehemu yenye majimaji?

Asubuhi hiyo familia ilikuwa imekusanyika kuzungukia eneo lenye moto kabla ya kuanza kupakia vitu kwenye mikoba kwa ajili ya safari kwenda katika hifadhi ya taifa. Sauti zilizochanganyika za baba, mama, na watoto sita ziliimba wimbo: "Baba tunakushukuru kwa ajili ya usiku, na kwa ajili ya nuru ifurahishayo ya asubui; kwa ajili ya pumziko, chakula, na ulinzi wenye upendo, pamoja na vingine vyote vinavyofanya siku ipendeze. Kutusaidia kufanya mambo tunayopaswa kufanya. Kuwa wema kwa wengine katika yote tunayofanya, kazini au katika michezo. Kukupenda wewe vizuri siku kwa siku."

Kadiri sauti ya mwisho ilivyoanza kufifia porini, baba alimsihi Mungu aiweke familia yake mikononi mwa Malaika mwenye upendo siku hiyo. Baada ya hapo, walianza kutembea kwenye kinjia kidogo kilichoelekeza umbali wa kama futi elfu mbili hadi kwenye maporomoko ya maji, wakiwa wamebeba mikoba iliyosheheni vyakula vya siku kumi na mbili.

Binti yetu mwenye umri wa miaka minne aitwaye Sandy, ambaye alikuwa mbele ya mdogo wake, alifika katika kambi ya usiku iliyokuwa ikifuata na baada ya kufungua mkoba wake, alibadili nguo na kuvaa nguo za kuogelea akaenda mtoni kuogelea kwenye maji yaliyokuwa yanaenda kasi. Mwanzoni alitoa sauti kali ya furaha kadiri alivyoingia majini. Alikuwa amepanga kwenda karibu tu katika eneo lenye maji mafupi, lakini mto ulikuwa na kasi ambayo hakutegemea, ghafla maji ya mto yakamgeuzia kwenye mkondo. Kwa haraka alivutwa na kupigwa kwenye mawe na kingo za mto akielekezwa uelekeo wa maji, huku akijaribu kushika kila alichoweza kushika. Akaanza kupiga kelele, "Eee Yesu nisaidie!" Ingawaje alijaribu kila alivyoweza, hakuweza kumudu kuvutwa na mkondo. Hofu ilimwingia kadiri alivyosukumwa kwenda chini kipande cha mwisho kabla mto haujamiminika kwenye maporomoko.

Charlene mwenye umri wa miaka kumi na saba akiwa katika matembezi yake alifika kwenye maporomoko wakati Sandy ndiyo anakokotwa na mkondo kuelekea kwenye ukingo wa maporomoko. Alimwona dada yake akivutwa na mkondo wa maji. Baada ya hapo dada yake alipokuwa amefikishwa na mkondo, maji yalikuwa yanaenda kushuka kwa kasi kwenye maporomoko yaliyokuwa na urefu wa futi mia kadhaa na kuangukia kwenye miamba kule chini. Kwa sekunde chache tu maji hayo yangefanikiwa kushuka kwenye maporomoko na mawindo yake. Ndipo Charlene aliona muujiza. Ghafla mbele ya macho yake aliona kama vile mkono fulani umemsukuma Sandy nyuma kidogo ya maporomoko na kumsogeza kwenye jiwe lililokuwa Jirani tu na miguu yake. Akionekana kujawa na hofu, Sandy alijisogeza kwenye jiwe na kujilaza pale katika hali ya kuzirai, akitetemeka na kuonekana kuchoka kabisa. Charlene alikimbia akilia kuelekea kwa baba yake. Kwa haraka baba alishuka mtoni nakumkuta binti yake akiwa kwenye jiwe ukingoni mwa mto katika hali ya kutisha akishindwa kuongea. Ndipo

alipoanza kulia, baada ya kumfariji, baba yake aliye mganga alimchunguza kuona kuwa alikuwa na michubuko yoyote mwilini wake. Bahati! Hakuwa na mchubuko.

Kwa neema kubwa familia ile ilimshukuru Mungu kwa ajili ya ulinzi wake katika ibada usiku ule. Hakuna aliyekuwa na mashaka kwamba Malaika alikuwa ameingilia kati na kumwokoa Sandy kutoka katika hatari ambayo ilikuwa karibu kutokea ambayo ingesababisha kifo chake. Mungu alikuwa ametimiza ahadi yake kwamba, "Kwa kuwa atakuagizia malaika zake Wakulinde katika njia zako zote. Mikononi mwao watakuchukua, Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe." (Zaburi 91:11, 12)

ULINZI DHIDI YA MUAFAKA WA KIROHO

Katika kitabu cha Ayubu pia tunaelezwa kuwa, "Ayubu hutuma kwao akawatakasa, kisha akaamka asubuhi na mapema, na kusongeza sadaka za kuteketezwa kama hesabu yao wote ilivyokuwa…" (Ayubu 1:5). Shetani alienda na kulalamika kwa Mungu akisema kuwa, "Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi."

Ellen G. White anatupatia ushauri ufuatao: "Wazo la kwanza kwa Wakristo kila asubuhi linapaswa kuwa kumhusu Mungu. Mahangaiko ya kidunia na shauku binafsi yapewe nafasi ya pili. Watoto na wafundishwe kuheshimu ule muda wa ibada na maombi… Ni wajibu wa wazazi Wakristo kuwajengea wigo watoto wao kila asubuhi na kila jioni kwa maombi ya dhati na Imani stahimilivu. Wanapaswa kuwaelekeza kwa uvumilivu, kwa upole bila kuchoka wakiwafundisha jinsi ya kuishi kwa utaratibu upasao ili kumridhisha Mungu." (*Child Guidance,* uk. 512)

Abraham alikuwa ni mjenzi mwingine wa madhabahu katika Agano la Kale. Biblia inatuambia kuhusu wakati alipofika katika nchi ya Kanaani. "Bwana akamtokea Abramu, akasema, Uzao wako nitawapa nchi hii. Naye huko akamjengea madhabahu Bwana aliyemtokea." (Mwanzo 12:7). Kisha akaondoka hapo na kuelekea Betheli na hapo pia, "…akamjengea Bwana madhabahu huko, akaliitia jina la Bwana." (Fungu la 8). Kwa sababu ya njaa katika nchi, Abraham alishuka hadi Misri. Kisha akarudi tena Kanaani karibu na Betheli "… napo ndipo palipokuwa na madhabahu aliyofanya hapo kwanza; naye Abramu akaliitia jina la Bwana hapo." (Mwanzo 13:4). Abraham alimwamini Mungu na kumwabudu, "…naye akamhesabia jambo hili kuwa haki." (Mwanzo 15:6). Hapo ndipo Mungu akabadilisha jina la Abram na kumwita Abraham (Mwanzo 17:5). Na katika Mwanzo 18:18-19 Mungu alisema kuwa, "akiwa Ibrahimu atakuwa taifa kuu, hodari, na katika yeye mataifa yote ya dunia watabarikiwa? Kwa

maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, wafanye haki na hukumu, ili kwamba Bwana naye akamtimizie Ibrahimu ahadi zake."

Kama pale wana wa Israeli walipokuwa tayari kuingia katika nchi ya ahadi, Musa aliwambia kuwa, "Bali ninyi mlioambatana na Bwana, Mungu wenu, mnaishi kila mmoja wenu, hata leo. Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama Bwana, Mungu wangu, alivyoniamuru, ili mzitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki. Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo?" (Torati 6:4-7) Mwelekeo huu wa kumwabudu Mungu na kufundisha njia yake ungewalinda wasizame katika ibada ya sanamu kama mataifa yanayowazunguka.

Hebu fikiria kwamba ni siku yako ya mwisho katika sayari hii ya dunia. Mfalme anakuja! Ujumbe wa Malaika watatu tayari umeshasikika kutoka mashariki hadi magharibi, kutoka ncha moja hadi ncha nyingine. Ulimwengu wote tayari ueshasikia sauti kuu ya "INJILI YA MILELE." Naam, ulikuwa ni ujumbe wa "KUMWABUDU YEYE [Muumbaji] aliyeziumba mbingu na nchi." (Tazama Ufunuo 14). Ni ujumbe huo huo ambao Elisha alishiriki alipokuwa akijenga madhabahu iliyokuwa imevunjika katika mlima wa Karmeli, kisha akaomba kwamba Mungu ageuze mioyo ya watu wake (Tazama 1 Wafalme 18). Ni ujumbe huo huo ambao Yohana Mbatizaji (Eliya wa Pili) aliuhubiri katika kingo za mto Yordani akisema, "Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" (Yohana 1:29)

Katika ujumbe wa Eliya wa siku za mwisho, "Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya. Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, (na mama zao)." (Malaki 4:5, 6). Na sasa kuna kutulia kidogo, na swali la dhati kwa wazazi linasikika, "…liko wapi kundi lako ulilopewa, kundi lile zuri?" (Yeremia 13:20). Ukiangalia wanaokuzunguka, familia zinakusanya wapendwa wao pamoja katika mduara, na kwa shukurani wananyenyekeza mioyo yao, na kuitikia kuwa, "Angalieni, mimi na watoto hawa niliopewa na Bwana tu ishara na ajabu katika Israeli…" (Isaya 8:18) Siku ya Utukufu!

Je, tunaweza kudai ahadi hizi? ""Je! Aliye hodari aweza kunyang'anywa mateka yake, au jeshi lao waliofungwa halali wataokoka? Naam, Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari wataokoka; kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana

wako wokovu. (Isaya 49:24, 25). "Na watoto wako wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa nyingi." (Isaya 54:13). Ni kwa namna gani unaweza kufanya jambo hili likawa kweli katika familia zetu leo?

UNATAMBUAJE KAMA IBADA YAKO IMEKUBALIKA KWA MUNGU?

Mtu fulani alisema kwamba wanadamu ni viumbe wanaoabudu. Sisi sote tunaabudu kitu fulani au mtu fulani. Wengine wnaabudu wasanii wakubwa. Wengine wanaabudu timu za michezo. Wangine wanaabudu mitindo. Wengine wanaabudu akaunti zao za benki. Kwa hiyo tunauliza kuwa, ni nini au ni nani anayepokea usikivu wako maishani mwako? Huyo ndiye, au ndicho unachoabudu. Katia Ufunuo 17:17 tunasoma kuwa siku za mwisho, waovu watakuwa na 'shauri moja… kumpa yule mnyama ufalme wao hata maneno ya Mungu yatimizwe." Maana yake maneno haya ni kwamba kila mtu atachagua ni nani atakayemwabudu, na wengine watachagua ibada ya uongo wakimpuuza Mungu Muumba na kujali vivutio vya kidunia ambavyo ni kinyume cha mashauri yaliyoko katika Neno la Mungu kuhusu ibada ya kweli, na kulazimisha watu wote kumwabudu mungu wa uongo.

Upande mwingine kuna kikundi kinachojielekeza katika ibada ya Mungu wa kweli na Yesu Kristo aliyeumba vitu vyote pamoja na wanadamu. Alituumba ili kumwabudu yeye peke yake. Katika Isaya 44:6 na 8 tunasoma kuwa, "Bwana, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wako, Bwana wa majeshi, asema hivi; Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu. Msiogope wala msifanye hofu; je! Sikukuhubiri haya zamani na kuyaonyesha? Na ninyi ni mashahidi wangu. Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine." Yule tunayechagua kumwabudu ndiye atakayejaa mawazoni petu. Kumwabudu Mungu kwa namna aliyotuchagulia inaamua hatima yetu maishani, hii ikiwa ni pamoja na uzima wa milele. Ni muhimu sana kwetu kufanya uchaguzi sahihi. Biblia inasema kuwa, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu." (Wafilipi 2:5). "Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo." (1 Wakorintho 2:16) "Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini." (Isaya 26:3). Kwa hiyo katika Maandiko tunaona mgongano wa mawazo, wa mitazamo, hasa kadiri tunavyopita katika siku hizi za mwisho za pambano kuu kati ya wema na uovu.

Kila mmoja ni lazima achague mwenyewe, ikiwa tutachagua mawazo ya adui wa wanaume, wanawake, na watoto, au ikiwa tutachagua mawazo ya Kristo. Kama vile tu

wana wa Israeli walivyoingia katika nchi ya Kanaani, kiongozi wao Yoshua aliwaambia kuwa, "Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia Bwana, chagueni hivi leo mtakayemtumikia; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng'ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana." (Yoshua 24:15)

Katika nyumba za Wakriso wa kileo, ibada ya familia inafundisha watoto wao kumhusu Mungu na mipango yake kwa maisha yao. Inahamisha elimu ya Biblia na umuhimu wake katika maisha yetu. Inawapatia watoto fursa ya kukubali mpango wa wokovu mapema katika maisha yao na kuwafanya kujitoa kikamilifu katika kumtumikia Mungu kwa namna yenye maana. Ibada ya familia inapokuwa ya furaha, iliyojengeka kwa Kristo, na ikijumuisha shughuli stahiki kwa kila umri, vifungo kati ya wanafamilia vinaimarishwa.

IBADA YA FAMILIA YAKO IKOJE?

Je, ungependa kufanya ibada ya familia yako ikawa na uzoefu wa kawaida, wenye mabadiliko hapo nyumbani kwenu? Ungependa kuwapatia watu wa familia yako mana ya kiroho iliyo moto ya uhusiano na Mungu unaokua? Je, nyakati hizi za kuburudisha zinaweza kuwa za thamani kubwa na kustawisha kwa watu wote wa fimilia yenu?

Mtu mmoja nayeitwa John Elick na mke wake walipoenda katika msitu wa Amazon eneo la juu ya Peru kama watangulizi kwa makabila ya wenyeji wa eneo lile, walikuwa na kasuku wa kufugwa. Yule kasuku aliwasikia wakiimba wimbo wakati wakishereheka ibada. Baada ya muda ule wakati wa ibada ulipofika, yule kasuku alianza kuimba wimbo wao wa ibada hata kabla hajaja mtu, kwa sababu tu alijua kwamba ulikuwa ni wakati wa ibada. Naam, ibada ya familia inapaswa kuwa tabia ya kawaida mara mbili kila siku ikiwezekana, hata kama baadhi ya wana familia watakuwa hawapo.

Jaribu kuwafanya watoto kushiriki katika ibada ya familia. Katika familia moja wakati watoto wao wawili wa kiume waliosogelea umri wa balehe, familia ilikusanyika jioni moja na baba akawapatia vikaratasi kila mmoja. Akasema kuwa, "Tumeshafanya mambo mengi pamoja, ninataka kila mmoja aorodheshe uzoefu wa kufurahisha tuliokuwa nao kama familia." Kila mmoja akaanza kuandika. Baada ya muda wakaanza kujumuisha yale yaliyoandikwa na kila mmoja. Baba alishangaa sana aliposoma ile orodha. Ni nini kilichotangulia? Ilikuwa ni likizo ya familia, kupiga makasia kwenye mtumbwi katika mto wa Pierre Marquette, ambao ni mmoja wa mito iliyo na kasi kubwa katika rasi ya chini ya jimbo la Michigan. Vijana walipanda kwenye mtumbwi

mmoja. Baba na mama wakaingia kwenye mtumbwi mwingine na chakula pamoja na mahema na vifaa vya kulalia.

Kabla tu hawajaenda mbali sehemu mto ulipopinda kwa mara ya kwanza ukiwa na kasi, wakati wakiwa bado wanarekebisha mizigo yao ndani ya mitumbwei. Lo! Mtumbwi wao ukagonga gogo lililokuwa ndani ya maji na ukapinduka na kuzama. Kamera ya baba ikaanguka majini, naye akapiga mbizi kuifuatilia. Hatimaye wakafanikiwa kufika kwenye sehemu yao ya kupiga kambi ya kwanza giza likianza kuingia. Walisimika mahema yaliyokuwa yamelowa pale mtumbwi ulipopinduka na kuwasha moto ili kukausha matandiko yao. Kijana wao aitwaye Yohana alikuwa akitembea ukingoni mwa mto, akitoa kicheko cha chini chini kwa namna wazazi wake walivyowashtukiza. Na lo! Alipofika kwenye tandiko lake la kulalia alilokuwa ameacha njiani, kwa bahati mbaya akajikwaa juu yake, likaserereka na kuangukia mtoni. Siku iliyofuata kijana Wes alikuwa amesimama upande mwingine wa mtumbwi akitazama kiota cha manyigu kilichokuwa kikining'inia kwenye mti wakati mtumbwi ulipogonga kwenye mwamba uliokuwa majini bila kuonekana kwa nje. Ilikuwa ni likizo ya siku 14 zilizo bora zaidi. Siku 10 katika hizo zote mvua ilinyesha. Na baada ya yote hayo, hakuna mtu aliyepata maumivu. Mungu alikuwa amewalinda, na walikuwa wamefurahia muda wa kuwa pamoja kama familia.

Walipomaliza ibada jioni ile, wakikumbuka likizo ya familia, vijana walisema kuwa, "Baba, tulikuwa na wakati mzuri hasa! Hebu tuwe na muda mwingine wa ibada kama ule!"

Katika tukio jingine, kijana Yohana na Wes waliamka na kuwa tayari kwenda shule wakati mama yao alipowaita kwa ajili ya kifungua kinywa. Walipokuja jikoni, hawa vijana kwa mshangao waliangaliana. "Kwani kuna nini? Siku yako ya kuzaliwa? Hapana, kwani ni siku yangu ya kuzaliwa? Hapana!" Meza ilikuwa imepambwa vizuri kwa mishumaa na maua ya kupendeza. Baba akasema kuwa, "Desemba 5 - ni nini kilichotokea tarehe hii?" Mara uso wa Yohana ukafunguka, "Nimekumbuka! Ilikuwa ni tarehe ya ubatizo wetu, miaka mitatu iliyopita." Ndipo mama akaleta vile vyeti vya ubatizo ambavyo walikuwa wameweka sahihi wakiahidi kumfuata Yesu. Waliwaambia vijana wao kwamba walikuwa wakijivunia maamuzi yao na kwamba wote walikuwa na ombi la kumshukuru Mungu kwa wema wake na kwa nyakati za pamoja walizokuwa nazo. Kisha mama akaleta kifungua kinywa kilichokuwa kitamu bila mfano. Hakuna aliyelalamika kuhusu ibada ya familia!

Kiunganishi katika visa vyote vitatu ni kushereheka. Ibada ya familia yenye ufanisi inajumuisha SHEREHE.

NI NINI KINACHOFANYA IBADA YA FAMILIA IWE NA UFANISI??

Daktari Edgel Phillips alipokuwa mwanafunzi katika chuo kikuu cha Andrews, alifanya utafiti katika malengo na mbinu za ibada za familia katika kanisa la Waadventista wa Sabato. Aligundua kwamba mbinu yenye nguvu katika kuwaunganisha wanafamilia na kuwaleta karibu na Mungu na karibu ya kila mmoja wao, ilikuwa ni katika vigezo vya mahusiano ambavyo vilihusisha mazingira ya asili ya ibada za familia.

Kuingiliana kwa namna binafsi:

- Kusalimiana na kukaribishana
- Kushiriki uzoefu wa siku husika
- Kujadili matatizo ya siku husika.
- Kuonesha shukurani kwa mambo mema yaliyotokea.
- Kuomba msamaha kwa mabaya yaliyofanywa na kila mtu kwa mwenzake.
- Kuzungumza kuhusu kile Mungu anachomaanisha kwa kila mmoja.
- Kunukuu ahadi zilizopo kwenye Biblia

Uthibitisho Binafsi

- Hisia za kukubalika na kuwa sehemu ya.
- Hisia za upendo na ustawi.

Kuomba pamoja:

- Kuomba asubuhi na jioni
- Kumkaribisha Roho Mtakatifu katika maisha binafsi ya kila mtu.
- Kushiriki mambo ya kuombea
- Kuomba kwa kupokezana kwa mzunguko.

Maombi yenye ufanisi ni pamoja na maombi yenye vigezo viwili.

1. Tunazungumza na Mungu. Tunashiriki shukurani zetu, mahitaji yetu, maombi yetu, na kuabudu kwetu. Tunawaombea watoto wetu, wale wanaopambana na adui, na kwa ajili ya mahitaji yetu ya kila siku.
2. Mungu anazungumza nasi. Maombi ni namna mbili za kuwasiliana – siyo tu kwamba tunazungumza na Mungu, bali pia mara nyingi tunasahau kusikiliza sauti yake akizungumza nasi. Naam, katika maombi tunatakiwa kumsikiliza Mungu kadiri tunavyochunguza na kusoma Neno lake – yaani Biblia. Mungu pia anaweza kuzungumza nasi katika ukimya kupitia katika mguso wa Roho Mtakatifu, lakini mara nyingi hatutulii kuisikiliza sauti yake. Mtoto Samweli alisikia sauti ya Mungu ikimwita,

> "Samweli, Samweli." Maandiko yanatuambia kwamba, "Na masikio yako yatasikia neno nyuma yako, likisema, Njia ni hii, ifuateni; mgeukapo kwenda mkono wa kulia, na mgeukapo kwenda mkono wa kushoto." (Isaya 30:21)

Miaka kadhaa iliyopita, John B. Youngberg na mke wake Millie walikuwa magotini, wakisoma na kudai ahadi zake katika maombi. John alikuwa ndiyo tu amemaliza shahada yake ya uzamivu na alisubiri kuitwa. Waajiri kadha walikuwa wamewasiliana naye kupitia katika konferensi kadhaa, lakini ni kama nafasi hizo hazikumvutia mke wake kwani yeye alikuwa ameajiriwa katika chuo kikuu cha Andrews. Je, Mungu atasikia maombi yao ili wapate nafasi karibu na chuo kikuu cha Andrews? Kadiri walivyoendelea kumsihi Mungu, kengele ya mlango iliita. Alipofungua mlango, profesa mmoja aliwaambia kwamba alikuwa ndiyo tu ametoka katika kikao cha kamati cha maprofesa katika idara ya Elimu, na kwamba walikuwa wamepitisha azimio kwamba John aajiriwe kwa ajili ya program ya Elimu ya Kidini (Religious Education Program). Mzigo wa kufundisha ulikuwa mwepesi muhula wa kwanza, na mkewe akapendekeza kwamba waanze semina za 'Maisha ya Familia,' ambayo yangeendeshwa hapo chuoni kwa semina za msimu wa kiangazi. Semina hizi zilizoitwa "Maisha ya Familia ya Kimataifa" zimeendelea kwa miaka 25 yenye matokeo mema hapa katika chuo kikuu cha Andrews, na kuwahudumia wanafunzi mbali mbali kuanzia ngazi ya sita ya kanisa la Waadventista wa Sabato. Je, Mungu alisikia na kujibu maombi yao? Naam! Kuliko walivyotazamia.

IBADA YA FAMILIA YENYE UFANISI INAKUWA NA MATOKEO GANI?

Umoja wa familia ni moja ya matokeo yenye ufanisi wa kudumu katika ibada ya familia. Kuna msemo uliozoeleka unaosema kuwa, "Familia inayoomba pamoja hubakia pamoja." Kielelezo cha jambo hili kinalinganisha familia na gurudumu la baisikeli lenye spoku zinazounganikia kwenye habu ya kati. Ile habu inamwakilisha Yesu. Wanafamilia ni mfano wa spoku. Kadiri spoku zinavyoelekea kwenye habu, zinazidi kusogeleana karibu. Vivyo hivyo, kadiri wanafamilia wanavyomsogelea Yesu – aliye kitovu kikuu – ndivyo wanavyozidi kusogeleana karibu na kuunganika kila mmoja na mwenzie.

Faida nyingine ni uimara wa jumuia ya kanisa, matokeo ya kawaida ya familia zilizojitoa kikamilifu kwa utukufu wa Mungu. Kadiri faida hizi zinavyozidi kufikia jumuia kwa mapana yake, ndivyo kuwafikia watu kwa ushuhuda wa Kikirsto kunavyokuwa na mguso katika kuinua jumuia. Ujumbe wa Eliya utarejesha kile kilichoharibiwa na utamaduni wa leo ulioanguka. "Wanafunzi wake wakamwuliza,

wakisema, Basi kwa nini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? Naye akajibu, akawaambia, Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote," (Mathayo 17:10-11). Ellen G. White anasema kuwa, "Kurejeshwa na kuinuliwa kwa ubinadamu kunaanzia nyumbani." (*Ministry of Healing,* uk. 349)

Kwa jinsi tulivyozungumza kuhusu vipengele mbali mbali vya ibada ya familia, unaweza kusema kwamba tumekuwa tukikusanya mawe yaliyovunjika ili tujenge upya madhabahu majumbani mwetu. Hiyo ni muhimu, lakini kadiri tunavyokusanya mawazo yetu pamoja, hebu turudi katika dhana muhimu. Ufunguo wa mafanikio katika ibada ya familia ni kuifanya ijikite katika Kristo. Kafara isiyokuwa na hatia, ikiwakilisha Mwanakondoo wa Mungu akiwa juu ya madhabahu. Anatukomboa kwa ajili yake mwenyewe, akiondoa dhambi zetu na kutuandaa kwa ajili ya ufalme wake wa utukufu.

Baba alikuwa akisafiri kikazi kwa siku kadhaa na kurejea tena nyumbani siku ya Ijumaa. Alikusanya familia yake kwa ajili ya ibada wakati jua likizama. Alijisikia kushiriki mafungu kuhusu kafara ya Yesu kama mada ya siku kutoka katika kitabu cha Isaya kwa namna binafsi, "Hakika (Yesu) ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona." (Isaya 53:4-5). Baba aliendelea kuelezea jinsi Yesu alivyotembea kwa maumivu makali nje ya kuta za Yerusalemu kwenda Kalvari, mahali ambapo wahalifu walisulubiwa.

Alishiriki na familia yake pia matamko saba ya Yesu pale msalabani. Matamko yake matatu yalikuwa ni kwa ajili ya wengine. Kwanza, kadiri maaskari walivyokuwa wakipigilia misumari kwenye minofu ya mikono laini na miguu ya Yesu, aliomba kuwa, "… Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake, wakipiga kura." (Luka 23:34). Matamko ya pili yalikuwa ni kwa yule mwizi pale msalabani mkono wake wa kulia aliyeamini kwamba Yesu alikuwa anasulubiwa kwa ajili ya dhambi zake, na hivyo akatubu. Yesu alimwambia kwamba, "Amin, nakuambia, leo hivi utakuwa pamoja nami peponi." (Luka 23:43). Kisha Yesu alipoona mama yake akitegemezwa na yule mwanafunzi aliyependwa, yaani Yohana pale chini ya msalaba, "…alimwambia mama yake, Mama, tazama, mwanao. Kisha akamwambia yule mwanafunzi, Tazama, mama yako." (Yohana 19:26, 27)

Baba aliendelea. Matamko yake manne yalimhusu yeye mwenyewe. Yesu alikuwa anateseka kwa ajili YAKO – Ralph, na Grace, na Bobby, na mimi na mama yenu. Alichukua nafasi yetu. Yeye alikuwa ni m-badala katika kipindi chote hicho cha maumivu na uchungu hakuweza kuona uso wa Baba yake, ingawaje Baba yake alikuwa karibu na msalaba, akiwa amefunikwa katika giza. Yesu alilia kwa sauti, "Eloi, Eloi,

lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Mathayo 27:46). Yesu alipoona kiu, aliomba maji kwa kusema "…Naona kiu." (Yohana 19:28). Hakuwa amekunywa maji tangu usiku ule kabla katika chumba cha ghorofani wakila pasaka. Aliona kiu katika hali yake ya kibinadamu ili tuwe na tumanini la kunywa kwa uhuru siku moja kutoka katika mto wa uzima kule mbinguni. Kisha kwa sauti nzito iliyotoa mwangwi katika viumbe vyote, Yesu alilia kuwa, "Imekwisha." (Yohana 19:30). Mpango wa wokovu kwa wenye dhambi wote ulikuwa umekamilika. Yule aliyekuja kutoka mbingu ili kumwokoa – Ralph, Grace, Bobby, Mama, Baba, na watu wote walioko duniani, alikuwa amefanikiwa. Shetani akawa adui aliyeshindwa! Ndipo alipoinamisha kichwa kilichokuwa kimebandikwa taji ya miiba kwa kukata roho, alirudia maneno ya mtunga Zaburi kuwa, "Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu." (Luka 23:46). Baba yetu alituangalia na kuona kwamba kulikuwa na machozi machoni pa watoto wake watatu, na machoni mwa mama pia. Akasema, "Lo, Yesu anatupenda kiasi gani kila mmoja wetu!" Ni furaha na tuamini gani tulilo nao kwa sababu ya kafara yake kuu!"

Kina mama, kina baba, na watoto walikuwa wanakaribia kuwa na "Ibada ya familia" tena. Hii haitakuwa katika dunia hii ya huzuni, bali itakuwa ni mbinguni. Yesu atakusanya pamoja "ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa" (Waefeso 3:15). Tambua "familia yetu yote" ambayo kwa miaka zaidi ya 6,000 ilikuwa imetenganishwa, sasa itaunganishwa hapo. Kisha kila goti litapigwa na kila ulimi utamkiri kwamba ndiye Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana! (Isaya 45:23, na Wafilipi 9:11)

KWA MOYO WAKO WOTE
MAISHA YOTE

NA JASMINE FRASER

AYA ZA MAANDIKO

Waefeso 6:1-4

"Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana,
maana hii ndiyo haki. Waheshimu baba yako na mama yako;
amri hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi, Upate heri, ukae siku
nyingi katika dunia. Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu;
bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana."

Torati 6:4-9

"Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.
Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa
roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo,
yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako
kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako,
na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.
Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako,
nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.
Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako,
na juu ya malango yako."

UTANGULIZI

Kisa kinaelezewa cha kijana mmoja aliyemvutia Jirani yake aliyekuwa mama wa makamo. Kila siku yule kijana alimsaidia yule mama kazi za hapa na pale katika uwanja wake, au kumsaidia kubeba mizigo kutoka kwenye gari lake. Siku moja yule mama kwa mshangao na hali kama ya udadisi alimuuliza yule kijana kuwa, "Mwanangu, uliwezaje kuwa kijana mzuri kiasi hiki?"

Kijana alijibu kuwa, "Nilipokuwa mvulana, nilikuwa na shida ya "kuburuzwa."

Kabla bibi hajauliza swali jingine, kijana aliendelea, "Unaona, wazazi wangu waliniburuza kwenda kanisani kwa ajili ya ibada ya Sabato, waliniburuza kwenda kwenye huduma usiku wa Jumapili, na kuniburuza kwenda kanisani kwenye mikutano ya maombi ya usiku.

Pamoja na kutiwa chumvi katika kisa hiki, kuna uhalisia wa jitihada za wazazi kuwalea watoto wao "katika adabu na maonyo ya Bwana." (Waefeso 6:4). Ninaamini wazazi wengi wanafanya kila wawezalo kukuza watoto wao katika namna ya kumpendeza Mungu. Lakini kadiri jamii inavyoingia katika zama za baada ya Ukristo, jukumu la malezi na maonyo ya watoto wao ili kumheshimu Mungu linazidi kuwa la kutisha.

Kitengo hiki cha familia kilianzishwa na kuwekwa wakfu na mbingu ili kuonesha na kuendeleza sifa za tabia ya Mungu, kuhifadhi utambulisho na ustawi wa kila mwanafamilia, na kutoa uongozi wa kutosha kwa ajili ya jamii iliyo thabiti.[10] Mahusiano ya familia yanajenga au kuvunja jamii. Baada ya muda tunaona ule utakatifu, wajibu, na kusudi la familia kuhatarishwa na hali tete ya maadili na viwango vya jamii. Hatimaye tunalazimika kutambua kwamba ni zaidi ya kuburuza, au kulazimisha watoto kwenda kwenye mazingira ya ibada ili kujenga mazoea ya kumheshimu Mungu.

Tunashtushwa na chunguzi zinazoendelea zinazodhihirisha kupungua kwa mahudhurio ya vijana makanisani. Vijana wengi na watu wazima wa umri wa kati wanaacha utiifu wao na kujiondoa katika dini zilizo katika mpangilio.[11] Kwenye mlipuko wa majanga yanayokumba dunia nzima, masuala ya familia yanakuwa magumu zaidi kadiri familia nyingi hasa zenye watoto wadogo, zinavyopambana na changamoto za mihemuko ya kiakili zinazoathiri mchakato wa ukuaji wa watoto na ubora wa mahusiano kati ya wazazi na watoto. Ni muhimu kwamba, kama kanisa tutafute namna ya kusaidia vijana wetu kurejea na kuthibitisha tena Imani yao katika Kristo na kubakia wakiwa wameunganika naye kupitia katika ibada ya pamoja. Wakati huo huo, ni muhimu kwamba sisi pia tuitikie kwa mahitaji ya wazazi walio na watoto wachaga, tukiwasaidia kupunguza changamoto za mihemuko ya kiakili na kuwawezesha watoto wao katika kukuza Imani ya kudumu na kujitoa kikamilifu kwa Kristo na jumuia ya Imani kwa ujumla.

---

[10] Gangel, K. O. (1977a). Toward a biblical theology of marriage and family: Part 1: Pentateuch and historical books. *Journal of Psychology & Theology*, 5(1), 55–69.

[11] Kinnaman, D., & Hawkins, A. (2011). *You lost me: Why young Christians are leaving church...and rethinking faith*. Grand Rapids, MI: Baker Books.

Uchunguzi umeonesha kwamba sababu moja inayochangia katika ukomavu wa Imani, maadili ya kudumu, na kujitoa kikamilifu kwa Kristo katika jumuia ya Imani ni mchakato mzima wa mawasiliano kati ya wazazi na watoto wao katika miaka ya ukuaji wao.[12] Uchunguzi pia umeonesha kwamba "mawasiliano ya familia yaliyo chanya yanaongoza katika kujenga maadili na uwezo wa kijamii kwa watoto."[13] Mara nyingi jitihada kubwa inawekwa ili kusaidia kuboresha mawasiliano kati ya wenzi katika ndoa. Hatimaye ni muhimu kwetu kuwapatia wazazi vitendea kazi vya kuwasaidia kujenga na kudumisha mahusiano hai na watoto wao.

MUKTADHA NA KUWEKA KATIKA UTENDAJI

Uhusiano kati ya mzazi na mtoto ni moja kati ya mahusiano yaliyo muhimu sana ambayo mtoto atapata uzoefu wake. Athari ya huu uhusiano inavuka ng'ambo ya kipindi cha utoto na kuathiri maendeleo kuelekea katika utu uzima, ikiwa ni pamoja na mahusiano ya ndoa.[14] Vigezo kama vile mwenendo wa wazazi, mtindo wa malezi wa wazazi, mtindo wa namna wazazi wanavyoambatana na watoto wao, na utendaji, vyote hivyo vina mguso katika ubora wa uhusiano uliopo kati ya mzazi na mtoto, na kuathiri ukuaji wa kiakili ulio chanya au hasi, kimhemuko na kiroho. Jinsi wazazi wanavyowajali Watoto wao na kuitikia kwa mahitaji ya kimwili, kimhemuko itaamua ubora wa uambatanisho wa kimhemuko wa mtoto pamoja na mabadiliko ya uhusiano wa mzazi kwa mtoto. Kimsingi, uhusiano wa mzazi kwa mtoto ni kigezo muhimu kinachoamua ubora wa maisha kipindi chote cha uhai wa kizazi.

Siyo jambo la kushangaza kwamba Biblia imejawa na maagizo kuhusu namna ya kukuza na kudumisha uhusiano unaotenda kazi wa mzazi kwa mtoto. Ingawaje mambo yanaweza kubadilika kulingana na kujaa na kupwa kwa utamaduni na jamii, Neno la Mungu halibadiliki. Linafaa kwa kuwaongoza wazazi katika kujenga uhusiano utendao kazi na kila mtoto.

Leo tutaangalia baadhi ya ushauri unaotolewa katika Biblia kuhusu mabadiliko ya uhusiano wa mzazi kwa mtoto, na mchakato mzima unaopendekeza jinsi ambavyo wazazi wanaweza kukuza na kudumisha uhusiano wenye ustawi na watoto wao. Hatimaye lengo letu ni kuwaandaa wazazi, na kuwasaidia katika kuwawezesha watoto wao kwa ajili ya kujitoa kikamilifu kwa Kristo na Kanisa maisha yao yote.

---

[12] Fraser, J. (2018). *Family relational dialectics: A systemic model for explaining relational factors contributing to adolescents' faith maturity, life values, and commitment to Christ* (Doctoral dissertation), Available from ProQuest Dissertations and Theses database. (UMI No: 10844479)

[13] LaBeach Pollard, P. (2012). *Raising a leader God's way.* Hagerstown, MD: Review and Herald. p. 23.

[14] Seegobin, W. (2014). The parent-child relationship – Chapter 4 from *"Christianity and Developmental Psychology: Foundations and Approaches."* p. 99. http://digitalcommons.georgefox.edu/gcp_fac/139

Moja ya aya katika Maandiko ambazo zinatumika mara nyingi kama mwongozo kwa uhusiano wa mzazi kwa mtoto ni Waefeso 6:1-4. Katika kutumia aya hizi, msisitizo kwa ujumla upo katika mafungu ya 1-3. Mara nyingi mkazo unawekwa katika haja ya watoto kuwa watiifu kwa wazazi wao kwa gharama yoyote. Lakini mara nyingi, fungu la 4 halitiliwi maanani. Hakuna shaka kwamba Mungu anawaagiza Watoto wawatii wazazi wao na hatimaye wamtii yeye mwenyewe. Lakini ni muhimu kuelekeza hapa kwamba moja ya sifa za uhusiano wenye ustawi ni ule ulio jumuishi. Ili kuendeleza hii hali jumuishi katika uhusiano, ni lazima kujali mahitaji ya pande zote za uhusiano. Kwa hiyo, mambo yanayojitokeza katika uhusiano wa mzazi kwa mtoto, yasifanywe kuwa ni jukwaa la wazazi kuweka sheria na mipaka kwa watoto wao. Badala yake ni lazima kuwepo na kiwango cha kubadilishana kwa namna ya kushibana kati ya mzazi na mtoto.

Hali jumuishi katika uhusiano wa mzazi kwa mtoto inajengwa katika "hali ya kujaliana na kuheshimiana pamoja na mawasiliano yaliyo wazi."[15] Maana yake ni kwamba, wazazi wamekaimishwa jukumu la kutengeneza mazingira salama ambapo mahitaji ya watoto yatatimizwa kwa utoshelevu, mambo yanayowahusu na shauku zao zimethibitishwa na kushughulikiwa, na kwamba wanajenga Imani yao kwa wazazi wao. Imani ni muhimu katika kubadilishana uhusiano kati ya wana familia na uhusiano ambao kila mmoja anajenga na Mungu wake. Wakati huo huo, Watoto wanatakiwa kunidhamishwa katika utii kwa wazazi wao. Zaozi la ujumuishi katika uhusiano kati ya wazazi na watoto limeunganishwa na masuala machache ya tabia, na kuongeza ustadi wa kijamii.[16] Hatimaye, wazazi na Watoto watanufaika kiakili, kimhemuko, na kiroho katika zoezi hili la ujumuishi.

Ni muhimu kufahamu kwamba mfano halisi wa ujumuishi imewekwa katika Maandiko. Biblia inatumia lugha ya malezi kuelezea "uhusiano kati ya Mungu Muumba na viumbe"[17] kwa kuweka jukumu la baba kwa Mungu. Ushuhuda wa ujumuishi wa mzazi kwa mtoto unaonekana katika Maandiko kupitia katika wito wa "Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana" na katika mchakato huo, kupata uzoefu wa ule upendo wake wa Baba na huruma yake (Isaya1:18; Zaburi 103:13; 2 Wakorintho 6:18). Ukija kwa Mungu Baba na kupata uzoefu wa ala za muziki zilizochanganyika kimbingu na kibinadamu tunajenga msingi wa uhusiano wa wazazi na watoto wao. Mahusiano ya wazazi na Mungu ama Baba ni muhimu kadiri wanavyojitahidi kuwaelekeza na kuwaongoza watoto wao katika njia ya Bwana. Haiwezekani

---

[15] Seegobin W. (2014). p. 101.

[16] Deater-Deckard, K., Atzaba-Poria, N., & Pike, A. (2004). Mother- and father-child mutuality in Anglo and Indian British families: A link with lower externalizing problems. *Journal of Abnormal Child Psychology,* 613, 616.

[17] Balswick, J. O., Balswick, J. K., and Thomas, F. V. (2021). *The Family: A Christian Perspective on the Contemporary Home.* Grand Rapid: MI. p. 6.

kufundisha kuhusu mada usiyoifahamu, au kumtambulisha mtu ambaye haumfahamu. Vivyo hivyo ni vigumu kwa mzazi kumfundisha mtoto wake kumhusu Mungu ambaye hana uhusiano naye.

Wazazi kadiri wanavyozidi kuingiza utendaji wa ujumuishi katika uhusiano na kila mtoto, wanahimizwa kuakisi katika mfano huu wa Biblia wa uhusiano wa mzazi kwa mtoto. Hebu uzoefu wako na Baba wa mbinguni ukuongoze jinsi ya kukabiliana na kila mtoto.

Aya nyingine za Maandiko ambazo ni za msingi katika kuelewa utendaji wa uhusiano hai kati ya mzazi na mtoto zinapatikana katika Torati 6:4-9. Mafundisho kadhaa ya namna wazazi wanavyoweza kuwafanya watoto wao kuwa wanafunzi yamejaa katika aya hizi. Kwa muktadha huu, tutajielekeza katika dhana tatu ambazo ninaamini ni muhimu katika kuwasaidia wazazi wanapokabiliana na watoto wao katika uhusiano. Dhana hizi zimebeba wajibu wa wazazi wa:

- Kumsikiliza Mungu
- Kumpenda Mungu
- Kuwafundisha Watoto.

KUMSIKILIZA MUNGU

Fungu la 4 katika Torati 6 linatoa mwangwi kwa sauti kuu ya wito wa kumsikiliza Mungu: "Sikiza, Ee Israeli!" Ni muhimu kutambua kwamba wito huo siyo kwa wazazi pake yao; bali pia ni wito kwa taifa zima la Israei na hatimaye ni wito wetu sisi sote. Wito wa kusikiliza ni msingi wa kusudi zima la maisha ya mwanadamu. Kusikiliza kunatoa mwelekeo au maagizo ya jinsi ya kuwa au kutenda kuhusiana na agizo maalum. Mwitikio wetu kwa wito wa kusikiliza unaweza kuwa wa hiari, kwa kuchagua. au kwa kuitikia. Mwitikio wa hiari ni sifa ya asili ya milango mitano ya fahamu (kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusikia). Tunasikia sauti za watu kwa hiari kadiri tunavyotembea kila siku. Tunasikia sauti za ndege au mtikisiko wa matawi upepo unapovuma, lakini mara nyingi hatuitikii moja kwa moja kwa kile tunachosikia kwa muktadha huo.

Ngazi nyingine ya kusikia ni ile ya uchaguzi: huu ni mchakato ambao unatufanya tuchague kusikia kitu fulani tunachopenda au kilicho muhimu kwetu na mara nyingi tunachuja kile ambacho hatutaki. Mzazi anasikia kicheko cha furaha au kilio cha mtoto kwa ukali kuliko sauti zingine zinazosikika katika uwanja wa mpira au katika kusanyiko. Kusikia kwa kuchagua, mwitikio wetu mara nyingi unajengeka katika haja yetu au matokeo yanayotazamiwa kulingana na hali husika.

Ngazi ya tatu ya kusikiliza ni kule kusikiliza kwa shauku au kwa kuitikia: mchakato wa kuwa makini kiakili, na kiroho kwa namna tunavyowasiliana na haja ya kutenda kwa kuitikia kile tunachosikia. Kwa muktadha huu, tutajielekeza katika kusikiliza kwa kuitikia kadiri tunavyotafuta kuelewa kile kinachowasilishwa katika fungu la 4. Musa aliyekuwa mtumishi wa Mungu aliwaambia Israeli kusikia, kusikiliza kimwili na kiakili ili kutambua kile kilichokuwa kikiwasilishwa, kwa nia ya kutenda kwa utiifu kile walichosikia. Wito wa kusikia ulikuwa ni wito wa kuwa sehemu ya; kufanya hivi, kulithibitisha utambulisho wao kama watoto wa Mungu. Lakini huo pia ulikuwa ni wito wa kurejea na kutafakri kuhusu Yeye aliye Mungu wa kweli. Israeli kama taifa walipokaribia kuingia katika nchi ya ahada, mazingira yaliyokuwa yamejawa na miungu na ibada za sanamu. Walihitaji kukumbushwa kumhusu Mungu ambaye wao, walikuwa ni mali yeke, na yeye aliyekuwa mwaminifu katika kuwahudumia katika hali zote za maisha yao. Walihitjai kukumbushwa ili wasije wakamchanganya huyu Mungu wa kweli na sanamu za vinyago katika ile nchi ya ahadi.

Kama vile Waisraeli wa kale, hapa kuna wito kwetu sasa kadiri tunavyosoma Neno la Mungu na kuwasiliana naye kwa maombi. Huu wito maalum wa kumsikia Mungu ni wito wa kila mmoja, pamoja na wazazi ambao wanatamani kuwaleta watoto wao katika kupenda maonyo ya Mungu. Katikati ya kelele za tamaduni zetu na jamii zetu, wakati mwingine ni vigumu kusikia kwa usahihi kile ambacho Mungu anatuambia. Kwa sababu hii, ni lazima tudhamirie kufundisha masikio yetu ya kiroho kusikia kile ambacho Mungu anamwambia kila mmoja wetu katika mazingira husika.

Tunaweza kufundisha masikio yatu ya kiroho kumsikia Mungu kupitia katika kusoma Neno lake kwa makini kwa sababu, "Neno lako ni taa ya miguu yangu, Na mwanga wa njia yangu." (Zaburi 119:105). Tunafundisha masikio yetu pia kumsikiliza Mungu kadiri tunavyopata muda wa kupumzika na kupata nyakati tulivu na Mungu. Kupitia katika Maandiko ya uvuvio, tunakumbushwa kwamba: Ni lazima kila mmoja kumsikiliza Mungu akiongea na mioyo yetu. Pale sauti zingine zinaponyamazishwa, na kwa utulivu kusubiri mbele yeke [Mungu], utulivu wa nafsi utafanya sauti ya Mungu kutambulika zaidi. Anatuambia kuwa, "Acheni, mjue ya kuwa Mimi ni Mungu, Nitakuzwa katika mataifa, nitakuzwa katika nchi." (Zaburi 46:10). Hapo ndipo mahali pekee ambapo pumziko la kweli linaweza kupatikana. Na haya ndiyo maandalizi ya ufanisi yanayoweza kufanywa kwa wale wote wanaofanya kazi kwa ajili ya Mungu. Katikati ya mahangaiko ya kutafuta shilingi, na maumivu ya shughuli za maisha, nafsi itakayohuishwa itazingirwa na angahewa lenye nuru na amani. Uhai utatoa harufu nzuri, na utadhihirisha nguvu ya kimbingu ambayo itaifikia mioyo ya watu.[18]

[18] White, E. G. (1898) *The Desire of Ages.* Mountain View, CA: Pacific Press Publishing. p. 363.

KUMPENDA MUNGU

Kufuatia wito wa haraka wa kusikia, kuna agizo la kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Katika agizo la kupenda, ni lazima tuhakikishe hatukosi msisitizo wa upeo wa kumpenda Mungu. Wito wa kumpenda Mungu kwa upeo mkubwa unaonesha matendo ya ibada na utii, ambayo yanafahamika na kusukumwa na uwezo wetu wa akili na mhemuko. Kumpenda Mungu kwa upeo mkubwa pia ni kumzoea, kuvutiwa naye na kutamani kuwa naye; ni wito wa kumfurahia. Kumpenda Mungu kunamaanisha kuelekeza mawazo yako katika huba ya upole; ni pamoja na kujiambatanisha kwake kumhemuko na kutamani kuishi kwa kusudi mbele zake. Kumpenda Mungu kwa upeo mkubwa kunamaansiha kuwa, Mungu amekuwa ni mwelekeo pekee wa uaminifu na ibada yetu.

Mwito huu wa kupenda unatuvuta kutoka kwenye mambo mawili makubwa: Kukiri kwa kurudia rudia upendo wa Mungu bila shauku wala msukumo; na shauku bila utii kwa agano. "Pale upendo wa kweli kwa Mungu unapodhihirika moyoni, utaonekana mtu anavyojali mapenzi yake na katika kutunza amri zake kwa uadilifu."[19] Wazazi na watoto wameitwa kwa namna moja kumpenda Mungu kwa upeo mkubwa, lakini jukumu la wazazi kwa agizo hili lina athari ya muda mfupi na muda mrefu katika uwezo wa watoto wao kumpenda Mungu kwa upeo mkubwa. Kile wazazi wanachofanya kinakuwa ni kielelezo kinachoonekana kwa watoto wao, na ni rahisi kwao kudaka kile wanachoona kwa urahisi kuliko kile wanachoambiwa. Hatimaye, kama wazazi wataitikia kwa shauku kubwa upendo wa Mungu, uzoefu wao utakuwa na mguso kwa mahusiano na watoto wao, na kutumika kama mfano wa ukuaji wa mtoto katika kumpenda Mungu.

KUFUNDISHA WATOTO WAKO

Baada ya kutikia wito wa kusikia na kumpenda Mungu, wazazi wanakaimishwa jukumu la kuwafundisha watoto wao. Wanatakiwa kuandika amri za Mungu kwa namna tambuzi na kwa upeo fanisi ndani ya watoto wao. Kwa kufanya hivyo, wanatapewa wajibu wa kuendeleza mahusiano ya agano walilo nalo na Mungu kwa watoto wao. Inavutia kutambua kwamba fungu la 6 linaonesha kwamba Mungu aliwaagiza Waisraeli kuhifadhi mioyoni mwao kile alichowaambia. Kuhifadhi moyoni ni kuthamini na kuchukulia kwa hali ya juu katika maisha. Walitakiwa kuthamini ahadi za Mungu na uzoefu wao kwa jinsi nguvu zake zilivyokuwa zikijidhihirisha katika maisha yao. Baada ya kufanya hivyo, walitakiwa kuwafundisha watoto wao kwa bidii. Kupitia katika mwitikio binafsi kwa wito wa kumsikia Mungu na kumpenda kwa upeo wa juu, wazazi sasa wanakuwa ni vilelelezo ambavyo watoto wao watatumia katika

[19] Spence-Jones, H. D. M. (1909). *Deuteronomy*, The Pulpit Commentary. New York, NY: Funk & Wagnalls, p. 119

kutafsiri mafundisho yanayotolewa kwao na kukua katika elimu yao wakimfahamu Mungu.

Katika kuweka uzito kwenye mvuto wa wazazi na jukumu lao kwa ukuaji wa kiroho wa watoto na usatawi wao kwa ujumla. Ellen G. White anapendekeza kwamba, "inategemea na mzazi mwenyewe" na kwamba "katika kukuza kile ambacho ni bora kwao wenyewe, wanaweka mguso na mvuto wa kuumba jamii na kuendeleza kizazi cha baadaye.[20] Kupitia katika mafundisho wanayotoa, wazazi wanahamisha uzoefu wao wa muda mrefu wa uaminifu wa Mungu kwa watoto wao na ule Ushahidi wa ibada kwake.

Wito wa kuwafundisha watoto amri za Mungu unarudiwa rudiwa, na katika maeneo tofauti ukipendekeza umuhimu na mguso wa kudumu wa mafundisho ya Mungu. Mafundisho kama hayo, yanahitaji muda mrefu wala hayategemei muda wa ibada siku ya Sabato tu, au ibada za jumapili usiku na maombi ya Jumatano. Hautegemei ibada za asubuhi na za jioni katika madhabahu za familia. Mafundisho ya Mungu yanabadilika, yanateka mawazo, na kuleta utambuzi, yana ufanisi na uwezo wa kitabia kwa maendeleo ya mtoto. Mafundisho haya yanategemeza uhusiano wa agano ambalo linatuunganisha sote kwa Mungu maisha yetu yote na kuvuka katika vizazi vyote.

Maagizo ya kufundisha watoto kwa mbinu mbali mbali, maeneo na muktadha unaoonesha kwamba Mungu anatakiwa kuheshimiwa na kutukuzwa katika nyanja zote za maisha yetu. Uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako, ikionesha kwamba walitakiwa kuacha Neno la Mungu liongoze kila fikira na matendo. Kuandika Maneno ya Mungu katika miimo ya milango ni kufanya amri zizame katika uzoefu wa maisha kwa kudumu. Katika utamaduni wa leo, ni jambo la kawaida kwa Wakristo kutenga maisha yao katika hali ya ukiroho na kidunia; huu ni mchakato unaohusu Kristo na baadhi ya utendaji wa viwango vya Kikristo kupuuzwa katika hali fulani za mkabala wa maisha. Mwitikio wa kufundisha na hivyo kumheshimu Mungu katika nyanja zote za maisha yetu unafedhehesha dhana na utendaji wa kutenganisha maisha ya kiroho ya Mkristo kutoka katika maisha ya kidunia. Mungu anataka kuwa hai katika maeneo yote ya maisha yetu.

[20] White, E. G. (1952). The Adventist Home: Counsels to Seventh-day Adventist Families. Southern Publishing Association, Nashville TN. p. 172.

HITIMISHO

Kwa muktadha huu, tumejadili umuhimu wa uhusiano hai tendaji wa mzazi kwa mtoto na mchango wake katika ustawi wa kiakili, kimhemuko na kiroho kwa wazazi na kwa watoto pia. Uimara wa mahusiano haya unawezeshwa kupitia katika kukabiliana kwa pamoja katika mchakato wa mawasiliano kati ya wazazi na watoto, na mwitikio wa wazazi katika "kumsikia" na "kumpenda" Mungu kwa upeo wa juu. Kadiri mfano wa wazazi unavyojirudia kimantiki katika mkabala wa uhusiano na watoto wao na kuitikia kwa utii mkamilifu wito wa kumsikiliza na kumpenda Mungu, uzoefu huu unachangia katika maendeleo chanya ya watoto kiakili, kimhemuko na kiroho, na kutumika kama utendaji ulio bora kwa uanafunzi wa familia.

Namna moja rahisi ambayo sisi kama kanisa tunaweza kusaidia katika huu mkabala wa uhusiano wa wazazi na watoto, ni kujenga mazingira ambamo wazazi wanalelewa kiroho na kimhemuko. Ninaamini kwamba pamoja na huduma maalum tuliyo nayo kwa ajili ya watoto, vijana wadogo, wanawake na vijana wakubwa, tunaweza pia kuwa na huduma ya wazazi au mkazo kwa uanafunzi. Kupitia katika huduma kwa wazazi, tunaweza pia kutegemeza akina mama na akina baba katika kuanzisha dhana ya utendaji unaojirudia katika uhusiano wao na watoto wao.

Lengo la huduma ya wazazi au uanafunzi ni kusaidia wazazi kukua na kufurahia uzoefu wao na Mungu. Kama matokeo ya uzoefu huu, wazazi watajengwa kuwa chanzo cha msingi cha uanafunzi wa watoto wao. Huduma ya wazazi au uanafunzi inaweza kufanyika kwa mfano wa moduli yenye kuhusiana kwa kufuatana kwa sehemu tatu; yaani uhusiano wa kanisa-wazazi, wazazi-watoto, na kanisa-watoto.[21] Maana yake ni kwamba tunawekeza katika kulea wazazi, kuwawezesha kulea Watoto wao kiroho na kimhemuko, na kupitia katika huduma yetu kwa Watoto, tunathibitisha kile kilichowekwa ndani yao na wazazi.

[21] Fraser, J (2018). p. 166-179.

SAFARI YA
KUKATA TAMAA

NA RICK McEDWARD

AYA ZA MAANDIKO

Isaya 6:1

"Katika mwaka ule aliokufa mfalme Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu."

Mathayo 25:37-40

"Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema,
Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu
tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha,
au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au
kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia,
Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea."

Jina lake ni Ahmed* mzaliwa wa Siria. Alipokuwa umri wa miaka saba, vita nchini kwao ilikuwa haistahimiliki kwa familia yake. Kijiji chao kilikuwa katika eneo la mstari wa mbele wa vita na hivyo, kulala usiku ilikuwa vigumu kwa sababu ya milipuko ya bunduki iliyokuwa ikisikika, na mara nyingine mabomu yaliyokuwa yakianguka karibu na nyumba yao. Alijua kuwa kifo siyo kitu ambacho wazazi wake walikuwa wamemwandalia, lakini kila alipogeuka alikiona. Wazazi wao kwa hofu kwamba pengine watoto wao wangechukuliwa kwenda kupigana hiyo vita ya "Islamic State" walifanya uamuzi mgumu… waliamua kuondoka katika maisha yao ya kipato cha kati, kuacha nyumba yao, samani zote, ajira, shule, marafiki, na hata ndugu wa karibu, na kukimbia vitisho vya vita, hadi mahali salama ambapo wangeweza kukuza familia yao.

Wakati wakitoroka, Ahmed na familia yake walipanda basi kwenda Dameski, lakini kabla hawajafika mpakani, wavulana wadogo walifichwa kwenye vifurushi na kufunikwa kwa maboksi wakitarajia kwamba hawatagundulika. Waliomba kuwa, "Ee Mungu mwenye rehema, walinde Watoto wetu leo." Baada ya kuvuka mpaka, wazazi

na watoto walishusha pumzi, machozi yakijaa machoni mwa wazazi, walikuwa wamevuka mpaka kwa mafanikio na kuingia Lebanon, mahali ambapo walitazamia kuwa huru kutoka katika hofu ya vita.

Walipofika, waliwasiliana na familia walizokuwa wanafahamiana nazo kabla. Walikaribishwa, wakakaa na familia zingine tatu kwenye eneo la kuhifadhi vitu lililokuwa na vyumba viwili, ambavyo havikuwa na dirisha.

Baba yake Ahmed alihangaika sana ili kupata hadhi ya kuwa mkimbizi, hatimaye alijiorodhesha katika shirika la Umoja wa Mataifa kama mkimbizi na kuanza mchakato mrefu wa miaka kadhaa wa kutafuta jinsi ya kwenda nchi za magharibi kutafuta mahali papya atakapopaita nyumbani.

Wakati wote huo familia ilikuwa ikiishi kwa kubangaiza, na kila mwana familia alitakiwa kuchangia. Ilikuwa vigumu kupata kazi, hasa kwa wakimbizi. Lebanon ilikuwa imekaribisha wakimbizi zaidi ya milioni moja kutoka Siria kwa kipindi cha miaka miwili, na kwa hiyo jinsi ya kuzalisha kipato ikawa changamoto.

Shule zilikuwa nje ya mipaka kwa wakimbizi na gharama zake kuwa za juu kwa familia zilizokuwa zikihangaika kupata mkate wa siku. Ahmed na wadogo zake walicheza muda mwingi mitaani na kwenye vichochoro katika ujirani, wakati mwingine waliingia katika mkanganyiko na wenye maduka. Siku moja walisikia kuhusu shule kwa ajili ya watoto wa wakimbizi pekee. Wazazi waliwahi kuandikisha Watoto wao, lakini walikuta tayari kuna wakimbizi 130 waliokuwa wamewahi. Ahmed na dada yake waliitwa kwenda kufanya mtihani wa kufuzu kuandikishwa.

Wakati wakifanya mtihani huo, mama yao alikuwa nje akisubiri kwa hofu. Watoto waliporudi, mmoja wa waalimu aliyekuwapo wakati Ahmed na dada yake wakifanya mtihani alisema, “Una watoto wazuri, wanaweza kuanza masomo juma lijalo.” Mama yao alitoa machozi kwa furaha akimshukuru Allah kwa fursa hiyo ya watoto wao.

Kipindi chote cha shule ya msingi, Ahmed na dada yake walihudhuria Kituo cha Mafunzi cha Waadventista katika Bourj Hammoud, jirani tu na Beirut. Katika shule hiyo, Ahmed alikutana na waalimu wazuri sana waliompatia elimu, stadi za maisha, na kumwonesha njia chanya ya maisha. Katika kituo hicho cha mafunzo, aliweza kukua na kuwa mtu wa nuru.

Hivi karibuni nilikutana na Ahmed, nikamuuliza kuwa angependa kufanya nini katika maisha yake. Alijibu kuwa, “Ninataka kuwa daktari au mtafsiri, lakini pamoja na hivyo ninavyotaka kuwa, ninataka kufanya kila kinachowezekana kumtumikia Mungu na wanadamu wengine.”

Sikuweza kuhimili tabasamu langu pale mtu mmoja wa makamo alipotusogelea wakati nikiwa ninaongea naye, "Huyu kijana anafaa. Tunataka vijana kama huyu, shukurani ziendee shule ya Waadventista iliyopo hapa."

Kwa sababu ya vita, njaa, majanga, na ugumu wa uchumi kulingana na Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) kulikuwa na watu milioni 84 waliolazimishwa kuwa wakimbizi duniani. Wengine takribani milioni kumi hadi kumi na tato wameacha nyumba zao kama matokeo ya vita vya Ukraine, na kusababisha idadi ya wakimbizi duniani kukaribia milioni 100. Karibia mtu mmoja kwa kila watu 75 duniani ameondoka nyumbani kwake kwa sababu ya mazingira yaliyo nje ya uwezo wake.

Sisi kama watu wa Mungu tunatakiwa kuitikiaje kwa familia zilizo katika mgogoro? Tunatakiwa kufanya nini kwa janga hili la kuhamishwa bila ridhaa? Je, Yesu angeitikiaje kwa kilio cha familia hizo zilizo katika mgogoro?

Tunapata muonjo tu wa mtazamo wa kristo kwa watu walio katika mgogoro anapotangaza huduma yake. Yesu alitupatia muhutasari wa utume wake katika Luka sura ya 4:

> 16 Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.
>
> 17 Akapewa chuo cha nabii Isaya, akakifungua chuo, akatafuta mahali palipoandikwa,
>
> 18 Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru waliosetwa,
>
> 19 Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa.
>
> 20 Akakifunga chuo, akamrudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho

Yesu akinukuu kutoka katika Isaya 61:1, 2 alielekeza utume wake kwa watu waliokuwa masikini, waliovunjika moyo, waliotekwa, vipofu, na waliosetwa. Hii inatuongoza katika swali kwamba: watu hawa wanawakilishwaje katika maisha yangu na katika kanisa langu? Je, ninawaonaje, na ninaonaje hali yao? Je, ninawaona waliotelekezwa kama watu wanaostahili kupendwa au kupuuzwa?

Lakini, kwa nini Yesu alikuwa anazungumza kuhusu huduma kwa watu walioachwa na kuwa katika hali ya chini, unadhani hili lilikuwa ni jambo jipya? Hebu tuliangalie hili kwa undani.

Tangu dhambi ilipoingia duniani, mwanadamu ameonekana kama mkimbizi, mtu wa kutangatanga, mpitaji na mgeni. Uchungu wa Kaini aliyesema kuwa, "Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki." (Mwanzo 4:13). Hata katika dhambi hii na kukataliwa kwake, Kaini aliwekewa alama ili yeyote atakayekutana naye asimuue. Hata kama Kaini hakumfurahisha Mungu, bado Mungu alifanya namna fulani ya ulinzi kwake. (Mwanzo 4:15)

Katika wakati fulani wa maisha yao, baadhi ya wahenga wanaonekana kama wageni na wapitaji, wasio kuwa na makazi maalum. Abraham aliyekuwa mtu wa Agano na Mungu akaondoka Harani, akavuka mataifa mengi kabla ya kufika katika nchi ya ahadi. Yakobo na wazawa wake wakawa wageni katika nchi ya Misri kama matokeo ya njaa, na wakahifadhiwa na Farao huko. Kisa cha Yusufu hasa ni kisa kinachoumiza na ni kielelezo cha mahangaiko ya mwanadamu anayeishi mbali na nchi ya nyumbani.

Kwa namna kisa cha Yusufu kinavyoumiza, mwisho wa kitabu cha Mwanzo una kumbukumbu zenye mwarobaini wa hisia hasi. Baada ya Yakobo kufariki, ndugu zake wanaingiwa na hofu kwamba pengine Yusufu atalipiza kisasi kwa vile walivyomuuza kama mtumwa kwa wafanya biashara wa mashariki. "Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo." (Mwanzo 50:20)

Kwa namna isiyo ya kawaida Mungu alitumia mazingira magumu ya maisha ya Yusufu ya kuuzwa na familia yake mwenyewe kama mtumwa, kushtakiwa kwa uongo, kufungwa, na kusahauliwa kabisa, kumbariki katika nchi ya ugeni na kuruhusu awe Waziri mkuu kwa wale wale ndugu zake waliomuuza. Ushairi wa haki wa Mungu unatuonesha kwamba ukuu wa kimbingu upo kazini hata katika mazingira yanayochochewa na migogoro.

Kisa cha Yusufu kinatoa kielelezo kwamba mazingira ya ulimwengu huu uliovunjika na kujawa na wasiwasi, siyo kusudi la Mungu kwa uumbaji wake. Hitaji halisi la Mungu ni kutupatia furaha.

Visa vya wageni waliokuwa katika kusafiri kwao, havikamiliki bila kutambua kisa cha "Kutoka" pale taifa la Israeli lilipogeuka likawa na umaarufu wa kutangatanga katika Maandiko wakati wa safari ya miaka arobaini ya kukatisha tamaa. Walipokuwa wakiingia katika nchi ya ahadi, walikumbuka ugeni wao na kuwakumbuka wengine walioko katika hali kama ya kwao. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati kina taarifa ya

sadaka ambazo Waisraeli walitakiwa kutoa baada ya kuingia katika nchi ya ahadi. "Naye kuhani atakipokea kikapu mkononi mwako, akiweke chini mbele ya madhabahu ya Bwana, Mungu wako. Nawe ujibu, ukaseme mbele za Bwana, Mungu wako, Baba yangu alikuwa Mwarami karibu na kupotea, akashuka Misri, akakaa huko ugenini, nao ni wachache hesabu yao; akawa taifa kubwa huko, yenye nguvu na watu wengi." (Torati 26:4-5)

Katika historia yote ya Waisraeli, walipitia katika uzoefu wa ukimbizi! Walifahamu hali ya wale ambao wamepoteza mahali panapoitwa nyumbani, au kuhamishwa kwa sababu tu ya utashi wa watawala wa mabavu au hali ya vita.

Kama matokeo ya ugeni wao, Mungu alipowapatia Israeli sheria, aliweka pia sheria ya ukarimu ya kushughulikia wasafiri na wageni kana kwamba walikuwa ni sehemu ya familia yao. Mungu anawaelekeza Israeli katika historia yao ya kuwa wasafiri na wageni, jinsi walivyokaribishwa, wakatendewa kwa wema na kulishwa. Ukarimu kwa wasafiri na wageni ikawa ni sehemu muhimu ya kuangaza nuru kwa Mungu kupitia kwao, kwa kuwatendea wengine kwa neama.

Baada ya Mungu kuwapatia amri kumi, aliwapatia pia sheria ambazo zilijengeka katika zile amri kumi. Kwa namna fulani kila moja ya amri kumi iliwekwa katika mkao na namna ambayo ingefanya Israeli kuwa ni taifa lenye haki, likiwakilisha wema na upendo wa Mungu kwa mataifa mengine. Baadhi ya sheria zilizotolewa zililenga mahususi wasafiri na wageni.

- "Usimwonee mgeni; maana, ninyi mwajua moyo wa mgeni ulivyo, kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri." (Kutoka 23:9)

- "Usimwonee mgeni, wala kumtendea jeuri; kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri." (Kutoka 22:21)

- "Usimwonee mgeni, wala kumtendea jeuri; kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri. Usimtese mjane ye yote aliyefiwa na mumewe, wala mtoto yatima." (Kutoka 22:21, 22)

- "Nawe utafurahi mbele ya Bwana, Mungu wako, wewe na mwana wako na binti yako, na mtumwa wako na mjakazi wako, na Mlawi aliye ndani ya malango yako, na mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe, walio katikati yako, katika mahali atakapochagua Bwana, Mungu wako, apakalishe jina lake." (Torati 16:11)

- "Basi, mpendeni mgeni, kwa sababu ninyi wenyewe mlikuwa wageni katika nchi ya Misri." (Torati 10:19)

- "Mgeni akaaye pamoja nawe atakuwa kama mzalia kwenu; mpende kama nafsi yako; kwa maana ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya Misri; Mimi ndimi Bwana, Mungu wenu." (Walawi 19:34)

- "Na alaaniwe apotoaye hukumu ya mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe. Na watu wote waseme, Amina." (Torati 27:19)

Hili ni jambo la kushangaza kwamba watu ambao mara nyingi wanahisi kutelekezwa na jamii, Mungu anaagiza watu wake kuwabariki na kuwainua? Wajane, Yatima, Wageni, wote walikuwa ni sahemu ya mpango wa Mungu. Kwa kweli sheria za Israeli zilikuwa ni sheria za haki ambazo zingewavutia mataifa mengine, kwa sababu zilitoa kielelezo cha Mungu mwenye haki. Ni ajabu kile ambacho Mungu anawaambia watu wake katika Torati 4:6-8 kuhusu sheria ambazo aliwapatia kwa ajili ya ustawi wao na kama kivutio kwa mataifa yaliyokuwa yakiwazunguka.

> 6 Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako;
>
> 7 nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo.
>
> 8 Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.

Kama Israeli wangeshika amri na kutunza sheria za Mungu ipasavyo, mataifa mengine wangesimama na kumshangaa Mungu wa Israeli kwa sababu ya sheria za haki za watu wake.

Miji ya wakimbizi ilitengwa ili kuwalinda wale ambao walijikuta wamewadhuru wenzao bila kukusudia ili haki isije ikatendwa kwa kifo cha bahati mbaya. (Hesabu 35).

Mungu aliwalinda wale waliotengwa na jamii. Kwamba watu wake walikuwa wasafiri na wageni ili wapate kuwakumbuka wale walio safarini mbali na nyumbani kwao. Kwamba Mungu ametoa kwa namna ya pekee kwa ajili ya ukarimu. Mara nyingi wageni wanatajwa katika aya hizo ambapo yatima na wajane wanatajwa. Kwamba Israeli wangeweza kuwakaribisha wasafiri ungekuwa mbaraka kwao, kama namna ya kumdhihirisha Mungu kwao. Makundi yote ya watu ambao Mungu aliwajali na kuwalinda, walikuwa ni familia zilizokuwa katika mgogoro.

- Wajane – wamepoteza wenzi wao

- Yatima – wasiokuwa na wazazi ambao wangewakuza.
- Wageni – wasafiri kwa ajili ya biashara, au majukumu mengine.

Lakini katika siku zao, safari ilikuwa ni ndefu na huduma kwa wasafiri ilikuwa ni huduma iliyofanyika kwa uchache sana. Neno wageni linaonesha dhahiri kwamba wale hawakuwa ni wa taifa lao, kabila lao, au dini yao.

Ni rahisi kwetu kuhisi huruma kwa wale ambao tunafanana nao, lakini utendaji wa Mungu ni kuhisi huruma kwa watu tusiofanana nao wala walio wa dini zetu. Biblia inahimiza waumini kukaribisha kama namna ya kudhihirisha upendo wa Mungu kwa wale wasio waumini.

Wasafiri waliruhusiwa kushiriki katika Pasaka, lakini kama tu wangekuwa wametahiriwa. Tohara ilikuwa ni ishara kwamba wageni walikaribishwa kuwa sehemu ya watu wa Mungu wa agano na kumwabudu Mungu kupitia katika sherehe za kufunguliwa. Ni dhahiri kuwa wasiokuwa Wayahudi walikaribishwa katika uhusiano na Mungu na kufurahia upendeleo wake pamoja na watu wake waliochaguliwa.

Sheria za Israeli zilitengenezwa kudhihirisha tabia ya Mungu kwa mataifa. Sheria za Mungu kwa Israeli zilikusudiwa kuonesha utukufu kwa mataifa kupitia katika haki na rehema. Kama Israeli wangefuata na kutii sheria hizo, wangevuta mataifa mengine kumwabudu Mungu. Bahati mbaya manabii wa Agano la Kale wanazungumza wazi wazi kuhusu uhamisho na jinsi Israeli walivyoshindwa kumfuata Mungu, na jinsi walivyonyanyasa masikini, wajane, na yatima. Mungu aliwahukumu watu wake, kwa sehemu kwa ajili ya kupuuza sheria zake za haki kwa familia zilizokuwa katika mgogoro.

- "Maana kama mkitengeneza kabisa njia zenu na matendo yenu; kama mkihukumu hukumu ya haki kati ya mtu na jirani yake; kama hamwonei mgeni, wala yatima, wala mjane, wala kumwaga damu isiyo na hatia mahali hapa, wala kuifuata miungu mingine kwa hasara yenu wenyewe; ndipo nitakapowakalisha mahali hapa, katika nchi hii niliyowapa baba zenu, tokea zamani hata milele." (Yeremia 7:5-7)

- "Tena itakuwa mtaigawanya kwa kura, kuwa urithi kwenu, na kwa wageni wakaao kwenu hali ya ugeni, watakaozaa watoto kati yenu, nao watakuwa kwenu, kama wazaliwa miongoni mwa wana Israeli; watakuwa na urithi pamoja nanyi kati ya kabila za Israeli." (Exekieli 47:22)

- "Bwana wa majeshi amesema hivi, ya kwamba, Fanyeni hukumu za kweli, kila mtu na amwonee ndugu yake rehema na huruma; tena msimdhulumu mjane,

wala yatima, wala mgeni, wala maskini; wala mtu awaye yote miongoni mwenu asiwaze mabaya juu ya ndugu yake moyoni mwake." (Zakaria 7:9, 10)

Hebu fikiria kwa muda kidogo… Walikuwa ni familia ya wakimbizi, mama, baba, na mtoto… wakitafuta mahali salama mbali na mtawala wa mabavu mwenye hasira, na hatimaye wakajikuta Misri. Kama vile Israeli walivyopaswa kukaribisa wageni, vibao vimebadilishwa, na kichanga kilichozaliwa ili kukomboa Israeli kinalazimika kukimbilia Misri na kukaribishwa na taifa ambalo halitambui sheria kamilifu za Mungu wala kudai kuziatii. Hata hivyo taifa hilo linampatia mtoto Kristo mahali pa kukimbilia.

Yesu, ambaye ni Mfalme wa wafalme, anawasili bila kuonekana wazi wazi, akiwa hafahamiki na kuishi katika pango katika nchi ya Misri. Anakaribishwa na wageini na kutendewa vyema na wale ambao hawakuelewa unabii kuhusu Masihi ambaye hawakumtambua. Wakati Yesu alipojitokeza, miaka 400 ya ukimya ilikuwa imepita tangu unabii wa mwisho ulipotamkwa na kuandikwa. Israeli walikuwa katika hali ya kikataliwa kwa namna iliyoweza kuonekana, hata hivyo, ni wao ndio walioshindwa kufuata njia ya Mung ya kuwatendea watu.

Hata hivyo, kwa sababu ya mtawala mwenye hasira, mtoto Masihi alichukuliwa na familia yake kwenda kuwa mgeni katika nchi ya Misri, kwa namna fulani iliyo dhahiri akirudia ugeni wa Israeli, taifa ambalo alikuwa analiwakilisha. Yesu alipotoka Misri, alikuja kuokoa wale ambao wangemfuata.

Hatimaye Kristo alipowasili na kutangaza mwanzo wa huduma yake ya hadhara, anatangaza uhuru, haki, na jubilii mpya (kuanzia hapo, tunapata neno Jubilii). Ni wazi kwamba Yesu anakusudia kuleta uhuru uliomaanishwa katika Agano la Kale kwa watu wake. Kuna ile hali kwamba Mungu anakaribia kutekeleza unabii wa kimasihi na kuokoa watu na kurejesha furaha ulimwenguni, kidogo kidogo akiondoa utawala wa adui.

Yesu anapofungua huduma yake, anarejea kuelezea historia ya Israeli iliyoshindwa kupitia katika maisha yake, na akaiishi tena kama Mungu alivyokusudia Israeli waishi. Kwa maneno yake mwenyewe na kwa matendo yake, Yesu anaandika upya kule kushindwa kwa Israeli, na kuishi misha ya kujikana nafsi kikamilifu na kwa ukarimu usiotafuta makuu. Lakini hebu tazama jinsi alivyofanya hivyo:

- Aliponya wagonjwa
- Alirejeshea vipofu uwezo wa kuona
- Aliwaweka huru waliosetwa
- Alilisha wenye njaa

Yesu katika huduma yake yote aliwapatia watu furaha na amani, na uhuru kwa wale waliotelekezwa ambao walimtazama kwa matumaini. Katika sura mbili za Mathayo

sura ya 8 na ya 9 Kristo anaponya na kutoa mapepo kwa kurudia. Utume wa Kristo uliwapatia watu uzima na ukamilifu wale waliokuwa katika safari ya kukata tamaa.

Kuanzia mwanzo wa huduma yake, aliwatangazia uhuru na akawapatia jubilii yeye binafsi. Katika Luka 4 tunaona maisha ya Kristo yakieleza upendo wa Mungu kwa vitendo na kuwajali watu ambao walikuwa wametelekezwa.

Yesu aliwahudumia watu wote: masikini, Watoto, wanawake, Warumi, Wakananayo, Wakoma, wagonjwa, wafu, wapweke, waliopagawa na mapepo, wadadisi, wasiokuwa na dini, wasiokuwa Wayahudi. Yeye na wafuasi wake walihudumia wale wote waliokuwa na uhitaji, waliokuwa wadadisi, waliokuwa wawazi.

Kote katika huduma yake, Yesu aliwaweka huru watu waliokuwa wamepagawa na mapepo, matatizo ya afya, shutuma, na hukumu. Akielekea mwisho wa huduma yake, alishiriki mfano wa kondoo na mbuzi, akionesha jinsi wale watakaookolewa watakavyowatendea wale waliotelekezwa katika jamii. (Mathayo 25:31-46)

Kuanzia katika Agano la Kale hadi katika maisha ya Yesu ni dhahiri kwamba Mungu aliwaita watu wake kuhudumia wengine, kwa jina lake, na kudhihirisha utukufu wake, upendo na tabia yake. Yesu alitimiza sheria za Agano la Kale kwa neama iliyo wazi kwa kutwatendea wengine, bila kujali vizuizi vya itikadi, tabaka, au ukabila.

Pamoja na furaha inayoandamana na ukombozi, Yesu anawaita watu wake waoneshe mfano wake. Hata leo hii, neno la Agano la Kale na huduma ya Kristo inajumuishwa kwa kutiwa moyo na Waebrania 13:1-3 "Upendano wa ndugu na udumu. Msisahau kuwafadhili wageni; maana kwa njia hii wengine wamewakaribisha malaika pasipo kujua. Wakumbukeni hao waliofungwa kana kwamba mmefungwa pamoja nao; na hao wanaodhulumiwa, kwa vile ninyi nanyi mlivyo katika mwili."

Kumbuka pale Yesu aliponukuu katika Isaya 61:

> 1 Roho ya Bwana MUNGU i juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta niwahubiri wanyenyekevu habari njema; amenituma ili kuwaganga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na hao waliofungwa habari za kufunguliwa kwao.
> 2 Kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote waliao;
> 3 kuwaagizia hao waliao katika Sayuni, wapewe taji ya maua badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa badala ya roho nzito; wapate kuitwa miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe.

Yesu anataka kuleta FURAHA badala ya kuvunjika kwa dunia hii, na anataka kufanya hivyo kupitia kwako wewe na mimi, kwa kuhudumia zile familia zilizopo katika mgogoro. Pengine hatujaangalia mada hii kwa kina kabla. Je, ungefikiria kuhusu

mwenendo wako kwa maombi; maneno yako na matendo yako kuhusu wasafiri, wageni, na wakimbizi wa dunia hii?

Katika Waebrania 11:13 tunakumbushwa kwamba bado sisi ni wasafiri na wageni katika ulimwengu huu: "Hawa wote wakafa katika imani, wasijazipokea zile ahadi, bali wakaziona tokea mbali na kuzishangilia, na kukiri kwamba walikuwa wageni, na wasafiri juu ya nchi."

Hatimaye, Mungu anatutaka tuangaze utukufu wake na kutoa tumaini ambalo tunalo. Kitabu cha Isaya 60:19-21 tunasoma kuwa,

> 19 Jua halitakuwa nuru yako tena wakati wa mchana, Wala mwezi hautakupa nuru kwa mwangaza wake; Bali Bwana atakuwa nuru ya milele kwako, Na Mungu wako atakuwa utukufu wako.
>
> 20 Jua lako halitashuka tena, Wala mwezi wako hautajitenga; Kwa kuwa Bwana mwenyewe atakuwa nuru yako ya milele; Na siku za kuomboleza kwako zitakoma.
>
> 21 Watu wako nao watakuwa wenye haki wote, Nao watairithi nchi milele;

Katika Mathayo 25:37-40 tunakumbushwa kwamba: "Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi."

Familia nyingine, lakini yenye kisa kinachofanana na hicho… waliondoka Siria katika safari ya kukata tamaa, wakiwatorosha Watoto wao ngambo ya mipaka wa Lebanoni. Watoto wao waliandikishwa kwenye Kituo cha Mafunzo cha Waadventista wa Sabato, na wakakua wakiona maisha kwa mtazamo mpya.

Imani ya baba yake ya Uislamu haikuwa hai, hakuwahi kuwa na uhusiano binafsi na Mungu. Baadaye aliugua ugonjwa mkubwa, akawa hajiwezi kabisa kiasi kwamba hakuweza kuhudumia familia yake. Aliogopa kwamba familia yake ingekosa chakula. Katika ugonjwa wake akiwa amekata tamaa, alimlilia Mungu, akapokea ahadi ya amani. Afya yake ikaanza kurejea kidogo kidogo, akaona Mungu akimwagiza kumtumainia. Alianza kutembea na Mungu na kwa namna hiyo akakua siku baada ya siku akimtumainia na kuona majibu kwa maombi yake. Alianza kuona upendo wa Mungu kupitia kwa baadhi ya washiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato kutoka katika chuo kikuu kilichokuwa Jirani cha Mashariki ya Kati. Profesa mmoja wa chuo

kikuu alimchukua na kumhamishia nyumbani kwake kwa majuma matatu ili kumwonyesha mapito yaliyo bora zaidi katika mtindo wa maisha wa afya. Mshiriki mwingine wa kanisa la Waadventista wa Sabato akampatia vyakula vyenye virutubisho na kuombea familia yake. Mungu akampatia fedha za kutosha kwa namna ya ajabu, akanunua vyakula kwa ajili ya familia yake. Kadiri Imani ilivyochanua ndani ya moyo wake, hatimaye alitoa maisha yake kwa Ywsu na kujitoa kikamilifu kuonesha upendo wa Mungu kwa familia zingine za wakimbizi. Leo hii Omari amejikabidhi kikamilifu kwa Bwana na anawasaidia wengine kufahamu kumhusu Yesu na marejeo yake yaliyo karibu. Omari anajifunza kila juma na watu wengi walio katika kundi gumu kulifikia, akishiriki nao Neno la Mungu.

Ukimuuliza Omari kwamba ni nini kilicholeta tofauti katika maisha yake, atakuambia kwamba, "Mungu alinionesha upendo wake kupitia katika maisha ya Waadventista wa Sabato walionichukua, wakanisaidia kuishi maisha ya afya, wakanisaidia kuacha kuvuta sigara, wakasaidia familia yangu kwa namna nyingi tu." Leo hii Omari anatangaza nuru ambayo aliiona kwa kuwasaidia wengine kwa namna inayoonesha kwamba upendo wa Mungu unatenda.

Familia ilichukua safari ya kikata tamaa, kwa tumaini dogo la kesho angavu. Leo hii familia yao yote inatoa tumaini kwa familia zingine zilizo katika mgogoro. Maisha ya Omari yanaonesha kwamba furaha ya Kristo inaambukiza, tunahitaji tu kuisambaza.

Je, ungependa leo kuombea mamilioni ya wakimbizi wanaovuka mipaka kutafuta maeneo huru yenye usalama? Tuwaombee wajaliwe haja za mioyo yao, wapate furaha na tumaini la Yesu na kurudi kwake kuliko karibu sana.

KUWEKA KATIKA UTENDAJI

- Ni kwa namna gani unaweza kumpatia tumaini mtu fulani ambaye ni mgeni katika jumuia yenu?
- Je, kanisa lako linajihusisha na kuwasaidia wakimbizi wakati huu, au kujiunganisha na watu wa dini zingine?

*Ahmed siyo jina lake halisi.

HADITHI NA VISA VYA **WATOTO**

Tumia visa vya Watoto kama sehemu ya juma la msisitizo wa Huduma za familia za Kiadventista. Jaribu kuainisha matumizi ya mambo yaliyomo humu na kile ulicho nacho mkononi. Kigezo muhimu ni kujihusisha na Watoto katika familia ya kanisa lako

KUPANDA NA KUKUZA
ZUKINI NZURI

NA ELAINE OLIVER

AYA ZA MAANDIKO

Luka 2:52
"Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo,
akimpendeza Mungu na wanadamu."

VIELELEZO

- Zukini 1 kubwa, biringanya, au aina nyingine ya boga inayoweza kupandwa
- Mbegu za mboga unazotumia katika kisa hiki
- Chombo kidogo cha kupanda mimea kikiwa na uchafu kidogo
- Kikapu kimoja au boksi dogo unaloweza kubeba na kuonesha kama kielelezo.

Waulize Watoto mboga wanayoipenda ni ipi. Wapatie Watoto 3 hadi 4 fursa ya kuinua mikono yao na kushiriki au unaweza kuwasikiliza jinsi wanavyojibu. Kisha waulize ikiwa wanafahamu mahali mboga zinapolimwa. SHAMBANI!

Mashambani ndipo mahali watu wanapolima na kupanda maua mazuri, mimea na vitu vingine tunavyokula. Shikilia zukini (au aina nyingine ya mboga) ili Watoto wote waweze kuona. Zukini hii ina ladha nzuri, na ni nzuri kwa ajili yetu. (Endelea kutazama zukini huku ukiongea na ujaribu kuepuka kupata maoni kutoka kwa Watoto kuhusu kama zukini ina ladha nzuri kwao au la!).

Je, kuna mtu anafahamu zukini zinatoka wapi? Zinatokeza tu shambani, kubwa na kijani? Hapana! (Tabasamu au cheka kidogo). Ili tuwe na zukini tunahitaji vitu 4: mbegu, (waoneshe pakiti ya mbegu za zukini), mazingira stahiki au mahali sahihi pa

kupanda na kukuza mbegu hizo (onesha chombo cha kupandia chenye uchafu ndani yake), maji (mvua), na mwangaza wa jua.

Kuna kitu kingine ambacho mbegu za zukini zinahitaji ili kukua na kuza zukini zingine. Unajua ni nini? Ili zukini zikue vizuri zinahitaji upendo na huduma kwa wingi. Tunahitaji kufanya kazi katika uchafu na kuhakikisha tunaondoa vitu vibaya kama vile magugu, na wadudu wenye njaa.

Unajua? Kuna jambo moja zaidi ambalo linahitajika ili zukini zipate kukua vizuri! Nani anaweza kukisia? IMANI! Naam, tunahitaji kuamini kwamba kama tutapanda mbegu za zukini katika mazingira sahihi, tukazipatia maji ya kutosha, mwanga wa jua na na huduma ya upendo, zitakua na kuzaa zukini zingine kubwa na tamu. (Inua zukini tena halafu utabasamu).

Huu ni ukweli kwako na kwangu pia. Ikiwa tutahitaji kukua na kuwa wema, waliofanikiwa na watamu (yaani wema na wenye huruma), tunahitaji kukua katika mazingira sahihi, wazazi wetu wanajitahidi kuweka mazingira mazuri nyumbani kwetu. Tunahitaji kula chakula kizuri, kama vile zukini, kunywa maji ya kutosha, na kupata mwangaza wa jua kwa kucheza nje penye jua badala ya kukaa ndani tukiangalia video. Tunahitjai kukaa mbali na tabia mbaya, kama magugu yanayodhuru mmea wa zukini, na kufanya chaguzi ambazo ni nzuri. Mwisho kabisa tunahitaji kujifunza kumhusu Yesu na jinsi alivyokuwa mtoto hadi akawa mtu mzima. Tunapaswa pia kumwomba Yesu atusaidie kuwa na Imani kama ile tuliyohitaji kwa ajili ya mbegu za zukini kukua na siku zote kumwamini kwa sababu yeye anatuamini. Yesu anatupenda na kutujali. Atatufanya tuwe watu bora kadiri iwezekanavyo!

Fungu letu la Biblia leo linatuambia kuwa, “Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” Maana yake ni kwamba, kadiri Yesu alivyokua, aliendelea kujifunza zaidi na zaidi. Mwili wake uliongezeka na kuwa imara, mawazo yake yalikomaa na kuwa na hekima, na aliwapendeza wazazi wake na Mungu.

Omba leo na kila siku uzidi kuwa kama Yesu.

KUSHUGHULIKA NA
HISIA ZA HASIRA

NA DAWN JACOBSON-VENN

AYA ZA MAANDIKO

Mathayo 19:26
"Yesu akawakazia macho, akawaambia,
Kwa wanadamu hilo haliwezekani; bali kwa Mungu
yote yawezekana."

VIELELEZO

Kipande cha jagi lililovunjika (au kitu kingine unachoweza kupata ili kutumia kama kielelezo), sufuria ya shinikizo (pressure cooker) bango la maagizo likiwa limeandikwa 'TOC' upande mmoja na 'SITISHA upande mwingine, na Biblia.

Sifahamu kukuhusu wewe, lakini wakati mwingine huwa mimi ninakasirika. Hisia za hasira zinaanza kujengeka ndani yangu pale mtu anaposema au kufanya jambo ambalo mimi sipendi. Wakati mwingine ninajikasirikia mwenyewe kwa kufanya makosa au ninapoharibu kitu fulani. Na ninapokuwa katika hali ya kukasirika, unatakiwa kuwa mwangalifu, kwa sababu ninaweza kusema jambo kwa sauti ya hasira. Hasira inaweza kuwa kama sufuria ya shinikizo (onesha pressure cooker), zile hasira zikijikusanya hadi mwisho wake zinalipuka.

Ninapohisi hasira, ndipo mara kwa mara ninapojikuta katika matatizo, kwa sababu ninashindwa kuwa mwangalifu katika kile ninachosema au ninachofanya. Kwa mfano, wakati mwingine baada ya kufanya usafi jikoni, mtu mwingine anaweza kuja na kutoa vitu nilivyopanga vizuri, ili avitumia wala asivirudishe mahali pake. Halafu baadaye ninaporudi jikoni, ninakuta vimevurugika, siyo kama nilivyoiacha. Huwa kwa kweli ninakasirika. Au siku moja mtu fulani aliingia chumbani na kuangusha jagi lililokuwa na maua (onesha vipande vya jagi lililovunjika). Hilo jambo lilinifanya nikasirike kwa sababu ni moja ya vitu vyangu nilivyokuwa nikivipenda.

Ni nini kinakukasirisha? Labda umejenga nembo nzuri ya gari inayobadilika na kuwa mtumbwi. Unafurahia kazi yako. Ndipo mdogo wako anaingia chumbani na kutaka kubadilisha gari yako ya mtumbwi ili iwe chombo cha anga? Na kabla hata haujasema kitu, yeye na huo uundaji wako anaondoka nao kwenda angani!

Pengine umechora picha yako nzuri ya gwaride la wanawake! Kisha unaamua kupeleka kazi yako hiyo ya kuchora kumwonesha mama na baba. Ukiwa njiani kwenda hapo ukiharakisha kwenye ushorobo, unagongana na dada yako aliyekuwa ameshikilia bilauri yenye maji baridi. Ile bilauri inaruka hewani na kumwaga maji, wewe na dada yako mnaanguka sakafuni na ule mchoro wako unalowa maji!

Au, pengine mdogo wako wa kiume ambaye ni mtoto amelala, na una midoli yote mwenyewe. Umeshaipanga kukuzungukia kwa mduara, na wewe umekuwa kama mwalimu wao. Wamekaa wakikusikiliza. Kisha mtoto anaamka toka usingizini na mama anamleta chumbani kwako. Anataka kucheza na wewe na anaanza kuvuruga midoli yako akianza na ule mkubwa. Utajisikiaje? Unaweza kupata hisia za hasira na kutaka kumwambia aondoke hapo.

Pengine upo nje na unajenga ngome nzuri kuliko. Inashangaza! Kisha unasikia baba anaita jina lako na kusema, "ni wakati wa kuacha kila kitu kwa sababu chakula cha mchana tayari…" Lakini hautaki kuacha kucheza na kwa kweli hautaki kuvuruga tena vile ulivyokuwa umeanza. Nina uhakika kwamba umeshapitia uzoefu kama huo pale mtu fulani alipokuudhi na ukahisi kukasirika.

Leo ninataka kushiriki nawe silaha ya siri unaweza kutumia unapojikuta umeudhika na kukasirika hata ukataka kutoa maneno ya hasira mdomoni mwako. Silaha hiyo inaitwa 'TOC' (yaani onesha ishara ya TOC). Haya ni maneno yenye maana ya "Tulia-Omba-Chagua"

TULIA – OMBA - CHAGUA

Fikiria harufi za 'TOC' kama ishara ya SITISHA (onesha ishara ya sitisha). Unapohisi hasira na unataka kusema jambo fulani lisilo zuri au la kuumiza: TULIA na kuvuta pumzi kwa wingi. Kisha OMBA na kumwambia Yesu akusaidie kuondoa mawazo yasiyokuwa mema unayoanza kuwaza na kuzuia maneno yasiyo mema kutoka kinywani mwako. Vuta tena pumzi kwa wingi. Kisha CHAGUA maneno mema ya kusema. Yesu atakusaidia kutumia maneno mema. Na ninakuhakikishaia kwamba maneno yasiyo mema yanapotoka kinywani mwako, kutakua na mabishano au ugomvi. Baada ya kutulia, unaweza kuzungumza kuhusu jinsi ulivyojisikia kwa sababu

ni muhimu kuwafahamisha watu ni nini kilichokuudhi. Kwa msaada wa Yesu, unaweza kutawala hali hiyo kwa utulivu na upendo.

Mimi siyo mzuri katika kuchagua namna njema ya kuitikia ninapokuwa nimeudhika. Lakini Yesu (inua Biblia yako) anatupatia ahadi maalum katika Mathayo 19:26. Inasema kuwa, "…kwa Mungu yote yawezekana." Hata kama siwezi kutawaka kile ambacho watu wengine wananiambia, Yesu anaweza kunisaidia kuchagua kuitikia kwa maneno mema na vitendo vyema.

(Inua kile kipande kilichovunjika ili Watoto wakione). Hiki kipande cha jagi lililovunjika siyo muhimu kuliko yule aliyelivunja, au siyo? Yesu hataki nitumie maneno makali ya hasira yanayoumiza yatakayoharibu uhusiano wangu kwa sababu ya jagi lisilokuwa na akili. Kwa hiyo, kumbuka TOC wakati mwingine utakapopata hisia za hasira au kuudhika.

Tumwombe Yesu atusaidie KUTULIA, KUOMBA na KUCHAGUA maneno mazuri na vitendo vizuri. (Omba ombi fupi na Watoto).

MPANGO WA
KUTOROKA

NA MINDY SLYERS

AYA ZA MAANDIKO

Wafilipi 4:6, 7
"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza
kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu;
vile vile kama ilivyo wajibu wangu kufikiri haya juu yenu nyote; kwa sababu ninyi
mmo moyoni mwangu; kwa kuwa katika kufungwa kwangu na katika
kazi ya kutetea Injili na kuithibitisha, ninyi nyote
mmeshirikiana nami neema hii."

Baada ya mtupo wa jicho, Willy aliyekuwa anaitwa Walrus alionekana kama kiumbe yeyote wa baharini anayeishi katika bahari ya ulaya ya Atlantic. Pamoja na ukubwa wake, huyu mnyama mwenye kilo takribani 908 anafanya kama walrus anavyofanya, kama vile kula Samaki kilevi, kulala usingizi hadi saa 42. Hata hivyo Wally siyo kitu bali ni kawaida tu. Kusema kweli yeye ni maalum sana.

Mnyama Wally alionekana kwa mara ya kwanza mwaka jana March 2021 na akavutia wengi. Wapitaji wakajazana kumzunguka Wally, wakipiga picha na kujaza mitandao ya kijamii kwa video za mnyama mashuhuri wa baharini. Alipewa jina la utani "Fungie" Umaarufu wa Wally uliongezeka kwa ucheshi kama vile kushikilia Samaki kwenye pua yake. Katika Wales, mahali ambapo Wally alidumu kwa majuma kadhaa, baadhi ya migahawa ilianza kulisha watu vinywaji vyenye jina Wally. Katika nchi ya Ufaransa na Italia uso wa Wally ulipata umaarufu na kupendwa na hivyo kujulikana sana.

Hata hivyo, mwezi wa tisa mwaka 2021 kitu fulani kilibadilika kwa Wally. Aliwekewa viungo vingi kwenye chakula, pamoja na kelele za watu waliokuwa wamefurika kutaka kushuhudia, na kelele za honi za magari barabarani, ile hali ya kawaida ya Wally

ilianza kubadilika. Alianza kuonesha kuchukizwa. Amani yake ya ndani ilianza kuvurugwa, ni kama alitaka kutoka hapo na kwenda mahali penye utulivu.

Akiwa amechukizwa kwa usumbufu, Wally aliamua kwenda kutafuta mahali penye amani ambapo angeweza kupata usingizi na kutoroka vurugu zilizokuwa zimemkera.

Akiogelea mbali na bandari, Wally aliona kitu kisichokuwa cha kawaida. Aliona mtumbwi. Akakumbuka kwamba kuna nyakati wanadamu walikuwa wakimpatia chakula kutoka katika kitu kama hicho. Je, hapa palikuwa ni mahali stahiki na salama pa kupumuzika? Akitumia viungo vyake kama mapezi alijivuta na kujaribu kupanda kwenye chombo kile kidogo, na akajilaza kwenye mito ya ngozi iliyokuwamo chomboni. Je, huu mtumbwi mdogo utaweza kumsaidia kuepuka vurugu za watu zilizokuwa zikimpatia msongo? Wally alitumaini hivyo.

Siku baada ya siku Wali aliogelea katika maji ya kisiwa cha Maria akitafuta mahali patulivu pa kupumzika. Alifahamu kwamba kupumzika kungemuwezesha kurejea katika hali ya "Fun-gie" aliyokuwa amezoea. Ni kwa namna gani aliendelea kuudhika hata baada ya kupanda juu ya mtumbwi. Bado alikuwa anavutia umati wa watu ambao walidhani kwamba walrus ndani ya mtumbwi alikuwa ni kivutio. Kuongezea hapo, uzito wake ulisababisha uharibifu wa mitumbwi, na baadhi ikazama. Willy aliweza kuhisi kwamba ustahimilivu wa wamiliki wa mitumbwi ulikuwa unaanza kupungua, wakimpa jina la "apendwaye, lakini mtukutu" na "kiumbe wa baharini avutiaye lakini tishio." Alihitaji msaada lakini hakujua afanye nini.

Hatimaye, wahusika wa idara ya kuokoa viumbe wa baharini walikuja na kumsaidia Willy. Walipoona kwamba kiumbe huyo alikuwa na msongo na amekata tamaa akihitaji kupumzika, Mkurugenzi Mtendaji kwa jina Melanie Croc alipendekeza mpango. Maofisa wake waliunda chombo kama mtumbwi karibu kama pantone ambacho kiliweza kuhimili uzito wa Willy. Hawa wataalam walipafanya kama kochi linaloelea na likawa kama nyumbani kwa Willy. Walimwondoa mbali na watu na kumwacha afurahie mwenyewe. Huu mpango wa kutoroka ulihakikisha usalama na ulinzi wa wengine huku wakimwezesha Willy nafasi iliyokuwa ikihitajika kwa ajili ya kupumzika bila usumbufu.

Miezi sita baadaye, Wally amerejea katika hali yake ya furaha aliyokuwa akiipenda. Amepumzika na kutulia, akijenga akiba ya mwonekano ili aweze kujumuika na walrus wenzake katika bahari kuu hatimaye kupata mwenzi. Tunashukuru huo mpango wa

kutoroka, hatimaye Wally walrus amepata mahali pa kwenda kila anapohisi kusongwa na kuwa na wasiwasi ili aweze kuchakata shinikizo kwa namna inayoleta afya.

Kisa cha Wally kinanifanya nifikirie kuhusu mtu mwingine anayehitaji mpango wa kutoroka. Katika kitabu cha Yohana sura ya 6, Yesu alifahamika kama "Mfalme wa Wayahudi," akawa maarufu kwa uponyaji wake wa kimiujiza na kuwalisha watu zaidi ya 5,000. Watu wengi kutoka maeneo mbali mbali walikusanyika kwenye uwanda wenye nyasi kuelekea katika bahari ya Tiberia wakitazamia kwa shauku kumwona "Huyu Nabii." Mafundisho ya Yesu na matendo yake ya ajabu yalikuwa yamemfanya kuwa maarufu.

Hata hivyo, uhitaji waliokuwa nao watu wa wakati ule ulimfanya kusongwa kila wakati. Alikuwa na shinikizo kutoka kwa kusanyiko la watu waliokuwa wakitazamia atende kitu fulani. Kwa shauku kubwa watu walizidi kumsonga kwa karibu, kelele kutoka kwa Watoto wenye njaa, na vurugu za Mafarisayo wenye hasira, Yesu alijisikia kukarisika, na kufadhaika. Amani yake ya moyoni ilivurugwa, hata kumfikisha mahali ambapo alikuwa na wasiwasi. Alihitaji kwenda mbali kidogo.

Akiwa amesongwa na kuvurugwa, Yesu alienda kutafuta mahali patulivu apate kupumzika. Alihitaji mahali ambapo angeweza kupata usingizi na kutoroka kutoka kwenye vurugu zile. Akiangalia bandari kwenye bahari ya Galilaya, Yesu aliona kitu cha kawaida. Mtumbwi! Je, hapa palikuwa ni mahali salama kwake kupumzika? Je mtumbwi huu ungeweza kumweka mbali na shinikizo la watu waliokuwa wakimsababishia msongo? Yesu alitazamia hivyo. Akapanda ndani ya mtumbwi, "Naye Yesu aliposikia; hayo, aliondoka huko katika chombo, akaenda mahali pasipo watu, faraghani. Na makutano waliposikia, walimfuata kwa miguu kutoka mijini mwao." (Mathayo 14:13). Bado alikuwa akivutia umati wa watu ambao walidhani huyu seremala akifanya miujiza lilikuwa ni jambo la kushangaza. Kama vile Wally tu, Yesu alihitaji msaada.

Hatimaye wanafunzi wa Yesu walikuja kumsaidia. Alijikuta na wasiwasi kiasi kwamba aliamua kutafuta mahali penye utulivu pa kupumzika ng'ambo ya ziwa. Baada ya kuwaaga makutano, walimchukua hivi hivi hadi kwenye chombo, nao wakaondoka mara moja." (*Desire of Ages,* uk. 333). Wale wanafunzi walitafuta namna ya kumwacha Yesu apigwe na baridi. Mpango wao wa kutoroka ulihakikisha usalama na ulinzi kutoka kwa Mafarisayo na Masadukayo na kwa hiyo kuwezesha Yesu kupata nafasi aliyokuwa akihitaji ili kupumzika bila bughudha.

Yesu kwa mfano wa yule Wally, anaweza kuudhiwa na kusumbuliwa. Shinikizo kutoka shuleni, nyumbani, na kutoka kwa marafiki inaweza kusababisha hisia za wasiwasi na kuudhika. Ingawaje hisia hizo ni kawaida, zinapokuwa nyingi na zenye

uzito fulani zinaweza kusababusha maumivu kwetu na hata kwa wengine. Ndiyo maana ni muhimu kwetu kuandaa mpango wa kutoroka. Kama vile Yesu alivyoingia kwenye mtumbwi na kuondoka, tunahitaji kuwa na mahali salama pa kwenda ambapo patatupatia uwezo wa kuondoa msongo na kupumzika. Jambo hili linaweza kuonekana kama ni muda wa kujitenga na kuwa na utulivu, au kukwepa "chumba chenye moshi." Kwa kutumia vifaa vya kuweka masikioni ili kupunguza sauti, inawezekana kupata utulivu. Hatimaye, kama vile tu wanafunzi wa Yesu walivyomkubali "Jinsi alivyo," sisi pia tunaweza kuwategemea marafiki zetu wa karibu pamoja na familia kama bandari salama pale tunapokabiliana na dhoruba za mihemuko.

Mwisho, mpango wetu wa kutoroka mihemuko unatupatia mkakati wa kupata amani na mawazo na hisia zetu. Mungu ameahidi katika Wafilipi 4:6-7 kwamba, "Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu."

SEMINA

Semina hizi zimekusudiwa kutumika wakati wa Juma la Msisitizo wa Huduma za Familia ya Kiadventista. Tafadhali zisome kwa makini ili kupata uzoefu wa maudhui yaliyomo na misamiati iliyotumika. Kuweza kupakua kutoka kwenye intaneti masomo ya kuwasilisha kwa PowerPoint tembelea tovuti hii: www.**family.adventist.org/2023RB**

KULEA USTAWI WA
KIMHEMKO NDANI YA FAMILIA

NA WILLIE NA ELAINE OLIVER

AYA ZA MAANDIKO

"Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee."
Mithali 22:6

TAMKO LA KUSUDIO

Semina hii inachunguza jinsi mazingira ya familia na muingiliano vinavyoweza kuathiri ustawi wa mtu wa kijamii, kiakili, kihisia, na kiroho katika maisha. Semina hii itatoa mapendekezo yaliyojengwa kutoka katika mitazamo ya kisaikolojia, kibiblia na kwa roho ya unabii.

UTANGULIZI

Wazazi wote wanataka kuwaona watoto wao wakikua na kufanikiwa kimwili, kiakili, kitaaluma, kiroho, na kijamii. Wengi huwataka watoto wao kupata kazi inayokamilisha na yenye kusudi na kutoa mchango katika familia yao, kanisa, na jamii. Hivyo, familia ni kiini cha msingi cha malezi kwa ajili ya ustawi wa ujumla wa watu katika jamii.

Watu wanategemewa kukutana na changamoto kadiri wanavyokua na kusonga katika maisha yao. Baadhi ya changamoto hizi hazitabiriki, kama vile ulemavu wa kuzaliwa, udumavu, ajali, n.k. Kinyume na hivyo, zingine ni kwa sababu ya uzoefu, mitazamo, na matendo ambayo mtoto hukabiliana nayo nyumbani na sehemu zingine au uzoefu wenye athari mbaya utotoni. Uzoefu wa utotoni, ulio chanya na wenye athari, hutujenga na kutupatia uelewa kila mmoja wetu tangu utotoni hadi utu uzima.

Mithali 22:6 inasema, "***Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.***" Fungu hili mara nyingi limetumika kuwahamasisha wazazi kuwanidhamisha watoto wao. Wakati kusudi hili linaweza kuwa sahihi kwa kiasi fulani, kuna maana pana zaidi nyuma yake. Tafsiri ya Kiebrania ya sehemu ya kwanza ya fungu hili ni, "*mlee mtoto kulingana na njia zake.*" Kisha hata atakapokuwa mzee, "*atatenda kwa adabu.*"

Ni katazo hasa ukizingatia asili ya mtoto, tabia, na kipaji katika elimu au malezi yanayotolewa ili mtoto anapokua, aweze kuhisi kuwa mwenye uwezo na ujasiri katika kuongoza ulimwengu wake. Elimu hii au malezi yanayoheshimu utofauti wa mtoto yatazaa matundi kwa maisha yake yote; itakuwa ni asili ya pili. Hivyo, hata atakapokabiliwa na mitazamo ya kidunia yenye kutofautiana na yenye uadui, haitaharibiwa. Kuna mafungu yanayofanana katika maandiko yanayotegemeza katazo hili:

> Waefeso 6:4: *"Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana."*
>
> Torati 6:7: *"Nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo."*
>
> 2 Timotheo 3:15: *"Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu."*
>
> Ellen G. White anaandika katika kitabu cha Uongozi wa Mtoto "*Child Guidance*",
>
> "Ili wazazi na waalimu waweze kufanya kazi hii, kwanza wao wenyewe wanatakatiwa kuelewa "njia" ambayo mtoto anapaswa kuiendea. Hii hujumuisha zaidi ya kuwa na ufahamu wa vitabu tu. Hujumuisha yote yaliyo mema, safi, yenye haki, na matakatifu. Hujumuisha kuwa na kiasi, kumcha Mungu, wema wa kindugu, na upendo kwa Mungu na kila mmoja kwa mwenzake. Ili kupata hili, elimu ya kimwili, kiakili, kimaadili, na kidini ya watoto inapaswa kuzingatiwa." CG 297.23

Kukuza ustawi wa kihisia ndani ya familia ni suala nyeti sana katika kujenga uthabiti wa familia na kutengeneza uimara ndani ya familia. Kuzuia au kupunguza changamoto zinazoepukika, tunapaswa kuongeza mazingira ya malezi nyumbani.

UZOEFU MBAYA WA UTOTONI

Mtoto anapokabiliana na changamoto ngumu, iwe ni msongo wa kihisia au mtikisiko wa kifamilia, anaathirika kwa namna nyingi. Neno lililotengwa kwa ajili ya uzoefu kama huo ni uzoefu mbaya wa utotoni. Uzoefu mbaya wa utotoni huwa wenye msongo na hali za hatari ambazo watoto hukabiliana nazo katika miaka 18 ya kwanza ya maisha yao. Uzoefu huu hujumuisha aina tofauti za unyanyasaji, kupuuzwa, na kutokufanya kazi za nyumbani vizuri.

Tafiti mbalimbali za kiulimwengu zinaonyesha kwamba theluthi moja ya watoto hupitia uzoefu mbaya utotoni kabla ya umri wa miaka 18, na takribani asilimia 14 hupitia uzoefu mbaya utotoni mara mbili au zaidi. Tangu mlipuko wa janga la UVIKO-19, kila mtoto tayari amepitia uzoefu mmoja mbaya wa utotoni. Aina ya uzoefu mbaya wa utotoni ulioripotiwa ni kifo cha mzazi, ukifuatiwa na unyanyasaji wa kimwili, talaka kwa wazazi, na vurugu za kifamilia. Karibia robo ya muda, talaka au kutengana huwa sababu ya uzoefu mbaya wa utotoni. Uzoefu mwingi mbaya wa utotoni huwa unahusiana, maana yake ni kwamba kuwa na uzoefu mmoja mbaya wa utotoni kunaweza kusababisha aina nyingine za uzoefu mbaya wa utotoni kutokea wakati wa utoto.

Uzoefu mwingine mbaya ni pamoja na yafuatayo.

- Kuwa mhanga wa vurugu, unyanyasaji, au kutengwa nyumbani
- Kutokuwa imara kutokana na kutengana/talaka kwa wazazi
- Kushuhudia matendo ya kikatili nyumbani au katika jamii
- Mwanafamilia kujaribu kujiua
- Matumizi mabaya ya dawa za kulevya
- Matatizo ya afya ya akili
- Kuwa na mwanafamilia aliye magereza au kifungoni
- Vita au mgogoro wa kisiasa, kuwa mkimbizi

Uzoefu mbaya hauhakikishi uwezekano wa kuwapo kwa tatizo katika siku za usoni; ingawaje, huongeza hatari ya mtoto kuwa na matatizo ya afya ya akili katika siku za usoni, majeraha, tabia hatarishi, magonjwa ya kuambukizwa au yasiyotibika na kukosekana kwa kipato au fursa za elimu. Kwa sehemu kubwa, kama inavyohusiana na mada hii, uzoefu mbaya wa utotoni unaweza kuongeza hatari ya msongo, wasiwasi, kujiua, na ugonjwa wa msongo baada ya kiwewe. CDC inakadiria kwamba visa milioni 21 vya msongo vingeweza kuepukika kama watoto wangelindwa dhidi uzoefu huu mbaya.

Nadharia ya kijamii ya kujifunza hutueleza kwamba watoto wanaoshuhudia tabia zisizo za kujichanganya kwa watu ambao ni sehemu ya mduara wao wa ndani wa kijamii, wana uwezekano mkubwa zaidi wa kujifunza na kujenga tabia za kutokujichanganya. Unyanyasaji wa kimwili, vurugu, matumizi mabaya ya madawa na pombe na mikakati mingine ya kutawala matatizo hurithishwa kwa watoto wanaoshuhudia mbinu za kukabiliana na mambo zisizofanya kazi na kukosekana kwa kujitawala. Utafiti umeonesha kwamba watoto waliojikuta katika vurugu (mfano: kushuhudia vurugu za nyumbani) au ambao wamepitia moja kwa moja uzoefu mbaya kama unyanyasaji wa kimwili au kingono wana uwezekano mkubwa zaidi wa kufanya uhalifu wa kikatili baadaye katika maisha yao.

Kujifunza na kujenga tabia isiyo ya kijamii kwa sehemu kubwa huwezekana kujitokeza katika hatua za awali za maendeleo, hasa ikiwa tabia iliyoonekana inatendwa na watu walio sehemu ya mduara wa ndani wa kijamii (Felson & Lane, 2009). Kwa sababu wanafamilia ni mfano wa kuigwa wakati wa ukuaji wa mtoto, matatizo ya awali huwa na madhara sana yanapotokea ndani ya familia. Watoto wanaweza kutambua uzoefu wa vurugu na wenye kuumiza (mfano: unyanyasaji wa kimwili, kushuhudia vurugu za ndani ya nyumba, matumizi ya madawa kwa wazazi, au matumizi ya pombe) kama mikakati sahihi ya kutawala matatizo, hasa ikiwa hao waliohusika kwa tabia hizo za vurugu hawakuwahi kukatazwa au, mbaya zadi ikiwa vurugu hizo dhidi ya watoto hutendwa na wanafamilia wengiine (Akers, 2017).

Uzoefu mwingi mbaya wa utotoni unaweza kuepukika. Hivyo, ni muhimu kuelewa na kushughulikia visababishi vinavyowaweka watu katika hatari na kujitoa kuwalinda dhidi ya uzoefu wa aina hizi. Wazazi wanaweza kufanya sehemu yao kwa kutengeneza na kudumisha mazingira salama na thabiti nyumbani na kukuza mahusiano yanayohakikisha watoto wanaweza kukabiliana na hisia ngumu wanapokua.

Katika kitabu cha Nyumba ya Kiadventista "*The Adventist Home*", Ellen G White anajadili umuhimu wa mazingira ya nyumbani:

> "Kwa kiwango kikubwa wazazi hutengeneza mazingira ya mduara wa nyumbani, na kunapokuwa na kutofautiana kati ya baba na mama, watoto hubeba roho hiyo hiyo. Fanya mazingira ya nyumbani kwako kuwa yenye kunukia kwa kujaliana. Ikiwa umesongwa na kushindwa kuwa Mkisto wa Biblia, badilika; kwani tabia unayoibeba wakati wa majaribio itakuwa ndiyo tabia utakayokuwa wakati wa kurudi kwa Kristo. Ikiwa utakuwa mtakatifu mbinguni, kwanza unapaswa kuwa mtakatifu hapa duniani. Tabia unazothamini katika maisha haya, hazitabadilishwa kwa kifo au kwa ufufuo. Utatoka kaburini ukiwa na tabia ile ile uliyoonyesha nyumbani kwako na katika jamii." AH 16.1

MTINDO WA MALEZI NA AFYA YA AKILI

Wakati baadhi ya wazazi wana hatia ya kutoa malezi hafifu, jambo jipya, au pengine si jipya sana, la malezi yaliyopitiliza linaweza kuleta changamoto kwa maendeleo ya mtoto na kuathiri uwezo wake wa kujifunza jinsi ya kushughulikia nyakati zenye kusumbua katika utu uzima. Wazazi wanaotoa malezi yaliyopitiliza mara nyingi huwa na nia njema kwa ajili ya watoto wao. Wanatambua hatari za jamii na mitazamo kinzani na hutafuta kuwalinda watoto wao dhidi ya mivuto hatari. Hata hivyo, malezi yaliyopitiliza yanaweza kuwa na athari hasi, ambapo watoto wanaohisi kulindwa kupita kiasi wanaweza kutofahamu kuhusu nyakati fulani hatarishi na wanaweza

kuwa na shauku ya kufahamu na kujaribu baadhi ya tabia hatarishi. Kushindwa kwa mtoto kushughulikia nyakati zenye kuleta msongo kunaweza kusababisha wahaka uliozidi na matatizo ya wasiwasi baadaye katika maisha yake.

Wakati huohuo, wazazi wakosaji, wanaojishusha hadhi, au wanaopuuzia mambo wanaweza kupunguza hali ya kujiamini ya watoto wao, jinsi wanavyohisi kuhusu wao wenyewe, na kujithamini kwao. Jinsi mtu anavyojifikiria yeye mwenyewe kama mtu mzima, iwe anajiamini sana au kidogo, mara nyingi huanzia utotoni ndani ya familia yao. Maisha ya familia yaliyojawa na ukosoaji, dharau, na kutokukubaliwa yote hayo yanaweza kumwandama mtu hadi katika maisha ya utu uzima. Kwa kushangaza, tabia hizi hasi pia zimehusiana na viwango hafifu vya ndoa, huzuni, na talaka. Ili kuwa na uhakika, kutokujiamini kunaweza kuwa tatizo kwa sababu ya mazingira hafifu ya shule au sehemu ya kazi isiyo rafiki. Vivyo hivyo, mahusiano yasiyo na furaha pia yanaweza kuathiri kujithamini kwa mtu.

Kwa ujumla, wazazi huangukia katika aina nne za mitindo ya malezi. Hapa kuna muhtasari wa kila kundi.

- **Mwenye kulazimisha utii.** Kuna sheria na adhabu zilizo dhahiri pale sheria hizo hazikufuatwa. Kuna wema mdogo au msaada kidogo na utawala mwingi. Katika mazingira haya yaliyoainishwa, jambo la msingi ni kufuata matakwa ya wazazi bila kujali sana mtoto huyo ni "nani" na asili au uhitaji wa mtoto (kumbuka, "mlee mtoto katika njia impasayo"). Bila msaada unaohitajika, watoto wanaweza kutokujisikia vizuri na kujenga msongo wanapokuzwa na wazazi wenye kulazimisha utii.

- **Mwenye kutoa uhuru.** Wazazi wana matarajio ya chini sana na kwa ujumla ni wapole zaidi na wenye sheria chache za kufuatwa. Hata sheria zinapovunjwa, wazazi wenye kutoa uhuru mara nying huepuka ugomvi. Bila adhabu za kutosha, watoto waliolelewa kwa namna hii wanaweza kuwa na mhemko zaidi na kuelekea katka kutafuta hatari. Hatari za wasiwasi na msongo pia zipo karibu.

- **Asiyejali.** Aina hii ya wazazi hawajihusishi wala hawana shauku na hutenga muda kidogo wa kuwa na watoto wao. Hawana sheria wala upendo wala msaada. Watoto wanaotokana na aina hizi za kaya wapo zaidi katika hatari ya kupambana katika mahusiano ya siku za usoni kutokana na kujiengua au hofu ya kutelekezwa. Mahusiano ya utu uzima, kwa ujumla, yanaweza kuwa yenye kuleta wasiwasi kutokana na malezi yao.

- **Mwenye mamlaka.** Wazazi hujenga viwango vya wazi na huitikia mahitaji ya watoto wao kwa njia ya kidemokrasia. Badala ya kuwa bosi, hukubali mawasiliano na watawasikiliza watoto wao. Kupata malezi katika nyumba yenye mamlaka humpatia mtoto msingi imara, lakini pia mtoto anakuwa na uwezekano mkubwa wa kudumisha muunganiko imara na wazazi wao hadi katika utu uzima.

Wakati mtindo wa malezi si kiashiria pekee cha kuonesha aina ya mtu mzima utakayekuwa, bado mtindo huo umekuwa ukihusianishwa na kuathirika kwa afya ya akili na maendeleo ya kijamii na kihisia. Tunaona katika Waefeso 6:4 kwamba mtume Paulo anatoa maelekezo mahususi kwa wazazi, *" Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana."* watoto wanapolelelewa katika mazingira yanayotoa changamoto lakini bado yakiwategemeza na kuwapatia upendo, wana uwezo mkubwa wa kukua na kuwa watu wazima wanaojitegemea ambao wana uwezekano mkubwa wa kumudu changamoto za maisha kwa namna chanya na yenye afya.

Ni muhimu kutambua kwamba utafiti unaonyesha kuwa historia ya familia ya matatizo ya afya hafifu ya akili au ugonjwa wa akili na uzoefu mwingine mbaya husababisha viwango vya juu zaidi vya wasiwasi na msongo. Hata hivyo, tafiti zinaonyesha kwamba watu ambao hawakuwalaumu wazazi wao, wao wenyewe, au watu wengine kwa sababu ya uzoefu hasi, walikuwa na afya bora ya akili na ustawi wa kihisia. Kwa maneno mengine, hata ikiwa wazazi wako hawakukulea vema au walikuwa na matatizo ya afya ya akili, kutafuta msaada kwa ajili ya uzoefu mbaya wa utotoni au kiwewe kunaweza kusababisha utu uzima wenye afya.

MIPAKA YENYE FUKUTO

Utafiti wa malezi umetambua sababu mbili zinazohusiana na elimumwendo ya mzazi na mtoto: msaada na utegemezi. Pengine njia bora ya kudhihirishi hilo ingekuwa fukuto na mipaka. Kila mtoto anahitaji kuhisi ile hisia ya kuwa sehemu ya kitu fulani. Utegemezi humaanisha kiwango ha upendo na wema ambao huchangia kwa mtoto kuhisi kwamba anategemezwa, anathaminiwa, na ni sehemu ya mazingira ya nyumbani mwao. Kunapokuwa na utegemezi mkubwa, wazazi huwa wenye kuitikia hitaji la upendo la watoto wao kwa namna wanavyohitaji kupendwa.

Weka akilini kwamba si watoto wote wanahitaji kupendwa kwa namna sawa. Hivyo, ni muhimu kuelewa tabia na haiba ya mtoto wako, yale wanayopenda, na vile Mungu alivyowaumba wawe. Wazazi wenye kutegemeza huonyesha upendo kwa watoto wao kwa njia ambazo huwafanya kuhisi kupendwa. Kuwa makini, kuonyesha upendo kwa mguso wenye afya, kutumia stadi bora za mawasilianoa, na kutoa uthibitisho chanya wa maneno ni njia nyingine za kuonyesha msaada. Haitoshi tu kuonyesha upendo; pia upendo unahitaji kutamkwa kwa maneno!

Utawala ni neno lingine la muundo au mipaka. Siyo kuhusu kumtawala mtoto wako. Kwa kweli, wazazi wanahitaji kufanyia kazi sanaa ya kujitawala (*Mithali 25:28; 2 Timotheo 1:7)* ili kuwa na mvuto wa pekee kwa watoto wao. Kila mtoto anahitaji muundo au mipaka ambayo inawiana na umri, jambo hili ni muhimu ili mtoto aweze

kuhisi ulinzi. Kwa kuongezea katika kuhisi kwamba wao ni sehemu ya familia, watoto wanahitaji kuhisi kuwa wako salama. Watoto hawakuzaliwa na nidhamu binafsi, hivyo wazazi wanapaswa kuweka sheria za familia na kutegemea utii. Watoto wanapopewa mipaka ya wazi katika utoto wao, hukua hadi utu uzima wenye kuwajibika ambao wana hisia sahihi ya utambulisho wao binafsi, wanachowajibika kwacho, wanachotawala, na ni nini na nani hawamtawali. Katika kitabu cha *Boundaries with Kids (Mipaka na Watoto)*, Dkt Henry Cloud na John Townsend wanasema: "Asili ya mipaka ni kujitawala, wajibu, uhuru, na upendo. Hii ndiyo misingi ya maisha ya kiroho. Pamoja na kumpenda na kumti Mungu, ni nini kinaweza kuwa matokeo bora ya malezi zaidi ya hayo?" uk.19

Watoto wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa watu wazima wenye kuwajibika walio na afya kihisia pale wazazi wanapokuwa na uwiano wa upendo wenye afya na mipaka (msaada na utawala). Pia kuna uwezekano mkubwa kwamba watakubali thamani za wazazi, watakua kimaadili kulingana na umri, na watakuwa watu wazima wenye kuwajibika kijamii na wenye kujali.

KUJENGA MAZINGIRA YA KIMBINGU NDANI YA NYUMBA YAKO

"Nyumbani kunapaswa kufanywa kwa namna yote ile ambayo neno hilo humaanisha. Kunapaswa kuwa mbingu ndogo duniani, sehemu ambapo upendo hujengwa badala ya kuhafifishwa. Furaha yetu hutegemea upandwaji huu wa upendo, huruma, na kuchukuliana. Aina nzuri zaidi ya mbingu ni nyumba ambayo Roho wa Bwana hukaa ndani yake. Ikiwa kusudi la Mungu litatimizwa, mume na mke wataheshimiana na kujenga upendo na kujiamini." AH 15.3, 4

Ellen G. White aliandika maneno haya miongo mingi kabla ya wanasaikolojia wa maendeleo kutambua vigezo kama wema, upendo, msaada vnahusiana na maendeleo yenye afya na ustawi wa kihisia wa watoto na vile tunavyokuwa kama watu wazima. Leo, tuna miundo mingi tofauti ya famila kuacha ule wa na mume na mke, lakini, asili ya maneno yake ni kuhusu aina ya mazingira ya nyumbani yanayomlea kila mwanafamilia na kumpatia kionjo cha mbinguni.

Hapa kuna dondoo 5 za kulea ustawi wa kihisia wenye afya ndani ya familia yako:

1. **Familia zenye afya hujenga mazingira ambapo malaika watataka kukaa.** Hii haimaanishi kwamba mambo yatakuwa makamilifu daima, au makosa hayatatendeka. Familia zenye afya hujifunza kuwa tayari kubadilika na hufahamu jinsi ya kuomba msamaha na kusamehe. Hutatua migogoro kwa kukusudia kwa namna ya Kikristo;

hufanya kazi pamoja kama timu katika kutatua matatizo. Huwa na vikao vya mashauri ya kifamilia vya mara kwa mara ili kujadili matatizo.

2. **Familia zenye afya hufanyia kazi mawasiliano mazuri.** Kila mmoja ana sauti, na kila mmoja husikilizwa. Hii hujumuisha maneno na sauti zenye heshima, wema na upendo. Kuna uelewa kwamba wazazi ndio viongozi. Lakini bado, watoto wanaruhusiwa kufanya chaguzi zinazoendana na umri – wanaweza kuongoza ibada nyakati fulani, kuendesha shughuli za familia, kuchagua nguo zao wenyewe. Wazazi ni watawala, na sio wenye kulazimisha utii.

3. **Familia zenye afya zina muda wa kuwa pamoja.** Kuwa na kawaida ya kula pamoja hujenga mazingira huru ya kujadili jinsi kila mmoja anvyoendelea. Si muda wa kugombeza au kuaibisha, ni muda tu wa kushiriki kama familia na kuwa pamoja. Kuna tafiti nyingi juu ya faida za chakula cha usiku cha pamoja kwa familia na namna mazoea hayo yanavykuwa na ulinzi dhidi ya tabia hatarishi kwa watoto na vijana.

4. **Familia zenye afya hucheza na kucheka pamoja.** Cheza michezo, tazama video za kufurahisha, na soma visa vya kufurahisha. Tenga muda wa kufurahi. Linda muda huu dhidi ya kutatua matatizo.

5. **Tamilia zenye afya humwabudu Mungu pamoja.** Jitoe katika kuwa na maombi ya pamoja kila siku kama familia. Hayahitaji kuwa marefu. Inaweza kuwa kwenye gari, wakati wa kifungua kinywa, wakati wa chakula cha jioni, au kabla ya kulala. Tumia muda kumweka Mungu katikati ya maisha yenu na kuwafundisha watoto wenu jinsi ya kumwabudu Mungu.

Ni muhimu kukumbuka kwamba familia zote hupitia mizunguko na hatua kadhaa za maisha kwa sababu watu wanaojenga familia hupitia mizunguko na hatua tofauti za maisha. Baadhi ya familia hukabiliana na changamoto zaidi ya nyingine, lakini zote zitapata uzoefu wa mtiririko wa maisha ambapo kuna kuzaliwa, vifo, talaka, kuunganika kwa familia za kambo, matatizo ya kiuchumi, magonjwa, au mambo mengine ya maisha. Ustawi wa kihisia wa wanafamilia unapoendelezwa, wakiwemo wazazi na watoto, familia huwa thabiti zaidi, na wanafamilia mmoja mmoja pia huwa thabiti. Uthabiti hutambua majaribu lakini huamini ustawi wa kihisia unawezekana dhidi ya changamoto.

Katika semina hii, tulijikita katika malezi ili kuonyesha mtiririko wa namna watu wazima wanavyojenga ustawi wa kihisia. Hata hivyo, ikiwa mtu hakulelewa kihisia tangu utotoni, bado kuna fursa ya kuanza safari hiyo katika utu uzima. Kutafuta kitabu kizuri cha ibada kinachokupatia tumaini la ustawi wa kihisia ni sehemu nzuri ya kuanzia. *"Utamlinda yeye ambaye moyo wake umekutegemea Katika amani kamilifu, kwa kuwa anakutumaini." Isaya 26:3*. Tafuta mshauri wa Kikristo mwenye kuaminika apate

kukusaidia kushughulikia maumivu, kiwewe, au kutelekezwa kulikopita. Omba kila siku na mara kwa mara ili Mungu aponye akili na nafsi yako.

REJEA

Spence-Jones, H. D. M. (Ed.). (1909). *Proverbs* (p. 422). London; New York: Funk & Wagnalls Company.

Dybdahl, J. L. (Ed.). (2010). *Andrews Study Bible Notes* (p. 818). Berrien Springs, MI: Andrews University Press.

White, Ellen G. (2001). *Child Guidance.* Review and Herald Publishing Association.

World Health Organization (WHO) Mental Health Surveys.

National Survey of Children's Health.

Centers for Disease Control (CDC). www.cdc.gov

White, Ellen G. (2001). *The Adventist Home.* Review and Herald Publishing Association.

Gottman, John. (2015). 7 Principles for Making Marriage Work. New York, NY: Harmony Books.

See Baumrind's Parenting Styles.

Cloud, Henry C & Townsend, John. (1998). *Boundaries with Kids.* Grand Rapids, MI: Zondervan.

Oliver, W. & E. (Ed.). (2021). *I Will Go With My Family: Family Resilience.* Resource Book 2022. Review and Herald Publishing Association.

KUISHI NA
MWENZI MWENYE UGONJWA WA AKILI

NA WILLIE NA ELAINE OLIVER

AYA ZA MAANDIKO

"Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi."
Wafilipi 4:9

TAMKO LA KUSUDIO

Kuishi na mwenzi mwenye ugonjwa wa akili siyo kazi rahisi. Inaweza kuwa ngumu sana na ya kuchanganya ikiwa mwenzi wako hakubali kwamba kuna tatizo. Mawasiliano, kumtegemeza mwenzi, na kujihudumia ni muhimu kwa ndoa zote ili zipate mafanikio na furaha, na ni muhimu zaidi katika hali ambayo kuna ugonjwa wa akili.

UTANGULIZI

Kwa ujumla ndoa huaminiwa kuwa na faida katika afya ya akili – ubora wa juu zaidi wa maisha, viwangu vya chini vya vifo, mapato zaidi, tendo la ndoa bora zaidi, afya bora ya kimwili na kiakili, na urafiki wa maisha yote pamoja na faida nyingine. Hata hivyo, kulingana na asili ya ndoa na mahusiano ya familia, afya ya akili inaweza kuimarishwa kwa namna chanya au kuathiriwa kwa namna hasi, hasa kwa watu ambao tayari wanapambana na ugonjwa wa akili. Nyakati fulani asili ya mahusiano inaweza kuchochea dalili ndani ya mtu ambaye aliwahi kupata ugonjwa wa akili.

Kwa muda mrefu, ugonjwa wa akili umekuwa ugonjwa wa "kimya" katika jamii za Imani na tamaduni nyingi. Kwa huzuni, ukimya huu umesababisha watu wengi kutokugundulika na hivyo, kukosa kutibiwa. Jambo hili linapotokea, wenzi na

wanafamilia wengine wanakuwa hawajajiandaa kushughulika na kile kinachoweza kuwa ugonjwa mdogo lakini pia wenye uwezo wa kuhatarisha maisha. Kwa hali fulani, husababisha kujenga kutokujiamini na udhaifu ndani ya ndoa na familia.

Katika semina hii, tutazungumzia kimsingi ugonjwa mbaya wa akili na kutoa mwongozo wa jinsi ya kutambua dalili na kutoa dondoo za jinsi ya kuishi na mwenzi anayepambana na ugonjwa akili. Kadiri tunapoanza kipengele hiki, tunataka kueleza kwamba kamwe hupaswi kutambua au kumshutumu mwenzi wako kwa kuwa na ugonjwa wa akili. Kukosoa au kumdharau mwenzi wako katika hali ya kawaida ni jambo la kuharibu kwa mwenzi wako na kwa ndoa yako, na huharibu zaidi ikiwa mwenzi wako ana ugonjwa wa akili.

KUTAMBUA DALILI ZA UGONJWA WA AKILI KWA MWENZI WAKO

Matatizo ya afya ya akili yanaweza kuathiri maisha ya mtu kwa namna kubwa sana, ikiwemo jinsi ya kushughulika na matukio ya maisha, kupata kipato, na kuhusiana na wengine. Wakati kila tatizo la afya ya akili lina dalili tofauti, kuna baadhi ya ishara za kawaida ambazo zinaweza kukusaidia kupata wazo la jumla linaloonesha kuwa kuna tatizo linalohitaji kushughulikiwa. Baadhi ya ishara hizi zinaweza kuonekana kama matatizo ya kawaida katika haiba, au unaweza kufikiri kwamba mwenzi wako anakuwa mvivu tu. Lakini, ikiwa dalili hizi zinaingilia utendaji kazi wa kawaida wa mwenzi wako, zinaweza kuwa dalili za ugonjwa wa akili.

- Huzuni iliyopitiliza
- Kusumbuka kulala au kuhisi uchovu
- Hisia kali za hasira au kuudhika haraka
- Wasiwasi au hofu iliyopitiliza
- Kuwa na mawazo ya kujiua
- Kubadilika badilika tabia (mfano, toka kuhisi huzuni hadi kuhisi furaha haraka)
- Kuwa na ndoto zisizo za kweli, au ugumu katika kufahamu uhalisia
- Kujitenga na marafiki
- Kujiengua kutoka katika shughuli za kijamii
- Kushindwa kushughulika na matatizo na msongo wa kila siku
- Mabadiliko katika mguso wa tendo la ndoa
- Mabadiliko katika hamu ya chakula
- Uzembe unaotetewa kuwa ni uchovu

Ikiwa umegundua dalili zozote hizi kwa mwenzi wako na kugundua kwamba ni zaidi ya kukereka kwako, hata ikiwa kwa mashaka, jadili ulichokiona pamoja na mwenzi wako na pendekeza kwamba mazungumzo na daktari au mshauri wa karibu. Hili linapaswa kutendeka kwa ukarimu bila kukosoa au kuwashambulia. Matatizo ya afya

ya akili hayatabiriki kila wakati, lakini kupata uchunguzi na tiba ambayo inapaswa kujumuisha kuhudhuria matibabu au aina nyingine ya ushauri, unaweza kuzuia tatizo lililopo lisizidi kuwa baya.

VIHATARISHI VYA AFYA YA AKILI

Magonjwa ya akili ni hali za kiafya zinazoathiri jinsi mtu anavyofikiri, anavyohisi, na anavyotenda. Baadhi ya watu wanaweza kugundulika kuwa na ugonjwa wa akili. Sababu hatarishi za kusababisha kuwepo kwa magonjwa ya afya ya akili ni pamoja na hizi zifuatazo:

- Historia ya familia ya ugonjwa wa akili
- Unyanyasaji au kutelekezwa kwa mtoto
- Uzoefu wenye kiwewe kama unyanyasaji wa kingono au mazoezi ya kijeshi
- Kuwa na ugonjwa wa akili uliopona
- Kukosekana kwa mahusiano yenye afya

Historia ya afya ya familia yako inaweza kuwa dondoo bora ya kutambua hatari ya kujitokeza kwa ugonjwa wa akili na magonjwa mengine mengi ya kawaida. Baadhi ya magonjwa ya akili huzunguka katika familia na kwa hiyo, ikiwa kuna na ndugu wa karibu mwenye ugonjwa wa akili inaweza kuwa kiashiria kwamba wewe pia upo katika hatari kubwa zaidi. Wengi wetu tunajifunza jinsi ya kuvumilia au kutovumilia kutoka katika familia zetu. Lakini, ukweli kwamba mtu katika familia yako ana ugonjwa wa akili haina maana kwamba wewe utakuwa nao. Sababu nyingine nyingi, zilizoorodheshwa hapo juu, zinaweza kuchangia kuwa na ugonjwa wa akili.

DONDOO ZA KUISHI NA MWENZI MWENYE UGONJWA WA AKILI

FANYA KAZI KAMA TIMU

Shughulikia tatizo la mwenzi wako kama tatizo letu "sisi" badala ya kuwa tatizo lake tu. Wakati mwenzi wako anaweza kuwa ndiye mwenye tatizo kitabibu, bado ndoa yenu inaathirika, na familia yenu pia. Jifunze yote unayoweza kujifunza kuhusu ugonjwa uliogundulika na ujaribu kuuelewa. Tafuta dalili ni zipi na onyesha huruma unapoona dalili zikijitokeza. Zungumza na mwenzi wako na muulize kila anachopitia.

Kuishi na mwenzi mwenye ugonjwa wa akili kunaweza kuchosha sana lakini kuonyesha huruma kutasaidia sana katika kuonyesha kujali kwa mwenzi wako. Ikiwa mwenzi wako atahisi kutegemezwa, anaweza kuwa na utayari zaidi wa kutafuta msaada na kudumu katika matibabu. Ikiwa mwenzi wako anakataa kutafuta msaada,

unaweza kutafuta matibabu kwa ajili yako mwenywe ili kukusaidia kushughulika vema na ugonjwa huo wa akili.

WASILIANA NA MWENZI WAKO KWA UWAZI NA KWA DHATI

Kuwa katika timu moja haimaanishi kuwa mwezeshaji au tambara la mlangoni. Muulize mwenzi wako jinsi unavyoweza kusaidia kutawala dalili zake lakini, mwisho wa siku ni juu ya mwenzi wako kuwajibika kwa tiba na ustawi wake mwenyewe. Kusikiliza haimaanishi kwamba unakuwa tabibu wa mwenzi wako; wewe uwe tu mwenzi mwenye msaada na endelea kumtia moyo na kumtegemeza katika matibabu yake au tiba nyingine.

Mwenzi wako anapofanya jambo linalokuumiza, hata kama hakumaanisha, hakikisha unazungumza naye kuhusu jambo hilo hapo baadaye. Shughulikia uhusiano wenu kwa namna ambavyo ungefanya kawaida kama ugonjwa wa akili usingehusishwa. Thibitisha yaliyo chanya ndani ya mwenzi wako na ndoa yako; fanya mambo maalumu kwa pamoja kila siku. Ikiwezekana, mnaweza kuhudhuria ushauri pamoja na mshauri wa Kikristo ili kuwasaidia kutawala changamoto hizo na pia kuimarisha ndoa yenu.

WEKA MIPAKA YENYE USTAWI

Kuishi na mtu mwenye ugonjwa wa akili kunaweza kusababisha mazingira dhaifu ikiwa mipaka yenye ustawi na upendo haijawekwa. Mruhusu mwenzi wako afahamu kwamba mlipuko ulio mbaya na wenye matusi hautavumiliwa. Unaweza kusema, "unapoitikia kwa jinsi hii, sitaweza kukaa karibu na wewe na itanibidi nitoke chumbani." Ugomvi wa kimwili haukubaliki kwa namna yoyote ile na ikitokea, unaweza kulazimika kutafuta sehemu ya usalama.

TAFUTA MSAADA

Kuna makundi mengi ya msaada kwa ajili ya watu na familia za watu wenye ugonjwa wa akili, zikiwemo nyenzo za mtandaoni (tazama tovuti katika rejea mwishoni). Kwa kuongezea, makanisa mengi hutoa makundi kadhaa madogo; ikiwa hakuna kundi kama hilo katika kanisa lako, jadili uwezekano wa kuanzisha moja pamoja na mchungaji wako. Unaweza kushangazwa kugundua kwamba washiriki wengine wanashughulika na wenzi au wanafamilia wenye tatizo la afya ya akili. Kama ilivyotajwa hapo awali, unaweza pia kutafuta matibabu kwa ajili yako mwenyewe. Tunakutia moyo kutafuta mshauri wa Kikristo wa afya ya akili anayeshiriki viwango vyako vya ndoa na Imani.

JIHUDUMIE

Moja kati ya mambo ya msingi zaidi unayoweza kufanya kama unaishi na mtu mwenye ugonjwa wa akili ni kujihudumia. Unapaswa kufanya afya yako ya akili kuwa

kipaumbele la sivyo utadhoofika kwa jinsi uhusiano wenu unavyodhoofu. Ni rahisi sana kupoteza hamasa ukiwa unaishi na mwenzi mwenye ugonjwa wa akili.

Anzisha ratiba inayohusisha maombi ya kila siku, kutafakari neno la Mungu, kusoma maneno chanya, na kufanya mazoezi. Kutumia muda mbali na mwenzi wako na kujichanganya na wanafamilia wengine na marafika mara kadhaa ni muhimu pia. Kwa uhusiano wowote kuwa na ustawi, ni lazima kuwa na uwiano mzuri wa kuwa pamoja na fursa ya kufanya shughuli na matamanio mengine yanayokufurahisha. Unaposhughulikia afya yako mwenyewe – kimwili, kiakili, kijamii, na kiroho, unaweza kuwa mwenzi anayejihusisha na mwenye msaada zaidi.

TUMAINI KWA WENZI

Licha ya takwimu za kuogofya, ndoa nyingi zimeendelea kuwepo zikiwa na mwenzi au mwanafamilia mwenye ugonjwa wa akili. Habari njema ni kwamba watu wengi zaidi wanafunguka kuhusu changamoto zao za afya ya akili, na mengi yanaandikwa wazi kuhusu athari za ugonjwa wa akili. Kutokana na ongezeko la watoto, vijana, na watu wazima wenye ugonjwa wa akili, ugonjwa huo umetajwa kuwa janga la afya la jamii kwa karne ya 21.

Kwa upande mwingine, wakati watu wengi bado hawapo tayari kukubali ugonjwa wa akili kama hali halisi ya kiafya, wengine wanaweza kusita kusema kuhusu mtu anayeonekana kutenda kwa namna ya ajabu – "mtu yule ni mwenye tatizo la akili, au mwenzi wangu ana mfadhaiko." Ukweli ni kwamba watu wengi zaidi hawawezi kutambua kwa urahisi dalili za ugonjwa wa akili; ukweli kwmba mwenzi wako au mtoto wako mara kadhaa anakasirika haimaanishi tu kwamba ana tatizo la akili. Jambo la muhimu ni kutambua ikiwa mwenzi, mtoto, au mpendwa mwingine anatenda kwa namna zisizotabirika na za kubadilika badilika ambazo husababisha kutokuelewana sana ndani ya familia. Unapotambua vurugu hizo, kupata msaada kutoka kwa mshauri wa kitaalamu, mwanasaikolojia, au tabibu wa magonjwa ya akili ni muhimu.

Kwa Wakristo wengi, kutafuta msaada kutoka kwa wabobezi wa masuala ya afya ya akili huonekana kuwa jambo lisilofikirika. Lakini, fikiria kwamba ikiwa unaumwa jino, usingejaribu kuling'oa mwenyewe. Au ikiwa una mkono uliovunjika, usingejaribu kuunyoosha mwenyewe? Kwa hali zote hizo, mhusika angetafuta msaada wa mtaalamu – daktari wa meno au daktari wa mifupa. Ugonjwa wa akili hautofautiani na ugonjwa mwingine wowote unaohitaji utambuzi na tiba sahihi. Ikiwa jino lililoathirika au mkono uliovunjika utaachwa bila kushughulikiwa, husababisha matatizo makubwa. Vivyo hivyo kwa ugonjwa wa akili; ni hali ya kitabibu inayochunguzwa.

Kuingilia kati mapema, maelezo sahihi, na tiba ni hatua za kwanza muhimu katika kutawala ugonjwa wa akili. Kama mwenzi mwenye msaada au mtoa huduma, jielimishe kadiri uwezavyo juu ya hali ya mhusika. Wenzi katika ndoa, na familia wananapaswa kutengeneza mikakati ya kukabiliana na hali hiyo na mipango ya usalama kwa ajili ya mtu mwenye ugonjwa huo na familia yote kwa ujumla. Mtu mwenye mfadhaiko, wasiwasi uliotambulika kitabibu, au aliyejaribu kujiua akapona anaweza kutumia majuma kadhaa au hata miezi kabla ya matibabu, ingawaje msaada mwingine wowote unaweza kupunguza dalili zao na hisia zao za kujiua. Huruma, wema, na msaada kutoka kwa wapendwa wake ni sehemu muhimu sana za matibabu yake. Kwa kweli, jambo hili linaweza kuwa gumu sana kwa wapendwa ambao wamechanganyikiwa, wanaogopa, na wenye hasira. Kujifunza kukabiliana na tabia, pamoja na mgonjwa wa akili mwenyewe na muitikio wake kwa tabia ile mara nyingi huhitaji ushauri kwa mwenzi wako na familia yote.

Imani kwa Mungu ni faida kubwa kwa Wakristo wanaoishi na ndugu mwenye ugonjwa wa akili. Tafiti za karibuni zimethibitisha kwmba Imani ya mtu ina jukumu muhimu sana katika kumsaidia mtu huyo kukabiliana na changamoto katika maisha yake – ikiwemo kusaidia wanafamilia kukabiliana na msongo wa kuhudumia ndugu mwenye ugonjwa wa akili. Lakini, Imani hii inapaswa kuwa ya ndani badala ya nje (*Pargament,* 2001), ikimaanisha kwamba mtu anapaswa kuamini kwa dhati kile anachodai kuamini – ***"Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi."*** Wafilipi 4:9

REJEA

Pargament, Kenneth. (2001). *The Psychology of Religion and Coping: Theory, Research, and Practice.* The Guilford
Press; Revised ed. edition).

Xu, Jianbin. (2016) *Pargament's Theory of Religious Coping: Implications for Spiritually Sensitive Social Work Practice.*
Br J Soc Work, 46(5):1394-1410.

https://www.nami.org/Blogs/NAMI-Blog/November-2018/How-to-Be-Supportive-of-Your-Partner-with-Mental-I

https://nami.org/About-Mental-Illness/Warning-Signs-and-Symptoms

https://www.nimh.nih.gov/health/publications/looking-at-my-genes

https://988lifeline.org/ The National Suicide Prevention and Crisis Lifeline (USA only)

MADHARA YA
UNYANYASAJI WA KINGONO KWA WATOTO

NA ALINA BALTAZAR

AYA ZA MAANDIKO

"Tazama, wana ndio urithi wa Bwana, Uzao wa tumbo ni thawabu."
Zaburi 127:3

"Amin, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni. Na ye yote atakayempokea mtoto mmoja mfano wa huyu kwa jina langu, anipokea mimi; bali atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, yamfaa afungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari." Mathayo 18:3-6

TAMKO LA KUSUDIO

Kusudi la semina hii ni kupitia madhara ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto, sababu zake, na jinsi ya kutambua jambo hilo ndani ya watoto, kuwalinda dhidi ya unyanyasaji, na sehemu ya kupata tiba kwa watoto ambao wamenyanyaswa kijinsia. Semina hii imejengeka katika mtazamo wa kibiblia.

VITENDEA KAZI VINAVYOHITAJIKA

Kompyuta mpakato, PowerPoint, na Projekta. Semina hii inaweza kutumia muda wa saa 1 hadi 1.5

MASWALI YA KUJADILI

Ni wangapi kati yenu wanamfahamu mtu aliye nyanyaswa kingono akiwa mtoto/kijana au mtu aliyefanya unyanyasaji wa kingono kwa mtoto/kijana?

UTANGULIZI

Watoto ni zawadi ya pekee kutoka kwa Mungu kwenda kwa mwanadamu kama ilivyotajwa katika Zaburi 127:3. Yesu anatuambia kwamba tunapaswa kuwa zaidi kama watoto wadogo katika unyenyekevu, upole, na utegemezi (Mathayo 18:3). Watoto huwategemea kabisa watu wazima kwa ajili ya huduma za mahitaji yao ya msingi na upendo na uongozi. Ubongo wao huchukua miaka kadhaa kujengeka, siyo tu ili uwee kuhudumia mahitaji yao lakini pia kuwa na uwezo wa kufahamu jinsi mwenendo wao wa wakati husika ulivyo na mguso katika siku zao za usoni. Ubongo wa mwanadamu unakuwa haujapevuka kabisa hadi ufikapo miaka ya 20 katikati. Mazingira imara na yenye malezi ni muhimu kwa watoto kuwa wachangiaji wenye afya wa jamii. Kuna njia nyingi ambazo kwazo dhambi huharibu maendeleo ya mtoto. Moja yenye kuharibu zaidi ni unyanyasaji wa kingono.

Kwa bahati mbaya, dhambi ya uzinzi ni njia iliyozoeleka ambayo shetani anatumia kudhuru uumbaji wa Mungu na uhusiano wetu na Yeye. Kuna mafungu kadhaa yanayohimiza usafi wa kijinsia na kupinga uchafu wa kingono. Katika nyakati hizi tulizo nazo, suala la ngono limechukuliwa kuwa tabia chanya na isiyo na madhara, lakini hata wapagani na wanasayansi wanafahamu athari za unyanyasaji wa kingono kwa watoto. Kutokana na matarajio ya juu zaidi ya tabia ya masuala ya ngono kwa Wakristo, uovu wa kingono unaotendeka kwa watoto, una makovu makubwa sana. hivyo, mada hii ni muhimu kushughulikiwa kwa muktadha wa kanisa.

VIWANGO

Kulingana na Vituo vya Kutawala na Kuzuia Magonjwa (2022). Unyanyasaji wa kingono kwa mtoto ni tatizo kubwa la afya ya jumuiya. Unyanyasaji wa kingono kwa mtoto ni pamoja na kuhusishwa kwa mtoto (mtu mwenye miaka chini ya 18) katika namna yoyote ya ngono inayokiuka sheria na matazamio ya kitamaduni ambayo mtoto haelewi kwa ufasaha, hakubali, au kiukomavu hayupo tayari kutoa utayari. Kile kinachoweza kuonekana kama uhusiano wa kingono wenye "muafaka" kati ya

msichana wa umri wa miaka 16 na rafiki yake wa kiume wa miaka 21 ni unyanyasaji wa kijinsia kulingana na viwango hivi. Kile mtu mzima anachoweza kufikiri kuwa ni tabia ya kingono ya hiari inayofanywa kwao na mtoto, ikiwa itatumika kwa kukusudia kuibua hisia za kimapenzi kwa mtu mzima yule, hilo pia ni unyanyasaji wa kijinsia kwa mtoto.

Mara nyingi watoto hawagundui unyanyasaji wa kingono kwamba umetendeka au kamwe hawatoi taarifa ya unyanyasaji wa kingono kwa sababu ya hofu ya kushutumiwa au kudhurika hivyo makadirio haya yanaweza kuwa madogo. Makadirio hutofautiana kulingana na tafiti na maeneo, lakini utafiti kwa ujumla umegundua kwamba:

- Mwanamke 1 kati ya 4 na mwanamume 1 kati ya 6 huko Marekani watapitia uzoefu wa unyanyasaji wa kingono kabla ya umri wa miaka 18.
- Asilimia 91 ya wahusika wa vitendo hivyo ni watu wanaofahamika kwa mtoto (marafiki au wanafamilia)
- Unyanyasaji huu haumuathiri mtoto na familia pekee, lakini pia jamii kwa mzigo wa kiuchumi wa maisha yote kwa angalau dola bilioni 9.3 hadi kufikia mwaka 2015.

MASWALI YA KUJADILI

Je, takwimu hizi zinakutisha au unafikiri haiwezi kutokea kwa mtoto wako?

MADHARA YA UNYANYASAJI WA KINGONO KWA WATOTO/VIJANA

Kati ya uzoefu wote mbaya ambao mtoto anaweza kuwa nao, unyanyasaji wa kingono ndiyo wenye uharibifu zaidi kutokana na matokeo yake ya muda mrefu kwenye maendeleo ya mtoto. Kulingana na CDC (2022), unyanyasaji wa kijinsia huwaathiri watoto/vijana/watu wazima kwa namna nyingi.

KITABIA

Wana uwezekano mkubwa wa kutumia vibaya madawa, yakiwemo madawa ya usingizi, hushiriki katika tabia hatarishi za kimapenzi (wapenzi zaidi ya mmoja au ngono isiyo salama), na wana uwezekano mkubwa zaidi wa kufanya uhalifu wa kingono.

KIHISIA

Viwango vya juu zaidi vya mfadhaiko, kujiua, na tatizo la msongo baada ya kiwewe (PTSD). Wana wezekano mkubwa zaidi wa kuwa wahanga baadaye katika maisha. Wanawake waliopitia unyanyasaji wa kijinsia utotoni wana uwezekano mkubwa zaidi ya mara 2-13 wa kushambuliwa kingono au kuwa na hatari mara mbili ya vurugu za nyumbani katika utu uzima.

KIMWILI

Viwango vya juu vya magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya ngono, majeraha ya kimwili, na baadaye magonjwa ya kudumu (ugonjwa wa moyo, unene, na saratani).

KIROHO

Kutokana na kwamba sehemu kubwa ya unyanyasaji wa kingono hutendwa na watu wazima wanaoaminika, hii inaweza kuathiri mtazamo wa mtoto kwa Baba wa mbinguni anayejali. Kwa kuongezea, mtoto anaweza kujiuliza ni kwa namna gani Mungu aliye hai anaweza kuruhusu unyanyasaji kutokea au kwa nini hakumwokoa kutoka katika nyumba yenye unyanyasaji. Yesu alifahamu jinsi mtoto anavyoweza kuwa na matokeo ya kuhafifisha aliposema, "Na ye yote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake, na kutupwa baharini." Marko 9:42.

SWALI LA KUJADILI

Wale kati yenu wanaomfahamu mtu aliyenyanyaswa kingono akiwa mtoto/kijana, ni kwa namna gani tukio hilo liliwaathiri?

Jadiliana na washirki katika hatua hii. Kufahamu athari za unyanyasaji wa kingono kwa mtoto kunaweza kuwa kichochezi kwa wale wenye hisia zaidi na hasa kwa wale waliopitia katika uzoefu wa kiwewe cha kihisia utotoni. Utataka kutambua hili na kuwahakikishia kwamba matokeo haya yote hayatokei kwa wahanga wote na kwamba kuna tumaini na uponyaji kwa wale watakaoathirika.

KUTAMBUA UNYANYASAJI WA KINGONO KWA WATOTO/VIJANA

Kwa asili watoto huchunguza ujinsia wao na via vya uzazi kadiri wanavyokua, hasa katika mafunzo ya kujisaidia na kisha katika umri wa balehe. Watoto wanapoacha kuvaa nepi, wanaonekana kugundua ghafla kwamba kuna sehemu ya mwili ambayo hawakugundua kwamba ilikuepo, yenye kazi inayohusiana na kujisaidia na yenye hisia fulani inapoguswa. Kama matokeo, watoto wanaweza kujishika zaidi na kujichunguza zaidi ili kupata mwitikio. Hali hii inaweza kuendelea hadi miaka ya awali ya shule ya msingi wanapoanza kukutana zaidi na wenzao. Watoto hugundua mwitikio wa watu wazima kwa tabia hizi. Nyakati fulani wanapenda umakini wanaoupata kwa tabia hizi zenye matatizo. Hizi ni dalili za maendeleo ya kawaida ya mtoto na si dalili za unyanyasaji wa kingono. Ni kweli, watoto wanahitaji kufundishwa kuweka mipaka inayohusiana na via vyao vya uzazi, lakini hawapaswi kuogopeshwa na sehemu zao za siri kulingana na mwitikio wa watu wazima. Wazazi wanapaswa kuhimizwa kufundisha watoto wao tofauti kati ya mguso mzuri na mbaya.

Watoto huingia hatua ya kujificha katika umri wa miaka 7 hadi balehe ambapo kuna maendeleo machache ya kijinsia. Watoto hujihusisha zaidi na wenzao wa jinsia moja na hujielekeza zaidi katika mahusiano hayo na shule. Kadiri watoto wanavyoingia umri wa balehe, wanaweza kugundua nywele zikiota katika sehemu zao za siri, na kisha hugundua mabadiliko ya kimwili yanayosababisha hisia mpya za kimwili. Huu ni wakati mwingine wa udadisi wa asili kuhusu via vyao vya uzazi, udadisi unaoweza kupelekea ongezeko la ufahamu na shauku zaidi katika ujinsia. Haya ni maendeleo ya kawaida ya mtoto.

Inaweza kuwa vigumu kutambua dalili za unyanyasaji wa kijinsia kwa watoto. Njia bora ni kugundua tu mabadiliko yoyote ya kitabia au kihisia ambayo huwezi kuyaoanisha na mabadiliko mengine yoyote katika maisha ya mtoto. Inaweza kuwa vigumu kuyatambua kwa sababu mnyanyasaji yupo vizuri katika kuficha kile anachofanya na pengine amemtishia mtoto asije akamwelezea mtu yeyote. Mara nyingi watoto hawatambui kinachotendeka kwao au jinsi ya kuelezea hofu na mashaka yao. Hapa kuna baadhi ya dalili kwamba pengine mtoto mdogo anapitia unyanyasaji wa kingono, kulingana na Mtandao wa Kitaifa wa Ubakaji Unyanyasaji & Ngono [Rape, Abuse & Incest National Network (RAINN, 2022)]:

Dalili za Kimwili:

- Magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya ngono
- Dalili za kiwewe maeneo ya sehemu za siri au damu isiyo na maelezo kwenye shuka, chupi, au nguo

Dalili za kitabia:

- Kuzungumzia sana au kuwa na ufahamu kuhusu mada za ngono
- Kutunza siri, kutokuongea sana kwa kiwango kile cha kawaida.
- Kutokutaka kuachwa na baadhi ya watu au kuogopa kuwa mbali na mlezi wa karibu, hasa hii ikiwa ni tabia mpya
- Tabia za kurudi nyuma, au kurudia tabia walizokuwa wameacha, kama kunyonya kidole au kukojoa kitandani
- Tabia ya kutii kupita kiasi
- Mwenendo wa kingono ambayo si sawa kwa umri wa mtoto
- Kutumia muda mwingi isivyo kawaida wakiwa wenyewe
- Kujaribu kukwepa kuvua nguo ili kubadili au kuoga.

Dalili za kihisia:

- Badiliko katika namna ya kula
- Mabadiliko katika haiba, kama kuongezeka kwa tabia ya uchokozi
- Kupungua katika kujiamini au kujithamini
- Wasiwasi au hofu iliyopitiliza
- Kuongezeka kwa matatizo ya kiafya yasiyoelezeka kama kuumwa tumbo na kichwa
- Kupungua au kukosa shauku ya shule, kazi, na marafiki
- Ndoto za kutisha usiku au hofu ya kuwa mwenyewe usiku
- Tabia za kujidhuru

Kwa vijana baadhi ya dalili ni sawa, nyingine ni tofauti. Ikiwa utagundua dalili hizi, ni vema kuzungumza hayo kwa kijana ili kuanzisha mazungumzo.

- Kuongezeka au kupungua wa zito
- Mfumo wa kula usio na afya kama kukosa hamu ya kula au kula kupita kiasi
- Dalili za unyanyasaji wa kimwili, kama michubuko
- Magonjwa yanayoambukiza kwa ngono au magonjwa mengine ya sehemu za siri
- Dalili za mfadhaiko
- Wasiwasi au hofu
- Kufeli darasani
- Mabadiliko katika kujijali, kama kutokuzingatia sana usafi, mwonekano, au mitindo kuliko walivyokuwa wakifanya mara kwa mara
- Tabia za kingono na mavazi yasiyostahili na badiliko kutoka katika tabia ya kawaida

- Tabia ya kujidhuru
- Kueleza mawazo kuhusu kujiua au tabia ya kutaka kujiua
- Pombe na matumizi ya madawa

Inaweza kuwa vigumu kukumbuka orodha hii na kuna maelezo mengine kuhusu tabia hizi. Jambo bora la kufanya ni kuamini hisia zako na kutokupuuza ukihisi kuna kitu hakipo sawa. Jambo la msingi la kukumbuka ni kumsikiliza mtoto ikiwa atasema hahisi kuwa salama karibu na mtu fulani au akikueleza kuhusu baadhi ya tabia zisizofaa za kingono pamoja na mtu mzima. Waamini, walinde, na wapatie msaada wanaohitaji. Si kosa la mtoto/kijana, hata kama alichagua kuwa peke yake au mwanzoni kukubaliana na tabia hiyo isiyofaa. Ni mtuhumiwa aliyeanza asili ya unyanyasaji wa kingono katika uhusiano huo.

Hakika, kuna tatizo kuhusu kumshutumu mtu kwa uongo kuhusu unyanyasaji wa kingono wakati haujatendeka, lakini ni vizuri zaidi kuwaruhusu wabobezi kushughulikia hilo. Kuna wataalamu wanaopitia mafunzo maalumu ya kuchunguza mashtaka ya unyanyasaji wa kingono ambao huelewa maendeleo ya mtoto na wanaweza kutambua kuwa ni taarifa na dalili gani zinahusiana na unyanyasaji. Ni vema kutokumuuliza mtoto kwa ukali kwa sababu inaweza kusababisha mkanganyiko katika akili ya mtoto ambayo bado haijapevuka kikamalifu. Sehemu ya kufika kwa ajili ya matatizo yote ya unyanyasaji wa kingono wa mtoto au kijana uliofanywa na mwanafamilia mtu mzima ni Taasisi ya Huduma za Ulinzi wa Mtoto au Huduma za Familia. Taarifa hizi hazimtaji aliyezitoa. Ikiwa unyanyasaji unafanywa na mtu mzima mwingine, basi idara ya polisi katika eneo mahalia ndiyo hatua ya kwanza. Hili hutendeka ili kumlinda mtoto na watoto wengine wanaoweza kudhurika. Wanyanyasaji wa watoto mara nyingi huwaathiri watoto wengi.

SABABU HATARISHI

Ni kwa namna gani mtu anaweza kusababisha madhara kama hayo kwa watoto? Unaweza kufikiri kwamba watu hawa ni wanyama na kwamba pengine hawahudhurii hata kanisani kwako, au hawaishi katika jamii yako. Kwa nje, wengi huonekana kuwa wananchi wema, wenzi na wazazi wazuri, na wanaweza hata kuhusishwa katika uongozi wa kanisa. Hiyo ndiyo sehemu ya mchezo mbayo hutumika pia kumuandaa mtoto kwa ajili ya uonevu. si wanyanyasaji wa watoto wote ni "pedophile" na si "pedophile" wote hunyanyasa watoto. "Pedophile" ni mtu mzima au kijana mwenye umri kubwa (takribani miaka 16 au zaidi) ambaye hupenda sana watoto walio katika umri kabla ya balehe (hasa watoto wadogo hadi watoto wa miaka 13). Vijana wenye

miaka 16 wanapaswa kuwa na tofauti ya miaka mitano kati yake na mtoto ili kuchukuliwa kama mnyanyasaji wa mtoto (DSM-IV, TR 2006).

Kujamiiana kumekuwa tatizo ndani ya familia tangu nyakati za Biblia. Hata Musa aliandika kuhusu hilo katika Walawi 18:6, "Mtu ye yote aliye wa kwenu asimkaribie mwenziwe aliye wa jamaa yake ya karibu ili kumfunua utupu; mimi ndimi Bwana." Mungu alifahamu hatari ambayo ngono hufanya kwa familia. Uhusiano wa kingono uliozoeleka ni wa baba na binti yake au baba wa kambo na binti wa kambo. Utafiti umegundua baadhi ya sababu hatarishi za uhusiano wa kingono kati ya baba na binti (Stroebel, 2013):

- Unyanyasaji wa kimwili au maneno ndani ya familia
- Familia zinazokubali hali ya kuwa uchi kati ya baba na binti
- Familia ambazo mama kamwe hambusu au kumkubatia binti yake
- Familia zenye mtu mzima wa kiume zaidi ya baba mzazi ndani ya familia (baba wa kambo au mpenzi wa mama)

Jamii inatambua zaidi unyanyasaji wa kingono unaoweza kutokea kwa wachungaji wa kanisa. Unyanyasaji huu hutendeka hata katika makanisa ya Waadventista wa Sabato. Baadhi ya tafiti zimegundua mkondo wa matukio ya unyanyasaji wa kingono unaotendeka na wachungaji, zikiwemo demografia za wale waliohusishwa katika unyanyasaji. Frawley – O'Dea (2004) aliripoti kwamba wanyanyasaji wengi wa kingono ndani ya Kanisa Katoliki walikuwa mapadri wapya waliowekwa wakfu ambao walijielekeza katika huduma ya vijana, ambayo ni sawa kwa makanisa ya kiprotestanti pia. Walijenga urafiki na vijana, mara nyingi vijana wa kiume wa umri kabla ya balehe na walio katika umri wa balehe. Taratibu urafiki huo ungehamia kuwa wa kimwili – kisha padre angeingiza shughuli za kingono ndani ya uhusiano. Katika uchambuzi wa kina wa hali hiyo, Timu ya Uchunguzi ya Chuo cha John Jay (2011) iligundua kwamba – kama wanyanyasaji wa watoto wasio mapadri – kulikuwa na baadhi ya udhaifu kwa wale waliofanya matukio haya. Wakosaji walikuwa na ulinganifu wa kihisia na watoto au vijana wadogo.

Ulinganifu wa kihisia ni mtu mzima kutambua na kujiunganisha zaidi kihisia na watoto (John Jay College, 2011). Ulinganifu huu unahusishwa katika uanzishaji na udumishaji wa mashambulizi ya kingono dhidi ya watoto na vijana wadogo kwa sababu watoto na vijana huitikia uhusiano huo kwa namna chanya na kuhisi kwamba wamepata mtu mzima anayewaelewa.

Wanyanyasaji mara nyingi ni wapweke, huwa na msongo sana kazini, na katika akili zao, wameficha tendo la kingono walilokusudia. Utambuzi tofauti pia huweza kutokea,

ukimlazimisha mnyanyasaji kupambana na mtazamo wake juu yake mwenyewe kama "mtu mwema," lakini aliyetenda tendo lisilo la kimaadili. Matokeo ya pambano hili mara nyingi ni kuifanya tabia hiyo ya kawaida, yakielekeza umakini katika mambo chanya ya uhusiano huo kama namna ya kufunika gharama ya unyanyasaji, hivyo kupunguza hisia za kuwajibika, hatia, na aibu (Finkelhor, 1984). Kwa uhalisia, wanamkuza mhanga na kufanya kazi kwa bidii kujihakikishia fursa za unyanyasaji wa kingono. Ukuaji wa hisia kali, hata muunganiko wenye kuaminiana na mtu aliye katika mamlaka mara nyingi ni sehemu muhimu ya kuanzisha na kuendeleza unyanyasaji wa kijinsia na kupunguza uwezekano wa kutoa taarifa. Mara nyingi mhanga huwa mshiriki "dhahiri" wa hiari na miaka mingi baadaye anaweza kuhisi kama ana "hatia" kama mkosaji alivyo, hali hii huwafanya wahanga kutokuwa na uhakika kama walinyanyaswa (Doyle, 2003).

Japo mnyanyasaji ndiye sababu ya unyanyasaji, kuna sababu hatarishi zinazofahamika kwa watoto. Kulingana na utafiti, mpangilio fulani umegundulika:

- Watoto ambao wazazi wao hawafanyi kazi
- Watoto wanaoishi katika umaskini
- Watoto wanaoishi katika maeneo ya vijijini (Sedlack, et al., 2010)
- Watoto wanaoshuhudia au ambao ni wahanga wa makosa mengine (Finkelhor, et al., 2010)
- Wanyanyasaji hutafuta watoto ambao ni wakimya, wanaosumbuliwa, na wapweke wanaotoka katika familia za mzazi mmoja au nyumba zilizovunjika (Elliot, et al., 1995)
- Watoto wanaoamini, ili mnyanyasaji aweze kutengeneza mahusiano ya kuaminika na mtoto kabla unyanyasaji haujatendeka (De Bellis, et al, 2011). Hii inaweza kuhusisha kujenga uhusiano wenye kuaminika na familia pia (Elliot et al., 1995).

SWALI LA UTENDAJI

Ni nini unachoweza kumwambia binti wa miaka 12 anayeamini kwamba alifanya uzinifu kwa sababu hakumkatalia mume wa binamu yake aliyejilazimisha kwake? Anaogopa kumwambia mama yake kwa sababu anafikiri baba yake wa kambo tayari hampendi na sasa atafikiri kwamba yeye ni mwenye dhambi.

KUWALINDA WATOTO DHIDI YA UNYANYASAJI WA KINGONO

Siyo watoto wote walionyanyaswa huendana na vigezo hatarishi, inaweza kumtokea mtoto yoyote. Hakuna njia isiyo na hitilafu ya kuwalinda watoto wote, lakini kuna hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza hatari, kulingana na RAINN (2022).

- Kuonyesha shauku katika maisha yao ya kila siku
- Kuwafahamu watu walio katika maisha yao
- Kuchagua walezi kwa umakini
- Kuzungumzia hilo. Kunapokuwa na visa vipya kuhusu mada hii, hiyo ni fursa ya kumwelimisha mtoto wako ili kumsaidia kuelewa.
- Kufahamu dalili za tahadhari
- Wafundishe watoto kuweka mipaka
- Wafundishe watoto jinsi ya kuzungumza kuhusu miili yao kwa kufahamu majina ya sehemu za via vya uzazi ili waweze kuwasiliana pale panapokuwa na tatizo
- Mruhusu mtoto wako afahamu kwamba unapatikana na upo tayari kuzungumza kuhusu kitu chochote kinachomsumbua na kisha hakikisha kwamba unaonyesha kumaanisha kile unachokisema.
- Hakikisha wanafahamu kwamba hawatakuwa katika matatizo. Wanyanyasaji mara nyingi huwatishia au kuwafanya wahisi kwamba ni kosa lao.
- Ikiwa una tatizo lolote, jaribu kutumia maswali ya wazi ili kuwahamasisha kuzungumza, kama "Ni jambo gani limetokea leo?"

Japo kuwa na watu wazima wanaojali katika maisha ya mtoto husaidia kujenga uthabiti, kunahitajika kuwapo na baadh ya ufahamu juu ya kuwalinda watoto dhidi ya unyanyasaji unaotendwa na watu wazima. Familia, mitaa, shule, na makanisa ni sehemu kuu za kukuza mahusiano haya. Kutokana na haari ya maendeleo ya ulinganifu wa kihisia unaoweza kupelekea uhusiano wa kingono kati ya mtu mzima na kijana, kuna haja ya kuwa na mipaka ambapo hakuna muda wa pekee uliopitiliza au mawasiliano ambayo yasingekuwa sawa ikiwa wengine wangekuwepo. Watu wazima wanahitaji kuwa na mahusiano na watu wazima wengine kwa ajili ya msaada wa kihisia ili wasiwageukie watoto na kujaza hitaji hilo lenye uwezekano wa kujengeka na kuwa uhusiano wa kingono. Watu wazima ambao wamegundulika kitabibu au wana ufahamu kwamba wana hali ya kupenda watoto wanapaswa kukaa mbali na watoto ili kuwalinda wote mtu mzima na mtoto.

Utafiti umegundua mapendekezo sita ya kuzuia unyanyasaji wa kingono kwa mtoto katika ngazi ya jamii:

(1) kutokuvumilia kabisa unyanyasaji,

(2) kuhusika kwa jamii katika uzuiaji na utambuzi,

(3) kutoa mafunzo katika kutambua wanyanyasaji,

(4) kuwasaidia wahanga wa unyanyasaji wa kingono kwa watoto,

(5) kuwalinda dhidi ya mashambulizi wale wanaosimama kwa ajili ya wahanga, na

(6) kwa jamii za kanisa kuunganisha ukatazaji wa unyanyasaji wa kingono kwa watoto na thamani za kidini (Pulido, et al., 2021).

SWALI LA UTENDAJI

Unaweza kufanya nini ili kuongeza usalama wa mtoto wako na wa watoto wengine katika maisha yako?

KUPATA MSAADA

Wazazi hupambana na hatia kubwa pale wanapogundua kwamba mtoto wao amenyanyaswa kingono. Kumlinda mtoto ni jukumu la msingi la wazazi, lakini hatuwezi kuzuia hatari zote. hatari kwa mtoto hutofautiana kulingana na jinsi alivyo mdogo, muda uliotumika, unyanyasaji uliotokea, jukumu la mnyanyasaji katika maisha ya mtoto, na msaada unaotolewa na watu wazima. Watu wazima wanapaswa kuangalia dalili hatarishi zilizoorodheshwa mapema na kumpatia mtoto msaada kutoka kwa mshauri aliyepata mafunzo ya kushughulikia kiwewe na hufanya kazi na watoto walionyanyaswa. Mtoto/kijana anaweza asipatane vema na tabibu. Kuwa huru kujaribu washauri tofauti hadi mtoto atakapokuwa na Amani. Ushauri unaweza usionekane kusaidia sana mwanzoni, hasa ikiwa mtoto anasita. Mara watoto hawa wanapokuwa watu wazima, mara nyingi huwaona washauri kama nyenzo ya wakati watakapokuwa tayari kupona kutoka katika viwewe vya utotoni. Ushauri wa kifamilia pia unaweza kusaidia kushughulikia ugomvi wowote uliosababisha au uliotokea baada ya unyanyasaji.

Kuuna msaada kwa makanisa kuwalinda watoto kwani wanyanyasaji mara nyingi hutumia uhusiano ule wenye kuaminiana ambao wazazi na watoto huwa nao pamoja na washiriki au viongozi wa huduma. “Imalize Sasa” ni nyenzo nzuri kutoka katika

kanisa la Waadventista wa Sabato. Tovuti yao ina taarifa juu ya ulinzi wa mtoto, sera za kuwachunguza wanaojitolea, kile wachungaji wanachofanya, taarifa kuhusu matendo mabaya ya kingono ya wachungaji, jinsi ya kudumisha mipaka yenye afya kwa viongozi wa kiroho, na jinsi ya kushughulika na wanyanyasaji wa kingono ndani ya kanisa.

HITIMISHO

Mungu alipomuumba mwanamume na mwanamke, alianza na uhusiano uliojengeka katika upendo na Imani ya pamoja. Uhusiano uliobuniwa kuwa msingi wa familia imara, yenye furaha ambapo washiriki wote hutendewa kwa heshima na thamani. Wazazi wanategemewa kuwalinda, kuwalea, na kuwatunza watoto.

Biblia inalaani kwa nguvu unyanyasaji wa kingono. Ni usaliti wa mpango wa Mungu wa awali. Kuaminiwa kunapopuuzwa na uhusiano huo na watu wenye mamlaka kusababisha athari kwa mtoto, hakumuathiri mtoto tu lakini pia huharibu mtazamo wake wa Mungu mwenye upendo. Yesu alifahamu hili hivyo alitumia lugha ngumu ya kumlaani yeyote atakayesababisha mtoto ajikwae.

Mwovu hataki kigine zaidi ya kuwaharibu watoto wa Mungu na kuharibu familia. Dhambi ya ngono ni kifaa kilichozoeleka kinachotumika. Biblia hutupatia mwongozo ulio wazi unaoweka vigezo, lakini vigezo hivyo visipodumishwa, vinaweza kuwa kovu linalowazuia watoto na familia zisipate msaada unaohitajika. Hebu sote tuwalinde watoto wetu na kuzungumza pale kunapokuwa na tatizo.

ZOEZI

Ni kwa namna gani tunaweza kuvuka kovu la kuzungumza kuhusu unyanyasaji wa kingono kwa watoto?

NYENZO

UNYANYASAJI WA KINGONO

National Sexual Assault Hotline
Available 24 hours crisis hotline
1-800-656-4673

National Organization for Victim Assistance (NOVA)
Available 24-hours crisis hotline

1-800-879-6682

Rape, Abuse, Incest National Network.
For additional resources check out this website:
https://www.rainn.org/national-resources-sexual-assault-survivors-and-their-loved-ones

NYENZO ZA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO

End it Now https://www.enditnownorthamerica.org/
Official statement on child sexual abuse:
https://www.adventist.org/official-statements/child-sexual-abuse/

WASHAURI

Substance abuse and/or mental health professionals
https://findtreatment.samhsa.gov/
Seventh-day Adventist Counselors
https://www.nadfamily.org/resources/counselors/

KUJIUA

National Suicide Prevention Lifeline
https://suicidepreventionlifeline.org/ or 1-800-273-8255

KIWEWE

Preventing Adverse Childhood Experiences
https://www.cdc.gov/violenceprevention/pdf/preventingACES.pdf
https://www.cdc.gov/injury/pdfs/priority/ACEs-Strategic-Plan_Final_508.pdf

VITABU VILIVYOPENDEKEZWA

Allender, D.B. (2014).
Wounded Heart: Hope for adult victims of childhood sexual abuse. NavPress.
Kearney, R.T. (2001).
Sexually Abused Children: A handbook for families & churches. InterVarsity Press.
Langberg, D.M. (2014).
On the Threshold of Hope. Xulon Press.

REJEA

Centers for Disease Control and Prevention (2022). Violence Prevention. Child Sexual Abuse (2022). https://www.cdc.gov/violenceprevention/childsexualabuse/fastfact.html

De Bellis, M. D., Spratt, E. G., & Hooper, S. R. (2011). Neurodevelopmental biology associated with childhood sexual abuse. Journal of Child Sexual Abuse, 20(5), 548-587

Doyle, T. P. (2003). Roman Catholic clericalism, religious duress, and clergy sexual abuse. Pastoral Psychology, 51(3), 189-231.

Elliott, M., Browne, K., & Kilcoyne, J. (1995). Child sexual abuse prevention: What offenders tell us. Child Abuse & Neglect, 5, 579-594.

Finkelhor, D. (1984). Child sexual abuse: New Theory and Research. Free Press: New York.

Finkelhor, D., Ormrod, R.K. & Turner, H.A. (2010). Poly-victimization in a national sample of children & youth. American Journal of Preventive Medicine, 38(3), 323-30. doi: 10.1016/j.amepre.2009.11.012.

Frawley-O'Dea, M. G. (2004). The history and consequences of the sexual-abuse crisis in the Catholic Church. Studies in Gender and Sexuality, 5(1), 11-30.

John Jay College Research Team (2011). The causes and context of sexual abuse of minors by Catholic priests in the United States, 1950-2010. USCCB.

Pulido, C.M., Vidu, A., Rodrigues de Mello, R., Oliver, E. (2021). Zero tolerance of children's sexual abuse from interreligious dialogue. Religions, 12(7), 549. https://doi.org/10.3390/rel12070549

Rape, Abuse, & Incest National Network (RAINN). (2022). Warning Signs for Children. https://www.rainn.org/articles/warning-signs-young-children

Rape, Abuse, & Incest National Network (RAINN). (2022). Warning Signs for Teens. https://www.rainn.org/articles/warning-signs-teens

Rape, Abuse, & Incest National Network (RAINN). (2022). How Can I Protect My Child From Sexual Assault? https://www.rainn.org/articles/how-can-i-protect-my-child-sexual-assault

Sedlak, A.J., Mettenburg, J., Basena, M., Petta, I., McPherson, K., Greene, A., and Li, S. (2010). Fourth National Incidence Study of Child Abuse and Neglect (NIS–4): Report to Congress, Executive Summary. U.S. Department of Health and Human Services, Administration for Children and Families.

Stroebel, S., Shih-Ya, K., O'Keefe, S.L., Beard, K. Swindell, S., & Kommor, M.J. (2013). Risk factors for fatherdaughter incest: Data from an anonymous computerized survey. Sexual Abuse, 25(6), 583-605.

KUUNDA MTAZAMO WA KIULIMWENGU WA MTOTO WAKO

KUPITIA KATIKA MIFANO, KUFUNDISHA, NA KUHUDUMIA

NA JOSEPH KIDDER NA KATELYN CAMPBELL WEAKLEY

AYA ZA MAANDIKO

"Katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu,"
Tito 2:7

"Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." Marko 10:45

"Katika familia, baba na mama wanapaswa daima kuwasilisha kwa watoto wao mfano wanaotamani waufuate. Wanapaswa kudhihirisha mmoja baada ya mwingine heshima kwa maneno, na mwonekano, na matendo. Wanapaswa kudhihirisha kwamba Roho Mtakatifu anawaongoza, kwa kuwasilisha kwa watoto wao tabia ya Yesu Kristo. Nguvu za kuiga ni kubwa; na katika utoto na ujana, kitengo hiki kinapokuwa hai zaidi, muundo kamili unapaswa kuwekwa mbele ya vijana. Watoto wanapaswa kuwa na Imani kwa wazazi wao, na hivyo kuchukua mafunzo ambayo watatoa." Ellen White

UTANGULIZI NA KUSUDI

Masomo ambayo mama na baba wanaweza kuonyesha kwa kukusudia au bila kukusudia humuathiri mtoto kwa kiwango kikubwa. Katika kitabu cha nyenzo za Huduma za Familia za Kiadventista cha mwaka 2022, *Nitakwenda na Familia yangu: Uthabiti wa Familia*, kuna Makala inayojadili jinsi mahusiano yenye upendo yanavyoleta tofauti katika kujenga mtazamo wa Kibiblia kwa mtoto wako. Katika semina hii, tutajadili njia ya pande tatu ya elimu ambayo ina uwezo, kupitia nguvu za Roho Mtakatifu, wa kujenga mtazamo wa kiulimwengu wa mtoto wako kupitia mafundisho ya Maandiko. Njia ya kwanza na iliyosambaa zaidi ya elimu ni mfano, ambao hutoa mafundisho yasiyo ya moja kwa moja kadiri mtoto wako anavyokutazama na kukuchunguza. Njia ya pili ni elimu ya moja kwa moja inayotolewa kupitia mafundisho ya kila siku yaliyojikita katika maisha ya kila siku. Njia ya tatu ni kuhudumu pamoja na mtoto wako, fursa ya elimu ya kiuchunguzi. Kwa kuumfundisha mtoto wako kupitia katika njia hizi tatu, unaweza kumsaidia kujenga mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia.

Kuunda Mtazamo wa Kiulimwengu wa Mtoto Wako Kupitia Mfano, Kufundisha, na Kuhudumia

Mtazamo wa kiulimwengu humaanisha jinsi tunavyoyatazama maisha yetu: mawazo yetu kuhusu ulimwengu na majibu yetu kwa maswali ya maisha ya kina zaidi. Mimi ni nani? Kwa nini nipo hapa? Ninatokea wapi? Ninakwenda wapi? Nini ni halisi? Nini ni

sahihi na siyo sahihi? Mungu ni nani? Maswali yote haya na mengi zaidi hujibiwa na mtazamo wa kiulimwengu anaoujenga mtoto wako, akijenga mwonekano wake na mawazo ya msingi. Hakuna uamuzi unaofanyika bila mtazamo wa kiulimwengu. Mitazamo yetu ya kiulimwengu hujengwa kupitia mivuto mbalimbali ndani ya maisha yetu. Kama Wakristo, tunatafuta kuwa na mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia. Mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia ni namna ya kufikiri iliyojikita katika Maandiko ambayo hutusaidia kutazama na kutafsiri ulimwengu unaotuzunguka kupitia katika uelewa wa Kibiblia. Ili kufanya maamuzi chanya na yenye afya, mtoto anahitaji mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia ambao ni chanya na wenye afya.

MJADALA WA KIKUNDI

Katika makundi ya watu 4-5, jadili maana ya kuwa na mtazamo wa kiulimwengu ulio wa kibiblia dhidi ya mtazamo wa kiulimwengu ulio wa kidunia. Jadili changamoto unazokabiliana nazo kama Mkristo na kama mzazi katika kuwa thabiti KWENYE kuhamisha mtazamo huu wa kiulimwengu kwa watoto wako.

KUTOA MFANO KAMA KRISTO

"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni" (Mathayo 5:16). Nuru tunayoangaza kwa ajili ya watoto wetu itawaelekeza katika Chanzo cha nuru yote, ikimaanisha kwamba matendo tunayochagua kufanya yana uwezekano wa kuwafundisha kumhusu Mungu.

Ikiwa hauzami katika Imani yako, watoto wako hawatazama katika Imani hiyo pia. Waumini waliojitoa zaidi ni wale wanaohamisha Imani kwa kizazi kinachofuata. Vern Bengtson anadondoa kwamba wazazi walio hai katika kuishi Imani yao huzaa watoto wenye uwezekano mkubwa wa kujikabidhi kwa Kristo. Lakini, "ikiwa wazazi wao wenyewe hawajihusishi na shughuli za kidini, ikiwa matendo yao hayawiani na kile wanachohubiri, ni mara chache watoto huhamasishwa kufuata katika hatua za kidini za wazazi wao." Wakristo walio dhaifu katika Imani yao wenyewe wana uwezekano mkubwa wa kukuza watoto watakaokuwa dhaifu katika Imani yao pia. Hivyo, wazazi wanahitaji kuonyesha viwango vya Kimbingu katika maisha yao wenyewe, la sivyo, masomo watakayofundisha yatakuwa maneno matupu tu. Yesu alipokuwa akihudumu duniani, maneno yake yalisindikizwa mara zote na tabia yake: jinsi alivyojihusisha na wengine, jinsi alivyoitikia hali fulani, na kwa urahisi jinsi alivyoishi maisha yake. Kufundisha huku kusiko kwa maneno ni kwa muhimu kama yalivyo masomo ya

kukusudia unayompatia mtoto wako. Ni katika kuchunga tabia yako ndipo mtoto wako hujifunza kilicho sahihi na kisicho sahihi.

Mtume Paulo anaandika kwa Timotheo, kijana wake wa muujiza, "Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na mwenendo, na katika upendo na imani na usafi" (1 Timotheo 4:12). Kuna vipengele 5 vya msingi vya kutoa mfano ambavyo Paulo anagusia katika fungu hili moja, japo anazungumza na kijana, kanuni hizi za mfano ni muhimu kwa wazazi, babu na bibi, na walezi wa rika zote ili kuonyesha kwa ajili ya watoto wao wenyewe.

Kunena: "Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia" (Waefeso 4:29). Mazungumzo yetu yanapaswa kuwa ya upendo na yenye msaada kwa wengine, tukijengana badala ya kuvunjana. Ni *kile* unachosema na *jinsi* unavyokisema ndivyo vinavyoleta tofauti. Kadiri unavyowasiliana na wengine, fanya hivyo kwa upendo. Watoto wako wataona na kujifunza kwamba hii ndiyo namna ya kuhusiana na wengine iliyo kama ya Kristo.

Kutenda: "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Wakorintho 10:31). Mweke Mungu na ufalme wake kwenye nafasi ya mbele katika akili yako kadiri unavyotembea katika siku yako. Toka katika vitabu unavyosoma hadi mwitikio wako mtu anapokupita katika mataa ya barabarani, tenda kwa namna ambayo si ya dunia hii. Jinsi watoto wako wanavyokuona ukitenda kutawaongoza katika tabia yao binafsi na kuwafundisha kinachostahili kwa mfuasi wa Kristo.

Kupenda: "Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi" (Yohana 13:35). Upendo unapaswa kuwa msingi wa yote unayotenda na kusema. Kudhihirisha upendo wa kujitoa, usio na ubinafsi kwa wengine na Mungu atampatia mtoto wako picha ya vile upendo wa Baba yao wa Mbinguni ulivyo. Wapende wengine vema na mtoto wako atafanya vivyo hivyo.

Imani: "Ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu" (1 Wakorintho 2:5). Weka Imani yako kwa Baba yako wa mbinguni. Nyakati zinapokuwa ngumu, mgeukie Mungu wako na uonyeshe Imani yako kwa mtoto wako. Ikiwa mwitikio wako ni kuweka Imani yako kwa Mungu, mtoto wako atajifunza kwamba Yeye ni wa kuaminika, na baada ya muda mfupi mtoto wako atafanya kule kuweka Imani yake kwa Mungu kuwa mwitikio wake wa asili pia.

Usafi: "Njia zote za mtu ni safi machoni pake mwenyewe; Bali Bwana huzipima roho za watu" (Mithali 16:2). Jiweke sambamba na nia za moyo wako. Jitoe kikamilifu kwa Mungu na mruhusu akusafishe dhidi ya mazoea yako ya dhambi. Kadiri Mungu anavyofanya kazi ndani yako, atakusafisha na kmpatia mtoto wako picha bora zaidi ya maisha anayotaka kutupatia.

Watoto wako daima hutazama na kusikiliza, wakiangalia kwa makini yote unayosema na kutenda. Wewe ndiye unayewapatia dondoo kuhusu kilicho sahihi na kisicho sahihi, hata usiposema mambo kama hayo. Hakikisha unaomba na kumuomba Mungu afanye kazi ndani ya maisha yako ili kadiri unapovutwa karibu naye, mtoto wako aweze kuvutwa karibu pia.

MJADALA WA KIKUNDI

Kila mmoja wenu, fikiria kuhusu wazazi, walezi au watu wazima wengine uliowaangalia kama mfano, ni nini unachoweza kukumbuka kutoka katika kuchunguza matendo yao. Je, matendo yao yaliendana na maneno yao? Tafakari juu ya namna kujitoa kwao kwa Mungu, mafungu waliyoshiriki, au kukosekana kwa kujitoa kulivyoathiri mtazamo wako wa kiulimwengu. Ni mfano gani kutoka kwa wazazi wako ungependa kuutunza kwa ajili ya watoto wako na ni upi ambao ungependa kuuacha?

KUFUNDISHA KAMA MUNGU ALIVYOAGIZA

Kadiri Waisraeli walivyokuwa wakizunguka jangwani, Bwana aliwapatia agizo kuhusu elimu kwa saa 24, siku saba kwa watoto wao. agizo hili, linalofahamika kama Shema, (linalotafsiriwa kama "sikia"), lilikaririwa na Waisraeli wote waaminifu katika nyakati zote, na litakuwa ni wazo la busara kwetu sisi pia kufuata.

> "Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamuru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako" (Torati 6:4-9)

Maana kubwa ya Shema ni uzoefu unaoendelea wa kuwafundisha watoto. Bwana anawaagiza wazazi kuwafundisha watoto wao kumhusu Yeye mwenyewe nyakati zote – tangu asubuhi hata jioni, nyumbani na safarini, katika kila fursa itakayopatikana. Upendo wa Mungu kwetu na upendo wetu kwake unapaswa daima kuwa vinywani mwetu, ukirithishwa kwa watoto wetu. Mawazo haya hunenwa katika Agano la Kale na katika Agano Jipya:

Zaburi 78:2-4: "Na nifunue kinywa changu kwa mithali, Niyatamke mafumbo ya kale. Mambo tuliyoyasikia na kuyafahamu, Ambayo baba zetu walituambia. Hayo hatutawaficha wana wao, Huku tukiwaambia kizazi kingine, Sifa za Bwana, na nguvu zake, Na mambo yake ya ajabu aliyoyafanya."

Mithali 22:6: "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee."

Waefeso 6:4: "Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu; bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana."

2 Timotheo 1:5: "Nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki, ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, nami nasadiki wewe nawe unayo." Kupitia mafundisho ya uaminifu ya Loisi na Eunike, Timotheo mhubiri kijana aliinuliwa kufundishe maelfu ya wengine kumhusu Mungu.

Ni kwa namna gani wazazi wanaweza kutumia muda wao *wote* kuwafundisha watoto wao? Tunapoanza kuangalia kupitia katika darubini ya maagizo ya kila siku, tunaweza kuanza kuona masomo kuhusu Mungu katika uzoefu wetu wote wa kila siku.

Kwa kweli, Maandiko yanaweza kutumika kuwafundisha watoto wetu. Shema hutukumbusha kuandika na kufahamu dhana za Neno la Mungu. Historia na matukio ya sasa katika maeneo yanayotuzunguka pia yanaweza kuwa fursa za kufundisha. Tunaweza kuonyesha jinsi Mungu anavyopatikana na kujihusisha na dunia leo. Uoto wa asili pia unaweza kuwa njia bora ya kuwafundisha watoto wetu kumhusu Mungu. Zaburi zimejawa na mifano ya njia za kuunganisha uumbaji na Muumbaji.

> "Ee Bwana, jinsi yalivyo mengi matendo yako! Kwa hekima umevifanya vyote pia. Dunia imejaa mali zako. Bahari iko kule, kubwa na upana, Ndimo mlimo viendavyo visivyohesabika, Viumbe hai vidogo kwa vikubwa" (Zaburi 104:24-25).

Kadiri familia yako inavyopita katika uzoefu wa maisha pamoja, iwe unaendesha gari kwenda shuleni au umesimama katika ukingo wa korongo kubwa, angalia ni nini unachoweza kupata kinachoweza kukuunganisha na Mungu. Ni masomo gani ya uadilifu yanaweza kujifunzwa? Ni kwa namna gani unaweza kuhisi uwepo wa Mungu katika maisha yako? Ni vipengele gani vya tabia ya Mungu vinaweza kuonekana? Omba kwamba Mungu aweze kufungua macho yako uweze kuona masomo unayoweza kupata kutoka katika maisha ya kila siku, na kisha anza kuyashiriki na watoto wako. Waulize maswali kuhusu kile wanachoona na kupitia. Waulize jinsi kile wanachoona kinavyohusiana na kile wanachofahamu kumhusu Mungu na Biblia. Kadiri unavyokuwa na mazungumzo haya na watoto wako taratibu, itakuwa ni shemu ya ratiba yenu ya kila siku, na watoto wako watajihusisha kwa shauku.

KUFUNDISHA KWA UHUSIANO

Thomas na Tabita ni wazazi wa vijana watatu wa kiume. Wamekusudia kusoma Biblia pamoja nao na hata kuwahamasisha kukariri mafungu ya Biblia. Hapa Thomas anatoa mfano wa jinsi Maandiko yanavyosaidia kujenga mtazamo wa kiulimwengu wa kijana wake Mkubwa Lukas, aliyekuwa na umri wa miaka minne wakati kisa hiki kinatokea:

"Tumekuwa tukisoma kitabu cha Kutoka, lakini usiku wa jana Lukas alichelewa kidogo kulala kuliko Philip, hivyo tuliamua kusubirisha sura inayofuata na kusoma moja ya visa kutoka katika 2 Wafalme ambacho Lukas alisikiliza karibuni katika Saa ya Kisa Chako "*Your Story Hour*." Hii ilikuwa sehemu yake: 'Ikawa, walipokuwa wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili; naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli' 2 Wafalme 2:11. Kwa kweli sikuwa nimefikiria kuhusu kile kinachotokea mwisho wa sura hii baada ya Elisha kuchukua vazi la Eliya, na baada ya kuponya maji ya Yeriko: "Akakwea kutoka huko mpaka Betheli; naye alipokuwa akienda njiani, wakatoka vijana katika mji, wakamfanyizia mzaha, wakamwambia, 'Paa wewe mwenye upaa! Paa wewe mwenye upaa!' Akatazama nyuma akawaona, akawalaani kwa jina la Bwana. Wakatoka dubu wawili wa kike mwituni, wakawararua vijana arobaini na wawili miongoni mwao. Akatoka huko akaenda mlima wa Karmeli, na toka huko akarudi mpaka Samaria' 2 Wafalme 2:23-25.

"Tulipomaliza kusoma, nilimuuliza Lukas, 'Kwa hiyo, unafikiri nini?' Na muda huo huo alianza kuzungumza kuhusu gari la farasi, na Eliya kwenda Mbinguni. Baada ya hapo, nilielekeza mazungumzo kwa sehemu inayohusu dubu na wale watoto. 'Kwa nini hilo lilitokea? Walikuwa wanafanya nini? Niliuliza. "Walikuwa wakimtania Eliya, na kwamba alikwenda Mbinguni,' Lukas alijibu.

"Ilikuwa dhahiri kutoka kwa yaliyofuata kwamba Lukas hakuwa na tatizo na kisa, na nimekuwa najiuliza kwa muda ni matokeo gani ambayo zoezi la kujifunza mafungu ya Biblia huwa nayo kwa watoto na jinsi yanavyounda mtazamo wao wa kiulimwengu. Hivyo, baada ya kuamka, nilimuuliza swali lifuatalo: 'Lukas, katika mafungu yote ya Biblia tuliyojifunza, ni lipi linakufanya ufikiri kwamba kilichotokea katika kisa hiki kilikuwa SAWA? Alisimama pale kwa sekunde kadhaa. Kisha alinitazama na kusema, 'Mhukumu ulimwengu wote asitende haki? Mwanzo 18:25.'

"Mimi na Thabita tulishangazwa sana. ninafahamu kwamba kuna mambo mengi ambayo haelewi, na anachoelewa ni dhahiri huchakatwa kwa namna yake ya utoto wa miaka 4. Lakini alifanya muunganiko! Alifahamu kwamba Mungu ni mwenye haki. Na hilo lilisaidia aliposikia kisa ambacho wengi wetu tungekuwa na mashaka nacho."

Lukas aliona Maandiko katika ukamilifu wake. Ili kufasiri kisa hiki katika 2 Wafalme, alienda katika Mwanzo 18:25. Hii huonyesha jinsi ilivyo muhimu kujazwa na Neno la

Mungu na kuwaongoza watoto wetu kujazwa na kuongozwa na Neno la Mungu pia. Kukiwa na Maandiko ndani ya mioyo ya vijana na mabinti zetu, tunaweza kuwaongoza katika kufasiri na kuelewa chochote wanachoweza kukabiliana nacho katika maisha kwa uwiano na kwa vitendo.

MJADALA WA KUNDI

Jadili uzoefu wa Tabita, Thomas na Lukas. Kujifunza mafungu ya Biblia kulikuwa na matokeo gani kwa Lukas, na ni kwa namna gani kulitengeneza mtazamo wake wa kiulimwengu?

KUHUDUMIA KAMA ROHO MTAKATIFU ANAVYOONGOZA

Wengi wamepata faida nyingi katika kujihusisha katika huduma: ni shughuli yenye afya ya kujifunza na kukua. Kutumia muda kuhusisha familia nzima katika huduma kunaweza kuwa uzoefu wenye nguvu na wa kiroho kwa watoto wako. Ellen White aliandika katika '*Christian Service*' – *Huduma ya Kikristo*, "Ibada ya kweli hujumuisha kufanya kazi pamoja na Kristo. Maombi, kusihi, na mazungumzo, ni matunda rahisi, ambayo mara nyingi hufungwa; lakini matunda yanayodhihirishwa katika kazi njema, katika kuwahudumia wenye mahitaji, yatima, na wajane, ni matunda halisi na hukua kwa asili katika mti mzuri. Thamani na masomo yanayofundishwa nyumbani inapaswa kuimarishwa kupitia katika matendo. Kando ya jambo hili, sisi kama Wakristo tunaitwa kutumika kupitia katika uongozi wa Roho Mtakatifu. Wagalatia 5:13b panasema, "bali tumikianeni kwa upendo," na Warumi 12:11 hutukumbusha kwamba huduma hii kwa Mungu inapaswa kutendeka kwa upendo na kwa ari. Mtazamo huu wa huduma unapaswa kurithishwa kwa watoto wetu, hasa kwa sababu huwafundisha kuhusu Mungu tunayemtumikia.

Wakati watoto wangu (Joseph) wawili walipokuwa bado wadogo, familia yetu ndogo ilianza utamaduni wa Krismasi. Familia yangu ilianza kuomba kuhusu jinsi ya kuhudumu pamoja, na Krismasi moja tulihisi Roho Mtakatifu akituongoza katika mradi fulani. Kila Desemba, kanisa letu lilishiriki katika programu ya Mti wa Malaika. Mti wa Krismasi uliletwa kanisani na kufunikwa kwa vikaratasi vyenye majina ya familia zenye uhitaji. Kila mwaka, familia yetu ya watu wanne tulichagua familia nyingine kutoka katika mti, na tungeenda kununua zawadi kwa ajili yao. Watoto wangu walifunga zawadi kwa shauku, na tulizipeleka kwa furaha kanisani ili ziweze

kutolewa kwa familia tuliyoichagua. Hii ilikuwa njia rahisi na ya kufurahisha ya kuwafanya watoto wangu waweze kuhusika katika utume, na ilikuza ndani yao moyo wa huduma na kuwajali wale walio na uhitaji.

Ellen White anaandika, "Watoto wanapaswa pia kuelemishwa sana kiasi cha kuweza kuhuzunika na walio wazee na wenye matatizo na watatafuta kupunguza mateso ya maskini na waliolemewa. Wanapaswa kufundishwa kuwa wenye bidii katika kazi za kimisionari; na kuanzia katika miaka yao ya awali kabisa hali ya kujikana na kujitoa kwa ajili ya wema kwa wengine na kuendeleza kusudi la Kristo inapaswa kujengwa ndani yao, ili waweze kuwa watenda kazi pamoja na Mungu."

Watoto husitawi katika utume wanapopewa fursa sahihi ya kufanyia kazi viwango vya Kikristo walivyojifunza. Hili halimpatii tu mtoto wako nafas ya kukua katika Imani yake, bali pia linaweza kuwasaidia wengine katika Imani zao. Cheri Fuller anaandika, "Usiwaambie wasubiri hadi wamekua ili Mungu aweze kuwatumia. Tambua vile ilivyo kushiriki upendo wa Mungu pamoja, ili waweze kuwa na uzoefu mzuri." Mruhusu mtoto wako afurahie uzoefu wa kuhudumu pamoja.

MJADALA WA KIKUNDI

Shiriki baadhi ya mifano ya maisha yako wakati wazazi wako, au wewe kama mzazi mlipokusudia kufundisha watoto wenu kutoka katika uzoefu wa maisha. (Kumbuka: kumbuka, si uzoefu wote wa maisha huwa na msaada, wala uhusiano, au unafaa kushiriki na watoto wako. Hakikisha unachunguza thamani ya uzoefu wa maisha unaoshiriki, uwe unafaa kwa umri husika, na kama utakuwa na msaada au utasababisha uharibifu zaidi.)

MATOKEO YA KUFINYANGA, KUFUNDISHA, NA KUHUDUMIA

Ellen White anaandika, "Unapaswa kufundisha, kuonya, na kushauri, daima ukikumbuka kwamba mwonekano, maneno, na matendo yako yana mguso wa moja kwa moja kwa hatima ya wapendwa wako. Kazi yako haitendeki ili kuchapa picha ya uzuri katika karatasi kubwa au kuijenga katika marumaru, lakini ni kujenga katika nafsi ya kibinadamu sura ya Uungu." Ni shauku na amri ya Mungu kwamba mama na baba wote wawafundishe watoto wao kumfuata Kristo. Kila kitu kilichotendeka – kila neno na tendo lililotendeka – kinapaswa kujikita katika Kristo, kikionyesha mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia kwa akili za vijana.

Katika Mwanzo 18:19, Mungu anazungumza kuhusu Ibrahimu, akisema, "Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana, wafanye haki na hukumu…" Hili ndilo wazazi wanaitwa kufanya: kukuza na kuelekeza watoto wao katika njia ya Bwana. Kama wandishi Craig Hills anavyosema, "Ikiwa wazazi hawatafanya kingine chochote katika dunia hii kuhusiana na watoto wao, kitu kimoja ambacho Mungu amekusudia wafanye ni kuhakikisha kwamba ni mawakala wa utangazaji wa Mungu wa utambulisho na hatma ya watoto wao…"

Mfano bora tunaoweza kupata wa mzazi aliyeacha urithi wa Imani kupitia nyenzo zote tulizojadili ulikuwa ni ule wa mwanamke aliyeitwa Susanna Wesley. Watu wengi wanamfahamu John na Charles Wesley, watu wawili maarufu katika Ukristo wanaofahamika kwa kuandaa nyimbo, kuhubiri na, kuanzisha Umethodist. Lakini si wengi wanaofahamu kuhusu mama yao, Susanna. Huyu mama alizaa watoto 19, japo ni 10 walioishi. Alichukua suala la malezi ya watoto wake kwa umakini sana na alijitoa katika elimu yao na ukomavu. Wakati Samueli, mume wake alipokuwa mbali na nyumbani mara nyingi, iwe akihubiri au akitumia muda jela kwa madeni ambayo hayajalipwa, Susanna alikuwa ndiye alilea watoto kumfuata Kristo.

Aliwapatia watoto wake elimu kamili, watoto wote wa kiume na wa kike. Watoto wake wote walifahamu kusoma katika umri wa miaka mitano, na wote walifundishwa Kilatini na Kigiriki. Hata hivyo, kinachovutia zaidi, ni jinsi Susanna alivyopandikiza mambo ya kiroho katika maisha ya kila siku nyumbani. Alitenga saa mbili kila siku za kuwa na muda binafsi na Mungu, na hivyo watoto wake walikua wakiona jinsi uhusiano wake na Mungu ulivyokuwa wa muhimu. kanisa mahalia lilipoonekana kufa, Sussana aliwaalika watu kuja nyumbani kwake alipoongoza ibada ya familia. Hili lilisababisha watu wengi zaidi kuhudhuria mikutano yake kuliko kanisani! Watoto wake walishiriki katika ibada na mama yao – kwao, ilikuwa tu ni namna ya maisha ndani ya familia. Kabla ya kulala kila usiku, Susanna alitumia saa moja akizungumza ana kwa ana na mtoto, msichana au mvulana tofauti kila usiku.

Kupitia katika mfano aliotoa, kuhudumia, kufundisha, na upendo, Susanna Wesley aliwalea watoto wake kuwa imara katika Imani zao. Athari aliyokuwa nayo kwao kama watoto iliendelea kusitawi ndani yao kadiri walivyokuwa watu wazima na muda mrefu baadaye. Athari hii iliendelea hata kwa Ukristo kwa sehemu kubwa kupitia michango ya vijana wake hasa Charles na John Wesley. Mguso ambao wazazi wanao kwa watoto wao unaweza kupita fahamu. Kwa kuwaanzisha katika safari iliyoelekezwa kwa Yesu, wazazi huwaandaa watoto kudumisha mtazamo wa kiulimwengu ulio wa Kibiblia na uhusiano wa karibu na Mwokozi wao kwa maisha yao yote.

Hii ndiyo maana ya kuacha urithi wa Imani. Susanna Wesley, Eunice (mama yake Timothy) na Lois (Bibi yake Timothy), na Paulo mwenyewe ni mifano halisi ya aina ya

urithi unaoweza kutengenezwa tunapokusudia kuunda mtazamo wa kiulimwengu wa watoto wetu. Maamuzi tunayofanya katika kusaidia kuunda mitazamo yao ya kiulimwengu yanaweza kuwa na madhara ya kudumu. Hebu urithi tunaoacha uwe ule unaowaelekeza watoto wetu na hata wengine kwa Kristo hata muda mrefu baada ya sisi kuondoka.

> "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee" (Mithali 22:6).

MJADALA WA KIKUNDI

Wewe binafsi, pamoja na mwenzi wako au katika vikundi vidogo, jadili na kuomba kuhusu yafuatayo:

1. Jadili maana ya kuunda mtazamo wa kiulimwengu wa mtoto wako kupitia katika kufinyanga, kufundisha, na kuhudumia.
2. Fikiri kuhusu namna matendo yako, elimu ya moja kwa moja, na uzoefu unaopanga utakavyoathiri maisha na mtazamo wa kiulimwengu wa watoto wako. Ni kwa njia gani unaweza kukusudia zaidi kuhusu kuhamisha Imani yako kwa watoto wako?
3. Ni miradi gani miwili ya kuwafikia wengine unayoweza kuruhusu familia yako kujihusisha nayo ili kuweka katika utendaji thamani za Kikristo zilizo muhimu kwa familia yako? Ziongeze katika kalenda yako leo!

REJEA

Ellen White, Child Guidance. (Silver Spring, MD: Review and Herald, 2002), 215.

S. Joseph Kidder & Katelyn Campbell Weakley, "Shaping Your Child's Worldview Through a Loving Relationship," in I Will Go with my Family: Family Resilience, (Silver Spring, MD: Review and Herald, 2021), 116-123.

For additional explanation of worldview, see James Sire, The Universe Next Door (Downers Grove, IL: InterVarsity Press, 1997); and George Barna, Think Like Jesus (Nashville, TN: Thomas Nelson , 2003); Kevin J. VanHoozer, "Being Biblical in a Pluralistic Age," Andrews University Seminary Studies 57 no. 2, 2019.

Curtis Miller, "Helping Kids Keep the Faith," Fuller Youth Institute, Dec. 15, 2013. https://fulleryouthinstitute.org/blog/helpingkids-keep-the-faith.

For more discussion on different types of teaching—nonverbal, situational, and planned teaching—see Dorothy Bertolet Fritz, The Child and the Christian Faith (Richmond, VA: CLC Press, 1964), 61-97

See also Debbie Rivera, "The Shema," Adventist Review. September 13, 2010. https://www.adventistreview.org/2010-1530-26.

As told to us by Thomas Rasmussen, March 28, 2019.

A few examples and discussions can be found at the following sites: Elizabeth Hopper, "Can Helping Others Help You Find Meaning in Life?" February 16, 2016. https://greatergood.berkeley.edu/article/item/can_helping_others_help_you_find_meaning_in_life/success; "7 Scientific Benefits of Helping Others," Mental Floss, accessed Dec. 16, 2021. http://mentalfloss.com/article/71964/7-scientific-benefits-helping-others; Adam Lupu, "How Do People Learn Most Effectively," November 20, 2017. https://www.forbes.com/sites/quora/2017/11/20/how-do-people-learn-most-effectively/#1b8753d01f05; Kimberly Yam, "10 Facts That Prove Helping Others is a Key to Achieving Happiness," accessed Dec. 16, 2021, https://www.huffpost.com/entry/international-day-of-happiness-helping_n_6905446.

Ellen White, Christian Service (Silver Spring, MD: Review and Herald, 1999), 96.

Ellen White, Testimonies, vol. 6, (Nampa, ID: Pacific Press Publishing Association, 2002), 429.

Cheri Fuller, Opening Your Childs Spiritual Windows: Ideas to Nurture Your Childs Relationship with God (Grand Rapids, MI: Zondervan, 2001), 209.

Ellen White, Child Guidance, 218.

Craig Hill, Bar Barakah (Littleton, CO: Family Foundational Int., 1998), 8.

See Diane Severance, "Susanna Wesley: Christian Mother," Christianity.com, May 3, 2010, https://www.christianity.com/church/church-history/timeline/1701-1800/susanna-wesley-christian-mother-11630240.html; Jackie Green and Lauren Green-McAfee, "The Praying Example of Susanna Wesley," Faithgateway, June 5, 2018, https://www.faithgateway.com/praying-example-susannawesley/#.XJu_QyhKhPY.

NYENZO

ZA UONGOZI

Nyenzo za Uongozi zimechaguliwa kwa umakini ili kukuandaa kushughulikia masuala husika ya kifamilia ya wakati huu wa sasa ukishrikiana na kanisa lako.

KWANI KUNA NINI
KATIKA USHOGA?

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

Ni jambo gani lililo kubwa katika ushoga? Wazee katika kanisa langu mara nyingi wanachukulia ushoga kama ni dhambi. Kwa nini iwe dhambi ikiwa Mungu alimuumba mtu jinsi hiyo? Kwani kuna tofauti gani mtu anapompenda huyu au yule? Je, ni kweli kwamba Mungu anategemea mtu aishi bila upendo maisha yake yote kama alizaliwa na silika ya ushoga? Nadhani hii siyo sawa, wewe unasemaje?

Swali lako ni moja ya maswali yanayoulizwa na Wakristo wengi waminifu wakijaribu kufahamu ukweli wa Mungu kuhusu suala hili la ushoga. Hata hivyo katika jamii ya kileo iliyoshambuliwa na sauti kengeufu zinazoonekana kama kweli fulani, siyo vigumu kuchanganya maadili ya Kikristo na maadili ya kidunia ya kibinadamu yanayotafuta kuridhisha wengi. Kwa hiyo tunaanza kwa kukuomba utafakari ujumbe ambao Biblia inatupatia kuwa, "Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni." (1 Wakorintho 2:14)

Katika kitabu cha Mwanzo tunaona mpango wa awali wa Mungu wa masuala ya ngono ukilenga moja kwa moja katika ndoa ya wenzi wawili kati ya mwanamume na mwanamke anaposema kuwa, "Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na mkewe, wala hawakuona haya." (Mwanzo 2:24, 25)

Dhambi ilipoingia duniani kupitia katika chaguzi za wazazi wetu wa kwanza yaani Adamu na Hawa, sayari yote ilighubikwa na ukosefu wa utii kwa Mungu, na matokeo yake yalikuwa ni kifo, pamoja na uwepo wa ukengeufu katika asili ambao haukutokana na mpango wa Mungu wa uumbaji. Kwa hiyo katika jitihada za Mungu za kuwaokoa wanadamu, badala ya kuwafanya wapitie uzoefu wa matokeo ya dhambi, yaani kifo, mtume Paulo anawasilisha kuwa, "Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati; kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu." (1 Wathesalonike 4:3-5)

Mungu anaendelea kufafanua mipaka ya mahusiano ya kingono kwa wale ambao wanachagua kuwa mitume wake katika ujumbe wa Paulo kwa Wakorintho kuwa, "Basi kwa habari ya mambo yale mliyoandika, ni heri mwanamume asimguse mwanamke. Lakini kwa sababu ya zinaa kila mwanamume na awe na mke wake mwenyewe, na kila mwanamke na awe na mume wake mwenyewe." (1 Wakorintho 7:1, 2). Hapa tena Mungu anaainisha mipaka ya vitendo vya kingono ndani ya ndoa ya mume mmoja na mke mmoja, na kama jambo la hatari ambalo linatakiwa kuondoa ukosefu wa uadilifu kingono.

Biblia pia inatushirikisha orodha ya watu ambao hawatakuwa na nafasi katika umelele wa Mungu - hao ni pamoja na wale wanaojihusisha na vitendo visivyo vya kimaadili vya ngono kati ya mwanamume na mwanamke, hasa inaposema kuwa, "Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti," (1 Wakorintho 6:9)

Ukweli ni kuwa, mfuasi wa Yesu anakuwa na sifa ya kujitoa kafara na utii wa kanuni zake kuhusu mwelekeo wa kingono wa mtu. Hata hivyo, ikiwa mtu ana mwelekeo wa ushoga au mwelekeo wa ngono ya mume kwa mke, ambao hauko chini ya utashi wa Yesu Kristo – ikimaanisha kwamba ni wanafunzi wa Yesu watiifu – watu kama hao watakuwa kwenye matatizo. Biblia bila kupinda pinda inaeleza kuwa, "Wakati huo Yesu aliwaambia wanafunzi wake, Mtu ye yote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate." (Mathayo 16:24). Hii ni changamoto ya kila mfuasi wa Yesu, bila kujali mwelekeo wake wa kingono.

Shauku yetu kubwa ya kupenda na kupendwa iliwekwa ndani yetu na Mungu wakati wa uumbaji. Alitufanya tuwe na shauku ya upendo wake kuliko vitu vingine. Upendo mkubwa ulio thabiti, usio na masharti ni upendo wa Mungu. Yesu mwenyewe anasema kuwa, "Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake." (Yohana 15:13). Jambo hili ndilo hasa Yesu alilofanya kwa ajili yetu sote, kwa sababu anatupenda kwa namna iliyo bora kuliko upendo mwingine wowote unaoweza kuupata hapa duniani. Tunapokuwa tumejazwa na upendo wake unaostahimili, tunawezeshwa kuwapenda wengine kwa usafi wa upendo wa Mungu. Upendo huu usije ukachanganwa ya mvuto au msukumo wa ngono – ambayo ndiyo namna upendo unavyotafsiriwa katika muktadha wetu wa kileo.

Pamoja na kwamba mahusiano ya upendo wetu wa kibinadamu mara nyingi hayana msimamo, yakivunjika mara kwa mara bila uhalisia, bado tunaweza kuutegemea upendo usiopimika na uwepo wa Yesu katika maisha yetu. Ni dhahiri anavyotuambia kwamba, "… na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." (Mathayo 28:20)

Tunaweza kupata ukubali, msamaha, kurejeshwa, na wokovu katika Kristo bila kujali asili ya dhambi yetu – hata kama ni vitendo vya ushoga – ikiwa tutaitikia kwa utii. Tunaona uthibitisho huu pale Yesu alipomwambia yule mwanamke aliyeshikwa katika uzinifu kuwa, "… Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena." (Yohana 8:11)

Tunatumaini kwamba kile tulichoshiriki kitakupatia fursa ya kuakisi zaidi nia ya Mungu kwa wafuasi wake. Tunaendelea kukuombea.

KUNIDHAMISHA WATOTO WETU
KWA UPENDO

NA DAVID & BEVERLY SEDLACEK

Wazazi wanashika nafasi ya Mungu katika maisha ya watoto wao. Kabla Watoto hawajajenga uhusiano binafsi na Mungu, wanajifunza kumhusu Yeye kwa uzoefu kupitia kwa walezi wao wa msingi. Mbegu za upendo zinaamshwa katika ukaribisho wa upendo anaopata mtoto mchanga anapozaliwa, heshima na ajabu ya kuzaliwa kwao, na jinsi mzazi anavyomwangalia mtoto machoni kwa upendo. Katika kukua kwa mtoto huyu hadi ukomavu, mbegu hizi zinachanua na kuwa mimea ambayo itatoa tunda, tunda la Roho: upendo, furaha, amani, na kadhalika. (Wagalatia 5:23)

Bahati mbaya wazazi wengine hawawezi kuwakaribisha watoto wao kwa upendo kama huo. Wazazi wanaoandamwa na kiwewe cha utoto ambacho hakikuwahi kupona, ambao hawakupata uzoefu wa mtu fulani kuwaona, kuwabembeleza, kuwahakikishia usalama, hawawezi kuwapatia watoto wao kile ambacho wao wenyewe hawakukipata. Tunasoma katika Torati kuwa, "Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, nawapatiliza wana uovu wa baba zao; hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao." (Torati 5:9). Neno uovu linamaanisha namna iliyopinda inayomharibu mtoto katika kumrekebisha. Utafiti katika makovu kama hayo unatusaidia kuelewa kwamba watoto wanapitia katika uzoefu wa athari za kuumiza za kiwewe cha vizazi vilivyopita. Hebu tuone kiwewe cha kiroho wanachopitia watoto mikononi mwa wazazi walio na nia njema.

Unyanyasaji wa kiroho katika familia ni aina fulani ya kutelekezwa, au ya kiwewe cha kimhemuko na kisaikolojia. Baadhi ya wazazi wanashindwa kumimina ndani ya watoto wao hali ya kiroho. Hawazungumzi nao kumhusu Mungu au kuhusu uhalisia wa kiroho. Hawa wazazi wanaweza kuwa wema na wenye upendo, na kwa jinsi hiyo wakaakisi upendo wa Mungu, lakini watoto wao wasiwe na mfumo wa kiroho wa kuweka uhalisia wao. Njaa ya kuwa na Mungu inapandwa, lakini mbegu zinashindwa kuchanua kwa sababu ya kupuuzwa au kutelekezwa kiroho.

Wazazi wengine wanaojitambulisha kama Wakristo wanaweza kuwa wamefundishwa mtazamo uliojengeka katika kumwogopa Mungu. Mpaka hapo watakaporejea kutazama upya kwa karibu, jinsi walivyopata uzoefu wa Mungu kupitia kwa wazazi

wao, watakuwa wanahamisha mtazamo huu wa Mungu kwa watoto wao bila kujua. Aina hii ya unyanyasaji wa kiroho ina sura nyingi sana. sura mojawapo inajitokeza pale wazazi wanapowataka watoto wao kutii ili wapate kupendwa na kukubaliwa. Yesu aliunganisha upendo na utii pale aliposema kuwa, "Kama vile Baba alivyonipenda mimi, nami nilivyowapenda ninyi, kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu; kama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake." (Yohana 15:9-10). Watoto wanapooneshwa upendo vizuri, watakuwa tayari kufanya kile ambacho wazazi wao wanawataka kufanya.

Aina moja ya unyanyasaji wa kiroho iliyozoeleka inajitokeza pale wazazi wanapotaka kuwatawala watoto wao, kwa kufanya hivyo wakashindwa kuwafundisha jinsi ya kufanya maamuzi. Pale wazazi wanapowaamulia watoto wao, ujumbe kwa watoto ni kwamba, "Ni lazima nifanye maamuzi kwa ajili yako kwa sababu hauna uwezo wa kufanya hili na lile wewe mwenyewe." Ni lazima watoto wahimizwe na kuwezeshwa kufanya mamuzi stahiki katika umri sahihi mapema iwezekanavyo. Watoto wanafaidi kutoka katika uongozi wa wazazi wanapofanya maamuzi na kukua katika mchakato huo huku wazazi wakiwasaidia katika kupitia matokeo ya maamuzi yao. Hatima ya huu mwingiliano kati ya wazazi na watoo ni pamoja na kuimarisha uhusiano na kuhamisha hekima kwa kizazi kinachofuata.

Sura nyingine ya unyanyasaji wa kiroho ni katika kutumia Biblia au maandiko ya Ellen G. White kama rungu la kuwachapia watoto. Kupeleka ujumbe kwa watoto kwamba hawafikii kiwango ambacho Mungu anatazamia kwa namna ambayo siyo ya kuelekeza kwa upendo, bali kuwadhalilisha au kuwakataa. Kufanya hivi kunajenga mtazamo wa aibu ndani ya mtoto. Unyenyekevu wa kinafiki unapeleka ujumbe wa uelewa kwamba hatuwezi kufikia kipimo cha matazamio ya Mungu, na kwamba ni vigumu kumridhisha. Huu unyenyekevu wa kinafiki kwa juu juu utaonekana kama hali ya kiroho. Hata hivyo inahitaji uangalifu mkubwa ili kutenda kwa ukamilifu kuweza kustahili upendo wa Mungu, au kuhakikisha kuwa hakasiriki.

Sayansi ya neva inadhihirisha kwamba uangalifu mkubwa unajenga wasiwasi na kusababisha msongo. Sehemu ya ubongo inayoitwa "amygdala" inahusika katika kuchunguza hatari zilizopo katika mazingira ya ndani na ya nje. Vitisho vikiwa vikubwa, hiyo sehemu ya ubongo ya "amygdala" inapeleka ishara na kuagiza mfumo wa huruma kujiandaa kupambana au kukimbia. Ikiwa vitisho havistahimiliki, mtu ananywea. Mfumo huo wa huruma unapokuwa katika msongo kwa muda mrefu, kinga ya mwili inaathirika, ndipo sehemu ya ubongo inayokupatia kufikiri inapooza. Upendo, ukuaji, mabadiliko, na tafakuri yenye afya inapungua pale hofu inapoongezeka (Jennings, 2020)

Hakuna hata mfumo mmoja wa jinsi hii unaoweza kujenga mazingira ya ukaribu au uhusiano wenye Imani kwa Mungu. Mtoto anaweza kufahamu kwamba Mungu ni

halisi lakini lazima awekwe mbali nasi kwa sababu anapasa kuogopwa. Mawazo ya mtoto yasiyokusudiwa yanaweza kuwa haya, "Kama Mungu angenifahamu, asingenipenda; angenikataa milele." Ukweli kwamba wanapendwa kwa upendo wa milele (Yeremia 31:3) unaweza siku zote kuwa sawa na ndoto za mchana kwao.

Kitu cha kuumiza zaidi kwa mtoto ni kiwewe cha kiroho ambacho kinatokea pale wazazi wanapowanyanyasa watoto wao kimwili wakidai wanawanidhamisha. Mara nyingi neno fimbo limeeleweka vibaya katika maandiko haya, "Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe; Bali yeye ampendaye humrudi mapema." (Mithali 13:24) pamoja na "Fimbo na maonyo hutia hekima; Bali mwana aliyeachiliwa humwaibisha mamaye." (Mithali 29:15). Kutokueleweka kwa neno hili kumewafanya wazazi wakawapiga sana watoto wao wakidai wanawapa nidhamu. Ile fimbo ya mchungaji ilitumika katika kuwaongoza kondoo na fimbo ya kujihami ilitumika katika kupigana dhidi ya wanyama washambuliaji walipojaribu kuwadhuru kondoo. Ellen G. White anapendekeza kwamba adhabu ya fimbo itumike kama uchaguzi wa mwisho kabisa baada ya kutumia mbinu zingine zote na kushindwa, tena fimbo hiyo itumike kwa upendo siyo kwa hasira. Mtoto anaweza kujenga dhana kwamba, Mungu ni mkatili na mnyanyasaji, na dhana hiyo ikakuzwa zaidi pale nidhamu kama hiyo inapotolewa na wazazi wakiwa na hasira. Agano la Kale na Agano Jipya yanafundisha kwamba upendo uwe kichocheo cha nidhamu ya mzazi. (Mithali 3:11-12; Waebrania 13:5)

Maneno yanaweza kuwa na athari. Yanakuwa kama mishale inayojeruhi hasa inapotupwa katika moyo wa mtoto. Moja ya hitaji la msingi la upendo kwa mtoto ni kuthibitishwa. Wazazi wanapojielekeza katika vigezo hasi vya uwepo wa mtoto, kwa mfano: 'Ungapaswa kupata A tupu katika mtihani wako,' 'Wewe siyo mzuri kama mdogo wako,' 'Wewe ni bure kabisa,' na kadhalika, vigezo hivyo vinamfanya mtoto ajenge mawazo hasi yenye kumjenga katika namna ya kujinyanyapaa. Hali hii inakomaza hisia za mashaka na wasi wasi kwa mtoto kuhusu thamani yake na stahiki yake. Hizi shoroba za neva ni vigumu sana kufutika. Hisia za mtoto za kujitambua na kujiona wa thamani zinajengwa kwa maneno na vitendo vinavyopeleka jumbe zilizo hasi. Kuna haja ya kutengeneza shoroba mpya za neva zitakazojengeka katika ukweli wa thamani ya mtoto, huku akijua kwamba yeye ni mtoto wa Mungu mwenye thamani isiyo na kikomo.

Unyanyasaji wa kingono una athari inayoangamiza kabisa katika mtazamo wa mtoto hasa anavyomchukulia Mungu. Mzazi anaposhindwa kumlinda mtoto wake kutoka katika wanyanyasaji, hisia za mtoto kumhusu Mungu kama mlinzi zinadhurika. Hasira za mtoto mara nyingi zinahamishiwa kwa Mungu, mtoto anakuwa na mawazo kwamba, "Mungu, kwa nini umeruhusu hili litokee kwangu? Kama ungenipenda, usingeruhusu hili likanitokea!" Ikiwa mzazi anayedai kumtumikia Kristo atamnyanyasa mtoto, swali analobaki nalo mtoto huyo ni kwamba, "Kwa nini Mungu

unipatie mzazi aliyechanganyikiwa kama huyu?" Mtazamo wake mwenyewe unaweza kuwa potovu kiasi cha kujichukia mwenyewe na kujiona kama chombo cha ngono na hivyo, akaanza kukumbatia maisha haribifu ya ngono katika namna ya uasherati na hata ukahaba, au akawa mraibu wa picha za ngono.

Matokeo ya kiwewe cha kiroho ni pamoja na hali iliyovurugika ya dhamiri ya ndani, na hata mtazamo wa ulimwengu ulio potovu. Hali iliyovurugika ya dhamiri ya ndani inajitokeza kama msongo baada ya kiwewe kama vile kumbukumbu zilizovurugika, hali ya kuweza kukasirishwa kirahisi, kujifanya kuwa makini kuliko kawaida, wasiwasi, msongo, kufa ganzi kwa baadhi ya viungo, kujitenga na watu, kuigiza mambo (kujifanya), kutokufanya mambo kwa ukamilifu, na kuvurugkikiwa kabisa. (Freedman, 2006). Mtazamo potovu wa kilimwengu ni pamoja na mambo ambayo mtu anadhani kwamba ni kweli, kama vile kuamini kwamba anakosea kwa sababu ya kiwewe cha nyuma, akidhani kwamba hayuko salama, au akiamini kwamba aina fulani ya watu ni hatarishi kwake au kwa wengine. (Panchuk, 2018)

Uponyaji unaanza kwa kutambua kiwewe cha kiroho kilichowahi kutokea. Wengi wanajikuta katika jumuia za kiroho zisizo na afya na kwa hiyo wanaikataa ile hali yao ya kiwewe cha kiroho. Wanaweza kuwa na hali ya kutokuelewa au kutokutambua hali halisi ya kiroho. Mara nyingi kunakuwa na haja ya kufumua mtazamo potovu wa mtu kumhusu Mungu na kujenga upya dhana iliyo sahihi. Watu wazima wengi bado wanahifadhi taswira potovu ya Mungu waliyojifunza katika utoto wao, na hivyo ni lazima kurejea upya katika sifa za Mungu waliyechagua kumwamini. Watoto na watu wazima ni lazima wawezeshwe kujifunza kusema "Hapana" na kujenga mipaka yenye ustawi katika safari yao ya uponaji. Itakuwa bora kwao kufanya kazi hii muhimu mara wanapomfahamu Mungu wa uelewa wao kwa namna binafsi.

Hatua hizo zinafungua mlango kwa ajili ya kuanza kuvumbua ulimwengu unaowazunguka kwa namna mpya na ya kusisimua. Watakuwa wametoka katika gereza la kiroho walipokuwa wamefungwa kwa muda mrefu. Wana uwezo wa kupata uzoefu wa Mungu kwa namna inayowezesha ukuaji wao binafsi. Mapito haya yanakusudia kuleta uzoefu wa Mungu akiwa pamoja nao, akiwaongoza na kukua pamoja nao. Baadhi ya watu wanajifunza kutoka katika uzoefu wa wengine wanaoweza kuhusiana nao na visa vya maisha yao. Wengine wanaweza kuhitaji msaada wa tabibu mwenye uelewa wa kiwewe. Kama utagundua kwamba uko kati ya wale ambao wamekuwa na kiwewe cha kiroho, tunakukaribisha uanze safari hii yenye maumivu ya uponaji.

REJEA:

Freedman, Karyn (2006) "The Epistemological Significance of Psychic Trauma." *Hypatia* 21 (2): 104–125. http://dx.doi.org/10.1111/j.1527-2001.2006.tb01096.x.

Jennings, Timothy (2013). The God Shaped Brain: How changing your view of God transforms your life. Downers Grove, IL: Intervarsity Press.

Panchuk, Michelle. THE SHATTERED SPIRITUAL SELF: A PHILOSOPHICAL EXPLORATION OF RELIGIOUS TRAUMA Res Philosophica, *Vol. 95, No. 3, July 2018, pp. 505–530 http://dx.doi.org/10.11612/*

ATHARI ZA MAJONZI

KIAKILI

NA CLAUDIO & PAMELA CONSUEGRA

Rachel McKinley alifariki juma moja baada ya mume wake kufariki akiwa na umri wa miaka hamsini. Kwa nini inatokea mara nyingi wenzi waliozeeka wanafariki pamoja, au vifo vyao vinapishana kidogo? Je, kuna kitu kama kufa kwa sababu ya moyo uliovunjika? Kulingana na Chama cha Moyo cha Marekani (American Heart Association), ishara za moyo uliovunjika, wakati mwingine hali hiyo ikiitwa 'athari za msongo kwa mfumo wa moyo' (Stress-induced Cardiomyopathy or Takotsubo Cardiomyopathy) zinaweza kuonekana kwa mtu mwenye afya. Ni dhahiri kwamba wanawake wana uwezekano mkubwa wa kupata uzoefu wa maumivu makali ya ghafla yanayoweza kusababishwa na matukio ya kimhemuko yanayoleta msongo; kama vile kifo cha mpendwa, talaka, usaliti, kukataliwa na kadhalika - kuliko wanaume.

Kwa hiyo tunafahamu kwamba majonzi yanaweza kusababisha madhara kimwili. Majonzi pia yanaweza kusababisha ugonjwa wa akili. Hanskey na Clayton (2008) wanaandika kuhusu masomo ya mlalo yaliyogundua kwamba mwezi mmoja baada ya mtu kufiwa, takribani asilimia 40 walikumbana na tukio la huzuni. Habari njema ni kwamba msongo unaosababishwa na majonzi unapungua baada ya muda, na baada ya mwaka mmoja, ni asilimia 15 tu ya watu wote hao ndiyo inabakia katika hali nzito ya msongo. Kulingana na Hanskey na Clayton (2008) wakati mwingine kwa uchache, majonzi yanaweza kusababisha kichaa au kuanzisha dalili za ugonjwa huo.

MAJONZI NI NINI?

Tunahitaji kutulia kwa muda na kuzungumza kwa kifupi kuhusu majonzi, ambayo ni maumivu makali yanayoandamana na upotevu. Na hasa kifo kinapohusu mpendwa wetu, mtu aliyekuwa karibu na sisi, tunapitia katika uzoefu unaotofautiana na uzoefu mwingine wowote kwa pamoja. Kama vile Consuegra na Consuegra (2021) wanavyoeleza kuwa, "Pamoja na kwamba huzuni haihusu tu kufiwa, inapotokea kwamba kifo kinamhusu mpendwa, inaweza kuwa ni hisia za huzuni iliyochanganyika

na hatia, na kuchanganyikiwa, hasa ikiwa uhusiano ulikuwa imara." C. S. Lewis anajaribu kueleza hisia hizo za majonzi kama ifuatavyo:

> "Hakuna aliyewahi kuniambia kwamba huzuni inakaribia kufanana na hofu. Mimi siogopi, lakini hsisia hizo zinafanana na kuogopa. Kama vile tumbo kuhama, kutokuwa na amani, kupiga miayo, ni kama niliendelea kumeza kitu kisichokuwapo." (Lewis, 1978, uk.1)

Mwanasaikolojia wa Kiswisi aitwaye Elizabeth Kubler-Ross (1969), alianzisha kitu alichokiita mfano wa hatua tano za majonzi katika kitabu chake kilichouzwa sana, kiitwacho "Juu ya Kifo na Kufa" (*On Death and Dying*). Wakati akifanya kazi ya kuhudumia wagonjwa waliokuwa katika hatua za mwisho za maisha yao, aligundua uzoefu wa kufanana ulioonekana kwa wagonjwa wake wengi. Hicho alichogundua kilimfanya aunde mfano uliompatia umaarufu mkubwa, ingawaje wengine wakimwelewa vibaya na kumshutumu. Mwanzoni aliandaa mfano unaoelezea mchakato wa kufiwa, lakini hatimaye alitumia mfano huo kusimamia kila aina ya majonzi, hasa yale yanayoshuhudiwa na yule anayekata roho. Kubler aligundua kwamba kila mmoja alipitia uzoefu wa hizo hatua tano za majonzi na kwamba baadhi ya watu wanaweza kurejea katika hatua fulani baada ya majuma kadhaa au hata miezi hadi kifo chao. Na wapendwa wao wanaweza kupitia hatua moja au zaidi katika hizo hatua kwa miaka mingi au hata maishani mwao. Shutuma nyingi za huo mfano zilitokana na Imani iliyoeleweka vibaya kwamba kila mmoja anapitia hatua hizo kwa mpangilio, kwa maana kwamba hatua moja inafuata nyingine hadi mwisho. Kwa mfano huu hapa chini

Hata hivyo, Kubler-Ross alieleza kwamba, hatua hizi hazifuatani kwa msitari ulionyooka, na baadhi ya watu wanaweza kupitia katika uzoefu wa hatua moja au mbili badala ya zote tano, au tatu, na kadhalika. Inaweza kuwa rahisi kuelewa uzoefu huu kama mwitikio ambao mtu anaweza kuwa nao kwa ugonjwa badala ya kujali hatua anayopitia. Mtaalam anayeshughulika na vivimbe vinavyosababisha saratani Robert Buckman (1989) anaunganisha na mwitikio wa namna nyingine walio nao watu kama vile hofu, wasiwasi, tumaini, na hatia. Fikiria kwa muda kuhusu kupanda na

kushuka kwa kila mwitikio wa mhemuko tuliopitia hapo juu. Kama tungeunganisha katika grafu, ungeonekana kama ifuatavyo:



Hatari nyingine ya kufanya kwa jinsi hii ni kwamba tunaweza kuwa tunafikiri kwamba mtu huyu anayeelekea kukata roho anapata uzoefu wa hisia moja au zaidi kwa mpangilio. Badala ya kufikiria hatua hizi kama utendaji mmoja baada ya mwingine, chukulia kama mwitikio wa kimhemuko ambao mtu anaweza kuwa nao wakati mmoja au mwingine au mara kadhaa kwa wakati mmoja, au katika nyakati mbali mbali. Wakaweza kuwa na hali hiyo kwa kitambo, kisha wakaingia katika hatua nyingine, lakini baada ya uzoefu huu, hali hiyo inarudi tena. Wanaweza kupata uzoefu wa hali mbali mbali, zikipingana kadiri inavyoonekana wakati mmoja huo. Unaweza pia kuuona kama mpira wa hisia na hali ambazo zinavingirika kuingia na kutoka, zikienda na kurudi pasipo uwezo wa kuzitawala, kuzibadilisha wala kusizuia. Inatokea tu.

Hebu tazama umbo hilo hapa pembeni kama kielelezo:

Badala ya kurikiria kuhusu uzoefu wa mwitikio kwa utambuzi wa ugonjwa mzito unaokaribia kuondoa uhai kwa namna ya mapito yanayofahamika katika mchakato wa huzuni, ambayo haina ukweli kwa mtu yeyote, fikiria kama uhalisia mpya wa mapito ya huzuni yalipopinda pinda na kuvurugika

Inachanganya, na kukasirisha, inavunja moyo na ni ya pakee kwako na kwa wale unaowapenda. Thamani ya kufahamu hili ni kwamba inaweza kumsaidia mtu anayepitia hali hii ya mwitikio wa mhemuko kuelewa kwa nini anajisikia hivyo, na kwamba ni nini kinachotokea kwake, na kuwa namna anavyojisikia ni kawaida tu. Inakusaidia kama rafiki au mlezi kuwa msaidizi mwenye ufanisi kwa mgonjwa huyo anayeelekea hatua zake za mwisho wa masiha yake hapa duniani.



Kwa nini baadhi ya watu wanamudu kuhimili huzuni hadi wakafikia hali ya kawada, lakini wengine wanagota katika bonde la uvuli wa huzuni? Inawezekana kwamba wengine huwa tayari wameshakuwa na tatizo la akili linaloongezewa na hali hiyo ya huzuni au majonzi, au maumbile ya akili, au matumizi ya ugonjwa wa akili, uraibu, au mabadiliko fulani ya ubongo ambayo yamefanya iwe vigumu kuchakata upotevu wake.

Kazi ya kuhuzunika siyo mapito yaliyonyooka yasiyo na vikwazo, bali wakati fulani ni mapito yaliyojawa na mikwaruzo na fujo nyingi, yakitupeleka katika hisia tofauti, mwitikio tofauti, na uzoefu unaoturudisha mara nyingi katika hali ya awali. Hata baada

ya miaka mingi, kitu fulani kinaweza kuanzisha kumbukumbu zinazoturudisha nyuma katika majonzi ya zamani baada ya wapendwa wetu kufariki, hata kwa muda mfupi. Kate Bowler anaandika kuwa, "Nilikuwa nikidhani kwamba huzuni inahusu kurejea kuangalia nyuma, watu wa zamani wakiwa wamejikunja kwa majuto, au vijana wakifikiria kile ambacho wangepata. Sasa ninaona kuwa inahusu macho kuchungulia katikati ya machozi katika kesho isiyoweza kuingilika. Ulimwengu hauwezi kuumbwa upya kwa nguvu za upendo. Ulimwengu mkatili unadai kujisalimisha katika kile kisichowezekana – kujitenga. Kuvunjika. Mwisho usiokuwa na mwisho." (Bowler, 2019, uk. 79). C. S. Lewis pia anaelezea uzoefu wake kwa uhalisia na kwa uzuri sana:

> "Nilidhani ningeweza kuelezea hali: tengeneza ramani ya huzuni. Hata hivyo, huzuni inageuka kuwa siyo hali bali ni mchakato. Haihitaji ramani, bali historia, na kama wakati fulani sitaacha kuandika historia hiyo, hakuna sababu kwa nini niachae. Kuna kitu fulani kipya cha kuelezea kila siku. Huzuni ni kama bonde refu, linalopinda pinda ambapo kila panapopinda panadhihirisha mwonekano mpya wa ardhi. Kama nilivyokwisha kudokeza, siyo kila palipopinda panapoonesha huo mwonekano mpya wa ardhi. Wakati mwingine jambo la kushtukiza ni lile lililo kinyume; unaoneshwa aina ya nchi uliyodhani umeiacha kilometa kadhaa nyuma yako. Hapo ndipo unaposhangaa ikiwa bonde hilo siyo korongo linalozunguka. Kumbe siyo. Kuna kujirudia rudia mara chache, lakini mtiririko huo haujirudii." (Lewis, 1978, uk. 68-69)

MCHAKATO WA KUHUZUNIKA

Kama tulivyoanza hapo awali, kuhuzunika ni mchakato, safari binafsi kuelekea katika kujifunza kuishi maisha mpya ya kawaida bila wapendwa wetu. Mchakato huu wa kuhuzunika unahitaji ufanye mambo ambayo yatakusaidia kuendelea kuelekea katika kupona na kurejea. Tunapendekeza yafuatayo

1. **Jipatie wakati wa kupona.** Hakuna ratiba fulani au mpangilio fulani wa jinsi ya kuhuzunika. Ni safari yako binafsi, na ni wewe mwenyewe unayeweza kuamua kasi ya kwenda katika mapito hayo. Kama vile Chuck Swindoll (2009) anaelezea, "Urefu wa kipindi cha kupona kwa mtu hauwezi kutoa taarifa yoyote kuhusu hali yake ya kiroho. Mchakato wa kuhuzunika au wa majonzi ni mchakato wa mtu mwenyewe na ni wa pekee kama vile zilivyo alama za vidole." Kwa hiyo basi, jipatie muda wa kupona kihisia, kuendeleza utaratibu, kupata mapumziko ya kutosha, na kuhakikisha hautumii nguvu nyingi, bali kuelekeza nguvu zako katika kupona. Na siku zote kumbuka kwamba hauko peke yako. Kukosa kujipatia muda wa kuhuzunika kutafanya hali izidi kuwa ngumu baadaye katika maisha, na ni wewe peke yako unayeweza kuamua ni lini na jinsi gani ya kuhuzunika. Smith na Jeffers wameandika kuwa:

> "Waombolezaji lazima wawajibike na kuamua kama utafika wakati wa kukoma kuhuzunika, au kukua kupitia katika uzoefu wa kutokwa na mpendwa, na uchaguzi

wowote utakaochukuliwa, utakuwa na matokeo ya muda mrefu. Siyo wachache walioomboleza baada ya mpendwa wao kuwatoka kwa mauti waliosema kuwa, "Afadhali wangenizika mimi pia." Lakini haiwi hivi, labda ufanye uamuzi huo. Kwa bahati, baadhi ya watu wamepoteza maisha baada ya wenzi wao au Watoto wao kufariki. Lakini mazishi yalicheleweshwa kwa miaka mingine mitano hadi ishirini na mitano." (Smith & Jeffers, 2001, uk. 4)

2. Fikiria. Jambo la kushangaza ni kwamba badhi ya watu watapendekeza kinyume na kukuambia "usiyafikirie hayo, yaondoe mawazoni mwako." Kama vile Chaplain Yeagley anavyoshauri kwamba, "Ninakutia moyo kwamba, usiogope fikira zako. Acha zijitokeze" (Yeagley, 1984, uk. 27). Kwa mfano, ikiwa utakumbuka mahali fulani maalum na tukio, nenda mahali hapo na katika fikira zako, rejea tukio lile na kumbukumbu nzuri zinazozalishwa na tukio lile. Nyumbani kwako, jaribu kutembelea shoroba za kumbukumbu kwa kujaribu kuingia chumba kimoja baada ya kingine ukikumbuka mambo yaliyotokea katika kila kimoja, maneno yaliyokuwa yakizungumzwa, na kumbukumbu ambazo zilifanyika.

3. Zungumza na wengine. Pata muda wa kuwa na marafiki na wengine; usijitenge. Kuzungumza kuhusu matukio ya maisha yako wakati ulipokuwa na huyo mpendwa wako, tangu mlipofahamiana hadi mwisho ni tiba, lakini pia inaweza kukusaidia kukubali uwezekano wa kuwa na mahusiano yenye maana baada ya kifo cha mpendwa wako. Kwa maneno mengine, kufanya hivyo kutakusaidia kuona kwamba kuna maisha na kuna watu ndani ya hayo maisha, kwamba maisha yako hayajafikia ukomo kwa sababu tu uhai wa mpendwa wako umefikia ukomo.

4. Andika kile kilichoko katika fikira zako na kile kilichomo moyoni mwako. Tunza kwenye shajara yako. Andika kwa undani hisia zako zilizoambatana na hicho kilichoko katika fikira na moyoni mwako. Ikiwa ulipata hisia za hasira, usiache kuandika na kueleza sababu ya kukasirika. Ikiwa ulijisikia mpweke, andika ukielezea, ikiwa uliogopa, ulichanganyikiwa, ulikatishwa tamaa, au pengine ulikuwa na siku nzuri, ukijawa na uzoefu wa furaha, jielekeze katika hilo pia.

5. Jiachie katika kulia. Pamoja na kwamba wale wanaokupenda na kukujali wanakuambia usilie, tunakushauri kujiachia katika kulia, acha machozi yatiririke kwa uhuru. Ni kweli kwamba kutakuwa na watu ambao hawajisikia vizuri wakikuona unalia, lakini Jennifer Stern anaandika kuwa:

> "Siyo kazi ya mwenye majonzi kuwafanya wengine wasijisikie vizuri katika mtazamo wao wa huzuni. Ni kazi ya mwenye majonzi kuhuzunika. Kuhuzunika ni namna hai ya kuhisi na kuonesha majonzi. Ikiwa machozi yako yataonekana kuwafanya wengine wasijisike vizuri, waeleze ukweli wako kwa utulivu, wafundishe kuhusu machozi yako. Waambie kwamba ninalia kwa sababu nina huzuni. Ninalia kwa sababu nina masikitiko makubwa kwa kutokwa na mpendwa wangu. Ninalia kwa sababu siku zote maisha yaliyokuwa matamu kwangu yatakuwa ni uchungu. Ninalia kwa sababu hakuna

> maneno ya kutosha kuelezea jinsi ninavyojisikia. Ninalia kwa sababu nina ujasiri wa kutosha kukabili siku nyingine, kustahimili na kusukuma mbele, kuishi na majonzi moyoni mwangu. Ninalia kuonesha, kukumbukia, na kuachia.

6. **Pata hisia za maumivu.** Kushughulikia kutokwa na mpendwa kwa namna yenye afya kunaweza kuwa ni njia fulani ya kukua na kuleta mabadiliko maishani. Kwa hiyo, endelea katika uzoefu huu wa majonzi. Hiyo kwa kweli ni namna yenye afya ya mchakato mzima. Wakati huo huo, hakikisha uwiano mzuri, wenye afya kwa kuunganika tena na walio hai kupitia katika kitendo cha kutoa na kupokea. Rafiki yangu mwema, mchungaji, mlezi na mshauri anayeitwa Tucker anaelezea kuwa, "Safari ya majonzi ina alama za kuonesha umbali. Kadiri unavyozipita, unatambua kwamba unasogea. Ukizipuuza, itakugharimu." (Tucker, 2018, uk. 37)

Unaweza pia kupuuza au kukataa hasira, na kwa kufanya hivyo ukazidisha tatizo na kurefusha safari yako ya kupita kwenye huzuni, au unaweza kuipatia jina, kuikubali, na kuidhihirisha (dondoo namba nne hapo juu), na kuiachia.

7. **Jihudumie mwenyewe – kimwili.** Siku chache za mwanzo baada ya kifo cha mpendwa wako, unaweza kukosa hamu ya kula, au kukosa kabisa nguvu za kusogeza mguu mmoja baada ya mwingine. Lakini ni muhimu kama sehemu ya uponaji wako baada ya kufiwa, na katika huzuni hiyo, kuwa makini katika kuhakikisha unakula, unakunywa, na kuwa na utaratibu wa kufanya mazoezi.

8. **Chukua likizo kutoka katika huzuni.** Hii ni dhana nyingine tunayojifunza kutoka kwa rafiki yetu mpendwa Mike Tucker. Siyo jambo lenye ustawi kuzama katika huzuni saa ishirini na nne, siku nzima, siku saba za juma, mwenzi hata mwezi. Mike anashauri kwamba uchukue likizo kutoka katika huzuni. Kwa maneno yake anasema kuwa:

> "Dhana ya likizo kutoka katika huzuni inaweza kuwa ni rahisi tu kama vile kwenda kuogelea, kusoma riwaya, au kutazama muvi. Au unaweza kuamua kusafiri kwenda sehemu ya mapumziko mwisho wa juma au hata kukaa huko juma moja au mawili. Mimi nilienda kucheza Golf mara kwa mara ili kuondokana na maumivu yangu, hata niliabiri chombo cha majini na kuzunguka sehemu mbali mbali katika jitihada za kupumua kutoka katika huzuni." (Tucker, 2018, uk. 122)

Ikiwa tutakupatia ushauri wa utendaji, kadiri unavyosafiri katika mapito haya ya majonzi, ingekuwa vyema kama ungejiachia katika mchakato mzima. Usijaribu kujizuia, usiukatae, usiupuuze. Kufanya hivyo kutakuletea hali hasi ya kimwili hata kiakili. Pamoja na maumivu yake, na ugumu wake, hatimaye kupita katika mapito haya kutakuwa ni hatua yenye afya kwako.

Angalizo la Mwandishi: Sehemu za Makala hii zimechukuliwa kutoka katika kitabu chetu kiitwacho "Kusaidia Kuandika Sura za Mwisho: Kuhudumia wanaokufa na wale

wanaowapenda" *(Helping Write the Final Chapter: Ministering to the dying and those who love them,* published by AdventSource, 2021)

REJEA

American Heart Association (n.d.) Is Broken Heart Syndrome Real? Retrieved from: https://www.heart.org/ en/health-topics/cardiomyopathy/what-is-cardiomyopathy-in-adults/is-broken-heart-syndrome-real#. WJITI1MrKUk

Bowler, K. (2019). Everything Happens for a Reason: And Other Lies I've Loved. Random House: New York.

Buckman, R. (1989) I don't Know What to Say: How to help and support someone who is dying. Random House: New York.

Hensley, P. & Clayton, P.J. (2008). Bereavement-related Depression. Retrieved from: https://www.psychiatrictimes. com/view/bereavement-related-depression

Kübler-Ross, E. (1969). On Death and Dying. Scribner: New York.

Lewis, C. S. (1978) A Grief Observed. Bantam: London (4th ed.)

Smith, H.I, and Jeffers, S. L. (2001). ABC's of Healthy Grieving: Light for a Dark Journey. Shawnee Mission Medical Center Foundation: Shawnee Mission, KS.

Stern, J. (2017). Tears. Transformative Grief. Transformativegrief.com. Downloaded from: https:// transformativegrief.com/2017/12/01/tears/

Swindoll, C. (2009). Hope Beyond the Hurt. Insight.org. Downloaded from: https://www.insight.org/resources/ article-library/individual/hope-beyond-the-hurt

Tucker, M. (2018) Tears to Joy. Pacific Press: Nampa, ID

Yeagley, L. (1984). Grief Recovery. Yeagley: Muskegon, MI

NAMNA YA KIUME

YA KUONGOZA

NA JEFF BROWN

Jamani, siyo kujisifu bali nimeshinda sehemu yangu ya medali za riadha. Maeneo yangu makubwa katika shindano hili yalikuwa, kuruka juu, mbio za umbali wa mita 200, na mbio za kupokezana vijiti. Katika mbio za kupokezana vijiti kuna jambo moja lililoniumiza: kimbia katika uchochoro wako mwenyewe. Ukivuka na kuingia katika uchochoro wa mwenzako tu, utaonekana haufai. Basi ngoja nikuambie kwamba ni wapi ambapo Makala hii haigusi.

Makala hii haihusu uongozi wa wanawake. Haihusu kile ambacho wanawake wanapaswa kufanya na kile ambacho hawapaswi kufanya. Wanawake watajisemea wenyewe. Makala hii inahusu uongozi wa wanaume. Kile tunachotakiwa kuwa na kile ambacho hatutakiwi kuwa. Tunachopaswa kufanya na kile ambacho hatupaswi kufanya. Hebu tujichunguze kwa haki, kwa undani na kwa kweli, kisha tuwaamini wanawake wetu kwamba wanaweza kufanya vivyo hivyo.

Mara nyingi tunakuwa wagumu kwa wengine ila laini kwetu wenyewe. Yesu alituagiza kwa kurudia rudia kwamba tuwe laini kwa wengine na kuwa wagumu kwetu sisi wenyewe. Hakusema kwamba hilo kundi jingine halina makosa. Alichoagiza ni hiki: "Au utamwambiaje nduguyo, Niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe! Mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe?" (Mathayo 7:4) na kwa hili, akashauri kwamba, "…Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe." (Yohana 8:7). Lengo letu katika riadha hii ni kukimbia katika uchochoro wetu wenyewe, kwa sababu nimeshashuhudia ile hali ya kuonekana haufai inavyofanana.

Mimi na mke wangu, Pattiejean tulikuwa tunaendesha semina kwa vijana kule Manchester, Uingereza. Katika zoezi moja, mimi nilienda na vijana mahali fulani, mke wangu akabaki na wasichana. Kazi tuliyotakiwa kufanya ni kuorodhesha jinsi tunavyoweza kuwa, au kile tuanchoweza kufanya ili kuboresha mahusiano. Nilikuwa na chati mgeuzo na kalamu yenye wino mzito tayari kwa hao vijana. Sikuwa nimejiandaa kwa kile walichoshusha.

Walianza kushusha: "Wanatakiwa kufahamu mipaka yao." "Wanatakiwa kutulia ninapokuwa na marafiki zangu." "Wanatakiwa kufahamu mahali pao." "Wanatakiwa kufahamu wakati wa kuzungumza na wakati wa kukaa kimya." Yaani kila mmoja alimhamasisha mwenzake hadi muda wa kurudi kuungana na wana wa kike ukafika. Wana wa kiume waliingia ndani kama jeshi. Wakiwa wameimarishwa na kauli ya kila mmoja, waliendelea kubadilishana huku wakiingia.

Wana wa kike walisisimka kwa zoezi hilo. Walikuwa wameorodhesha kwa shauku kila walichoweza kufanya kwa ajili ya wanaume. Wangekuwa wavumilivu, wa kuvutia, wangefanya kazi kwa bidii, wangekuwa na shauku ya mema, wangekuwa waaminifu. Ndipo waliposikia: sauti kama za jeshi linaloingia.

Mazungumzo ya wana wa kiume yaliwafadhaisha. Walisikia maneno: "Safari hii tutawaambia…" "Sasa watatusikiliza…" Upendo wote uliyeyuka ndani ya wana wa kike. Wana wa kiume walipoingina tu, walifunika chati mgeuzo yao. Tabasamu ziligeuka kuwa nyuso zilizokunjamana, na mikono iliyokuwa imejiachia sasa ilikunjwa. Wanaume hawakutazama chati mgeuzo ya wanawake. Nililia ndani yangu kwa sababu wote, wanaume na wanawake wamepotezana. Wote walionekana hawafai.

Viongozi wa kanisa na Norman Miles wanaelezea kisa cha mtu aliyevunja nyumba ya mganga wa kienyeji. Alipoamshwa na sauti ya wadukizi, alichukua bunduki yake na kuwatangazia hao wezi: "Enyi watu, sina maana ya kumdhuru mtu, lakini nakaribia kupiga risasi kuelekea hapo mliposimama."

Makala hii itapitia nafasi ya mwanamume katika uongozi kulingana na mtazamo wa Kiblia. Kuelewa jukumu letu kunaweka umuhimu katika kutambua utume wetu: "Kurejesha ndani ya wanaume na wanawake ule mfano na sura ya Muumba wao, kuwaleta tena katika ukamilifu ule walioumbwa nao – hii ilikuwa ndiyo kazi wa ukombozi." Hapa tunapata muhutasari wetu, matendo matatu ya igizo la kibiblia: Uumbaji, Kuanguka, na ukombozi. Safari yetu itapita kwenye milima na mabonde, pongezi na shutuma, kuthibitishwa na kukatishwa tamaa. Ninaweza kupiga risasi hapo uliposimama – ila sikusudii kukudhuru.

UUMBAJI

Maandiko yako wazi – wanaume na wanawake waliumbwa kwa mfano na sura ya Mungu na wote kwa pamoja wakapewa utawala juu ya dunia. "Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatiishe na kutawala… dunia yote… kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Hapa tunaona dhahiri chimbuko la mwandamu, pamoja na kumbukumbu za imbingu zikieleza wazi wazi kwamba hakuna namna ya kuwa na hitimisho lenye makosa." Hili

ni hitimisho gani lisiloweza kuhojiwa? "Mungu alipomuumba Hawa, alikusudia kwamba asiwe na hali yoyote ya udhalili, wala ubora na ukubwa kuliko mwanamume, bali katika mambo yote wawe sawa.

Richard Davidson anatoa maoni yake kuwa, "Tunajifunza kutoka katika Mwanzo moja kwamba mwanamume na mwanamke walishiriki kwa hali ya usawa katika mfano na sura ya Mungu. "Kwa hiyo Mungu alimuumba mwanamume [Kwa kiebrania, *ha'adam,* yaani ubinadamu] kwa mfano wake mwenyewe. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba." Wote waliagizwa wazi wazi kwa namna iliyo sawa bila kubagua; kutiisha na kutawala, siyo kumtawala mwenzi wake, bali wote kwa pamoja kutawala viumbe vingine vyote vya uumbaji wa Mungu kwa utukufu wa Muumbaji.

Dhana kwamba mwanamke aliumbwa kutoka kwenye ubavu ni moja ya vigezo ambavyo wanaume wengi wanashikilia na kujichukulia utawala kwa makosa. Hata hivyo, majukumu waliyopewa yalikuwa shirikishi katika uumbaji, hakuna dokezo kwamba kulikuwa na cheo kwa mtu mmoja dhidi ya mwingine. Dhana kwamba kuumbwa kwa Hawa kulifuata kuumbwa kwa Adam siyo kigezo kinachoamua cheo kubwa kwa Adamu, ingawaje Uumbaji hauelezei hicho kisa katika mpangilio wa kushuka au umuhimu.

> "Watetezi wa jinsia ya kike, pamoja na watetezi wa mfumo dume, wote wanahitaji kukombolewa."

Katika kitabu cha Mwanzo 2 inaelezwa wazi wazi kwamba mpango mzima ni mali ya Mungu. Mungu anamletea mwanamume usingizi mzito. Hajui ni nini kinachoendelea, hana ufahamu, hawezi kuitikia, wala kuwajibika. Hitaji halikuwa kukamilisha jukumu au majukumu fulani, bali kushirikiana katika majukumu. Mungu aliumba mzingira ambamo wanaume na wanawake wangehitajiana. "[Yesu] Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke?" (Mathayo 19:4). Kwa hiyo, "… siyo mfumo dume wala mfumo jike unaomaanisha tofauti katika cheo au utendaji."

Uumbaji wa mwanamke ni muhimu kwa mada ya wanaume katika uongozi kwa sababu Maandiko yanaonesha muunganiko usioweza kutenganishwa. "Bwana Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya." (Mwanzo 2:18). Werner Neuer anatafsiri kimakosa neno "Msaidizi" na anahitimisha kwamba mwanamke ni msaidizi, mtegemezaji, aliye katika nafasi ya pili. Neno la Kiebrania la "msaidizi" limetumika kwa wingi sana katika Agano la Kale kumwelezea Mungu mwenyewe, na kwa hiyo ni neno ambalo halitumiki kumaanisha majukumu ya chini ya mwanamke: "Mungu wa baba yangu alikuwa msaada wangu"

(Kutoka 18:4), naye alitoa msaidizi (Mwanzo 2:18) ili kumtoa mtu katika ombwe la upweke."

Uongozi katika bustani ya Edeni ulikuwa shirikishi. Wote wawili walikuwa ni viongozi na wote walikuwa wasaidizi. Ellen G. White anasema kuwa, "Mungu alimuumba mwanamke kutoka kwa mwanamume ili wawe mwenzi na msaidizi wake, atakayekuwa sawa naye, ili kumfurahisha, kumtia moyo, na kumbariki. Na upande mwingine mwanamume alitakiwa kuwa msaidizi menye nguvu kwa mwanamke." Uongozi katika Bustani ulikuwa ni uongozi uliokuwa sawa. "Hakutakiwa kumtawala mwanamume kama kichwa, wala kumkanyaga miguuni mwake kama kitu dhaifu, bali kusimama pembeni yake katika hali ya usawa, kupendwa na kulindwa na mwanamume. Uongozi katika bustani ya Eden ulikuwa ni uongozi wa kushirikiana. Frances na Paul Hiebert wanakubaliana kwamba Adamu na Hawa walikuwa na furaha kamilifu kabla ya anguko, "uhusiano wa ukomavu mkuu na usawa." Ellen G. White anasema kuwa, "Katika uumbaji Mungu alikuwa amemfanya Hawa sawa na Adamu. Wangebakia katika utiifu mkamilifu kwa Mungu – kwa upatanifu na sheria kuu ya upendo – wangeendelea kuwa na upatanifu wao kwa wao." Kwa hiyo, "uhusiano mkamilifu wa kibiblia wa mume na mke hauhusu usawa bali ukomavu, kushirikiana katika kila hatua ya maisha."

ANGUKO

Katika kitabu cha Mwanzo sura ya tatu kuna kumbukumbu ya anguko la binadamu. Nafasi ya Adamu na Hawa baada ya anguko ni ile ya mwanamke kutawaliwa na mume wake. "na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala." (Mwanzo 3:16). Dhambi ilikuwa imeleta ukosefu wa upatanifu, na sasa muunganiko wao uliweza kuendelezwa na upatanifu ukalindwa pale tu mmoja alipojiweka chini ya mwingine akatawalilwa. Hawa alikuwa wa kwanza katika uasi: alikuwa ameanguka katika majaribu kwa kujitenga na mwenzi wake kinyume na maelekezo ya mbingu. Ni kwa ushawishi wake kwamba Adamu alianguka katika dhambi, na kwa hiyo sasa alitakiwa kumtii mume wake na mume wake kumtawala."

Wanateolojia wanakubaliana kwa wingi na utambuzi huu. Walter Brueggeman anatoa maoni yake: "Katika bustani ya Mungu kama mapenzi yake yalivyo, kulikuwa na ushirika wenye usawa. Katika bustani ya Mungu sasa kumejipenyeza kutokuaminiana, kuna utawala na upotoshaji. Lakini huo upotoshaji siyo haukubaliki hata kidogo kama mapenzi ya mwenye bustani."

David na Diana Garland wanasema kuwa: "Matokeo ya dhambi yao yalikuwa ni ya kutisha kwa uhusiano wao: sasa mume alikuwa ni mtawala dhidi ya mke wake. Hii hali

mpya inamaanisha kwamba huu sasa siyo uhusiano ambao Mungu aliukusudia tangu awali."

Ellen G. White anasema kuwa, "Kama kanuni zilizoanishwa na sheria ya Mungu zingeshikiliwa na hawa walioanguka, tamko lililotamkwa japo chimbuko lake ni katika dhambi, lingekuwa ni mbaraka kwao; lakini mwanadamu aliopotumia vibaya uwezo, lakini pia alivyotumia vibaya fursa alizopewa; lakini kwa mwanadamu kutumia vibaya ukuu aliokuwa amepewa kumesababisha uchungu mkubwa kwa mwanamke na kufanya maisha yake kuwa mzigo."

Kadiri muda ulivyopita, ule mfano na sura ya awali iligeuka na kuwa sura ya mbali na isiyoonekana dhahiri. Upotoshaji uliwaongoza siyo tu kutumia vibaya mamlaka waliyopewa, bali pia kutumia vibaya fursa walizopewa. Garland na Garland wanasema kuwa, 'Ule mpangilio wa mamlaka katika ndoa ulikuwa ni pungufu kwa ule Mungu alioukusudia kwa mwanadamu… Huo unaonekana kama ukengeufu kutoka katika kusudi la Mungu.

Ellen G. White pia anasema kuwa, "Bwana wetu Yesu Kristo hakuwakilishwa kwa namna iliyo sahihi katika uhusiano wake na kanisa ndani ya wanaume wengi katika mahusiano yao na wake zao, kwa sababu hawafuati njia ya Bwana. Wanadai kwamba wake zao lazime wawatii katika kila jambo. Lakini huo haukuwa mpango wa awali wa Mungu kwamba mwanamume awe mtawala, kama kichwa cha kaya, wakati yeye mwenyewe hajisalimishi kwa Kristo. Ni lazima awe chini ya utawala wa Kristo ili kwamba aweze kuwakilisha uhusiano wa Kristo na kanisa. Ikiwa ni mtu mwenye vurugu, mwenye kujiona, mbinafsi, mkali asiyevumilika, hebu na asitamke neno kwamba mume ni kichwa cha mkewe, na kwamba ni lazima atii katika kila jambo; kwani yeye siyo Bwana, yeye siyo mume kwa maana halisi ya neno hilo."

Ubinadamu uliangukia kwenye dhambi iliyoharibu ile halisi ya Mungu. Kama Gilbert Bilezikian anavyosema kuwa, "Yale maneno kwamba 'naye atakutawala' yasije yakachukuliwa kama ndiyo makusudi ya Mungu, kama vile tu kifo kisivyochukuliwa kama mapenzi ya Mungu, wala agizo lake. Phyllis Trible anasema kuwa: "Tunanyanyasa tukiamua kwamba maamuzi haya ni agizo. Yanaelezea, wala siyo agizo. Yanalinda siyo kwamba yanapuuza… Kauli hii (ya Mwanzo 3:16) siyo ruhusa ya ukuu wa mume, bali ni lawama kwa mfumo wenyewe. Vitendo vya ukandamizaji, na kujiinua ni upotoshaji wa uumbaji."

Lazima kuwa waangalifu sana ili kuhakikisha kauli na nukuu zinakidhi "sheria na… ushuhuda" (Isaya 8:20). Kwa sababu kuna kuvuka viwango kuelekea kushoto na kulia. Ndiyo maana Mary Stewart Van Leeuwen anathibitisha kuwa: mifumo yote miwili, yaani mfumo dume na mfumo jike yote inahitajika kwa ajili ya ukombozi.'

UKOMBOZI

Dunia inashuhudia vita – na wakati huo huo tukijiuliza kwamba, ni kwa nini. James anauliza kuwa, "Chanzo cha vita na sababu ya ugomvi kati yenu ni nini? Yote haya hayatokani na tamaa inayosababisha vita ndani yenu?" (James 4:1, HCSB). Pamoja na kuwa na mwenendo wa ukandamizaji na wa kulaumu nje ya kanisa, ni lazima turudi na kuchunguza mwenendo wa unyanyasaji ulio ndani ya kanisa. Ellen G. White anaunganisha haya mawili kuwa, "Ni lazima nipate maagizo maalum kutoka kwa Mungu kwa ajili ya watu wake, kwa kuwa hizi ni nyakati za hatari. Huko duniani, uharibifu na vurugu vinaongezeka sana. Uwezo wa wanaume unaendelea kupungua kanisani; wale waliopewa jukumu la kushika nafasi kanisani wanadhani kwamba ni haki yao isiyojadiliwa kutawala.

"Uwezo wa wanaume" ni shauku ya kutawala ambayo watu wengine wanafikiri ni haki ya kimbingu. Hii husababisha unyanyasaji mkubwa unaoleta uovu. Yesu alisema kuwa huu "haukuwa mpango wa awali wa Mungu." Ninawaelekeza katika mpango wa awali" (Mathayo 19:8). Kwani mpango wa awali ulikuwaje? Ellen G. White anasema kuwa, "Mwanamke anatakiwa kushika nafasi ambayo Mungu alikusudia tangu mwanzo, yaani kama anayelingana na mume wake.

Kabla hali ya kupenda uongozi haijaanza kanisani, ni lazima idhihirishwe nyumbani; "Urejeshwaji na kuuinua ubinadamu kunaanzia nyumbani." Hapa msisitizo wa kibiblia siyo zaidi juu ya utiifu wa mke kwa mumewe, bali katika badiliko halisi linalotazamiwa katika mwenendo wa mume. "Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili." (Waefeso 5:23).

Ikiwa tutakosa ule upya wa Agano Jipya, tutakuwa tumekosa kila kitu.

Dhana elekezi hapa ni uongozi na kujisalimisha. Neno la Kigiriki la "kichwa" (*kephale*) limetumika mara 75 katika Agano Jipya, halikuwahi kuhusisha hali ya utawala. Uongozi wa mwanamue haupeleki ishara ya ukuu; na kule kujisalimisha kwa mke hakumaanishi kwamba huo ni udhaifu. Mume hana jukumu la uongozi, bali ni upendo usiokuwa na ubinafsi wa kujitoa mhanga, upendo wa agape. Kujisalimisha kwa mke ni hali ya kuchagua kwa uhuru kuukubali upendo wa Kristo. Kwa hiyo, kujisalimisha siyo utashi wa mume, bali ni upendo wa mume. Elizabeth Achtemeire anaelekea katika Waefeso 5 kwa uongozi na kujisalimisha kwa namna ya ubunifu mkubwa. Kule kujisalimisha kunahifadhi mtazamo wa kitamaduni wa mwanamume kama kichwa cha familia, lakini hata hiyo hali ya kuwa kichwa ni katika utendaji tu, siyo katika masuala ya hadhi na ukuu. Uelewa wa hali ya kuwa kichwa na uhusiano wa mwanamke ni dhana zilizobadilishwa sana."

Kwa mtazamo wa S. Miletic: "Aya hiyo ni rahisi kwa namna idanganyayo. Ina kila namna ya kunaswa katika mtazamo wa kidunia wa mfumo dume na inaweza kueleweka vibaya kama ukandamizaji wa mfumo dume. Kwa sehemu kubwa ni "kondoo katika ngozi ya mbwa mwitu." Kwa hiyo ni lazima isomeke katika nuru ya ujumbe wake kiteolojia kuhusu nguvu ya kuishi kwa wengine badala ya sababu ya kuhalalisha ukandamizaji wa mfumo dume, na nama fulani ya kupinga asili ya upendo wa agape." Na kwa William Barclay: "Msingi wa aya hiyo siyo kutawala; bi upendo."

Magumu siyo mzigo wa wanadamu, ni mzigo wa mume. Mfano wa mume wa hali ya kuwa kichwa nyumbani unaakisi hali ya kichwa ya Kristo, na unatakiwa kudhihirisha mamlaka ya kiroho katika kanisa linalowekwa katika utendaji na mwanamume na mwanamke. Kujisalimisha siyo sehemu ya mwanamke; bali ni ya mke. Mfano wa mke wa kujisalimisha nyumbani, unaakisi kujisalimisha kwa Kristo, unatakiwa kudhihirisha utiifu wa kiroho katika kanisa linalowekwa katika utendaji na viongozi ambao ni mwanamume na mwanamke pamoja na wafuasi.

Hali ya kuwa kichwa nyumbani haiwezi kulinganishwa na hali ya kuwa kichwa kanisani. Mwanamume anaweza kuwa kiongozi wa familia yake nyumbani, lakini mke wake au watoto wake wanaweza kuwa ndio viongozi wake katika jamii au kanisani. "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa." (Waefeso 5:31, 32)

KWANI KUWA "MPYA" KUNAHUSIANAJE NA JAMBO HILO?

Kauli mbili za Biblia zinaweka msingi wa kile kinachotakiwa kuwa au kutokuwa uongozi wenye upendo: "Lakini haitakuwa hivyo kwenu…" (Mathayo 20:26) na "Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo." (Yohana 13:34) Suala lililopo katika kauli hizi kwa muktadha wake, ni kwamba lazima pawepo na badiliko kubwa kati ya uongozi kanisani na ule utawala wa duniani.

Ellen G. White ametoa maoni yake kuhusu agizo la Yesu la kupenda kama alivyowapenda, (Yohana 13:34): "Kwa wanafunzi wa Yesu, agizo hili lilikuwa jambo jipya; kwa sababu hawakuwa wanapendana wao kwa wao kama Kristo alivyowapenda… Agizo hili la kupendana wao kwa wao liklikuwa na maana mpya katika nuru ya kujitoa kwake mhanga. Kazi yote ya neema ni kazi endelevu ya upendo, ya kujikana nafsi, katika jitihada za kujitoa kafara."

Garland na Garland anakubaliana kuwa, "Ni dhahiri halikuwa jambo jipya kuwaambia waume wawapende wake zao, bali upendo huu unapewa upeo mpya pale upendo wa Kristo unapokuwa kipimo kwa watu wake…. Kristo alipenda kupitia katika kafara

yake; alikuwa tayari kulipa gharama kubwa na kumfurahia mpendwa wake (kanisa), hata kama hakustahili upendo huo. (Warumi 5:8). Alipenda bila masharti. Alipitia katika uzoefu wa kushindwa kwa wapendwa, bado akajitoa mwenyewe ili kuwashinda. Huu ndio upendo ambao mume anatazamiwa kuwa nao kwa mke wake, na ni dai nyeti lisilolinganishwa katika ulimwengu wa kale."

Tukiukosa ule upya wa Agano Jipya, tutakuwa tumekosa kila kitu. Sasa kulikuwa na kipimo kipya cha upendo; upendo ulio tofauti kabisa kutoka katika desturi na tamaduni. Kipimo kipya hiki kilikuwa na uwezo wa kudhoofisha unyanyasaji wa jamii iliyo chini ya utawala fulani kama watumwa, bila kudai mabadiliko ya jamii. "Upendo kama huo hauna mfano."

Sasa kuna mahusiano ya wawili kwa pamoja. Ni lazima pawepo kujisalimisha kwa wote wawili ikiwa kutakuwa na ufanisi katika mahusiano. (Waefeso 5:21). Hata hivyo wake wana wajibu wa kuwaheshimu waume wao, na wanaume sasa wanapaswa kuwapenda wake zao kama Kristo naye alivyolipenda kanisa (Waefeso 5:21). Kama David Field anavyofikiria kwamba, "Paulo sasa haonekani kupata ufumbuzi wa mgogoro uliopo kati ya mtazamo wa wanawake wanaoshikilia huu mtazamo mpya wa Kikristo na mtazamo aliorithi kutoka kwa Wayahudi wa kale." Kwa hakika Paulo alipozungumza kuhusu wanaume katika uongozi, alikabiliana na changamoto za kuweka divai mpya katika kiriba cha zamani. Yesu pia alikabiliana na changamoto hiyo hiyo: "Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake. " (Luka 6:40). Huo ndio uongozi.

Kuna mpangilio mpya wa mahusiano. Kiongozi sasa ndiye mtumwa. Yule aliyekuwa mkubwa sasa ndiye mdogo, wa mwisho ndiye wa kwanza. Hakuna tena Myahudi, wala Mmataifa. Mwanamume wala mwanamke, aliye katika ndoa na asiye katika ndoa. Hizo tofauti zipo, lakini umuhimu wake umesalimishwa kwenye utume wa kanisa. chaguzi zinasalimu amri katika wito, matakwa yanasalimishwa kwa vipaumbele, na hisia zinazidiwa na kujitoa.

Muundo wa Agano Jipya wa uongozi unafanana na ile halisi ya Mungu katika uumbaji. Kuondoa ule ukuu au kujisalimisha katika familia na kanisani, kunafunika ustahimilivu na usawa katika familia na kanisani, hadi kufikia kujisalimisha katika umoja huo. Muundo huu wa kibiblia wa uongozi haubagui wala kumkweza mmoja dhidi ya mwingine. Usawa haupuuzwi, bali unavuka kiwango. Mamlaka hayaelekezwi kwa binadamu, bali yanajikita kwa Kristo.

Kuna kutegemeana kati ya mume na mke ambako kuliharibiwa na anguko na kusiribwa katika ukombozi. Huku kutegemeana katika ndoa unapaswa kuonekana kanisani. Mwelekeo saa siyo katika kuanguka kwa mwanamke wa Mwanzo 3, bali ni

wito wa mwanamke katika Matendo 2. Siyo suala la jinsi ya kiume au ya kike tena, bali ni suala la yule aliyetuma.

JUKUMU LA MWANAMUME.

Je majukumu ya uongozi yanategemea jinsia – au katika hali hasi yanategeme usahihi? David Williams anasema kuwa, "Watu wengi katika jamii yetu wana mtazamo wa majukumu yaliyoainishwa kijamii kwa waume na wake kama yaliyoanzishwa na Mungu kwa ajili ya tamaduni zote, jamii zote na nyakati zote." Alitambua kwamba fungu, "Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu," (Waefeso 5:22) ni fungu maarufu sana linalitumiwa kuhalalisha unyanyasaji wa wanaume kwa wake zao: "Wake wengi wanakubali vurugu kama sehemu waliyopangiwa na Mungu katika maisha." Anakubali kwamba baadhi ya waume wanadhani kwamba Maandiko yanawapa uhuru kutumia unyanyasaji wa nguvu katika jitihada zao za 'Kwa maana nimemjua ya kwamba atawaamuru wanawe, na nyumba yake baada yake waishike njia ya Bwana…' (Mwanzo 18:19)

Kuna jukumu la kutegemeana kati ya wanaume na mwanawake. Naam, "mama ni malkia wa nyumbani, na watoto wanamtegemea, lakini Watoto ni wa mume pia kama walivyo wa mke, na yeye pia anawajibika kwa ustawi wao." Naam, mume ni kuhani na mama ni mwalimu, lakini Ellen G. White anawaita baba na mama makuhani na vichwa vya familia. Wazazi wanasimama kama vichwa vya familia, makuhani wa kaya, kama waalimu na waawala ni lazima "Watii mamlaka iliyo juu."

Garland na Garland wameendelea kusema kuwa, "Maandiko hayaweki matazamio katika jukumu fulani maalum au kutoa mwongozo wa jinsi ya kufanya katika ndoa. Jambo lililo wazi ni kwamba Mungu haagizi majukumu ya uhusuiano kulingana na jinsia. Katika roho hiyo, wenzi walio katika ndoa wanaweza – ni lazima – kuchagua kuelekeza maisha yao yajae katika muktadha wao na wajibu walioitiwa."

Shauku ya mwanamume ya ukubwa ilitakiwa kubadilishwa kuwa upendo uanzishao. "Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu;" (Warumi 12:10). H. Page Williams anasema kuwa, "Mara nyingi ninazungumza na wanaume wanaosema, 'Mimi nitabadilisha mtazamo wangu mke wangu atakapobadilisha wa kwake.' Lakini kwa mtazamo wa Mungu, waume wanatakiwa kuanzisha upendo, na wao kama viongozi wa kiume wanatakiwa kuanzisha upatanisho. Siyo suala la kujisalimisha, bali ni suala la kuwa mkweli na kushika nafasi ya kuongoza katika majukumu uliyopewa na Mungu.

> Magumu yanayojitokeza nyumbani siyo sawa na magumu yanayojitokeza kanisani.

Pasiwepo msitari kwenye mchanga ambao wanawake hawapaswi kuuvuka. Hasa sisi wanaume, tusije tukachora msitari. Katika pambano kuu kati ya Yesu na Shetani, ishara ya uharibifu ni mwanamume. "Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja…." (Warumi 5:17). Katika pambano hili kuu, ishara ya wokovu ni mwanamke. "Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu" (Ufunuo 12:17). Kwa hiyo ni jambo la kushangaza kwamba tunawaza kuhusu wanawake kuungana na wanaume katika kutangaza injili.

Hebu jiulize kama jambo hili linaonekana kama kiongozi wa kiroho: "Ni Mariamu ndiye alihubiri kwa mara ya kwanza kuhusu kufufuka kwa Yesu…. Kama kuna wanawake ishirini mahali ambapo kwa sasa yupo mmoja, ni nani anayeweza kufanya huu utume mtakatifu uwe ni kazi wanayoifurahia, tunatakiwa kuona wengi wakiongoka na kufuata ukweli." "Mwokozi atawaangazia nuru ya uso wake wale wanawake wanaojitoa kafara, na hiyo nuru itawapatia uwezo utakaozidi ule wa wanaume. Wanaweza kutenda kazi katika familia kuliko ile wanaume wanayoweza kutenda, kazi ambayo inafikia maisha ya ndani. Wanawake wanaweza kufika karibu na mioyo ya wale ambao wanaume hawawezi kuwafikia. Kazi yao inahitajika." "Tunaweza kusema bila kukosea kwamba kazi bainishi za wanawake ni takatifu, kuliko zile za wanaume."

Tunasimama katika hofu ya vipaji vya wanawake na namna wanavyoinuliwa kuongoza wengine. Ellen G. White anasema kuwa, "Kazi ya Mungu wakati huu kwa namna maalum inahitaji wanaume na wanawake walio na sifa kama za Kristo katika kazi, uwezo wa utendaji, na nguvu kubwa ya kazi, ambao wana mioyo iliyojaa wema yenye huruma inayoingilika, yenye kutumia mantiki bila kuegemea upande wowote katika maamuzi…. Wakijaribu kwa kudumu kuinua na kurejesha ubinadamu ulioanguka." "Pale kazi kubwa na ya kuhitimisha inapotakiwa kutendeka, Mungu anachagua wanaume na wanawake wa kuifanya, na kutakuwa na hasara kama talanta zao wote hazitaunganishwa.' Maandiko yanakazia majukumu tofauti, lakini kamwe hayathibitishi vyeo.

UFUASI

Maumivu ya vita vinavyosababishwa na wanadamu yanafanana kwa uovu na maumivu ya mwanamume kumuua mkewe. Namshukuru Mungu kwamba leo hii bado tunaweza kupata wanaume waadilifu. Siyo tu kwamba utashangaa, bali utatambua kwamba kuna wanawake wacha Mungu wanaliona hilo – hata katikati ya maumivu yao hayo. "Hebu tukumbuke pia kwamba kuna wanaume katika dunia hii ambao wanatimiza jukumu walilopewa kwa namna ya kuvutia; jukumu la kujali na

kulinda, na tunahitaji kukiri na kuwakubali hawa watu na kwa kweli kutumaini kwa dhati kwamba wengine wangejitahidi kufuata mfano wa hao."

Pengine mwisho wa siku, hicho ndicho tunatachotaka – yaani watu kufuata mfano wetu. Paulo alisema kuwa, "Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo." (1 Wakorintho 11:1). "Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi." (Wafilipi 4:9). "Nanyi mkawa wafuasi wetu na wa Bwana, mkiisha kulipokea neno katika dhiki nyingi, pamoja na furaha ya Roho Mtakatifu. Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya." (1 Wathesalonike 1:6, 7). Wafuasi wanajiungamanisha na viongozi na hatimaye kuwa wanafunzi.

Pengine "ufuasi" umebezwa na uongozi ukakuzwa kuliko inavyostahili. Lengo la wafuasi na viongozi ni kuwa wanafunzi. "Akawaambia, Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu." (Mathayo 4:19). Becky De Oliveira anasema kuwa, "Kule kupenda viongozi badala ya wafuasi kulidhihirika katika kanisa ka Kikristo. Kuna semina zisizokoma zinazotengenezwa na vitabu vinaandikwa kwa lengo la kuelekeza watu jinsi ya kuwa viongozi, lakini kuna maelekezo machache sana ya kushughulikia ile maana ya kuwa mfuasi."

Lunden na Lancaster wanaafiki kuwa: "Sisi sote tunafahamu kwamba viongozi wanatazamiwa kuwa watu wa maono, maamuzi, mawasiliano, wenye nguvu, waliojitoa kwa dhati, na wawajibikaji. Lakini ni vipi kwa wafuasi? Je, sifa za wafuasi wenye mafanikio ziko tofauti kuliko zile za viongozi? Kwa nini siyo mtumishi anayeongoza? Bwana wetu na kiongozi wetu anasema kuwa, "…mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." (Mathayo 20:27). Moduli ya uongozi haiwezi kutupiliwa nje ya moduli ya familia. Kigezo kinachotofautisha katika huduma ya Kikristo siyo nani aongoze. Maandiko hayajali mpangilio wa madaraka. Wafuasi wakati mwingine ni viongozi, na viongozi mara nyingi wamekuwa wafuasi, na wote siku zote wamekuwa wanafunzi "waliotengwa na Mungu wazae tunda."

> Wanaume na wanawake kwa pamoja wanapaswa kurejesha na kuakisi ule mfano na sura ya Mungu kwa huduma yao iliyoungana katika ukombozi.

Hawa ndio ulimwengu unaowataka. "Hitaji kubwa la ulimwengu ni hitaji la wanaume na wanawake watakasimama imara, wasiweze kununuliwa wala kuuzwa, wale ambao ndani ya nafsi zao kabisa ni wakweli na waadilifu, Wale ambao hawaogopi kuiita dhambi kwa jina lake, wale ambao wana dhamiri safi na ya kweli katika wajibu kama vile sindano ya dira inavyojielekeza katika ncha, wale watakaosimamia haki hata kama mbingu zitaanguka."

Ni pale tutakapoelewa tu kimo cha muunganiko mmoja wa mwili katika uumbaji na kina cha uharibifu katika ule mfano na sura ya Mungu katika anguko, ndipo tutakapoelewa mapana ya huduma inayohitajika kurejesha kwenye ukombozi. Ule mfano na sura ya Mungu ilichafuliwa na dhambi za kujitegemea na za kuendekeza. Sura hiyo itarejeshwa na huduma ya muunganiko wa wawili katika mmoja. Wanaume na wanawake walikuwa pamoja kabla ya anguko. Walitengana na kujificha kwa pamoja kutoka mbele ya Mungu. Sasa wanaume na wanawake wanapaswa kuwa pamoja katika urejeshwaji. Siyo vinginevyo.

Wanaume na wanawake kwa pamoja walipinga na kuharibu mpango wa Mungu kwa kuunganisha hatua zao zilizopotoka katika anguko. Wanaume na wanawake kwa pamoja ni lazima warejeshe na kuakisi mfano na sura ya Mungu kwa huduma yao iliyounganika katika ukombozi. Utambulisho ni lazima ufutwe na hadhi iondolewe, na Yesu ndiye kichwa cha wote. Hawa ni Adamu na Hawa waliorejeshwa. Ni Pambano kuu likihitimishwa. Ni kisa cha upendo wa dunia umemalizwa. Huo ni ule ukaribu katika ukubwa wake. Ni kujumuishwa kwa upana wake. Ni upendo katika upeo wake mkuu.

VUA KOTI LAKO

Kumbukumbu ya baba yangu iliyo dhahiri, yaani Maurice Brown ni ya majira ya baridi kule Birmingham, Uingereza. Tulikuwa tunasafiri kurudi nyumbani kutoka kwenye nyumba ya shangazi Rubby tukiwa na mama yangu na wadogo zangu wanne. Theluji ilikuwa ikidondoka kwa nguvu, na tulikuwa tumefika katika ule mtaa katikati ya mji palipoonekana dhahiri kuwa ni mtaa wa Kilimani. Tulikuwa na gari yenye uwezo mkubwa iliyoitwa Ford Zodiac, lakini ilikuwa haimudu. Magurudumu yakaanza kuzunguka, kisha tukasikia – tulianza kuserereka kurudi nyuma. Baba yangu kwa haraka kama mng'ao wa tochi alisimamisha gari na kuvuta breki ya mkono huku akisema, "Bakini hapa!" ninachokumbuka ni kuwa baba aliruka akatoka nje ya gari akavua koti lake na kuliweka chini ya magurudumu. Mara akarudi tena ndani ya gari akijaribu kuligeuza kwa ustadi (Baba alikuwa ametufundisha kuendesha gari), hatimaye tukamaliza kile kilima.

Sasa hivi baba yangu ana umri wa miaka 90, akifurahia miaka yake ya kustaafu kule Mandeville, Jamaica. Macho yake baba, kama vile Musa, bado hayajafifia, wala nguvu zake hazijapungua. Tunabaki tukiwiwa na baba yetu tukishukuru milele kwa siku tuliyoshuhudia kujiamini, kujali, na huruma, kutoka kwa mtu aliyetupeleka salama nyumbani. Sikumbuki kama mama alizungumza na baba kabla yake kuruka kutoka kwenye gari, lakini yeye kama mfanyakazi na mhadhiri katika chuo kikuu cha Oxford Brookes, nina uhakika kwamba lazima atakuwa alisema jambo.

Mama yangu hakukubaliana na falsafa ya "Mama wa nyumbani" ambayo wanawake wengi wanapenda kuikubali kutoka kwa wenzi wao kwa kushikana na mtazamo wa "Kubaliana na namna yake ya maisha. Kubali marafiki zake, chakula chake na mtindo wake wa maisha kama wa kwako vile." Wala mama hakuchukua tu analojia ya kumfananisha mwanamume kama meneja wa kampuni na mke wake kama meneja msaidizi "ambaye anafurahia kushiriki mawazo yake kuhusu utawala wa kampuni na hachukii anapopandwa kichwani."

> Mwelekeo sasa sio katika kuanguka kwa mwanamke katika Mwanzo 3, bali ni katika wito uliopo katika Matendo 2

Mama yangu alikuwa ni mke, mama, mhadhiri, na mwanaharakati – na wazazi wangu walikuwa wamekubaliana kwamba bibi yangu ahamie kwetu na kuishi nasi. Ellen G. White anasema kuwa, "Waadventista wa Sabato hawapaswi kwa namna yoyote ile kudhalilisha kazi ya mwanamke. Ikiwa mwanamke ataweka kazi zake katika mikono ya msaidizi mwaminifu mwenye bidii, na kuacha Watoto wake katika ulinzi bora, akajishughulisha katika kazi, konferensi na iwe na hekima ya kuelewa kwamba ana haki ya kupokea mshahara." "Swali hili siyo la watu kushughulikia. Bwana ameshalishughulikia."

Tumeshikika katika gari linaloserereka kuelekea katika uangamivu. Sababu za kuserereka ni nyingi na ngumu. Sauti za hasira zinafifia, na vidole vya lawama ni vingi. Lakini Mungu anawaita wanaume kufanya sehemu yao katika kuzuia kuserereka na kuhakikisha gari linafika linakoenda. Hatukuitwa kuacha uongozi; tumeitwa kuachana na utawala. Mungu anatuagiza kuweka utumishi mahali pa unyanyasaji.

Wakati umefika wa wanaume kuvua makoti ya nafasi walizo nazo na ile hali ya mamlaka, na kuyaweka chini ya magurudumu. Hebu nguvu yenu isiwekwe kwenye uwezo na kiburi. "Lakini Yesu akawaita, akasema, Mwajua ya kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu ye yote anayetaka kuwa mkubwa kwenu, na awe mtumishi wenu; na mtu ye yote anayetaka kuwa wa kwanza kwenu na awe mtumwa wenu; kama vile Mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." (Mathayo 20:25-28). Wanaume! Hebu tuvue makoti yetu.

Jeff Brown ni Katibu Mwenza wa idara ya Huduma ya Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato na mhariri mwenza wa gazeti la Ministry, ambalo ni jarida la kimataifa la wachungaji.

REJEA

[1] Bible texts credited to Phillips are from *The New Testament in Modern English* by J. B. Phillips, copyright © 1960, 1972 J. B. Phillips. Administered by The Archbishops' Council of the Church of England. Used by permission.

[2] Scripture quotations credited to MEV are taken from the Modern English Version. Copyright © 2014 by Military Bible Association. Published and distributed by Charisma House.

[3] Ellen G. White, *True Education* (Nampa, Idaho: Pacific Press Pub. Assn., 2000), p. 11.

[4] Ellen G. White, *Daughters of God* (Hagerstown, Md.: Review and Herald Pub. Assn., 1998), p. 22.

[5] Ellen G. White, *Testimonies for the Church* (Mountain View, Calif.: Pacific Press Pub. Assn., 1948), vol. 3, p. 484.

[6] Richard Davidson, *Flame of Yahweh: Sexuality in the Old Testament* (Grand Rapids: Baker Academic, 2012), p. 12.

[7] Texts credited to Message are from *The Message,* copyright © 1993, 2002, 2018 by Eugene H. Peterson. Used by permission of NavPress, represented by Tyndale House Publishers, a division of Tyndale House Ministries. All rights reserved.

[8] Gilbert Bilezikian, *Beyond Sex Roles: What the Bible Says About a Woman's Place in Church and Family* (Grand Rapids: Baker Book House, 1985), p. 21.

[9] Scripture quotations marked NLT are taken from the *Holy Bible,* New Living Translation, copyright © 1996, 2004, 2015 by Tyndale House Foundation. Used by permission of Tyndale House Publishers, Inc., Carol Stream, Illinois 60188. All rights reserved.

[10] See Werner Neuer, *Man and Woman in Christian Perspective* (Wheaton, Ill.: Crossway Books, 1990), p. 74.

[11] F. Hiebert and P. Hiebert, "The Whole Image of God," in C. Kettler and T. Speidell, eds., *Incarnational Ministry* (Wipf & Stock Pub., 2009), p. 272.

[12] Ellen G. White, *The Adventist Home* (Nashville: Southern Pub. Assn., 1952), p. 99.

[13] Ellen G. White, *Patriarchs and Prophets* (Washington, D.C.: Review and Herald Pub. Assn., 1890, 1908), p. 46.

[14] Hiebert and Hiebert, p. 31.

[15] E. G. White, *Patriarchs and Prophets*, p. 58.

[16] B. Kisembo, L. Magesa, and A. Shorter, *African Christian Marriage*(London: Geoffrey Chapman, 1977), p. 107.

[17] E. G. White, *Patriarchs and Prophets,* p. 58. (Italics supplied.)

[18] Walter Brueggeman, *Genesis: An Interpretation* (Atlanta: John Knox Press, 1982), p. 15. (Italics supplied.)

[19] David Garland and Diana Garland, *Beyond Companionship: Christians in Marriage* (Louisville, Ky.: Westminster John Knox Press, 1986), p. 29. (Italics supplied.)

[20] E. G. White, *Patriarchs and Prophets,* pp. 58, 59.

[21] Garland and Garland, p. 30.

[22] E. G. White, *The Adventist Home*, p. 117.

[23] Bilezikian, p. 41.

[24] Phyllis Trible, "Depatriarchalizing in Biblical Interpretation," *Journal of the American Academy of Religion* 41, no. 1 (March 1973): 41.

[25] Mary Stewart Van Leeuwen, *Gender and Grace* (Downers Grove, Ill.: InterVarsity Press, 1990), p. 208.

[26] Texts credited to HCSB are taken from the *Holman Christian Standard Bible,* copyright © 1999, 2000, 2002, 2003, 2009 by Holman Bible Publishers. Used by permission.

[27] E. G. White, *Testimonies for the Church*, vol. 9, p. 270.

[28] E. G. White, *The Adventist Home*, p. 231.

[29] Ellen G. White, *The Ministry of Healing* (Mountain View, Calif.: Pacific Press Pub. Assn., 1905), p. 349.

[30] Elizabeth Achtemeier, *The Committed Marriage* (Philadelphia: Westminster Press, 1976), p. 86.

[31] Stephen Francis Miletic, *"One Flesh"—Eph. 5:22-24, 5:31: Marriage and the New Creation* (Rome: Editrice Pontificio Instituto Biblico, 1988), p. 118.

[32] William Barclay, *The Letters to the Galatians and Ephesians* (London: Geoffrey Chapman, 1977), p. 107.

[33] Ellen G. White, *The Desire of Ages* (Mountain View, Calif.: Pacific Press Pub. Assn., 1898, 1940), pp. 677, 678.

[34] Garland and Garland, p. 36.

[35] Ellen G. White, *Steps to Christ* (Mountain View, Calif.: Pacific Press Pub. Assn., 1956), p. 15

PEMBETATU
ZA FAMILIA

NA SVEN OSTRING

Neno "pembetatu" katika mawasiliano ya familia huwa mara moja linaleta hisia hasi. Masengenyo, mawasiliano yasiyokuwa ya moja kwa moja, kuvunjika kwa mahusiano, na baadhi ya wanafamilia kutengwa, ni katika mambo machache tu. Maana yangu ni kwamba, ni nani angependa kuwa sehemu ya aina hii ya elimumwendo ya familia isiyokuwa na afya? Uhalisia kwa kweli kulingana na nadharia ya Murray Bowen ya mfumo wa familia, pembetatu ya uhusiano inahusika muda wote katika familia. Kuwa na watu wawili tu katika uhusiano ni kama hakuna uimara. Kwa kawaida hali ya asili ni kuleta mtu wa tatu na kujenga pembetatu ya familia.

PEMBETATU YA KALE YA FAMILIA

Hiyo kwa uhakika ilikuwa ni kweli katika familia yangu. Dada yangu na mimi ni mapacha, ambalo ni jambo maalum. Hata hivyo pamoja na kwamba umri wetu unafanana, bado tunatofautiana kwa haiba, na tuna mahusiano tofauti na wazazi wetu. Kama vile nilivyo na uhakika kwamba umaona, haichukui muda kwa mtoto kutambua kwamba ni mzazi gani anakuwa mzito unapoomba vitu vya kuchezea au chakula, hata kama mzazi mwingine ameshasema "Ndiyo!" Mara unapogundua hivyo, jambo la kufanya ni kutumia ulaini wa mzazi mmoja ili kupata kile unachotaka. Hiyo ni hali ya kawaida ya asili ya mwanadamu. Pembetatu za familia zinajengeka kirahisi.

Kuna elimumwendo nyingine ya uhusiano iliyo muhimu, na hiyo ni kujitofautisha mwenyewe. Nilitumia miaka mingi kuishi na familia yangu nyumbani. Nilikulia Hong Kong kisha nikahamia New Zealand kusomea uhandisi wa umeme. Ni baada ya kuhitimu shahada ya uzamivu katika utandawazi wa komputa ndipo nilipohama kabisa kutoka nyumbani na kupata nafasi ya utafiti baada ya shahada ya uzamivu katika chuo kikuu cha Cambridge kule Uingereza. Nilipokuwa karibu na wazazi wangu wote wawili, nilihitaji kujitofautisha mwenyewe, kujichunguza nje ya pembetatu yangu nzuri ya familia na kuanzisha namna yangu ya pekee ya kujitambulisha.

Rafiki yangu mmoja kutoka New Zealand anaitwa Jared alikuwa na wasi wasi kuhusu kuondoka kwangu kutoka Uingereza. Alidhani kwamba ningeweza kuacha Imani yangu kwa Mungu. Hata hivyo pamoja na kukutana kwangu na wale wasioamini kwamba kuna Mungu mara kadhaa sikutetereka na niliendelea kujenga Imani yangu. Sasa ulikuwa ni wakati wangu nikiwa Uingereza kuulizwa swali; "Kuna uthibitisho gani kwamba kuna Mungu?" na mmoja wa wasioamini uwepo wa Mungu, na hiyo ikanifanya nigeuze mwelekeo wangu wa ajira na kufuata wito wa Mungu kuingia katika huduma.

PEMBETATU MPYA ZA FAMILIA

Kupitia katika mchakato wa kupona hadi kwenye huduma, nilijenga uhusiano wenye nguvu na Mungu. Niliishia pia kukutana na msichana wa ndoto yangu Marilyn na kumuoa. Sasa tumeshakuwa katika ndoa kwa miaka kumi na mitano na tuna Watoto wawili wazuri. Kadiri familia yangu inavyokua, ninaona pembetatu za familia zikianza kuumbika katika famila yetu pia.

PEMBETATU ZA MAOMBI

Pembetatu za familia kwa kawaida zinaonekana kama hasi. Hata hivyo, pembetatu za uhusiano zinaweza kuwa za kujenga na kuimarisha. Mahusiano ya karibu ya familia hata pembetatu za familia zinaweza kuwa chanya na kuwa na tunda la thamani.

Hebu twende pamoja katika aya nzuri inayopatikana katika Waefeso 3:

> Kwa hiyo nampigia Baba magoti…

Hapa ndipo linapoanzia ombi adhimu na lenye maono katika Biblia. Tunaweza kuona uhusiano wa pembetatu ukianza kuundwa. Paulo anaomba kwa Baba kwa niaba ya kanisa la Efeso.

Kuna takwimu za kufurahisha ambazo zinastahili kuoneshwa moja kwa moja mwanzoni mwa hili ombi lililosisitizwa katika jedwali hili hapa chini:

Sehemu	Rejea kwa Mungu	Anaitwa Baba	Asilimia
Agano la Kale	1,448	15	1.0%
Agano Jipya	413	245	59.3%

Kuna rejea nyingi kwa Mungu katika Agano la Kale, lakini anatambulishwa kama Baba kwa asilimia 1 tu ya idadi zote hizo. Hata hivyo, katika Agano Jipya, Mungu

anatambulishwa kama Baba kwa asilimia 59.3 ya idadi zote hizo. Hiyo ni tofauti kubwa sana! Ni nini sababu ya ongezeko kubwa hilo?

Jawabu ni rahisi tu – ni kwa sababu ya Yesu. Ni nini kinachodokezwa katika Agano la Kale kinachokuwa halisi wazi wazi katika Agano Jipya, na ndivyo ilivyo, kuna pembetatu imejumuishwa kwa kina ndani ya asili ya Mungu: yaani Baba, Neno, na Roho. Uhusiano uko katika kiini cha asili ya Mungu. Ndiyo maana Mungu ni pendo! Ilikuwa ni Yesu aliyetudhihirishia kwa uwazi hii pembetatu ya kimbingu.

PEMBETATU ZA WOKOVU

Biblia inatuambnia kisa cha pembetatu nyingine ya uhusiano iliyovunjika haraka sana. kwa asili Adamu na Hawa waliumbwa ili wawe katika uhusiano wa karibu wa pembetatu na Yahwe aliye Muumba wao. Hata hivyo, katika upendo wao kwa ubinadamu, huo Utatu uliamua kutekeleza mpango wa wokovu ambao ungerejesha uhusiano uliovunjika. Yesu aliacha mbingu na kuja hapa duniani. Katika mchakato huo, aliunda pembetatu ya wokovu kati yetu na Baba ili kwamba tuweze sasa kumwita Mungu Baba yetu tena kama vile Paulo alivyoomba.

Ni kwa sababu ya upendo mkuu wa Mungu kwetu na utashi wa Yesu kutoka katika pembetatu ya uhusiano wake mbinguni ambao Paulo sasa aliweza kuomba hili ombi zuri la Utatu.

Mwelekeo wa Kimbingu	Ombi
Baba	Kwa hiyo nampigia **Baba** magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa,
Roho	awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya **Roho** wake katika utu wa ndani.
Kristo	Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wake **Kristo**, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi,
Mungu	mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa **Mungu**.

Ni wazo la ajabu kiasi gani! Mungu alihiari kwamba uhusiano wa pembetatu yake ya kimbingu uvunjike ili kwamba uhusiano wetu wa pembetatu pamoja naye urejeshwe! Na jambo la kushangaza ni kwamba familia zote duniani zitabarikiwa.

> "Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu;

> naam, atukuzwe katika Kanisa na katika Kristo Yesu hata **vizazi vyote** vya milele na milele. Amina." (Waefeso 3:20-21)

Ni muhimu kwamba tutambue pembetatu za familia. Lakini pembetatu ya uhusiano iliyo muhimu zaidi tunayohitaji kutambuliwa ni pembetatu ya uhusiano unaoongoza kwanye wokovu.

Sifa zimwendee Mungu wetu aliye katika utatu!

MAKALA

ZILIZOCHAPISHWA UPYA

Sehemu hii ina Makala zisizopitwa na wakati, ambazo zimechaguliwa kwa uangalifu ili kukuandaa kwa mlolongo mkubwa wa mada mbali mbali.

KUFARIJI

WENYE HUZUNI

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

SWALI

Mmoja wa marafiki zangu aliondokewa na mume wake kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19, akiwa na umri wa miaka 49 tu. Anajisikia kupotea, na mwenye hasira dhidi ya Mungu kwa kuruhusu jambo hili kutokea. Siku moja alinieleza kwamba ana uchungu ndani yake na kukata tamaa kwa sababu ya tundu kubwa lililoko ndani ya nafsi yake, na kwamba haamini kwamba litakuja kujazwa. Ninataka kufanya jambo fulani ili kumsaidia ajisikiea vizuri na kufikia mahali pa kukubali kile kilichotokea kwake, lakini sifahamu nisemeje au nifanyeje. Tafadhali nisaidie.

Tunasikitika kwa kuondokewa na rafiki yako. Na kwa namna unavyozungumza, upotevu huu unakuhusu pia. Hakuna mtu anayestahili kuondokewa na mpendwa wake katika umri mdogo kama wa kwako. Ni jambo la kusikitisha. Hata hivyo huu ni uhalisia ambao wengi wanaupitia kutokana na janga hili ambalo limeukumba ulimwengu.

Wengi wetu hawajui wafanye nini au waseme nini pale mmoja wa watu walio karibu anapoondokewa na mpendwa wake, hasa mwenzi katika ndoa. Ukweli ni kwamba, mtu anapopitia uzoefu wa kufiwa na mpendwa wake, mihemuko yake inaweza kuwa na mabadiliko. Panaweza kuwapo na nyakati za utulivu, kisha ghafla nyakati za kulia kusikoweza kutawaliwa kadiri anavyopitia katika huzuni kubwa na kujikuta asiye na msaada wowote. Kwa hakika, huzuni inakuja kama mawimbi.

Pamoja na kwamba kifo cha mpendwa kinaweza kuwa na maumivu makali – kama hisia ambazo rafiki yako ameelezea – bado kuna mengi unayoweza kufanya kumtegemeza kupitia katika nyakati hizo za changamoto katika maisha yake. Hebu fikiria orodha hii ya mawazo unayoweza kutumia katika kumsaidia rafiki yako katika nyakati hizi za huzuni:

Hakikisha upo. Mpigie simu rafiki yako au umtumie ujumbe wa maneno kumfahamisha kwamba, "Nipo kwa ajili yako." Inawezekana katika hali hiyo, rafiki yako asingependa kuzungumza na mtu. Hata hivyo jitahidi kumfahamisha kwamba uko karibu naye, ni kiasi cha yeye kupiga tu simu pale atakapojisikia anahitaji mtu wa kuongea naye.

Nenda katembee kwenye maeneo ya mapumziko. Kwenda nje mahali ambapo atapata hewa safi kutamtuliza, kutapunguza kiwango cha msongo, na kuimarisha kinga ya mwili wake.

Mpitishe katika ushoroba wa kumbukumbu. Usiogope kuzungumza naye kuhusu nyakati nzuri ulizokuwa nazo huyo rafiki yako na mume wake aliyefariki. Kuangalia picha za zamani na kukumbukia yale mliyokuwa mkifanya pamoja ni namna nzuri ya uponyaji kwa mtu mwenye huzuni itokanayo na kufiwa.

Mletee chakula. Hakuna kinachozungumza katika jumuia kuliko kushiriki mlo na rafiki yako. Watu wanapokuwa katika huzuni, wanapoteza nguvu ya uhai, na hata ya kufanya mambo mengine, pamoja na kupika, pia kula. Chakula kitamu chenye afya kinapeleka ujumbe wa kujali kuliko unavyoweza kudhani.

Msaidie shughuli. Ikiwa utaona kwamba jikoni panahitaji kufanyiwa usafi au nyumba inahitaji kuwekwa katika hali nzuri unapomtembelea, ni vyema ukasaidia. Kufanya hivi kutapeleka ujumbe kwamba unajali na kwamba una nia ya dhati ya kumsaidia.

Usiwe katika hali ya haraka. Hebu rafiki yako afahamu kwamba una muda wa kuwa naye kadiri atakavyokuhitaji, siyo kwa kusema tu, bali kwa kutenda hivo. Kisha uwe tayari kuwa rafiki hasa katika mabadiliko hayo makubwa.

Mtegemeze kiroho. Hata watu wa Imani mara nyingi wanayumba kutoka kwa Mungu, au hata kumkasirikia wanapofiwa na wapendwa wao. Uwe tayari kumsomea mafungu ya Biblia rafiki yako, mafungu yatakayompatia faraja na uhakika kwamba Mungu anajali. Kisha omba kwamba Mungu ampatie amani na ahadi ya uwepo wake.

Kwa kawaida hizi ni siku ngumu, na nyingi zaidi bado ziko usoni. Hata hivyo, dumu kuwa karibu na Yesu kwa ajili ya amani yako mwenyewe, faraja, na uimara ili kwamba uweze kuwatia moyo wale unaowajali.

Tunakuacha na faraja ya Zaburi 46:1 “Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.” Tunakuombea.

UPOTEVU
WENYE UTATA

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

SWALI

Mimi ni mzazi pekee nisiyekuwa na mwenzi, mwenye watoto watatu. Mmoja wao ni mtu mzima ambaye hajatoka nyumbani, na hivi karibuni amegundulika kuwa na ugonjwa mzito wa akili. Ingawaje nimeshapitia uzoefu wa changamoto wanazopitia wazazi wasio na wenzi, hali ya kumtunza huyu binti yangu mwenye ugonjwa wa akili imeniwia ngumu. Mara nyingi ninajikuta katika mfadhaiko bila kujua nifanye nini. Ninatumaini kuna kitu fulani unachoweza kunishirikisha ili kunisaidia kukabiliana na changamoto hii kwa namna bora kuliko ambavyo nimekuwa nikifanya kwa miezi kadhaa iliyopita.

Tunasikitika kusikia kuhusu hali unayopitia wewe na binti yako. Hata hivyo hii ni fursa ya kukubaliana na mambo ya maisha yasiyotabirika duniani hapa. Ukweli ni kwamba mahali pekee pa usalama katika ulimwengu huu panapatikana ndani ya Yesu. Tunasoma katika Maandiko kuwa, "Yesu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele." (Waebrania 13:8)

Nadharia zinazoibuka kuhusu huzuni, kama vile "upotevu wenye utata" zinaweza kutusaisia kuelewa uzoefu unaoupitia pamoja na binti yako aliyeonekana kuwa na ugonjwa mkubwa wa akili. Tofauti ya ugonjwa huo na ile hali ya kuondokewa na mpendwa wako kwa kifo – kwani hiyo ni hatima – na ule upotevu wa maisha ya "kawaida" ya mpendwa ambaye hivi karibuni aligundulika kuwa na afya ya akili, siyo inayoelezea uzoefu unaoupitia kama upotevu wenye utata.

Upotevu wenye utata unakosa udhihirisho wa huo upotevu. Uzoefu wa hisia za mzazi pale mtoto wao aliyeingia katika utu uzima anapogundulika kuwa na ugonjwa wa akili – kama katika hali ya mtoto wako – ni moja ya mambo yasiyoeleweka yanayoleta mkanganyiko, pamoja na upeo wa juu wa msongo, huzuni, na unyanyapaa.

Kinachofanya ugonjwa huo wa akili kuwa mzigo ni kwamba huwa unajitokeza baadaye kwenye utu uzima, wakati ambapo wazazi wana matazamio kwamba mtoto wao atajitegemea na kufanya maamuzi yake mwenyewe kwa ukomavu. Hivyo ugonjwa huo unapojitokeza katika kipindi hiki ambacho hakitazamiwi katika uhusiano wa mzazi na mtoto, unakuwa ni uzoefu usio wa kawaida na wa kukatisha tamaa.

Wewe uliye mzazi – kama wazazi wengine tu – umeshakuwa na uwekezaji wa mihemuko katika ustawi wa usoni wa watoto wako. Sehemu ya matazamio hayo ni kwamba malezi unayompatia yataendelea kupungua kadiri mtoto anavyokua kuelekea katika utu uzima na hata kufikia mahali pa kujitegemea. Kuna matazamio pia kwamba uwekezaji ulioweka katika kukua kwa mtoto utatamatika katika matumaini na njozi zako kuwahusu – ikiwa ni pamoja na kumaliza elimu yao, kupata ajira, kujenga mahusiano ya urafiki watu wenye maana, pamoja na kupata mwenzi ambaye watasaidiana kuanzisha familia yao wenyewe.

Kile ulichoelezea kuhusu jinsi unavyojisikia, ndiyo huzuni yenyewe hiyo. Kwa hivyo tunakutia moyo kutafuta program nzuri ya huzuni – ikiwezekana iwe ni ile inayothibitisha Imani yako kwa Mungu – itakayokusaidia kutambua huzuni yako na upotevu wako, na kukusaidia kuchakata hiyo huzuni kwa namna yenye afya.

Kadiri unavyoshughulikia huzuni yako, kumbuka kwamba kuna wazazi wengine wengi wanaoshughulika na uzoefu kama huo wa kwako. Muhimu zaidi, kumbuka kwamba hauko peke yako. Yesu mwenyewe amesema kuwa, “Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.” (Yohana 14;1). Anaendelea kusema kuwa, “Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu.” (Yohana 16:33)

Tunatumaini kwamba utapata msaada unaohitaji kadiri unavyofuata ushauri tuliokupatia. Tafadhali pia, elewa kwamba tutaendelea kukuombea. Dumu kuwa mwaminifu bila kukata tamaa.

TUMAINI MKABALA NA TALAKA

SEHEMU YA 1

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

SWALI

Baada ya miaka kumi ya ndoa, ghafla mume wangu anataka tuachane. Huwa hatukubaliani katika karibu kila kitu tunachozungumzia. Hata hivo ninafahamu kwamba kwetu sisi kama Wakristo, talaka siyo mpango wa Mungu. Nimemuomba mume wangu aongozane nami kwenda katika ushauri ili tupate ufumbuzi wa mtanziko wetu, lakini ni kama haoni umuhimu. Tunao Watoto wawili walio katika shule ya msingi, na mimi nasumbuka kwamba pengine wakaathirika ikiwa tutatalikiana. Tafadhali nisaidie.

Ahsante kwa swali lako la kufikirisha. Tunasikitika kusikia kuhusu mtanziko wako, lakini pia tunafurahi kwamba una shauku ya kutafuta suluhu ili ndoa yenu isivunjika.

Ndoa ni mpango wa Mungu kuanzia mwanzo. Tunasoma kuwa, "Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja." (Mwanzo 2: 18, 24)

Ndoa nyingi, kama vile ya kwako zimejawa na kutokubaliana na kutoelewana kwingi. Ukweli ni kwamba hakuna ndoa iliyo kamili kwa sababu hakuna watu waliokamilika. Paulo anawaandikia Warumi akisema, "kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu." (Warumi 3:23). Na kwa sababu basi, wote tumefanya dhambi, ni lazima tutazamie kutokuelewana na kutokubaliana kwenye ndoa.

Kulingana na utafiti wa sayansi ya jamii na usoefu binafsi tuliokuwa nao na baadhi ya wenzi walio katika ndoa tuliofanya nao kazi, tunachofahamu ni kwamba tofauti kati ya wenzi walio katika ndoa wanaofanikiwa na wale wenzi walio katika ndoa ambao hawafanikiwi ni mtazamo wao. Wale wanaoingia katika ndoa wakitazamia kukuta magumu wakifahamu kwamba juhudi kubwa itahitaji kufanya kazi pamoja ili

kujifunza stadi za kumudu tofauti zao, wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa. Kwa upande mwingine, wenzi wanaoingia katika ndoa wakitazamia kuishi kwa furaha milele wana uwezekano kutokufanikiwa na pengine kushia kwenye talaka.

Uko sahihi kwamba talaka siyo mpango wa Mungu. Kwa kweli Biblia iko wazi kuhusu azma ya Mungu. Tunasoma kuwa, "Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamjaribu, wakimwambia, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe kwa kila sababu? Akajibu, akawaambia, Hamkusoma ya kwamba yeye aliyewaumba mwanzo, aliwaumba mtu mume na mtu mke, akasema, Kwa sababu hiyo, mtu atamwacha babaye na mamaye, ataambatana na mkewe; na hao wawili watakuwa mwili mmoja? Hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. Basi aliowaunganisha Mungu, mwanadamu asiwatenganishe." (Mathayo 19:3-6).

Wanandoa wengi wanakata tamaa wanapojikuta wakitofautiana mara nyingi katika mazunguzo yao. Tunafahamu hilo. Hata hivyo, tunawahimiza wanandoa kuiona ndoa yao kama jino lenye kishimo. Kunakuwa na maumivu na hata kuharibika kwa jino ikiwa hapatakuwa na matunzo mazuri. Lakini watu wengi hawaendi tu kwa daktari wa meno kung'oa jino kwa sababu hiyo. Mantiki inatuhabarisha kuwa, kumtembelea daktari wa meno – ambaye amefundishwa kukarabati vishimo katika meno – ili kupata msaada wa kitaalam ili kukarabati jino lako na kuliokoa. Vivyo hivyo katika ndoa. Siyo kwamba sasa kwa sababu kuna changamoto katika ndoa, basi tukubali kushindwa.

Tunakuhimiza uendelee kumwomba Mungu abadilishe mtazamo wa mume wako. Kisha mwendee msahuri mzuri wa Kikristo anayeweza kusaidia kukarabati maeneo yasiyofanya kazi katika uhusiano wenu. Sisi pia tutaendelea kumwomba Mungu atende muujiza unaohitajika katika ndoa yenu, ili familia yenu ivuke na kushamiri siku zilizoko mbele yenu.

TUMAINI MKABALA NA TALAKA
SEHEMU YA 2

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

SWALI

Baada ya miaka kumi ya ndoa, ghafla mume wangu anataka tuachane. Huwa hatukubaliani katika karibu kila kitu tunachozungumzia. Hata hivo ninafahamu kwamba kwetu sisi kama Wakristo, talaka siyo mpango wa Mungu. Nimemuomba mume wangu aongozane nami kwenda katika ushauri ili tupate ufumbuzi wa mtanziko wetu, lakini ni kama haoni umuhimu. Tunao Watoto wawili walio katika shule ya msingi, na mimi nasumbuka kwamba pengine wakaathirika ikiwa tutatalikiana. Tafadhali nisaidie.

Uzoefu wetu katika masuala ya ndoa, na maandiko mbali mbali yanayohusu talaka, ni dhahiri kwamba wanandoa wengi ambao ndoa zao zinaishia kwenye talaka huwa wamepoteza matumaini katika uwezekano kwamba ndoa yao inaweza kurejeshwa tena. Ni dhahiri kwamba, hapa hatujielekezi katika ndoa zilizo na unyanyasaji endelevu wa aina yoyote, au ukosefu wa uaminifu uliokithiri. Hata hivyo tunaamini kwamba kwa msaada wa Mungu ndoa zote zinaweza kupata uzoefu wa mabadiliko – na zikapona na kushamiri – ikiwa wahusika wana nia ya kufanya sehemu yao katika kusaidia kukarabati uhusiano kwa msaada wa tabibu mwema wa Kikristo.

Mtume Paulo anamhimiza kila mtu kukabili hali yoyote akiwa na ujumbe huu, "Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu." (Warumi 15:13). Ni Mungu pekee anayeweza kutoa tumaini la jinsi hii. Na linatolewa kwa wale tu wanaokuja kwa Mungu – wakiwa na wenzi wao – kwa unyenyekevu mkubwa wakiamini katika miujiza ya Mungu na kuitazamia.

Ukweli kuhusu ndoa ni kwamba inahitaji jitihada kubwa pamoja na kujitoa mhanga, bila kujali umeoa au kuolewa na nani. Hakuna kitu kama ndoa kamili kwa sababu hakuna watu walio kamili. Wenzi wanaofanikiwa lazima wakubali kutambua kwamba

walioana na mwanadamu. Maana yake - kwa uhakika – ni kwamba, watahitaji kukuza uwezo wa kushughulikia maudhi, na kuchukuliana na hali zote zinazovunja moyo.

Changamoto kubwa katika kuhakikisha ndoa inasimama na kuwa endelevu, ni kukubali ukweli kwamba zile hisia za furaha zilizokufanya useme "Ndiyo" siyo endelevu – bila kujali jinsi ulivyokuwa umezuzuka katika upendo hapo mwanzo. – bila shaka utakumbana na nyakati za kuona kwamba ndoa si kitu wakati matazamio ya kila mmoja yatakaposhindwa kutimia kwa namna kila mmoja alivyodhani. Wakati mwingine hata mahaba halisi bila kujali jinsi upendo wenu uliovyoonekana wakati wa uchumba na ndoa ikiwa changa, inatosha kutegemeza ndoa ya kuogofya.

Je, sasa ndoa inawezaje kufanikiwa? – inawezekana hilo likawa swali lako wewe na wengine. Hilo ni swali zuri. Kusema kweli, hatua ya kwanza iliyo muhimu ni kwa hawa wanandoa kukubali kwamba ndoa nzuri ni bora kuliko nyakati chache za mahaba – pamoja na uzuri wake. Upendo huo, yaani mafuta yanayofanya ndoa istahimili, siyo hisia kama watu wengi wanavyoamini. Badala yake upendo ni uamuzi ambao kila mmoja katika ndoa lazima afanye kila siku ili ndoa idumu. Unaweza kuuliza kuwa, "Maamuzi gani?" Jawabu ni kuwa mvumilivu na mwema kama mtume Paulo anavyoeleza, "Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni." (1 Wakorintho 13:4). Na, ili kuwa mwaminifu, mpole, mwenye kujitawala kama anavyoelekeza kuwa, "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria." (Wagalatia 5:22-23).

Kwa hiyo tunamwomba Mungu afanye muujiza katika ndoa yenu. Tunatumaini kwamba wewe na mume wako mtakuwa mmepata fursa ya kukubali dhana ambazo tumewashirikisha na mkatambua kwamba ndoa yenu inaweza kufanikiwa kadiri mnavyomtumaini Mungu ajitokeze na kuleta mabadiliko kwenye uhalisia wa ndoa yenu kila siku kwa kipindi cha maisha yenu kilichobaki.

NI WAPI
TULIPOKOSEA?

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

SWALI

Mimi na mume wangu tuna kiwango fulani cha masikitiko na fadhaa kwamba watoto wetu – ambao sasa ni watu wazima wanaofanya kazi, wahitimu wa vyuo vikuu na wanishi maisha yao wenyewe – wameliacha kanisa. tunajua kwamba hatukuwa wazazi wakamilifu, lakini hata hivyo tulifanya kila tulilloweza kuwaonesha upendo watoto wetu, na kuwapatia mazingira thabiti na ya kiroho nyumbani kwetu. Tuliwapeleka pia katika shule ya kanisa. Pamoja na kwamba watoto wa rafiki zetu pia wameliacha kanisa, hatukutegemea kuwa ingekuwa hivyo kwetu sisi. Ni wapi tulipokosea? Je, tungefanya nini kwa ubora zaidi? Kuna kitu chochote tunachoweza kufanya sasa hivi? ahsante kwa msaada wenu.

Tunakushuru kwa kutuamini katika masuala nyeti na binafsi kama haya. Sisi pia tunasikitika kusikia kwamba watoto wenu wameliacha kanisa. Huu ni uhalisia mgumu sana ambao wazazi wengi wa Kikristo wanapitia baada ya kufanya wajibu wao kadiri walivyoweza kulea watoto wao katika kumpenda Mungu. Bado ulimwengu wetu umejawa na dhambi na uovu, ambao kwa namna tu ya asili unawavuta wanadamu wote. Hali hii imekuwa ndani ya vinasaba vyetu tangu Adam na Hawa walipochagua kutokumtii Mungu katika bustani ya Edeni.

Kufikia hapo sasa, wewe na mume wako mnaweza kuchagua au kumruhusu Shetani awafanye kuhisi kushindwa, au mnaweza kuamini kuwa Mungu atawasaidia kuvuka maumivu ya uzoefu wenu na kuendelea kushiriki kuwaonesha watoto wenu upendo wake katika kila namna mnavyoingiliana nao. Hii ni fursa yenu ya kufanya huu uzoefu ulete ukuaji kwenu ninyi wenyewe na kwa watoto wenu pia. Tafuta uthabiti na tumaini katika Biblia. "Uniongoze katika kweli yako, Na kunifundisha. Maana Wewe ndiwe Mungu wa wokovu wangu, Nakungoja Wewe mchana kutwa. Usiyakumbuke makosa ya ujana wangu, Wala maasi yangu. Unikumbuke kwa kadiri ya fadhili zako, Ee Bwana kwa ajili ya wema wako." (Zaburi 25:5, 7).

Kwa hakika, sisi sote ni kazi ya kiroho iliyo endelevu, hata wale ambao hawajaacha kanisa na kuendelea na huduma kama kawaida. Bado tunahitaji uongozi wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Mtume Paulo anatuambia kuwa, "Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana." (Waefeso 5:15-17).

Ni lazima wewe pia muendelee katika nidhamu ya kiroho ya kuomba na kusoma Biblia ili badala ya kukatishwa tamaa, mvutwe karibu na Mungu ninyi wenyewe, kadiri mnavyomtumaini kwa wokovu wa watoto wenu. Dai ahadi kama zile zinazopatikana katika Luka 11:9, 10 "Kwa kuwa kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Maana ni yupi kwenu aliye baba, ambaye mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe au samaki, badala ya samaki atampa nyoka?"

Hatimaye, kumbuka kwamba Mungu hakutenda jambo lolote kwa namna isiyo sahihi, lakini pamoja na usahihi wake, theluthi ya watoto wake (Malaika wa mbinguni) walimgeuzia mgongo. Kwa hiyo badala ya kujiadhibu mwenyewe – ukitambua kwamba hakuna wazazi walio wakamilifu kwa sababu hakuna mwanadamu aliye mkamilifu – utadai ahadi inayopatika katika kitabu cha Isaya, "Naam, Bwana asema hivi, Hata jeshi la wafungwa wake aliye hodari watapokonywa mikononi mwake, na mateka yake aliye jabari wataokoka; kwa maana nitateta na yeye atetaye nawe, nami nitawaletea wana wako wokovu." (Isaya 49:25)

Dumuni kuwa waaminifu bila kukata tamaa.

NYENZO

Kanisa la Waadventista wa Sabato linadumu kuandaa vitendeakazi vipya vya kukuwezesha katika utumishi na familia.

KUJENGA UPYA
MADHABAHU YA FAMILIA

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

Review and Herald Publishing Association
July, 2022
Kurasa 42

Katika juma la familia mwaka 2022, tamanio letu lilikuwa ni kujenga au kujenga upya madhabahu ya ibada ya familia nyumbani kwao. Ibada ya familia inapatia kila familia fursa ya kujenga upya madhabahu ya Mungu kila siku.

Kujenga upya madhabahu ya familia maana yake ni kuanzisha tabia ya kila ziku ya kutenga muda wa kumwabudu Mungu kama familia. Jambo la muhimu ni kujitoa kikamilifu kufanya kitu kitakachoelekeza familia yako kwa Mungu kila siku. Mlete Mungu katika nyakati zako ndogo na nyakati kubwa.

MAZUNGUMZO HALISI YA FAMILIA:

MAJIBU KWA MASWALI KUHUSU UPENDO, NDOA NA TENDO LA NDOA

NA WILLIE & ELAINE OLIVER

Pacific Press® Publishing Association
Nampa, Idaho, 2015
Kurasa 127

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa safu zinazohusu mahusiano, zilizoandikwa na Wilie na Elaine Oliver kwa gazeti la Message kama mwitikio kwa maswali kutoka kwa watu halisi. Waandishi wanatoa ushauri wa wazi, wakiujenga katika kanuni za kibiblia, kwa maswalil kuhusu ndoa, tendo la ndoa, malezi, kuwa mzazi mmoja na masuala mengine mengi ya mahusiano halisi. Katika ushauri wao, waandishi hawa, wanatukumbusha uhalisia kwamba sisi sote tunakabili changamoto katika mahusiano yetu na majumbani mwetu. Majibu yao ya umaizi yanatuelekeza kutafuta uongozi wa Mungu, yakitukumbusha kwamba mpango wa Mungu ni kwa ajili yetu ili tuwe na nyumba zenye ustawi na mahusiano yenye afya, mahali ambapo kila mtu anatafuta upatanifu ambao Mungu amekusudia uwe ndio uzoefu wetu.



MAZUNGUMZO
HALISI YA FAMILIA

NA WILLIE NA ELAINE OLIVER

www.hopetv.org

Kupitia mijadala shirikishi, iliyojawa taarifa, mijadala ya kiroho kuhusu masuala yanayokabili familia, kitabu cha "*Mazungumzo Halisi ya Familia*" hutafuta kuimarisha familia na kutoa tumaini. Katika kila toleo, wanandoa Olivers hueleza kutoka katika uzoefu wao wa kichungaji, kielimu, na kiushauri ili kuendeleza mijadala kuhusu maisha yetu, wakiikabili kila mada kwa suluhisho halisi na kanuni za kibiblia.

Msimu wa 11 wa Mazungumzo Halisi ya Familia na Willie & Elaine Oliver pamoja na episodi mpya zitaanza kurushwa juma la kwanza la July 2022. Tafuta matoleo ya sasa na yaliyopita kupitia katika Programu tumishi ya HopeTV au tembelea tovuti ya www.hopetv.org

KUUNGANISHWA:

IBADA KWA WENZI WANAOPENDANA KATIKA NDOA

NA WILLIE NA ELAINE OLIVER

The Stanbourough Press Ltd., 2020 - Kurasa 162

Fikiri ikiwa unaweza kuihamisha ndoa yako na kuipeleka katika nafasi nyingine. Je, vipi kama inawezekana kutoka katika uhusiano unaopambana kuwepo na kuwa na ule unaonawiri? Vipi kama kungekuwa na namna ya kuimarisha maagano yenu kila mmoja kwa mwenzake? Vipi kama mawasiliano bora yangeweza kujenga Imani kubwa zaidi? Na, bora kuliko yote, vipi ikiwa neema inaweza kukusaidia kuona yaliyo bora ndani ya mwenzi wako?



Katika kitabu cha *Connected: Devotionals for an intimate marriage*, Willie na Elaine Oliver wanashiriki uzoefu wa ziadi ya miaka 35 ya ndoa, wakikua pamoja, wakijifunza kila mmoja kwa mwenzake, na kulea watoto. Wanafahamu namna ya kufanya mawazo ya 'vipi ingekuwa' yakawa ni uhalisia.

Kitabu hicho kikiwa na mawazo 52 ya ibada, kuna wazo kwa kila juma la mwaka, mawazo yaliyobuniwa mahususi kuwasaidia wanandoa kutulia (kutafakari mawazo yaliyoshirikishwa), kuomba (kuhusu mawazo yaliyoshirikishwa na kufahamu namna yanavyoendana na uzoefu wao) na kisha kuchagua (kuamua kupata uzoefu wa badiliko pamoja). Gundua mengi zaidi ndani yake! Kinapatikana katika tovuti ya **www.lifesourcebookshop.co.uk**

https://adventistbookcenter.com/connected-devotional-reading-for-an-intimate-marriage.html

BIBLIA YA WENZI

Safeliz, 2019

Kurasa 1,500

Biblia ya Wenzi imebuniwa kusaidia kujenga na kulea mahusiano. Kuna zaidi ya mada 170 ambazo zimegawanywa katika vipengele vitano juu ya namna ya kuimarisha ndoa, na mahusiano ya malezi ya wazazi, pamoja na namna ya kukabili changamoto wanazokabili wanandoa. Vipengele muhimu ni kama:



- Ndoa katika Biblia, Teolojia ya Kibiblia ya Familia, Misingi inayoongoza Huduma za Familia, Jumbe Maalumu kwa Wanandoa na zaidi.
- Kozi maalumu ya Biblia juu ya nyumba na familia
- Mawazo 101 ya Uinjilisti wa Kifamilia
- Kamusi ya maneno ya Ndoa na ramani
- Na mengi zaidi…

Biblia hii inapatikana kwa lugha kadhaa ikiwemo Kiingereza, Kiispaniola, na Kifaransa na inaweza kuagizwa katika Vituo vya kuuza Vitabu vya Kiadventista ulimwenguni kote au kwa kutembelea: www.safelizbibles.com

TUMAINI KWA
FAMILIA ZA LEO

NA WILLIE NA ELAINE OLIVER

Review and Herald Publishing Association, 2018
Kurasa 94

Kitabu cha mwaka cha kimisionari ulimwenguni kwa mwaka 2019 bado ni kizuri katika kusaidia kuimarisha ndoa na familia kwa wakati wo wote. Hutoa *Tumaini kwa Familia za Leo* kwa kutumia kanuni zilizothibitishwa kwa muda mrefu ambazo zitasaidia kuwa na maisha ya furaha na yenye maana.

Kinapatikana kwa lugha nyingi katika Vituo vya Vitabu vya Kiadventista ulimwenguni au kupitia nyumba ya uchapishaji katika eneo lako.



MUNGU ANANIPENDA
PAMOJA NA HISIA ZANGU ZOTE

NA TARA J. VINCROSS

AdventSource, 2020



Mungu ananipenda mimi pamoja na hisia zangu zote ni kitabu kinachowapatia watoto lugha ya kuzipatia hisia zako jina, na kuwawezesha kufahamu nini cha kufanya katika kuitikia kile wanachohisi. Kitabu hiki kinaweka msingi wa ukubali wa Mungu na upendo wake kwa ukanda wote wa uzoefu wa kibinadamu, kujenga ustahimilivu na utayari wa kukabili hisia ambazo wakati mwingine ni ngumu. Kwa watoto wenye umri kati ya miaka 2-8 ikijumuisha maswali ambayo mtu mzima mwenye upendo anaweza kuuliza wanaposoma kitabu na watoto.

NDOA:

VIPENGELE VYA KIBIBLIA NA KITEOLOJIA

GOMBO LA 1

EKKEHARDT MUELLER NA ELIAS BRASIL DE SOUZA, WAHARIRI

Taasisi ya Utafiti wa Kibiblia. Review and Herald Publishing, 2015
Kurasa 304

Kitabu hiki hutoa masomo ya kina na ya tafakuri kuhusu maeneo kadhaa yanayohusisha wachungaji, viongozi wa kanisa, na washiriki. Baada ya kuonyesha uzuri wa ndoa na uhusiano wa Maandiko katika uelewa mzuri wa ndoa na ujinsia, gombo hili hushughulikia mada muhimu kama hali ya kutokuwa na mwenzi, jinsia na majukumu katika ndoa, ujinsia, ndoa zenye mchanganyiko wa dini, na talaka na kuoa/kuolewa tena.



NGONO:
MASUALA YA KISASA KWA MTAZAMO WA KIBIBLIA
GOMBO LA 2

EKKEHARDT MUELLER NA ELIAS BRASIL DE SOUZA, WAHARIRI

Taasisi ya Utafiti wa Kibiblia, 2022
Kurasa 643

Ngono: Masuala ya kisasa kwa mtazamo wa Kibiblia ni mwendelezo wa ndoa katika Biblia na vipengele vya Kiteolojia. Gombo hili likijielekeza katika masuala ya ngono, linashughulikia mada mbalimbali za umuhimu wa kisasa kwa Wakristo mmoja mmoja, na kanisa kwa ujumla kama jumuia zilizoko duniani. Linang'ang'ana na masuala yanayohusu ndoa moja kwa moja kama vile kuishi pamoja bila ndoa, na ndoa za mitala. Pia linachunguza mada ambazo siyo lazima zihusiane na ndoa, kama vile uraibu wa ngono, ngono ya mitandao, ngono na maroboti, ubakaji, kukeketwa kwa watoto wa kike, unyanyasaji wa watoto kingono, na nadharia chafu zenye kupotosha na vitendo vinavyohusiana na nadharia hizo.



FARAJA YA SIKU

KUISHI KIPINDI CHA MAJONZI

NA STEVE & KAREN NICOLA

Westbow Press, 2016



Moyo wako umepondwa pondwa. Inakuwa vigumu hata kupumua, unatambua uhalisia kwamba mtu uliyekuwa karibu naye sana amekutoka. Kifo kimekunyang'anya mikononi mwako mpendwa wako. Na sasa kazi ngumu isiyobebeka ya kuishi katika majonzi inaaanza. Je, kuna jambo lolote linaloweza kupunguza maumivu hayo? Kuna mahali salama pa kupeleka hasira hizi? Je, huu msongo unaweza kugeuka mwenzi wa kudumu? Je, maumivu haya yatadumu milele? Nifanyeje nipate kuvuka kipindi hiki? Faraja ya Siku ni kitabu kinachokupatia uzoefu binafsi wa kuvuka majonzi, kilichojengeka katika chanzo cha Faraja zote, yaani Mungu. Neno lake litakuwa ni kiongozi na rafiki kadiri msomaji atakavyoendelea kuishi na kuvuka hiki kipindi cha majonzi.

KIAMBATISHI 'A'

UTEKELEZAJI WA HUDUMA ZA FAMILIA

Tafadhali tumia machapisho haya kama sehemu ya kazi yako katika Huduma za Familia. Maudhui yake ni matokeo ya kufanya kazi na familia ndani ya kanisa ulimwenguni kote.

Kumbuka kwamba: Baadhi ya mapendekezo yaliyoorodheshwa katika fomu hizi yatahitaji kuchukuliwa na kuboreshwa kulingana na mahitaji maalumu na sharia za maeneo hayo ambapo nyenzo hii itatumika.

VITENDEA KAZI VINAVYOWEZA KUPAKULIWA

Kupakua fomu na maswali ya uchunguzi ya Kiambatishi 'A' tafadhali tembelea tovuti yetu: **family.adventist.org/2021RB**

SERA YA HUDUMA ZA FAMILIA

NA TAMKO LA KUSUDIO

Wafanyakazi na kusanyiko la:

.....

Makanisa yana wajibu wa kutoa mazingira salama ya kusaidia watoto kujifunza kumpenda na kumfuata Yesu Kristo. Ni kusudi la kusanyiko hili kuzuia aina yo yote ya unyanyasaji wa watoto kimwili, kihisia au kingono na kuwalinda watoto na wale wanaofanya kazi pamoja nao.

Makanisa yenye programu kwa ajili ya watoto hayawi na kizuizi cha kuwazuia kutoka kwa hawa wanaofanya unyanyasaji: hivyo, kusanyiko hili linaamini kwamba ni muhimu sana kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba kanisa na programu zake ni salama, likitoa uzoefu wa furaha kwa watoto na vijana. Sera zifuatazo zimeanzishwa na zinaakisi agano letu la kutoa huduma za ulinzi kwa watoto wote wanapohudhuria shughuli yo yote inayosimamiwa na kanisa.

- Watu wa kujitolea wanaofanya kazi pamoja na watoto na vijana wanapaswa kuwa washiriki hai wa kusanyiko hili kwa angalau miezi sita, na wanapaswa kuruhusiwa na watumishi wa kanisa hilo kabla ya kuanza kufanya kazi moja kwa moja na watoto, isipokuwa kumekuwa na udhihirisho wa maandishi wa hapo awali.
- Wafanyakazi wote na watu wa kujitolea wa NAD ambao mara kwa mara hufanya kazi na watoto wanapaswa kukamilisha fomu ya maombi (tazama tovuti ya Huduma za Watoto za NAD: https://www.childmin.org/childrens-safety). Rejea zote zinapaswa kutoka kwa watu wa kujitolea walio na uzoefu. Watumishi au wafanyakazi wanapaswa kuchunguza rejea hizo. Vitengo vingine vinahamasishwa kufuata utaratibu huu.
- Wafanyakazi wote wanaohusiana na watoto wanapaswa kuzingatia kanuni ya "watu wawili," ambayo humaanisha kwamba wafanyakazi hao wanapaswa kuepuka hali ya kuwa mfanyakazi mmoja na mtoto mmoja po pote inapowezekana.
- Watu wazima walio wahanga wa unyanyasaji wa kimwili na kingono wakati wa utoto wao wanahitaji upendo na kukubalika katika familia ya kanisa. Watu

wenye historia kama hiyo wanapaswa kujadili shauku yao ya kufanya kazi na watoto na vijana wakiwa na mmoja wapo wa wafanyakazi katika mahojiano ya siri kabla ya kupokea ruhusa ya kufanya kazi katika maeneo haya.

- Watu waliowahi kufanya unyanyasaji wa kimwili au kingono, iwe wamekutwa na hatia au la, hawawezi kufanya kazi katika shughuli au programu kwa ajili ya watoto na vijana zinazosimamiwa na kanisa.
- Fursa za mafunzo katika kuzuia na kutambua unyanyasaji wa watoto zitatolewa na kanisa. Wafanyakazi watatazamiwa kuhudhuria katika mafunzo haya.
- Wafanyakazi wanapaswa kuripoti mara moja kwa mchungaji au utawala tabia yo yote au matukio mengine ambayo yataonekana kuwa ya unyanyasaji na yasiyo kawaida. Taarifa inapopatikana, hatua sahihi zitachukuliwa na taarifa kutolewa zikiambatana na taratibu za kiutendaji za sera hizi.
- Miongozo kwa wanaojitolea wanaofanya kazi na ninyi pamoja na watoto wenu itatolewa kwa kila mtu anayejitolea.
- Watoto hawapaswi kuzurura maeneo ya kanisa bila uongozi wa mtu mzima. Wazazi wana jukumu la kuwasimamia watoto wao kabla na baada ya Shule ya Sabato.
- Mtoto ye yote asiruhusiwe kwenda uwani asipokuwa na mtu mzima au ndugu aliye mkubwa kuliko yeye.
- Mtu mzima mmoja atapewa jukumu la kuzunguka ndani na maeneo ya kuzunguka kanisa, ikiwemo sehemu za kuegesha magari ili kuhakikisha usalama. Hili ni muhimu wakati ambapo kunakuwa na mtu mzima mmoja katika baadhi ya shughuli za watoto, kama migawanyiko ya Shule ya Sabato.
- Tukio lo lote la kinidhamu litatendeka sehemu ambapo kuna mtu mzima mwingine anayeona. Aina yo yote ya adhabu kali hairuhusiwi kabisa.
- Mikutano yote ya watoto au vijana inapaswa kuwa na ruhusa ya mchungaji na/au baraza la kanisa, hasa shughuli za usiku. Watoto wanapaswa kuwa na ruhusa iliyotiwa sahihi na mzazi kwa kila safari, ikiwemo ruhusa ya matibabu ya dharura.
- Ikiwa kuna mtu ye yote aliye mnyanyasaji wa kingono anayehudhuria kanisani, shemasi au mtu mwingine aliyeachiwa jukumu anapaswa kupangwa kumsimamia mtu huyo anapokuwa katika shughuli za kanisa iwe katika eneo la kanisa au nje. Mtu huyo anapaswa kuelezwa utaratibu huo. Ikiwa mnyanyasaji wa kingono atahama au kuhudhuria kanisa lingine, uongozi wa kanisa hilo unapaswa kupatiwa taarifa.

KIONGOZI

WA HUDUMA ZA FAMILIA

Kiongozi wa huduma za familia hubuni huduma kwa familia ambayo itagusa mahitaji mahususi ya kusanyiko hilo na jamii. Kipengele hiki hutoa msaada wa kupanga kwa ajili ya viongozi wa huduma za familia. Kupanga ni muhimu kwa ajili ya kuhudumia watu binafsi na familia katika kusanyiko. Huduma za familia pia ni njia bora ya kufikia familia katika jamii. Kiongozi wa huduma za familia ni mjumbe wa baraza la kanisa na huhusisha shughuli za huduma za familia na programu ya kanisa zima. Yafuatayo ni majukumu na shughuli.

1. Andaa na kusimamia kamati ndogo ya huduma za familia inayoakisi utofauti wa kusanyiko. Inaweza kujumuisha mtu aliye mzazi mmoja, wanandoa vijana, familia zenye maisha ya kati, waliostaafu, wajane na wenye talaka. Watu wanaohudumu katika kamati hii wanapaswa kuchaguliwa kwa umakini kama watu wenye njozi wanaoakisi neema ya Mungu.
2. Kuwa wakili wa familia. Huduma za familia hazielekezi tu katika programu, lakini zinapaswa kuitazama programu ya kanisa zima kwa umakini katika matokeo yake kwa familia. Katika nyakati fulani kiongozi wa huduma za familia anaweza kuhitaji kuwa wakili wa muda wa familia. Kwa maneno mengine, kunaweza kuwa na ratiba nyingi zinazoendelea katika kusanyiko kiasi kwamba watu wanakuwa na muda mchache kwa kuishi maisha yao wenyewe kama familia.
3. Chunguza mahitaji na shauku za familia katika kusanyiko lako. Utafiti wa tathmini ya mahitaji na karatasi ya wasifu wa familia inaweza kutumika kutambua mahitaji ya kusanyiko lako.
4. Panga programu na matukio ya mwakwa ambayo yanaweza kujumuisha uwasilishaji kwa njia ya video, safari za nje au wazungumzaji maalumu watakaowasilisha warsha na semina. Pia mipango inapaswa kujumuisha shughuli rahisi ambazo zitapendekezwa kwa familia kupitia vijarida au karatasi za matangazo ya kanisa.
5. Fanya kazi pamoja na mchungaji na baraza la kanisa ili kuwa na uhakika kwamba mipango yako imehusishwa katika bajeti ya kanisa.

6. Tumia nyenzo zinazopatikana kutoka katika idara ya huduma za familia ya konferensi. Hizi zinaweza kuokoa muda, nguvu na kutumika kupunguza gharama kwa kanisa. Unapopanga vipindi maalumu, mkurugenzi wa huduma za familia wa konferensi anaweza kusaidia katika kutafuta wawasilishaji wazuri na wenye vigezo.
7. Wasiliana na kusanyiko lako. Huduma za familia hazipaswi kutambuliwa tu kama tukio la mara moja kwa mwaka. Dumisha umuhimu wa stadi bora za familia kwa mabango, vijarida na/au karatasi za matangazo kwa mwaka mzima.
8. Shiriki mipango yako na mkurugenzi wa huduma za familia wa konferensi.

FAMILIA

NI NINI?

Moja ya jukumu la kiongozi wa huduma za familia ni kutambua familia ambazo wanazihudumia katika kusanyiko lao. Kwa mfano, huduma kwa wanandoa wenye watoto pekee, inaweza kunufaisha asilimia ndogo ya watu ndani ya kanisa. Familia za aina zote zinaweza kuhitaji uongozi kadiri wanavyosonga kuelekea katika mahusiano yenye afya. Kazi ya kukabiliana na shughuli za kila siku za kushiriki nyumba na kusimamia mikwaruzano haijawahi kuwa rahisi pale watu wanaposhiriki nafasi na nyenzo au wanapotoka katika nyumba zenye viwango na thamani tofauti. Hapa kuna baadhi ya namna familia za leo zinavyopangwa.

- Familia za Kitovu – yenye Mama, Baba na watoto waliozaliwa na wazazi hawa.
- Familia za wazazi wa kambo – familia hizi hutokea pale wazazi wanapotalakiana au kufiwa na kisha kuoa/kuolewa tena. Baadhi ya familia huwa za kambo pale mzazi asiye na ndoa anapooana na mtu ambaye si baba/mama wa mtoto wake.
- Familia za wasio na wenzi – nyakati fulani ni mimi na paka wangu tu – tukiishi peke yetu. Wanaweza kuwa waliopewa talaka, waliofiwa au ambao hawajawahi kuolewa/kuoa, lakini wanaishi katika nyumba tofauti. Baadhi ya watu wasio na wenzi wanaweza kuishi na wengine wasio na wenzi katika nyumba moja.
- Familia za mzazi mmoja – Hii huweza kutokea pale mzazi anapopewa talaka au kufiwa na hajaoa/kuolewa tena, au ni mzazi ambaye hajawahi kuoa/kuolewa.
- Familia ni za viota vitupu – Mama na Baba wakati watoto wakiondoka nyumbani.
- Familia zinakua zilizounganishwa tenaa – kijana mkubwa anaporudi nyumbani kuishi na Baba na Mama yake – mara nyingi ni mipango ya muda mfupi. Familia inaunganishwa tena pale mzazi mzee anapoishi na familia ya kijana au binti au mjukuu wake.
- Familia ni sehemu ya familia ya Mungu. Wengi huwafikiria watu katika kusanyiko lao kama familia na wanaweza kuhisi vifungo vya karibu zaidi nao kuliko wale walio na undugu kwa kuzaliwa au kwa ndoa.

Zaidi ya demografia za kawaida za familia, mtu anaweza pia kuhamasisha watu kufikiri kuhusu mahusiano yao ya muhimu, wakiwemo wale walio katika familia ya kanisa, kwa kuuliza maswali kama haya:

- Ikiwa tetemeko litaathiri mji wako, ni nani utakayekuwa na shauku zaidi ya kumtafuta na kuhakikisha yupo sawa?
- Ikiwa unahama kwenda eneo la mbali, ni nani angehama na wewe?
- Ni nani utadumu kuwasiliana nao, bila kujali ugumu wo wote utakaokuwepo?
- Ikiwa utapata ugonjwa wa muda mrefu, ni nani unaweza kumtegemea kukutunza?
- Ni nani watakuwa familia yako sasa hadi utakapokufa au watakapokufa?
- Ni nani unaweza kumkopa fedha na kutokuhisi kama unahitaji kumlipa mara moja?

MIONGOZO

YA KAMATI NA KUPANGA

Viongozi wa huduma za familia ambao ni wageni katika cheo hicho au hawajawahi kuwa viongozi hujiuliza ni wapi pa kuanzia! Kipengele hiki ni kwa ajili ya kumsaidia kiongozi kuanza. Mara nyingi huwa na msaada kuchagua kamati ndogo ambayo kiongozi anaweza kufanya nao kazi vema – watu wenye uelewa katika neema ya Kristo na wasiokuwa na sababu za siri za kuharibu. Kamati ya huduma za familia, inapaswa kutafuta kutengeneza familia, kuliko kamati nyingine yo yote. Zifuatazo ni baadhi ya njia za kukamilisha hilo. Mawazo haya si namna pekee inayoweza kutumika, lakini bado yanaweza kusaidia kundi kufanya kazi pamoja vizuri. (Yanaweza kusaidia katika kamati nyingine pia).

- Chagua idadi ndogo ya watu wenye makusudi sawa kwa ajili ya familia. Wanapaswa kuwakilisha familia za aina tofauti zinazopatikana katika kusanyiko. Kamati hii inaweza kuwa na mzazi mmoja, wanandoa, wenye talaka, waliostaafu au waliofiwa, na kuakisi jinsia na utofauti wa kjamii wa kanisa.
- Kamati haipaswi kuwa kubwa sana – watu watano hadi saba wanatosha. Mtu mmoja anaweza kuwakilisha kundi zaidi la familia zaidi ya moja.
- Hasa katika kikao cha kwanza, kusanyikeni katika sehemu isiyo rasmi – pengine katika nyumba ya mtu au katika chumba kizuri kanisani. Anza kwa ombi kwa ajili ya mbaraka wa Mungu.
- Toa viburudisho vyepesi kama maji au soda, juisi ya matunda, biskuti, au karanga. Fanya kikao kiwe cha kuvutia, lakini kisichotumia nguvu nyingi.
- Tumia muda kuelezea kisa cha kila mmoja katika mkutano wa kwanza. Hiki siyo kipindi cha tiba, kwa hiyo watu na waelewe kuwa wanatakiwa kueleza yale tu yasiyokwaruza masikioni. Miongozo michache itasaidia: kutunza siri na kuheshimiwa na kila mmoja, na kila aliyehudhuria aonekana kama zawadi kwa mwenzake. Inaweza kuwa vyema kwa kiongozi kuanza kwa sentensi kama: "Nilizaliwa mahali fulani… nikakulia katika familia ya … (pengine Waadventista wa Sabato, au Wakatoliki, au Walokole, n.k.)" Ongezea na mambo mengine kama shule uliyosoma, majina ya watoto wako na taarifa zingine utakazoona zinafaa. Pamoja na hayo unaweza kueleza ulivyopata kuwa Mkristo wa kanisa la Waadventista wa Sabato, au kisa kingine chochote kutoka katika

utoto wako kitakachofurahisha. Kufanya hivi kunaweza kuonekana kama kupoteza muda, lakini unaweza kushangaa kusikia kisa cha mwingine uliyekuwa ukidhani unamfahamu kwa muda mrefu. Kueleza visa vyetu ni namna moja ya kujiunganisha na wengine. Zoezi hili litafanya kazi zenu kwenda kwa urahisi zaidi. Pia litarahisisha ile hali ya wajumbe wa kamati kuchukulia kwa uzito mahitaji ya kila mmoja.

- Katika mikutano mingine yote, jaribu kutumia sehemu ya muda – pengine dakika 10 hadi 20 katika kujiunganisha na wajumbe wa kamati. Mtu mmoja anaweza kuelezea alivyofurahishwa na tukio fulani. Mwengine anaweza kuhitaji msaada kwa jambo fulani. Hapa pana baadhi ya maswali unayoweza kuuliza ili yakuwezeshe kuanza mkutano wako.
    - Ni watu gani unaodhani wanaweza kuwa sehemu ya familia yako ya karibu?
    - Je, mnaishi namna gani Imani yenu pamoja kama familia?
    - Unadhani kanisa lingefanya nini ili kusaidia familia yako?
    - Ni nini unachopenda zaidi kuhusu familia yako?

Baada ya hapo hamia kwenye dondoo za siku:

- Pitia upya matokeo ya uchunguzi wako.
- Zungumza kuhusu malengo. Je, ungependa kukamilisha nini? Utafanyaje ukamilishe malengo yako? Je kufanya hivi kutakufanya kukidhi hitaji? Je, unajaribu kumfikia nani? Je, utakamilishaje malengo yako?
- Mwombe Mungu ili awabariki, panga kwa hekima ili watu wasivurugane kwani huduma imekaribia.

Nyenzo muhimu kwa kiongozi wa huduma za familia ni hiki kijitabu cha "Mpango wa Huduma za Familia" (Family Ministries Planbook). Toleo jipya la nyenzo hii linachapishwa kila mwaka likijumuisha progam, mpangilio wa mahubiri, semina na mambo mengine mengi ambayo yanaweza kutumika kama sehemu ya program yako ya mwaka.

WASILISHO ZURI
LITAKUWA NA MAMBO MANNE

1. **Fahamisha –** Watu wanatakiwa kujifunza kitu ambacho hawakuwa wanakijua kabla hawajaingia katika wasilisho lako.

2. **Burudisha –** Watu wanastahili kuchangamka wasichoke!!

3. **Gusa hisia –** Taarifa inayopeleka tu ujumbe kichwani haiwezi kuleta mabadiliko katika mtazamo au katika mwenendo.

4. **Ingia katika Utendaji –** Ikiwa washiriki wataondoka katika wasilisho lako bila haja ya kufanya jambo fulani lililo tofauti – umepoteza muda wako na wa kwao!

Vitini

- Gawa vitini baada tu ya wasilisho lako kueleweka
- Wakati mwingine ni bora usigawe vitini hadi mwisho wa mkutano ili hadhira isianze kushughulika na makaratasi wakati wewe unaendelea kuzungumza.
- Hadhira yako inatakiwa kusoma na kuelewa lahaja na lahani yako.
- Usinakili wasilisho la mwenzako ukaliweka katika vitini vyako

Utambulisho

- Amua ni nani atakutambulisha
- Andika utambulisho wako mwenyewe
- Wasiliana na huyo atakayefanya utambulisho angalau siku mbili kabla na kumpatia huo utambulisho
- Usiweke matamko yasiyo ya kweli kwenye utambulisho wako.

AMRI KUMI
ZA UWASILISHAJI

1. **Jifahamu Mwenyewe** – Lugha ya mwili na lahani ya sauti yako ina asilimia 93 za kukubalika kwako. Je, wewe mwenyewe ungejikubali?

2. **Jitayarishe** – Fahamu vizuri kile unachoenda kuwasilisha, vifaa vyako, na pia hali ya kujiandaa kwa yale yasiyotazamiwa. Mara nyingi balbu za projecta zinaungua katikati ya wasilisho la muhimu, kwa hiyo uwe na akiba ya balbu na ujue jinsi ya kubadilisha ikibidi.

3. **Pima na kuchunguza hotuba yako** – Tumia namna ya kujieleza moja kwa moja, usitafute kuzuzua hadhira yako – umeenda pale kuwasiliana.

4. **Fika mapema** – Walengwa wako na wageni wanaweza kuwa wamekaa wakikusubiri. Hivyo hakikisha unakuwa pale kama nusu saa kabla ya kuanza, ili kuhakiki baadhi ya mambo na kuona kama yote yako kwa namna uliyotaka yawe.

5. **Waeleze kile wanachotazamia** – Kuwaambia walengwa wako kile hasa wanachotazamia kujifunza katika mkutano huo, na namna watakavyoweza kuweka katika utendaji elimu yao mpya. Malengo yaliyo dhahiri yatawafanya waliohudhuria kujelekeza katika wajibu wao kama washiriki walio hai.

6. **Kidogo ni Kingi** – Hadhira yako inaweza kupokea kiasi fulani tu, kwa hiyo jiwekee ukomo wa dondoo. Dondoo saba zinaweza kuwa ni kiwango cha juu kwa hadhira kupokea na kufanyia kazi.

7. **Dumisha mguso wa macho** – Tumia kadi ulizoandika dondoo zako badala ya kusoma hotuba yote, ili uweze kupata namna ya kudumisha mguso wa macho na hadhira yako. Epuka msukumo a kusoma wasilisho lako. Itikio la hadhira yako litakuwa ni shukurani ya kutosha kwa kuzungumza nao ukiwaangalia.

8. **Tumia vielelezo** – Tumia maneno yaliyotiliwa mkazo na takwimu. Wasilisho lako linatakiwa kujawa na kauli zilizosheheni mambo ya kugusa, wewe

mwenyewe ukiteka uzikivu wa hadhira yako. Usikwepe kuchekesha, vicheko haviumizi.

9. **Hamasisha –** Hitimisha wasilisho lako kwa wito wa utendaji. Iambie hadhira yako kile hasa wanachoweza kufanya katika kuitikia washilisho lako.

10. **Vuta pumzi kwa nguvu, tulia! –** Using'ang'anie kibweta unachotumia kuzungumza. Ikiwa umesimama nyuma yake, jiachie na kusimama wima. Zunguka zunguka. Tumiwa mwonekano wako kusisitiza dondoo. Kumbuka kuwa namna unavyosema jambo ndivyo unavyoliwekea umuhimu kulingana na ulivyolisema.

UCHUNGUZI WA MAELEZO MAFUPI YA
MAISHA YA FAMILIA

Jina ……. Tarehe ya Kuzaliwa …….

Kundi la Umri ◯ 18-30 ◯ 31-40 ◯ 41-50 ◯ 51-60 ◯ 61-70

Jinsia ◯ Me ◯ Ke

Anuani ……..……

Simu (nyumbani) …….……. Simu(kazini) ……..……

Umebatizwa katika kanisa la Waadventista wa Sabato ◯ Ndiyo ◯ Hapana

Ikiwa wewe ni mshiriki wa kanisa mahalia ……..…….

Ikiwa siyo, wewe ni dini gani au dhehebu gani? ……..……

Uhusiano wa ndoa

◯ Sijaolewa/sijaoa wala sikuwahi

◯ Sina mwenzi nimepewa talaka

◯ Sina mwenzi, ni mjane/mgane

◯ Nimeoa/olewa – Jina …… Tarehe ya kuzaliwa …….

◯ Mwenzi ni mshiriki katika kanisa la Waadvenista wa Sabato mahalia

◯ Mwenzi siyo mshiriki, dini/dhehebu lake ni ……

Watoto unaokaa nao

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Anasoma darasa la …….. Shule anayosoma …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Anasoma darasa la …….. Shule anayosoma …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Anasoma darasa la …….. Shule anayosoma …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Anasoma darasa la …….. Shule anayosoma …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Wanafamilia wengine unaokaa nao:

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Uhusiano wa kifamilia …….

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Uhusiano wa kifamilia …….

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Uhusiano wa kifamilia …….

Jina ……. Tarehe ya kuzaliwa …….

Amebatizwa SDA? ……. Kanisa ulipo ushirika …….…..

Uhusiano wa kifamilia …….

Ni jambo gani unalodhani kamati ya huduma za familia ingefanya mwaka huu ili kushughulikia shauku/haja ya familia yako?

……

……

……

……

Shauku yangu kubwa ni huduma kwa familia, na niko radhi kusaidia kwa:

- ◯ Kupiga simu kadiri itakavyohitajika
- ◯ Kushiriki katika kupanga vipindi
- ◯ Kuwezesha usafirishaji
- ◯ Kuandaa matukio
- ◯ Kutayarisha vyakula/vinywaji
- ◯ Kulea watoto
- ◯ Kufanya matangazo
- ◯ Mengineyo.
- ◯ Kuwasilisha mihadhara/semina/warsha au mawasilisho mengine kadiri ya maeneo mengine ya shauku

  ……..

  ……..

  ……..

MAELEZO MAFUPI YA
MAISHA YA FAMILIA

Kanisa …….……. Tarehe …….

Kitengo cha Familia:

Washiriki Hai

- ◯ Wenye watoto wa umri chini ya 18
- ◯ Wasio na watoto wa umri chini ya 18

Washiriki Wasio Hai

- ◯ Wenye watoto umri chini ya 18
- ◯ Wasio na watoto umri chini ya 18

Mwenzi ni Mshiriki

- ◯ Umri wa 18-30
- ◯ Umri wa 31-50
- ◯ Umri wa 51-60
- ◯ Umri wa 61-70
- ◯ Umri wa 71+

Mwenzi siyo Mshiriki

- ◯ Umri wa 18-30
- ◯ Umri wa 31-50
- ◯ Umri wa 51-60
- ◯ Umri wa 61-70
- ◯ Umri wa 71+

Wasio na Wenzi – Hakuolewa/hakuoa

- ◯ Umri wa 18-30
- ◯ Umri wa 31-50
- ◯ Umri wa 51-60
- ◯ Umri wa 61-70
- ◯ Umri wa 71+

Wasio na Wenzi – Hawakuoa/olewa

- ◯ Umri wa 18-30
- ◯ Umri wa 31-50
- ◯ Umri wa 51-60
- ◯ Umri wa 61-70
- ◯ Umri wa 71+

UCHUNGUZI WA SHAUKU YA
HUDUMA ZA FAMILIA

Kundi la Umri ◯ 18-30 ◯ 31-40 ◯ 41-50 ◯ 51-60 ◯ 61-70 ◯ 71+

Jinsia ◯ Me ◯ Ke

Kutoka katika mada hapa chini, tafadhali chagua mada tano ambazo zinakuvutia. Weka alama mbele ya kila mmoa inayokuvutia

- ◯ Kujitayarisha kwa ajili ya ndoa
- ◯ Masuala ya fedha za familia
- ◯ Nidhamu nyumbani
- ◯ Malezi ya vijana waliopevuka
- ◯ Kujitayarisha kwa jili ya watoto
- ◯ Kuzinduka kutoka katika talaka
- ◯ Malezi ya mzazi mmoja
- ◯ Masuala ya Ngono
- ◯ Kustawisha ndoa yako
- ◯ Kuzinduka kutoka katika majonzi
- ◯ Kuelewa Haiba
- ◯ Maisha ya ibada na ushirika
- ◯ Mawasiliano
- ◯ Maisha ya Kuishi bila mwenzi
- ◯ Kuendeleza hali ya kujithamini
- ◯ Kutatua migogoro na hasira
- ◯ Runinga na mitandao ya kijamii
- ◯ Matayarisho ya kustaaafu
- ◯ Masuala ya utegemezi a kemikali
- ◯ Familia iliyounganika
- ◯ Kifo na Kufariki
- ◯ Kuukubali ujane.
- ◯ Mengine (Tafadhali orodhesha) ……..

Mgeni rasmi au mzungumzaji aliyependekezwa ……

Jina ……..

Anuani ……...…….. Simu ……

Eneo la Utaalam ……

Ni muda gani wa siku na ni siku gani ya juma unayoona kuwa bora kwako kuhuduria program ya saa 1 ½ hadi 2 katika moja ya mada zilizoorodheshwa hapo juu? (weka alama kwa sehemu ya muda unaoona unafaa kulingana na mipango yako)

	J/pili	J/tatu	J/nne	J/tano	Alh.	Ijm	Jmmsi
Asubuhi	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯
Mchana	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯
Jioni	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯

UCHUNGUZI WA ELIMU YA
MAISHA YA FAMILIA YA JUMUIYA

1. Je, unaamini tatizo namba moja linalokabili familia katika jumuia hii sasa hivi ni nini?
   ……
   .
2. Je, ungefikiria kuhudhuria moja ya semina hizi za maisha ya familia kama zingeendeshwa katika eneo lako? (chagua nyingi kadiri unavyotaka)

◯ Jinsi ya kushughulikia migogoro
◯ Kuwasiliana katika ndoa
◯ Kustawisha ndoa
◯ Kuwaelewa watoto
◯ Kujiamini
◯ Stadi za malezi
◯ Kushugulika na vijana
◯ Kuzinduka kutoka katika talaka
◯ Kumudu msongo
◯ Kushinda upweke wa mwisho wa juma
◯ Masuala ya fedha kwenye familia
◯ Kuzinduka kutoka katika huzuni
◯ Kumudu muda vipaumbele vya maisha
◯ Kupanga kustaafu
◯ Darasa la Matayarisho ya kujifungua
◯ Mengineyo (tafadhali orodhesha) …….

3. Ni muda gani wa siku na ni siku gani ya juma ni bora kwako kuhuduria program ya saa 1 ½ hadi 2 kwa moja ya mada zilizoorodheshwa hapo juu? (weka alama kwa katika sehemu unayoona inafaa kwa muda wako)

	J/pili	J/tatu	J/nne	J/tano	Alh.	Ijm	Jmmsi
Asubuhi	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯
Mchana	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯
Jioni	◯	◯	◯	◯	◯	◯	◯

4. Itasaidia kuimarisha uchunguzi huu ikiwa tutapata taarifa zifuatazo kukuhusu:

   Umri:

◯ <18 ◯ 18-30 ◯ 31-40 ◯ 41-50 ◯ 51-60 ◯ 61-70 ◯ 71+

Jinsia ◯ Me ◯ Ke

Je una watoto wenye umri chini ya miaka 18 nyumbani kwako?

◯ Ndiyo ◯ Hapana

Je, wewe:

◯ Hukuwahi kuoa/kuolewa

◯ Umeolewa/umeoa

◯ Mmetengana

◯ Ni mhanga wa talaka

◯ Ni mjane

◯ Umeolewa/oa baada ya talaka

KIELELEZO CHA
TATHMINI

1. Ni nini kilikusukuma zaidi kuhusu warsha hii?

   ……

2. Ulijifunza nini ambacho ulikuwa haujui kabla?

   ……

3. Je, maudhui katika warsha hii yaliwasilishwa kwa uwazi?

   ……

4. Ni shughuli/kipindi gani hakikuwa na thamani kabisa kwako?

   ……

5. Hii warsha ingewezaje kuboreshwa

   ……

6. Kwa kipimo cha 1 hadi 5, tukiwa na 1 kama ishara ya kutokuridhika kabisa na 5 kama ishara ya kuridhika kabisa, ni kwa namna gani unaweza kupima hii warsha? (weka alama kwenye mojawapo ya nambari)

◯ 1	◯ 2	◯ 3	◯ 4	◯ 5
Sikuridhika Kabisa	Sikuridhika Kiasi fulani	Nimeridhika Kidogo	Nimeridhika Kiasi fulani	Nimeridhika Kabisa

7. Ni nani amefanya tathmini hii?

Kundi la Umri ◯ 18-30 ◯ 31-40 ◯ 41-50 ◯ 51-60 ◯ 61-70 ◯ 71+

Jinsia ◯ Me ◯ Ke

Hali ya ndoa yako:

- ◯ Hukuwahi kuoa/kuolewa
- ◯ Umeolewa/umeoa
- ◯ Mmetengana
- ◯ Ni mhanga wa talaka
- ◯ Ni mjane
- ◯ Umeolewa/oa baada ya talaka

Ni kwa muda gani umekuwa katika ndoa, umeachika, umetengana au umekuwa mjane?

Miaka …….. miezi …….

Ahsante sana kwa maoni yako ya dhati, yatatusaidia katika kupanga warsha zijazo.

KIAMBATISHI ‘B’

MATAMKO YALIYOPITISHWA

Haya *Matamko Yaliyopitishwa* ni msimamo rasmi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato juu ya mada tajwa.

UTHIBITISHO
WA NDOA

Masuala yanayohusiana na ndoa yanaweza kuonenaka katika nuru yake ya kweli pale tu yatakapoangaliwa dhidi ya usuli wa dhana bora ya kimbingu ya ndoa. Ndoa ilianzishwa na mbingu katika bustani ya Edeni na kuthibitishwa na Yesu Kristo kuwa ni ndoa ya jinsia mbili tofauti lakini pia mume mmoja na mke mmoja, muunganiko wa misha yote wenye upendo na ushirikiano kati ya mwanamume na mwanamke. Katika upeo wa shughuli zake za uumbaji, Mungu aliunda ubinadamu kama jinsia ya kiume na ya kike kwa mfano wake mwenyewe, na kuanzisha taasisi ya ndoa, iliyojengeka katika muunganiko kimwili, kimhemuko, na kiroho wa agano la jinsia mbili unaotamkwa katika Maandiko kama "mwili mmoja."

Chimbuko lake likiwa ni tofauti ya jinsia za kibinadamu, umoja huu wa ndoa unaibuka katika namna moja ya umoja ndani ya tofauti za Uungu. Kote katika Maandiko, muunganiko wa jinsia mbili katika ndoa umetukuzwa kama kielelezo cha muunganiko kati ya Uungu na ubinadamu. Ni ushuhuda wa kibinadamu kwa upendo wa kujitoa wa Mungu na agano na watu wake. Kule kuhusiana kwa mwanamume na mwanamke kwa upatanifu katika ndoa kunaleta uwakilishi mdogo wa umoja kijamii ambao umedumu kwa muda mrefu kama kiambato cha jamii iliyo thabiti. Lakini pia Muumbaji alikusudia tendo la ndoa katika ndoa litumike kwa kusudi la kuunganisha, pamoja na kuwezesha kuendeleza vizazi vya familia ya kibinadamu kwa uzao. Katika kusudi la kimbingu, kuendeleza vizazi kuna chimbuko lake katika mchakato ambao mume na mke wanafurahia, na kupata raha katika utimilifu wa kimwili. Ni katika upendo kati ya mume na mke ndipo wanapoweza kufahamiana kwa undani katika tendo la ndoa linalowaunganisha na mtoto akajaliwa. Mtoto wao huyu ni udhihirisho ulio hai wa kuwa mmoja. Mtoto huyu anapokuwa anahangaika katika mazingira ya upendo wa ndoa na umoja uliomwezesha kupatikana, na hivyo kuwa na faida ya uhusiano na kila mmoja wa wazazi hawa wa asili.

Muunganiko wa mume mmoja na mke mmoja unathibitishwa kama msingi wa kimbingu uliowekwa wakfu wa familia na Maisha ya kijamii, pia ndiyo mtazamo sahihi pekee wa maadili katika namna wanavohusiana kwa undani kupitia katika viungo vyao kwenye tendo la ndoa. Hata hivyo taasisi ya ndoa siyo mpango pekee wa Mungu wa kuwezesha mahitaji ya uhusiano wa mwanadamu, au wa kufahamu uzoefu wa familia. Useja pamoja na urafiki wa waseja pia upo katika mpango wa kimbingu. Ushirikiano na kutegemeza kwa marafiki kunajitokeza kwa umuhimu katika Biblia

kote katika Agano la Kale na katika Agano Jipya. Usharika wa kanisa, yaani kaya ya Mungu, ipo kwa wote bila kujali hali yao ya ndoa. Hata hivyo Maandiko yanaweka mipaka thabiti kijamii na kingono kati ya uhusiano wa kirafiki kama huo na ndoa.

Kwa mtazamo huu wa kibiblia wa ndoa, kanisa la Waadventista wa Sabato linashikilia bila kigugumizi, na kuamini kwamba kushusha kwa namna yoyote ile mtazamo huu uliotukuka ni sawa na kushuhsa viwango wa kimbingu. Na kwa sababu ndoa imeharibiwa na dhambi, ule usafi na uzuri wa ndoa kama ulivyokusudiwa na Mungu unahitaji kurejeshwa. Kupitia katika kutambua kazi ya ukombozi ya Kristo na kazi ya Roho wake katika mioyo ya wanadamu, lile kusudi la awali la ndoa linaweza kurejeshwa na uzoefu wa kufurahisha na wa ukamilifu wa ndoa ukatambuliwa na mume na mke wanaounganisha maisha yao katika kiapo cha ndoa.

TAMKO JUU YA
NYUMBA NA FAMILIA

Afya na usatawi wa jamii unahusiana moja kwa moja na ustawi wa sehemu zinazojenga kitengo cha familia. Leo hii familia zina shida pengine kuliko wakati mwingine wowote uliopita. Wachangiaji kwenye mitandao ya kijamii wanakosoa huku kusambaratika kwa maisha ya kisasa ya familia. Dhana ya Kikristo ya ndoa kati ya mume mmoja na mke mmoja sasa hivi inashambuliwa. Katika wakati huu wa wasiwasi mkubwa katika familia Kanisa la Waadventista wa Sabato linahimiza kila mwana-familia kuimarisha hali yake ya kiroho na uhusiano wa kifamilia kwa upendano, heshima, staha na kuwajibika.

Sehemu ya 22 ya Imani za msingi za kanisa zilizojengeka katika Biblia inatamka dhahiri kuhusu uhusiano wa ndoa kama, "uhusiano unaoakisi upendo, usafi, ukaribu, na hali ya uhusiano wa kudumu kati ya Kristo na kanisa lake." Ingawaje baadhi ya mahusiano ya familia yanaweza kuwa na mapungufu kutoka kwa ukamilifu, hawa wenzi walio katika ndoa ambao wamejitoa kikamilifu kwa kila mmoja wao katika Kristo wanaweza kufikia umoja wa upendo kupitia katika uongozi wa Roho Mtakatifu na malezi ya kanisa. Mungu anabairiki familia na anakusudia kwamba wale waliopo katika familia wasaidiane kuelekea katika ukomavu mkamilifu.

"Wazazi wanatakiwa kukuza watoto wao wakiwafundisha kumpenda na kumtii Bwana. Wanatakiwa kuwafundisha kwa mfano wao wenyewe na kwa maneno yao, kwamba Kristo ni mnadhimu mwenye upendo, siku zote akiwajali na kutaka wawe ni washiriki katika mwili wake, ambao ni familia ya Mungu."

Ellen G. White ambaye ni mmoja wa waanzilidhi wa kanisa anatamka kuwa, "Kazi ya wazazi ni msingi wa kazi zingine zote. Jamii imejengwa na familia, na ni kile ambacho kichwa cha familia kinakusudia. "Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo; Maana ndiko zitokako chemchemi za uzima"(Mithali 4:23); na moyo wa jumuiya, moyo wa kanisa, na moyo wa taifa ni kaya. Ustawi wa jamii, mafanikio ya kanisa, maendeleo ya taifa, vyote vinategemea mivuto ya nyumbani." The Ministry of Healing, uk. 349.

Hili tamko kwa umma lilitolewa na kiongozi mkuu wa Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato, Neal C. Wilson baada ya kushauriana na wazaidizi wake 16 duniani kote tarehe 27 June, 1985 katika mkutano mkuu wa kanisa kule New Orleans, Louisiana.

TAMKO KUHUSU
UNYANYASAJI WA WATOTO KINGONO

Unyanyasaji wa watoto kingono unatokea pale mtu mzima au mwenye nguvu kuliko mtoto anapotumia uwezo wake au mamlaka yake, au nafasi ya kuaminiwa aliyo nayo kumhusisha mtoto katika mwenendo wa kingono au vitendo vya jinsi hiyo. Kujamiiana kwa maharimu ambako ni aina maalum ya unyanyasaji wa watoto kingono unafafanuliwa kama vitendo vya kingono kati ya mtoto na mzazi wake, mdogo au mkubwa wake, mmoja wa familia ya karibu au mzazi wa kambo au wa kupanga.

Hawa wanyanyasaji wa kingono wanaweza kuwa ni wanaume au wanawake, na wanweza kuwa ni watu wa umri wowote, taifa lolote, au walio katika hali yoyote ya kiuchumi. Mara nyingi ni wanaume ambao wameoa na wana watoto, wakiwa na kazi za maana, na hata wakiwa ni wahudhuriaji wazuri wa kanisani. Mara nyingi ni kawaida kwa wakosaji wa jinsi hii kukataa kwa nguvu huu mwenendo wao wa unyanyasaji, wanakataa kuona vitendo vyao kama tatizo na wakati mwingine kuhalalisha mwenendo wao au kuhamisha lawama kwa mwingine au kwa hali au kitu kingine. Pamoja na kwamba hawa wanyanyasaji wanakuwa na hali ya hofu iliyozama ndani yao na kutokujiamini, haya matatizo kamwe yasikubalike kama sababu ya kuwafanya wanyanyase watoto kingono. Mamlaka nyingi zinakubaliana na dhana kwamba suala halisi katika unyanyasaji wa watoto kingono linahusiana zaidi na tamaa ya kuonesha uwezo na umiliki kuliko kitendo chenyewe cha ngono.

Mungu alipoumba familia ya mwanadamu, alianza na ndoa kati ya mwanamume na mwanamke akijenga katika upendo na uaminifu. Uhusiano huu bado umekusudiwa kuwa msingi wa familia iliyo imara yenye furaha ambayo inaonesha heshima, staha na uadilifu kwa kila mwana familia, vyote hivi vikilindwa na kudumishwa. Kila mtoto, awe ni wa kiume au wa kike, anatakiwa kuthibitishiwa kwamba amedhaminiwa kwao na Mungu. Watoto wanatakiwa kuweza kuheshimu, kustahi, na kuwatumainia wazazi wao pamoja na wana-familia wengine bila hofu ya hatari ya kunyanyaswa.

Biblia inakataza unyanyasaji wa watoto kingono kwa matamko thabiti kadiri iwezekanavyo. Inaonekana kuwa kila jitihada za kuchanganya, kuweka kiwingu, au kudhalilisha mipaka ya kizazi, au jinsia kupitia katika mwenendo wa unyanyasaji kingono inachukuliwa kama kitendo cha usaliti na ukiukwaji wa utu wa mtu. Inakataza matumizi mabaya ua mamlaka, utawala na wajibu, kwa sababu haya maeneo yanagusa moja kwa moja moyo wa hisia za mhanga kuhusu wao wenyewe, wengine, na Mungu, na kusambaratisha kabisa uwezo wao wa kupenda na kutumainia. Yesu alitumia lugha

kali kukata vitendo vya yeyote ambaye kupitia katika maneno au matendo atamsababishia mtoto kujikwaa.

Jumuiya wa Wakristo wa kanisa la Waadventista wa Sabato kama jumuiya zingine tu, haina kinga dhidi ya unyanyasaji wa watoto kingono. Tunaamini kwamba mafundisho ya Imani ya Waadventista wa sabato yanatutaka tujihusishe kikamilifu katika kuzuia. Tumeitwa kusaidia kiroho wale walionyanyaswa na wanaonyanyasa pamoja na familia zao katika mchakato wa kupona na kurejea, na kuwawajibisha wataalam waliopo kanisani na viongozi walei kanisani kuhakikisha mwenendo wao binafsi ni stahiki kwa watu wa nafasi hiyo ya kutumainiwa kama viongozi wa kiroho.

Kama kanisa, tunaamini kwamba Imani yetu inatutaka kufanya yafuatayo:

1. Kutetea kanuni ya Kristo ya mahusiano ya familia ambayo yanatambua heshima, usafi, na uadilifu wa watoto kama haki ya msingi ya kimbingu

2. Kuleta mazingira ambamo mtoto aliyenyanyaswa kingono anaweza kujihisi salama anapotoa taarifa ya kunyanyaswa kingono na anaweza kuhisi kwamba kuna mtu anayeweza kumsikiliza.

3. Kuwa na taarifa kamili kuhusu unyanyasaji kingono na athari zake katika jumuiya ya kanisa letu.

4. Kusaidia wachungaji na viongozi walei kutambua ishara zinazotahadharisha kuhusu unyanyasaji wa watoto kingono na kufahamu jinsi ya kutikia kwa namna iliyo stahiki pale hisia za unyanyasaji zinapojitokeza au mtoto anapotoa taarifa ya kunyanyaswa kingono.

5. Kuanzisha mahusiano ya kurejesha wakishirikiana na wataalam wa ushauri, mawakala wa mashambulizi ya kingono, ambao kwa kutumia stadi zao za kitaaluma wanaweza kumsaidia mhanga wa unyanyasaji pamoja na familia yake.

6. Kuandaa miongozo/sera katika ngazi stahiki ili kusaidia viongozi wa kanisa katika:

    a. Kuhakikisha mtu aliyeshutumiwa kunyanyasa mtoto au watoto kingono anatendewa kwa haki.
    b. Kumwajibisha aliyetuhumiwa kunyanyasa watoto kingono kwa ajili ya vitendo vyake visivyokubalika kwa kuhakikisha utawala unachukua hatua stahiki za nidhamu.

7. Kutegemeza elimu na ustawi wa familia na wana-familia kwa kufanya yafuatayo:
    a. Kuondoa Imani za kitamaduni na za kidini zianzoweza kutumika kuhalalisha au kufunika unyanyasaji wa watoto kingono.
    b. Kujenga hali ya kujiamini yenye ustawi ndani ya mtoto ambayo itamwezesha kujiheshimu yeye mwenyewe na kuheshimu wengine pia.
    c. Kudumisha uhusiano kama wa Kristo kati ya jinsia ya kiume na jinsia ya kike nyumbani na kanisani.

8. Kutoa msaada na huduma ya ukombozi iliyojengeka katika Imani ndani ya jumuiya ya kanisa kwa wahanga wa unyanyasaji pamoja na wanyanyasaji wenyewe wakati huo huo ukiwawezesha kujiunga na mtandao wa vyanzo vya wataalam katika jumuiya hiyo.

9. Kuhimiza mafunzo yanayoendeshwa na wataalam wa familia ili kuwezesha mchakato wa uponyaji na urejeshwaji wa wahanga na hao wakosaji wenye hatia.

(Tamko hilo linatolewa kwa kanuni inayooneshwa katika mafungu yafuatayo: Mwanzo 1:26-28; 2:18-25; Walawi 18:20; 2 Samweli 13:1-22; Mathayo 18:6-9; 1 Wakorintho 5:1-5; Waefeso 6:1-4; Wakolosai 3:18-21; 1 Timotheo 5:5-8)

TAMKO JUU YA
MIGOGORO YA KIFAMILIA

Vurugu za familia ni pamoja na mashambulizi kimwili, kimhemuko, kingono, kwa maneno, au kwa kupuuza wajibu yanayofanyika na mtu au watu dhidi ya mwingine ndani ya familia, iwe ni kati ya wana-ndoa, wana-ndugu au watu wanaohusiana wakiishi pamoja au mbalimbali, au wahanga wa talaka. Utafiti wa kimataifa uliofanyika hivi karibuni unaonesha kwamba vurugu za kifamilia ni tatizo la kilimwengu. Linatokea kati ya watu wa umri wote na mataifa yote katika jamii za ngazi zote za uchumi, na katika familia za aina zote za dini na hata wasio na dini. Kiwango cha matukio kimeonekana kufanana kwa miji, viunga vya miji na hata vijijini huko.

Vurugu za kifamilia zinajidhihirsha kwa namna nyingi. Kwa mfano, inaweza kuwa ni mashambulizi ya kimwili kwa mwenzi mmoja wa ndoa, matukio ya mlipuko wa hasira, kudorora kwa tabia, na madai yasiyokuwa halisi kwa ukamilifu pia yanachukuliwa kama unyanyasaji. Inaweza kuwa pia katika hali ya kulazimisha kwa nguvu au kwa vurugu tendo la ndoa kwa wanandoa, au kutishia kwa kutumia njia mbalimbali za udhalilishaji kwa maneno au bila maneno. Ni pamoja na mwenendo kama vile kujamiiana kwa maharimu au kutowatendea na kuwapuuza watoto walio katika umri mdogo kwa wazazi au walezi wengine ambao matokeo yake ni maumivu au madhara. Vurugu dhidi ya wazee zinaweza kuonekana kimwili au kisaikollojia, kingono, kwa maneno, kwa vitendo hata kwa kuwanyima tiba.

Biblia inaonesha waziwazi kwamba alama inayotofautisha waumini wa Kikristo na wengine ni thamani ya uhusiano wao wa kibinadamu kanisani na katika familia. Ni katika roho ya Kristo kupenda na kukubali, kutafuta kuthibitisha na kujengana kila mmoja na mwenzake badala ya kuraruana na kusulubiana. Hakuna nafasi kati ya wafuasi wa Kristo kwa utawala wa kiimla na kutukana mamlaka na uwezo ambao mtu anao. Kwa kusukumwa na upendo kwa Kristo, wale wote ambao ni wanafunzi wake wanaitwa kuonesha heshima na kujali kwa ustawi wa wengine, wakiwakubali wanaume na wanawake kama sawa, huku wakitambua kwamba kila mtu ana haki ya heshima na uadilifu. Unaposhindwa kuhusiana na wengine kwa namna hii ni sawa na kukiuka ukuhani wako na kudhalilisha binadamu aliyeumbwa na kukombolewa na Mungu.

Mtume Paulo analeza kanisa kama "kaya ya Imani" ambayo inafanya kazi kama familia kubwa, ikitoa ukubali, uelewa, na faraja kwa wote hasa wale ambao wanaumia au hawakujaliwa. Maandiko yanaonesha kanisa kama familia ambapo ukuaji binafsi wa

kiroho kadiri hisia za usaliti, kukataliwa na huzuni zinavyoondoka na kutoa nafasi kwa hisia za msamaha, matumaini, na ukamilifu. Biblia pia inazungumza kuhusu wajibu binafsi wa Mkristo wa kulinda mwili wake ambalo ni hekalu, kutoka katika kuuchafua maana hayo ndiyo makao ya Mungu.

Kwa masikitiko, vurugu za kifamilia huwa zinatokea pia katika nyumba nyingi za Wakristo. Hatuwezi tukapuuza hili. Vurugu hizi zinaathiri sana maisha ya wote wanaohusika na baada ya muda, hata kusababisha mtazamo ulio potovu kumhusu Mungu, wewe mwenyewe na wengine pia.

Ni Imani yetu kwamba kanisa lina wajibu wa kufanya yafuatayo:

1. Kuwajali wale wanaohusika katika vurugu za kifamilia na kuitikia kwa mahitaji yao kwa kufanya yafuatayo:
    a. Kuwasikiliza na kuwakubali wale ambao wanateseka kutokana na unyanyasaji, kuwapenda na kuwathibitisha kama wanadamu wa thamani na wenye staha.
    b. Kukazia hali ya ukosefu wa haki inayotokana na unyanyasaji na kuzungumza kwa kutetea wahanga wa unyanyasaji ndani ya jumuiya ya waumini na ndani ya jamii kwa ujumla.
    c. Kujali na kutoa huduma inayotegemeza familia zilizoathirika kwa vurugu na unyanyasaji, ukitafuta kuwezesha hao wahanga na wakosaji waweze kufikia ushauri wa wataalam wa kanisa la Waadventista wa Sabato wanapoweza kupatikana au wataalam wengine wowote waliopo katika jumuiya.
    d. Kuhimiza mafunzo na kuleta huduma ya wataalam wa kanisa la Waadventista wa Sabato wenye leseni kwa washiriki na jumuiya inayozunguka.
    e. Kutoa huduma ya upatanisho pale toba na maungamo ya mkosaji yanapowezesha uwepo wa msamaha na kurejeshwa katika mahusiano. Siku zote toba inahusu kukubali kabisa na kuwajibika kwa mabaya yaliyotedwa, ukubali wa kurejesha kwa kila hali iwezekanayo na kubadilisha mwenendo ili kuondoa kabisa unyanyasaji.
    f. Kujielekeza katika nuru ya injili katika asili ya mume-mke, mzazi-mtoto, na mahusiano mengine ya karibu ukiwawezesha watu na familia kukua kuelekea katika halisi aliyokusudia Mungu katika maisha yao pamoja.
    g. Kulinda dhidi ya kutengwa na jamii kwa wahanga au wahalifu ndani ya familia au katika jumuiya ya kanisa, wakati huohuo ukimwajibisha mhalifu kwa vitendo vyake.

2. Kuimarisha maisha ya familia kwa kufanya yafuatayo:

a. Kutoa elimu ya familia ambayo inaelekezwa kwenye neema ikihusisha uelewa wa Biblia wa upendano na mapatano, usawa na heshima ambavyo haviepukiki katika uhusiano wa Kikristo
b. Kuongeza uelewa wa vigezo ambavyo vinachangia katika vurugu za kifamilia.
c. Kuendeleza namna ya kuzuia unyanyasaji na vurugu pamoja na mzunguko unaojirudia rudia unaoonekana mara kwa mara ndani ya familia na katika vizazi.
d. Kurekebisha Imani za kidini na za kitamaduni ambazo kwa kawaida zimeshikiliwa zinazoweza kutumiwa kuhalalisha au kutetea vurugu za kifamilia. Kwa mfano, wakati wazazi wanaelekezwa na Mungu kuwarekebisha watoto wao, wajibu huu hauwapatii haki ya kutumia mbinu za kikatili kuwanidhamisha.

3. Kukubali wajibu wetu wa kimaadili kuwa waangalifu na wasikivu kwa unyanyasaji ndani ya familia za makusanyiko yetu na jumuiya zetu, na kutamka wazi wazi kwamba mwenendo wa unyanyasaji kama huo ni ukiukaji wa viwango vya Kikristo vya Waadventista wa Sabato. Ishara zozote au taarifa za unyanyasaji ni lazima zichukuliwe kwa uzito wote wala zisipuuzwe. Kwa washiriki wa kanisa kunyamaza na kupuuza bila kukemea ukosaji wa jinsi hii, ni sawa na kukubaliana, kupalilia na hata kushadadia vurugu za kifamilia.

   Ikiwa tunataka kuishi kama watoto wa nuru, ni lazima tuangaze giza ambamo hizi vurugu za kifamilia zinatendeka. Ni lazima tujaliane sisi kwa sisi, hata pale ambapo inakuwa rahisi kwetu kutohusika.

(Tamko hilo linatolewa kwa kanuni inayooneshwa katika mafungu yafuatayo: Kutoka 20:12; Mathayo 7:12; 20:25-28; Marko 9:33-45; Yohana 13:34; Warumi 12:10, 13; 1 Wakorintho 6:19; Wagalatia 3:28; Waefeso 5:2, 3, 21-27; Wakolosai 3:12-14; 1 Wathesalonike 5:11; 1 Timotheo 5:5-8)

TAMKO KUHUSU MTAZAMO WA KIBIBLIA WA WATOTO AMBAO HAWAJAZALIWA NA MATOKEO YAKE KATIKA KUTOA MIMBA

Wanadamu wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Sehemu ya zawadi waliyopewa na Mungu aliyowapatia ni ule uwezo wa kuendeleza kizazi kwa uzao, uwezo wa kushiriki katika uumbaji pamoja na Mwanzilishi wa uhai. Hii zawadi takatifu inatakiwa kuthaminiwa siku zote na kuhifadhiwa kwa uangalifu. Katika mpango wa mwanzo kabisa wa Mungu, kila mimba ilitakiwa kuwa ni matokeo ya udhihirisho wa upendo kati ya mwanamume na mwanamke waliojitoa kikamilifu kwa kila mmoja wao kwenye ndoa. Mimba inatakiwa kuthaminiwa, na kila mtoto anatakiwa kupendwa, kuthaminiwa na kulelewa hata kabla ya kuzaliwa. Bahati mbaya tangu dhambi ilipoingia, Shetani amefanya jitihada kubwa kuchafua huo mfano wa Mungu kwa kuondoa ile zawadi ya Mungu – pamoja na zawadi ya kuendeleza kizazi kwa uzao. Hatimaye watu wakati mwingine wanakabiliwa na mashaka makubwa na ugumu sana katika kuamua kuhusu mimba.

Kanisa la Waadventista wa Sabato limejitoa kikamilifu kwa mafundisho ya kanuni za Maandiko Matakatifu zinazoonesha thamani ya Maisha mbele za Mungu na kutoa mwongozo wa huyo atakayekuwa mama au baba, wafanyakazi wa idara ya afya, kanisa na waumini wote katika masuala ya Imani, mafundisho, mwenendo wa kimaadili na mtindo wa misha. Pamoja na kwamba kanisa siyo dhamiri ya muumini mmoja mmoja, bado lina wajibu wa kutoa kanuni na mafundisho ya Neno la Mungu.

Tamko hili linathibitisha utakatifu wa Maisha na kanuni za Kibiblia za sasa kuhusu kutoa mimba. Kutoa mimba kwa namna kunavyotumika katika tamko hili, kunaelezewa kama kitendo kinachokusudia kukomesha mimba na kitendo hiki hakijumuishi kuharibika kwa mimba.

KANUNI ZA KIBIBLIA NA MAFUNDISHO YANAYOHUSU KUTOA MIMBA

Kwa kuwa zoezi la kutoa mimba linatakiwa kupimwa katika nuru ya Maandiko, kanuni zifuatazo za Kibiblia na mafundisho zinatoa mwongozo kwa jumuia ya Imani na watu mmoja mmoja walioathirika na chaguzi hizi:

1. ***Mungu anathibitisha thamani ya utakatifu katika Maisha ya mwanadamu.*** Maisha ya mwanadamu ni ya thamani kubwa kwa Mungu. Kwa kuwa Mungu

ndiye aliyemuumba mwanadamu kwa mfano wake (Mwanzo 1:27; 2:7), ana shauku kubwa kwa wanadamu. Yeye anawapenda na kuwasiliana nao, na wao pia wanatakiwa kumpenda na kuwasiliana naye.

Uhai ni zawadi ya Mungu, na Yeye ndiye mtoaji wa uhai. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. (Yohana 1:4). Na Yeye anao uzima ndani yake (Yohana 5:26). Yeye ndiye Ufufuo na huo uzima (Yohana 11:25; 14:6). Yeye alikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele. (Yohana 10:10). Wale walio na Mwana, wanao uzima (1 Yohana 5:12). Yeye pia ndiye anayetegemeza uzima (Matendo 17:25-28; Wakolosai 1:17; Waebrania 1:1-3), na Roho Mtakatifu anaelezewa kama Roho wa Uzima (Warumi 8:2). Mungu anawajali viumbe wake kwa kina na hasa wanadamu.

Pamoja na hayo, umuhimu wa uzima wa mwanadamu unawekwa wazi baada ya anguko (Mwanzo 3), Mungu "aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16). Mungu angeweza kumkataa, na kukomesha ubinadamu wenye dhambi, Alichagua uzima badala yake. Matokea yake, wafuasi wa Kristo watafufuliwa kutoka kwa wafu na wataishi katika mawasiliano ya uso kwa uso na Mungu (Yohana 11:25-26; 1 Thesalonike 4:15-16; Ufunuo 21:3). Kwa sababu hiyo basi, uzima wa mwanadamu ni wa thamani isiyopimika. Jambo hili ni kweli katika ngazi zote za uhai wa mwanadamu: kichanga ambacho hakijazaliwa, Watoto katika umri mbali mbali, vijana wapevu, watu wazima, na wazee – wenye uwezo binafsi wa kiakili, kimwili, na kimhemuko. Ni kweli pia kwa wanadamu wote bila kujali jinsia, asili, tabaka katika jamii, dini, na tofauti zingine zozote zinazowatofautisha. Uelewa huu wa utakatifu wa uzima unatoa thamani iliyo sawa isiyoweza kuharibiwa kwa kila uhai wa mwanadamu unatakiwa kuchukuliwa kwa heshima kubwa na kwa namna ya kujali.

2. ***Mungu anachukulia kichanga ambacho hakijazaliwa kama mwanzo wa uhai wa mwanadamu.*** Uhai kabla ya kuzaliwa pia ni wa thamani mbele za Mungu, na Biblia inaeleza kuwa Mungu anamtambua mwanadamu kabla hajaingia tumboni mwa mama yake. "Macho yako yaliniona kabla sijakamilika; Chuoni mwako ziliandikwa zote pia, Siku zilizoamriwa kabla hazijawa bado." (Zaburi 139:16). Katika hali fulani, Mungu aliongoza moja kwa moja Maisha ya wazazi. Samsoni alikuwa awe "…mnadhiri wa Mungu tangu tumboni" (Waamuzi 13:5). Isaya mwenyewe anasema kuwa, "…aliyeniumba tangu tumboni niwe mtumishi wake" (Isaya 49:1, 5). Yeremia alikuwa ameshachaguliwa kama nabii kabla ya kuzaliwa kwake (Yeremia 1:5), Kama na Paulo pia katika Wagalatia 1:15, Yohana

Mbatizaji anasemwa kuwa, "…atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye." (Luka 1:15). Kuhusu Yesu, yule malaika Gabrieli alimweleza Mariamu kuwa, "…hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu." (Luka 1:35). Katika hali yake ya kuuvaa mwili wa binadamu, Yesu mwenyewe alipitia uzoefu wa kuwa na uzima kabla ya kuzaliwa kama mwanadamu na atakatambuliwa kama Masihi, Mwana wa Mungu baada tu ya kubebwa mimba (Luka 1:40-45). Biblia tayari inaelezea furaha ya mtoto ambaye hajazaliwa (Luka 1:44) na hata ushindani (Mwanzo 25:21-23). Wale ambao hawajazaliwa bado wana nafasi thabiti na Mungu (Ayubu 10:8-12; 31:13-15). Sheria ya kibiblia huonyesha hali kubwa ya kujali ulinzi wa uhai wa binadamu na huchukulia hatari au kupoteza mtoto au mama kama matokeo ya kitendo cha kikatili kuwa ni suala kubwa sana (Kutoka 21:22-23).

3. ***Mapenzi ya Mungu kuhusu uhai wa mwanadamu yanadhihirishwa katika Amri Kumi na kuelezewa na Yesu katika hubiri lake katika Mlima wa Baraka.*** Amri kumi za Mungu zilitolewa kwa watu wa Mungu na kwa ulimwengu ili kuongoza Maisha yao na kuwalinda. Sheria zake ni kweli zisizobadilika zinazopaswa kutunzwa, kuheshimiwa, na kuzitii. Mtunga Zaburi anasifu sheria za Mungu (kwa mfano, Zaburi 119), na Paulo anaziita ni takatifu, na za haki, na njema (Warumi 7:12). Amri ya sita inasema: "Usiue" (Kutoka 20:13), ambayo huagiza kuhifadhi uhai wa binadamu. Kanuni ya kuhifadhi uhai iliyotunzwa katika amri ya sita huweka kitendo cha kutoa mimba ndani ya mipaka yake. Yesu aliongeza msisitizo wa amri ya kutokuua katika Mathayo 5:21-22. Uhai unalindwa na Mungu. Haupimwi kwa uwezo wa mtu mwenyewe au faida yao, bali kwa viwango ambavyo uumbaji wa Mungu na upendo wake wa kujitolea umeviweka. Utu, thamani ya mwanadamu, na wokovu havilipiwi gharama yoyote wala kwa kutunukiwa bali hutolewa kwa rehema na Mungu.

4. ***Mungu ndiye mwenye uhai, na mwanadamu ni wakili wake.*** Maandiko hufundisha kwamba Mungu anamiliki kila kitu (Zaburi 50:10-12). Mungu ana madai mawili juu ya wanadamu. Ni wa kwake kwa sababu yeye ndiye aliyewaumba, na hivyo anawamiliki (Zaburi 139:13-16). Ni wa kwake pia kwa sababu yeye ni Mkombozi wao na amewanunua kwa gharama kubwa zaidi – Uhai wake mwenyewe (1 Wakorintho 6:19-20). Hii humaanisha kwamba wanadamu wote ni mawakili wa cho chote ambacho Mungu amewapatia, ikiwemo uhai wao wenyewe, uhai wa Watoto wao, na wa wale ambao hawajazaliwa.

Uwakili wa uhai pia hujumuisha kubeba majukumu ambayo kwa namna fulani hupunguza chaguzi zao (1 Wakorintho 9:19-22). Kwa sababu Mungu ndiye Mtoaji na Mmiliki wa uhai, wanadamu hawana utawala wo wote juu yao wenyewe na wanapaswa kutafuta kutunza uhai wakati wo wote itakapowezekana. Kanuni ya uwakili wa uhai huipatia jamii ya waamini jukumu la kuongoza, kutegemeza, kujali, na kuwapenda wale wanaokabiliana na maamuzi kuhusu mimba.

5. ***Biblia inafundisha kuwajali wadhaifu na walio katika hali ya kudhurika kirahisi.*** Mungu mwenyewe anawajali na huwalinda.wale wenye shida na walioonewa "Asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa. Huwafanyia yatima na mjane hukumu ya haki, naye humpenda mgeni, akimpa chakula na mavazi" (Torati 10:17-18, Zaburi 82:3-4; Yakobo 1:27). Hawaadhibu Watoto kwa sababu ya dhambi za baba zao (Ezekieli 18:20). Mungu anategemea vivyo hivyo kwa Watoto wake. Wanaitwa kuwasaidia watu wadhaifu na kupunguza maumivu yao (Zaburi 41:1; 82:3-4; Matendo 20:35). Yesu anazungumza kuhusu ndugu zake walio wadogo (Mathayo 25:40), ambao wanafunzi wake wanapaswa kuwashughulikia, na walio wadogo ambao hawapaswi kudharauliwa au kupotezwa (Mathayo 18:10-14). Walio wadogo zaidi, ambao hawajazaliwa, wanapaswa kujumuishwa kati yao.

6. ***Neema ya Mungu inatetea uhai katika ulimwengu ulioharibiwa na dhambi na kifo.*** Ni asili ya Mungu kulinda, kutunza, na kuwezesha uhai. Kama nyongeza katika majaliwa ya Mungu kwa uumbaji wake (Zaburi 103:19; Wakolosai 1:17; Waebrania 1:3), Biblia hutambua athari za dhambi zilizosambaa, zinazoharibu, na kushusha hadhi juu ya uumbaji, ikiwemo miili ya wanadamu. Katika Warumi 8:20-24 Paulo anaeleza matokeo ya Anguko kama kuufanya uumbaji kuwa kitu kisichokuwa na maana. Hivyo, katika hali chache na za kutisha, utungaji mimba wa mwanadamu unaweza kutengeneza mimba zenye matarajio ya kufisha na/au matatizo ya uzazi yanayohatarisha Maisha ambayo huwaacha watu au wanandoa katika hali ya mtanziko usioepukika. Maamuzi katika hali kama hizo yanaweza kuachwa kwa dhamiri ya wahusika na familia zao. Maamuzi haya yanapaswa kuelezewa vema na kuongozwa na Roho Mtakatifu na mtazamo wa kibiblia wa uhai ulioainishwa hapo juu. Neema ya Mungu hukuza na kulinda uhai. Watu walio katika hali hizi zenye changamoto wanaweza kuja kwake kwa dhati na kutafuta uongozi, faraja, na amani katika Bwana.

VIDOKEZI

Kanisa la Waadventista wa Sabato huchukulia kitendo cha kutoa mimba kuwa kinyume na upatanifu na mpango wa Mungu kwa uhai wa mwanadamu. Huathiri kiumbe ambacho hakijazaliwa, mama, baba, wanafamilia wa karibu na wa mbali, familia ya kanisa, na jamii kwa ujumla, kwa athari za muda mrefu kwa wote. Waumini wanalenga kumwamini Mungu na kufuata nia yake kwa ajili yao, wakifahamu kwamba ana makusudi bora akilini mwake kwa ajili yao.

Pamoja na kwamba utoaji mimba haufumbiwi macho, kanisa na waumini wake wanaitwa kufuata mfano wa Yesu, "amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14) ili:

1. Kuleta mazingira ya upendo wa kweli na kutoa malezi ya kichungaji yaliyojawa na neema huku wakitegemezwa kwa upendo wale wanaokabiliana na maamuzi magumu kuhusu kutoa mimba
2. Kutafuta msaada wa familia zilizosimama imara na kuzielimisha namna ya kuhudumia huyo anayehangaika au kama ni wenzi wawili, au familia.
3. Kuhimiza washiriki kufungua milango ya nyumba zao kwa wale wenye uhitaji, pamoja na wazazi wasiokuwa na wenzi, Watoto wasiokuwa na wazazi na wale waliochukuliwa na wazazi ambao hawakuwazaa.
4. Kujali kwa undani na kutegemeza kwa namna mbalimbali wanawake wenye uja uzito ambao wameamua kuhifadhi Watoto wao ambao hawajazaliwa.
5. Kutoa msaada wa kiroho na kimhemuko kwa wale waliotoa mimba kwa sababu mbali mbali, au walilazimika kutoa mimba na pengine wameumia kimwili, kiroho au kimhemuko

Suala la kutoa mimba linaandamana na changamoto nyingi, lakini pia linawapatia watu mmoja mmoja, na kanisa fursa ya kuwa kile wanachotarajia kuwa, usharika wa ndugu na dada, jumuia ya waumini, familia ya Mungu wakidhihirisha upendo usioshindwa wala kupimika.

MIONGOZO KWA KANISA LA WAADVENTISTA WA SABATO JINSI YA KUITIKIA KATIKA MABADILIKO YA MTAZAMO WA KITAMADUNI KUHUSU

USHOGA NA VITENDO VYA NGONO M-BADALA

NDOA NA MASUALA YA NGONO KATIKA NDOA ILIYO KAMILIFU KIMBINGU

Masuala yanayohusiana na ngono katika ndoa yanaweza kuonekana katika nuru yake ya kweli yakiangaliwa kutoka katika usuli wa ukamilifu wa kimbingu kwa wanadamu. Kitendo cha uumbaji cha Mungu kilihitimishwa kwa kuumbwa kwa mwanadamu kwa mfano na sura yake, mwanamume na mwanamke, hivyo akaanzisha taasisi ya ndoa. Ndoa kama zawadi ya ajabu kwa ubinadamu ni muunganiko uliojengeka katika viapo vya jinsia mbili kimwili, kimhemuko, na kiroho kama "mwili mmoja" kwa jinsi tunavyoelezwa katika Maandiko. Yesu Kristo alitamka ndoa kuwa ya mume mmoja, mke mmoja, muunganiko wa kudumu maisha yote wenye uelewano na upendo kati ya mwanamume na mwanamke. Zaidi ya hapo, kote katika Maandiko muunganiko huo wa ndoa unainuliwa kama ishara ya muunganiko kati ya uungu na ubinadamu.

Uhusiano wenye upatanifu wa mwanamume na mwanamke katika ndoa unatupatia mfano wa umoja wa jamii ambao ni wa kudumu kama kitovu cha viambata vya jamii thabiti. Muumba alikusudia kwamba ngono katika ndoa itumike siyo tu kama kiungo, bali pia ilete furaha na raha katika utimilifu wa kimwili. Wakati huo huo ni wajibu wa mume na mke ambao upendo kati yao umewawezesha kufahamiana kwa undani wa kuunganishwa kwa ngono kiasi cha kudhaminiwa mtoto. Mtoto huyo, ambaye ni udhihirisho ulio hai wa kuwa kwao mwili mmoja, atastawi katika mazingira ya upendo na umoja wa ndoa na kupata bahati ya uhusiano na kila mmoja wa wazazi wake wa asili.

Pamoja na kwamba muunganiko wa mwanamume mmoja na mke mmoja katika ndoa unathibitishwa kama msingi wa kimbingu ulioagizwa kwa familia na maisha ya jamii na ndiyo kitengo pekee stahiki cha maadili na maisha ya jamii kama udhihirisho wa

uhusiano wa karibu wa kingono,[22] bado hata hivyo kuna wanaobakia bila muunganiko wa ndoa kwa muktadha wa usanifu wa kimbingu pia. Maandiko yanatofautisha kati ya mwenendo unaokubalika katika mahusiano ya kirafiki na mwenendo wa kingono katika ndoa.

Bahati mbaya mausala ya ngono na ndoa yamevurugwa na dhambi. Kwa hiyo, Maandiko hayajielekezi katika vigezo chanya tu vya ngono kwa wanadamu, bali pia kwa namna potovu ya ngono pamoja na matokeo yake yaliyo hasi kwa watu na jamii kwa ujumla. Hayo Maandiko yanaonya kuhusu mwenendo mchafu kingono kama vile uzinzi, uasherati, ngono kati ya jinsia moja, kujamiiana kwa maharimu, na mitala. (Kwa mfano, Mathayo 19:1-12; 1 Wakorintho 5:1-13; 6:9-20; 7:10-16, 39; Waebrania 13:4; Ufunuo 22:14, 15). Na hivyo anawaita wote kutenda kwa namna yenye afya na ya kunufaisha.

Kanisa la Waadventista wa Sabato linashikilia bila kupepesa macho katika uhusiano wa kingono ulio mkamilifu wa kimbingu, wenye heshima na upendo katika ndoa ya mume mmoja na mke mmoja, likiamini kwamba kukiuka utaratibu huu wa juu ni hatari kwa ubinadamu. Kanisa pia linaamini kwamba usafi mkamilifu na uzuri wa ndoa kwa jinsi Mungu alivyoikusudia unaweza kurejeshwa, na uzoefu wa utimilifu wa unyumba wa kufurahisha upokelewe na mwanamume na mwanamke walioounganisha maisha yao katika kiapo cha ndoa ya kudumu maisha yao yote.

KANISA NA JAMII

Kanisa la Waadventista wa Sabato wanaamini kwamba wameitwa na Mungu ili kuutangazia ullimwengu wote ujumbe wa milele, na kuwaita watu wa kila mahali kuwa tayari kwa ajili ya kuja mara ya pili kwa Yesu. Kanisa linafuatilia utume wa Mungu ulimwenguni kote kwa kufundisha, kuhubiri, kujali, na kutoa huduma katika mataifa zaidi ya 200. Kanisa la Waadventista wa Sabato, hawana tamko la Imani: wanaamini kwamba mafundisho yake yanatokana na mamlaka ya Biblia pekee. Wanayaweka kwa muhutasari wa Imani, hivyo kuwa na tamko la Imani za msingi ambazo sasa ni 28. Fundisho la "Ndoa na Familia," ni kitovu cha uelewa wa mpango wa Mungu wa kuelekeza jamii ya wanadamu.

Kwa sababu Waadventista wa Sabato wanaishi, wanafanya kazi, na kuhudumu sehemu zote za ulimwengu, waumini mmoja mmoja na taasisi zinazotumiwa na kanisa kufuatilia utume wa Mungu zinahusiana na kuingiliana katika ngazi zote za serikali za

[22] See the Seventh-day Adventist Church's Official Statements about "Same-Sex Unions" and "Homosexuality."

kibinadamu. Biblia inawaagiza Wakristo kuwa watiifu kwa sheria zinazowekwa na serikali, na kwa namna yoyote ya kimaadili, washiriki wa kanisa hili watatafuta kutii mamlaka za kiserikali, kwa kufuatana na ushauri wa jinsi ya kuitikia pale madai ya serikali yanapopingna na ukweli wa Biblia na Imani za Msingi za Kanisa.

UHUSIANO WA KANISA NA SHERIA ZA KIRAIA KUHUSU USHOGA NA MWENENDO M-BADALA WA KINGONO

Neno la Mungu limejawa na maagizo na melekezo kuhusu uhusiano wa waumini na mamlaka na sheria za serikali. Kwa sababu kanisa la Waadventista wa Sabato linathamini ukamilifu wa Neno la Mungu kama mamlaka yake ya ukweli, mafundisho, na namna ya kuishi, siku zote likitafuta kuakisi ujumbe wa Maandiko kuhusu namna sahihi ya kuingiliana na serikali ya kiraia. Hadi hapo, kanisa litatoa ushauri kwa vipindi mbali mbali kwa watu mmoja mmoja, viongozi, na taasisi zake, inapotokea kuwa madai ya serikali ya kiraia yakaonekana kupingana na Biblia. Andiko hili linajielekeza katika kujitokeza kwa mgawanyiko kati ya sheria zinazotungwa na baadhi ya serikali za kiraia na Imani za kanisa la Waadventista wa Sabato kuhusu mwenendo wa kingono unaokubalika.

Kanuni zifuatazo zinategemeza kanisa katika namna linavyoweka katika utendaji kweli za Biblia kwa jamii na tamaduni linapotenda kazi na mwitikio wake kwa serikali. Kanuni hizi zitakuwa muhimu katika kuunda mwitikio stahiki kwa huduma za kanisa au shirika kwa ujumla katika ngazi yoyote ya serikali ya kiraia itakayojaribu kushinikiza mtazamo wake kwa kanisa kisheria au kimaadili kuhusu mwenendo wa kingono unaokubalika:

1. **Serikali zote za kibinadamu zinakuwapo kupitia katika majaliwa na ukubali wa Mungu.**
   Mtume Paulo anawaelekeza Wakristo na kanisa kwa uwazi kutii bila shuruti serikali za kibinadamu ambazo zimewekwa na Mungu ili kuhifadhi uhuru waliopewa na Mungu, kuendeleza haki, kulinda amani katika jamii, na kuwajali wale wasiobahatika (tazama WArumi 13:1-3). Mpaka hapo ikiwa watatenda sawa sawa na maagizo na kanuni zilizoainishwa katika Neno la Mungu, serikali za kiraia zinastahili heshima na utii wa waumini mmoja mmoja na kanisa kama shirika. Pale inapowezekana, waumini mmoja mmoja na kanisa kwa ujumla katika eneo au jimbo fulani wataeleweka kwa mwenendo wao na matamko yao kuwa raia wema, wakishiriki katika haki na majukumu ya uraia. zaidi ya hapo,

waumini wanaagizwa kuwaombea wenye mamlaka ya kiraia (1 Timotheo 2:1, 2) ili kwamba waumini waweke katika utendaji wema wa ufalme wa Mungu.

2. **Ingawaje mamlaka ya serikali za kibinadamu inatokana na mamlaka ya Mungu, madai na utekelezaji wa sheria za serikali za kiraia siyo maamuzi ya mwisho kwa waumini mmoja mmoja au kwa kanisa zima. Waumini mmoja mmoja pamoja na kanisa wanastahili kumtii Mungu pekee.**
   Inapotokea kwamba madai ya serikali ya kiraia yanapingana moja kwa moja na kukanusha mafundisho ya Neno la Mungu kwa namna yanavyoelewaka kwa kanisa la Waadventista wa Sabato, washiriki wake pamoja na kanisa kwa pamoja wanafungwa na Neno la Mungu kutii maagizo yake kuliko maagizo ya serikali za wanadamu (Matendo 5:29). Maelezo haya ya utii kwa Neno la Mungu ni maalum pale tu madai ya serikali yanapopingana na Neno la Mungu, na hayahafifishi au kuondoa wajibu wa kanisa au waumini mmoja mmoja kuishi wakitii mamlaka ya kiraia katika masuala mengine.

3. **Kwa sababu waumini mmoja mmoja, na kanisa kwa ujumla wana haki na uhuru waliopewa na Mungu, na kuthibitishwa na serikali, wanaweza kushiriki kikamilifu katika mchakato ambao jamii zinaendesha maisha ya kijamii, wakiupatia umma pamoja na mpangilio wa uchaguzi na mfumo wa mahusiano ya kiraia.**
   Hii ni pamoja na matamko ya Imani za kanisa katika mambo kama:
   i. Kulinda uhuru wa dhamiri
   ii. Kuwalinda wanyonge na wasiobahatika
   iii. Wajibu wa serikali kutenda kwa haki na kulinda haki za binadamu
   iv. Hali ya ndoa iliyoanzishwa na mbingu kati ya mwanamume mmoja na mwanamke mmoja na familia ambayo itakuwa ni matokeo ya muunganiko huu.
   v. Maadili aliyotoa Mungu kuhusu kanuni za afya na utendaji wake katika kujenga ustawi wa jamii na uchumi wa taifa.

   Hakuna muumini wa kanisa la Waadventista wa Sabato, wala jumuiko, taasisi, au kitengo chochote cha kanisa kinachojihusisha na utume waliopewa na Mungu watakaosalimisha stahiki na haki zao kama matokeo ya upinzani kwa utiifu wao kwa mafundisho ya Biblia. Kanisa la Waadventista wa Sabato pamoja na historia yake ya kutetea uhuru wa dini na haki ya kuabudu duniani kote, linatetea haki ya watu wote, wa Imani yoyote, kufuata dhamiri zao na kujihusisha katika masuala ya kidini katika Imani zinazowahusu.

4. **Kwa sababu kanisa la Waadventista wa Sabato wanaamini na kujihusisha na uelewa mkamilifu wa injili ya Yesu Kristo, uinjilisti wake, elimu, machapisho, tiba na huduma zingine zinazoendeshwa kama sehemu ya udhihirisho usiogawanyika wa utekelezaji wa agizo la Yesu kwamba, "Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." (Mathayo 28:19, 20)**

   Pamoja na kwamba jumuiko, huduma za uchapaji, vyombo vya Habari, taasisi za elimu, hospitali na vituo vya afya, na huduma zingine za Waadventista wa Sabato zinaonekana kushiriki baadhi ya mambo yanayofanana na taasisi zingine za kijamii na kitamaduni, wameanzishwa na wanaendelea kujengwa katika Imani na misingi ya umisioanari. Wapo kwa kusudi la kuwasilisha elimu iokoayo ya Yesu Kristo kupitia katika mbinu za aina mbali mbali na za kufundisha wakiendeleza utume wa kanisa la Waadventista wa Sabato, huku wakifurahia matokeo mazuri, na uhuru unaotolewa kwa mashirika ya kidini pamoja na hilo la kwao. Kanisa la Waadventista wa Sabato wanatamka kwa msisitizo na kutetea kutokuwepo na mgawanyiko katika aina mbali mbali za utume wake, na kuhimiza serikali zote za kiraia kuruhusu shirika na vitengo vyaka kupewa haki ya mawazo na uhuru wa dini katika utendaji kama ilivyo katika tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za binadamu na kuingizwa katika katiba za mataifa mengi.

5. **Kanisa la Waadventista wa Sabato na waumini wake mmoja mmoja, katika kuingiliana na serikali za kiraia pamoja na jamii kwa ujumla wake, wanapaswa kutenda kama wawakilishi wa ufalme wa Kristo, wakionesha tabia yake ya upendo, unyenyekevu, uadilifu, upatanifu, na kujitoa kikamilifu katika ukweli wa Neno la Mungu.**

   Kila mwanadamu wa jinsia yoyote, rangi, taifa, daraja katika jamii, Imani, mwelekeo wa kingono, anastahili kutendewa kwa heshima na utu na kanisa la Waadventista wa Sabato pamoja na vitengo vyake, na muundo wake wote unaotumika katika utume wa Mungu. Kwa sababu kanisa linajitambulisha kama mwili wa Kristo ambaye "alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi" (Warumi 5:8), kanisa linasimamia kiwango cha juu cha matamko na mwenendo kuhusu wanadamu wote. Kanisa linatambua kwamba Mungu ndiye hakimu mkuu wa wanadamu wote, na kuamini katika fursa kwa watu wote kujumuishwa katika ufalme wa mbinguni kadiri wanavyokiri na kuacha dhambi zao wakimkiri Kristo kama Bwana na Mwokozi wao, na kukubali haki yake badala ya ile ya kwao wenyewe, wakitafuta kutii amri zake, na kuishi maisha ya

utumishi. Kanisa linathibitisha haki yake ya kuelezea baadhi ya mwenendo, namna ya kuishi, na mashirika yanayotangaza kinyume na Neno la Mungu. Kanisa pia linawajibika katika kutofautisha kwa uwazi kati ya uhakiki wa Imani hizo na tabia, na kuheshimu mtu anayeeleza Imani na tabia hizo. Kanisa halitapuuza wala halitaruhusu matamko yake ya hadhara kuhusu masuala ya jamii kuchukuliwa kama dharau au aina fulani ya unyanyasani kwa wale ambao halikubaliani nao. Katika kuhakikisha uhuru wake, matamko yake ya hadhara ni lazima yadhihirishe neema ile ionekanayo kwa Yesu. Vitengo vyote vya kanisa la Waadventista wa Sabato na mashirika yake, pamoja na waumini mmoja mmoja, wanahimizwa kuonesha heshima kwa vikundi vya watu vyenye mwenendo na mawazo yanayotofautiana nao, kwa sababu ya utii wao katika Neno la Mungu. Kanisa lina heshima ya kushiriki katika masuala magumu ya kijamii na kitaifa kwa kujitambulisha wazi wazi kama kitengo cha ukombozi.

Katika nuru ya kanuni hizo hapo juu zitokanazo na Neno la Mungu, kanisa la Waadventista wa Sabato linatoa ushauri kwa makusanyiko, mashirika ya dini na vitengo vyake, pamoja na wale wote wanaoongoza mashirika ya makanisa na vitengo mbali mbali. Suala tata linaloghubika mwitikio wa serekali kwa uhalisia wa ushoga na vitendo vya ngono m-badala katika jamii za kileo linaweka uzito kwenye ushauri huu.

CHANGAMOTO ZA SHERIA YA NCHI

Katika kuongezeka kwa mataifa, serikali zinatunga sheria maalum au ulinzi wa kimahakama ili kuzuia kile wanachochukulia kama mwenendo wa kibaguzi. Ulinzi huo wakati mwingine unaonekana kuathiri haki ya uhuru wa dini wa wachungaji, viongozi, taasisi za shirika la kanisa la Waadventista wa Sabato kuajri mtu, kufunga ndoa, kutoa mafao ya ajira, kuchapisha machapisho ya utume, kutoa matamko ya hadhara, na kutoa elimu au majumba ya kuelimisha kwa misingi ya mafundisho ya Waadventista wa Sabato kuhusu namna Maandiko yanavyozuia dhambi katika mwenendo wa ngono.

Kinyume chake katika baadhi ya mataifa, ushoga na vitendo vya ngono m-badala vinaadhibiwa kwa adhabu kali kulingana na sheria. Lakini taasisi za Waadventista wa Sabato na waumini wake wanaweza kutetea kwa namna sahihi kuhifadhi taasisi ya pekee ya ndoa iliyotolewa na Mungu, ya mume mmoja na mke mmoja katika jamii zao na kanuni za kisheria, ni msimamo wa kanisa kushughulika na wale wanaoendekeza ushoga na vitendo vya ngono m-badala kwa upendo wa ukombozi aliofundisha Yesu na kuuishi

UHURU WA KIDINI NA KIMAADILI WA KANISA

Kanisa la Waadventista wa Sabato litahimiza majumuiko yake yote, waajiriwa, viongozi wa huduma, mashirika, na vitengo vyake vyote kutetea mafundisho na utendaji uliojengeka katika Imani kwa ushirika wake, ajira, elimu, sherehe za ndoa, pamoja na kufungisha ndoa. Mafundisho hayo na utendaji uliojengeka katika Imani, msingi wake ni maagizo ya Biblia kuhusu ngono kwa wanadamu, na kwa namna hiyo hiyo kwa mahusiano ya jinsia tofauti na yale ya jinsia moja. Ni kinyume na msimamo wa uelewa wa kanisa wa mafundisho yatokanayo na Maandiko kumwingiza katika ushirika na kumlea mtu mwenye mwenendo wa ngono usiopatana na mafundisho ya Biblia. Wala haikubaliki kwa mchungaji wa kanisa la Waadventista wa Sabato kufanya huduma ya ndoa kwa watu wenye jinsia moja.

Katika kutetea viwango vya Maandiko, kwa kawaida kanisa linategemea misamaha iliyojengeka katika Imani inayotolewa na serikali za kiraia kwa mashirika ya kidini na huduma zinazoambatana nayo katika kujipanga kulingana na uelewa wa kweli za kimaadili. Kanisa litajaribu kutoa ushauri wa kisheria na vitendea kazi kwa viongozi wake, mashirika yake na vitengo vyake ili watende kwa upatanifu na uelewa wa Kibiblia wa masuala ya ngono kwa wanadamu.

Viongozi wa makundi, waajiriwa wa kanisa, viongozi wa huduma, na taasisi wanashauriwa kupitia upya kwa uangalifu sera za kanisa zilizopo kuhusu ushirika, ajira, na elimu ili kuhakikisha kwamba utendaji katika ngazi husika una upatanifu na mafundisho ya kanisa kuhusu mwenendo wa kingono. Maelezo ya msimamo na kuweka katika utendaji sera za shirika na mafundisho yake kuhusu mwenendo kama huo yatakuwa ni kiini cha kudumisha msamaha unaotolewa na serikali ukijengeka katika Imani.

MAAMUZI YA KUAJIRI NA KUANDIKISHA KWA KIGEZO CHA IMANI

Kanisa la Waadventista wa Sabato linatetea na kutunza haki kwa vitengo vyake vyote kuajiri watu kulingna na mafundisho ya kanisa kuhusu mwenendo wa kingono unaokubaliana na mafundisho ya Maandiko kama yanavyoeleweka na kanisa la Waadventista wa Sabato. Pamoja na kwamba kila taasisi na huduma hufanya kazi katika mazingira ya jamii husika na sheria zake, bado kila moja ya taasisi hizo kuonesha mfumo wa Imani wa kilimwengu na mafundisho ya kanisa la ulimwengu. Kanisa

linahifadhi haki ya huduma hizo pamoja na taasisi kufanya maamuzi kulingana na mafundisho ya Maandiko na kutoa ufafanuzi wa kisheria kwa sheria na maagizo.

Pale inapowezekana, kanisa litaendelea kutetea kisheria, na mahakamani, mwelekeo wake wa kuajiri na kuandikisha kwa misingi ya Imani kwa ajili yake na huduma zake.

KANISA NA HOTUBA ZA HADHARA

Kanisa linatetea haki ya kuonesha kujitoa kwake kikamilifu katika ukweli wa Biblia kupitia katika mawasiliano linayofanya kwa waumini wake na kwa hadhira zingine mbali mbali, pamoja na kutetea haki ya uhuru wa kujieleza wa wafanyakazi wake katika kuonesha mafundisho ya kanisa kuhusu mwenendo wa kingono katika mazingira ya umma, pamoja na huduma za ibada, mikutano ya kiinjili, madarasa ya kuelimisha, na katika majukwaa ya umma. Viongozi wa kanisa wanakubali wajibu wa kuhabarisha kanisa na waajiriwa wake kuhusu kanuni za serikali kuhusu hotuba zinazokubalika, na kupitia kisheria mara kwa mara ili kuona jinsi hizo kanuni zinavyoathiri utume wa kanisa. Wale wanaofanya mawasiliano rasmi ya kanisa, pamoja na wale wanaohubiri na kufundisha wanatakiwa kusisitiza umuhimu wa kusalimisha mwenendo wote, pamoja na mwenendo wa kingono katika uwezo ubadilishao wa Yesu Kristo. Kiwango cha machapisho, na matamko ya hadhara kuhusu mwenendo wa kingono ni lazima yatambuliwe kwa upana wake kama "safi na yenye heshima," yakidhihirisha ukweli wa Biblia kwa upole na kwa wema wa Yesu Kristo mwenyewe.

KANISA NA HOTUBA ZA HADHARA

Ili kupata namna endelevu ya kuweka katika utendaji kiwango cha "safi na yenye heshima" katika huduma zake, kanisa linahimiza huduma zake zote, pamoja na uchungaji, uinjilisti, elimu, uchapaji, vyombo vya Habari na huduma za afya na tiba, kuendesha mafunzo mara kwa mara na kutoa ushauri kwa waajiriwa wanaoingiliana na umma kupitia katika mitandao na uwasilishaji wa hadhara. Mafunzo haya yanaweza kujumuisha mapitio ya sheria za taifa au jumuia zilizopo kuhusu hotuba ya hadhara inayolenga mwenendo wa kingono, na mifano ya namna sahihi ya kuwasilisha Imani na mafundisho ya kanisa.

Nyenzo hii pia inajumuisha mawasilisho ya semina na vitini bila malipo.
Kupaua nyenzo hizi, tafadhali tembelea tovuti hii:
www.family.adventist.org/2023RB